

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 11 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.192

**Serikali Kusimamia Sheria ya Udhibiti wa Mazingira**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA K.n.y. MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu inaathirika na uharibifu mkubwa wa mazingira hasa uharibifu wa misitu kutokana na uchomaji wa mkaa na ukataji wa miti ovyo kwa ajili ya kilimo:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani kusimamia Sheria zilizotungwa kudhibiti uharibifu huo?

(b)Je, ni lini Serikali itaweka mazingira rahisi ya utumiaji wa Nishati ya mkaa ya mawe na kuhimiza matumizi ya umeme kwa kupikia ili kuokoa mazingira?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkansi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Bunge lako tukufu lilipitisha sheria ya usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na sheria ya misitu ya mwaka 2002. sheria ya misitu inahimiza usimamizi shirikishi wa misitu na inawapa uwezo Halmashauri za Wilaya kutunga sheria ndogo katika usimamizi bora wa mazingira na misitu. ili kusimamia sheria hii pamoja na mambo mengine Serikali inafanya juhudi zifuatazo:-

(i) Imeandaa mwongozo wa uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu ya mwaka 2006. mwongozo huo unasisitiza uvunaji bora unaozingatia mpango wa usimamizi;

(ii) Inaendelea kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya teknolojia rahisi ya nishati mbadala na jadidifu na kufanya utafiti kupitia Tume ya Sanyansi na Teknolojia zinazolenga kupunguza mahitaji ya kuni na mkaa;

(iii) Imeanzisha vikosi vitano vya doria hadi sasa ili kukabiliana na biashara haramu ya mazao ya misitu ikiwemo kukata miti ovyo na kuchoma mkaa;

(iv) Imeanzisha vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu katika maeneo yanayosafirisha mazao hayo kwa wingi nchini;

(v) Imeandaa mwongozo wa mpango wa usimamizi wa misitu ambao utaanza kutumika katika usimamizi wa misitu asili, kwa mujibu wa mpango huo hairuhusiwi kuvuna misitu ambayo haina mpango wa usimamizi;

(vi) Imeongeza idadi ya hifadhi asilia za misitu ambapo usimamizi wake umeboreka zaidi na hivyo kuzuia shughuli za ukataji miti ovyo na uchomaji wa mkaa; na

(vii) Inatekeleza mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, mkakati huu unawashirikisha wadau mbalimbali na unatekelezwa Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia inafanya utafiti wa vitofali vya makaa ya mawe (*coal-clay briquettes*) katika mgodi wa Kiwira ili kupunguza muda wa kuwasha vitofali, makali ya moto na gesi chafu zenye oksidi za *sulfur (Sox)* zinazozalishwa na kutengeneza majiko ya bei nafuu.

Hadi sasa utafiti umefanikiwa kupunguza ukali wa moto wa vitofali vya makaa ya mawe, utafiti unaendelea katika kupunguza muda wa kuwasha vitofali, wingi wa gesi chafu zinazozalishwa na makaa ya mawe na utengenezaji wa majiko ya bei nafuu. mapungufu hayo yakipata ufumbuzi Watanzania wengi zaidi watatumia makaa ya mawe kupikia na hivyo kuhifadhi mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali inahimiza uendelezaji wa matumizi ya nishati mbadala na jadidifu kama vile nishati ya jua, upepo, gesi asilia na *bio-gas*. Pia kuendeleza matumizi ya jiko sanifu mkaa unaotengenezwa kwa taka za nyumbani na jiko za moto poa. Ni matumaini yangu kuwa kupitia wakala wa nishati Vijijini maeneo mengi yatapata nishati ya kupikia ikiwemo ya umeme kwa gharama nafuu.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri:-

(i)Je, Serikali haioni kwamba sheria ndogo ndogo hizi zinazotungwa na Halmashauri zinashindwa kutekelezwa vizuri kwa sababu Maafisa Misitu wanaopaswa kusimamia miradi hii ya kutokata misitu hawatoshi.

Katika Wilaya ya Nkasi ambayo ina misitu mingi sana Maafisa Misitu hawatoshi, na katika Halmashauri ya Sumbawanga vijijini ndiyo maana msitu mkubwa wa Kalambo na Msitu mkubwa wa Dwafi unaendelea kufekwa kwa ajili ya kutengeneza mkaa na kwenda kuuza katika Miji ya Namanyere na Sumbawanga. Je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hawa maafisa wanaosimamia misitu wanaongezwa ili kuweza kusimamia hizo sheria ndogo ndogo za Halmashauri.

(ii)Vipo vikundi vya akina mama ambao wamejitolea kufanya kazi ya kueneza matumizi ya Mkaa wa Mawe unaochanganywa kidogo na udongo wa mfinyanzi ili kujaribu kuzuia watu wasikate miti kutengeneza mkaa na badala yake watumie ule mkaa tulionao wa Kiwira na sehemu nyingine.

Je, Serikali haioni kuwasaidia hawa akina Mama ambao wamejitokeza katika maonesho mbalimbali itakuwa ni jawabu la kusaidia kupunguza ukataji na uharibifu wa misitu katika nchi hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Lodovick Mwananzila, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kuhusu jitihada za Serikali katika kuongeza Maafisa Misitu, napenda kumhakikishia kwamba kufuatana na hotuba inayoendelea sasa ya Wizara ya Maliasili na Utali kumeonyeshwa kabisa jitihada za kuongeza wataalamu hao. Lakini vilevile Serikali kupitia Ofisi yetu ya Makamu wa Rais Kitengo chetu cha Mazingira tupo katika hatua za mwisho za kuweza kuwaajiri Maafisa Mazingira katika maeneo yote ya Wilaya yetu, tayari Wilaya kadhaa zimesha ajiri Maafisa hao ambao kwa kweli kazi yao watashirikiana pamoja na Maafisa Misitu katika kuhakikisha kwamba Mazingira yetu yanalindwa na kuhifadhiwa.

(ii) Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mwananzila kwa jitihada zake za kuwa mwanaharakati na mpenzi wa kulinda Mazingira, mimi binafsi nilikutana na akina mama hao katika maonesho ya Saba Saba na tumekubaliana kwamba tutashirikiana nao katika maonesho ya Nane Nane hapa na kupitia Ofisi yetu ya Makamu wa Rais kitengo chetu cha Mazingira tutahakikisha kabisa kwamba tunashirikiana nao na kuhakikisha teknolojia hii rahisi ya kutumia vumbi za makaa ya mawe ambayo wanachanganya taka zingine inaweza kuendelezwa na kuweza kuokoa misitu yetu na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimpongeze Waziri kwa majibu

mazuri aliyotupatia, Mkoa wa Rukwa hususani Wilaya ya Mpanda pamoja na Nkansi kuna mapori mazuri sana pamoja na hifadhi za wanyama, sasa hivi hawa waharibifu wameshaanza kuingia katikati ya mapori hayo na kuzidi kuharibu mapori hayo.

Je, Waziri yupo tayari kuja Mkoa wa Rukwa kuja kuona hali halisi ya mapori yetu jinsi yanavyoharibika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Rukwa swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze na yeye kwa jitihada zake za kuweza kufuatilia masuala ya mazingira na nijibu tu kwamba mimi niko tayari kabisa kuandamana naye Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Ponsiano Nyami na Mheshimiwa Mwananzila kwenda Mkoa wa Rukwa na kuweza kuangalia hali ilivyo.

Lakini niwaeleze tu Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma kwamba tarehe 25 tutakuwa na mkutano nao kuwaelezea masuala ya maendelezi ya ziwa letu Tanganyika kwa hivyo pamoja na hayo tutazungumzia mambo yote ya uhifadhi wa mazingira.

**MHE. ELIATA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasikwa kuwa Mkoa wa Rukwa unayo Makaa yam awe ambayo sasa hivi yanachimbwa na mchimbaji mdogo lakini misitu yetu inaendelea kuteketea, Je Serikali inasemaje kama ingeweka nguvu ili makaa hayo ya mawe yaweze kutumika Mkoani Rukwa kupunguza uharibifu wa mazingira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliata Switi, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Rukwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kuna maeneo ambayo yanahifadhi hiyo ya makaa ya mawe na kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nilieleza kwamba tafiti zile ili kuhakikisha kwamba makaa ya mawe katika kutumika kwa matumizi ya kupikia hayatakuwa na madhara kwa binadamu.

Lakini pia tuangalie ni jinsi gani tunaweza kupunguza ukali wa moto ule wa makaa ya mawe, kwa hivyo nakubaliana na wewe kabisa kwamba tafiti zitaendelea na pale tutafikia katika hatua nzuri ya kuweza kuhakikisha kwamba inaweza kutumika sasa tutahakikisha kwamba na watu wenye rasilimali hizo wanaweza kutumia na tunataka

lifanyike hivi kwa haraka kwa sababu tunataka kupunguza matumizi makubwa ya mkaa na kuni ambao unaharibu sana misitu yetu.

Na. 193

### **Shamba la Mifugo Linalomilikiwa na SMZ huko Bagamoyo**

**MHE. MOSSY SULEIMANI MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliwahi kuwa na shamba kubwa la mifugo (ng'ombe) ranchi huko Bagamoyo:-

- (a) Je, Serikali ya SMZ bado inamiliki shamba hilo?
- (b) Je, hadi kufikia kuboreshwa kwa shamba hilo SMZ ilitumia shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleimani Mussa Mbunge wa Mfenesini lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika kwa kuzingatia Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) iliyoko Makurunge katika Wilaya ya Bagamoyo inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ranchi hiyo ilianzishwa mwaka 1976 baada ya kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Ardhi chenye kumbukumbu namba *LD/70254/12/TBR* cha tarehe 24/09/1971, hivyo kwa taarifa hizo Wizara yangu bado inaamini shamba la RAZABA bado ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hata hivyo kwa vile swali linaloulizwa na Mheshimiwa Mbunge linahusu mali zilizo chini ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi sio Wizara ya Muungano napenda kumjulisha Mheshimiwa kuwa Wizara yangu haiwajibiki kujua kama Serikali ya Mapinduzi Zanzibar bado inamiliki au haimiliki shamba hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijui kama shamba hilo ambalo liko chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilitumia shilingi ngapi katika kuliboresha, namshauri Mheshimiwa Mbunge akapate majibu ya takwimu hizo Wizara inayohusika katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba kutoa maelezo ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, shamba hilo ambalo ni kweli kama alivyosema Naibu Waziri lilimilikishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini kwa miaka mingi sana karibu 30 halitumiki, kwa hivi karibuni Serikali imemega sehemu na kuwapa wawekezaji, watawekeza katika mambo ya biofuel na Sehemu bado inaendelea kuwa mali ya SMZ.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waheshimiwa Mawaziri, lakini nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa mali hii imemilikishwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na leo imechukua hatua ya kulimega, hawahisi kwamba wanaleta matatizo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali hatudhani kwamba tunaleta mgogoro wowote, kwa miaka karibu 30 halitumiki, kwa hiyo tunataka sasa sehemu ya shamaba hilo lianze kutumika, sehemu iliyobaki tunawaomba waanze kulitumia isipowatosha bado ardhi ipo tutawapa maeneo mengine.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa jawabu zuri la Waziri, nataka maelezo sahihi kwa nini Serikali ilishindwa kutoa hati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye shamba hilo na hivi sasa wamechukua maamuzi ya kulimega?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza hakuna tatizo kama wakihitaji hati miliki kwa sababu ni la kwao, lakini pia isieleweke kwamba Serikali ya Muungano ndiyo imemega kwa mabavu, ni kwa ridhaa ya SMZ yenyewe kwa sababu hili eneo ni kubwa sana hawawezi kutumia lote.

Kwa hiyo, wakaruhusu kwamba sehemu nyingine inaweza ikatumiwa na watu wengine na wenyewe wabakiwe na sehemu ile ambayo wanadhani wanaweza wakaitumia.

Na. 194

### **Tatizo la Wizi wa Mifugo Katika Wilaya ya Karagwe**

**MHE. GOSBERT BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, vitendo vya wizi wa mifugo vimekuwa vinajirudia mara kwa mara na wananchi wa Karagwe wamekata tamaa ya kufuga kutokana na kukosekana kwa usalama wa mifugo yao;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudumu wa kumaliza tatizo hilo la wizi wa mifugo Wilayani Karagwe?

## **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ni kweli kwamba pamekuwepo matatizo ya wizi wa mifugo nchini hususani katika baadhi ya maeneo ya mipakani, katika Wilaya ya Karagwe kati ya mwaka 2005 na 2008 matukio ya Wizai 671 yanayohusisha jumla ya mifugo 7,918 yalitokea. kati ya mifugo hiyo 2,323 (29%) ilipatikana na kurejeshwa kwa wenyewe, watuhumiwa 449 walikamatwa na kesi 246 zilifikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo, Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Kagera limekuwa likifuatilia matukio ya wizi wa mifugo kwa kushirikiana na wananchi pindi matukio hayo yanapotolewa taarifa, aidha Jeshi hili limekuwa likifanya doria katika maeneo yaliyokithiri kwa matukio ya wizi na ujambazi ukiwemo wa msitu wa Kimisi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Serikali imeimarisha utaratibu wa kutoa vibali kusafirisha mifugo kwa kushirikiana na uongozi wa vijiji na kudhibiti uhamishaji holela wa mifugo kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kwa mfano kati ya mwezi Julai 2007 hadi Machi 2008 jumla ya vibali 268 vilitolewa kwa ajili ya kusafirisha ng'ombe 3,481 Wilayani Karagwe na vibali 37 vilitolewa kusafirisha ng'ombe 1,080 nje ya Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, Aidha katika 2008/2009 Serikali imepanga kujenga vituo 6 vya ukaguzi wa mifugo mpakani (*Veterinary Inspection Centres*) ili mifugo yote inayoingia na kutolewa nje ya nchi ikaguliwe. Utaratibu huu utaimarisha ulinzi wa mipaka yetu kwa lengo la kuwabana wale wote wenye nia ya kuingiza ama kutoa mifugo nchini bila utaratibu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na mfumo wa kudumu wa kutatua tatizo la wizi wa mifugo hususani katika maeneo ya mipakani ikiwemo Wilaya ya Karagwe, Serikali ina mikakati wa kuandaa na kutekeleza mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji Mifugo (*Identification, Registration and Traceability*) utakaoambatana na sheria inayoandaliwa ya kutekeleza azma hiyo pamoja na kuthibiti usafirishaji holela wa mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa baada ya kuanza kutekelezwa kwa mfano huo kutakuwa na udhibiti wa uhakika wa vitendo vya wizi wa mifugo hapa nchini. Napenda kutoa wito kwa wananchi wa Karagwe washirikiane na vyombo vya dola katika kudhibiti wizi wa mifugo katika maeneo yao kwani imegundulika baadhi ya watuhumiwa wa wizi huu ni wakazi wa Wilaya ya Karagwe.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Pamoja na juhudi zote hizi za Serikali lakini bado wizi wa mifugo Wilayani Karagwe unazidi kushamiri na tatizo kubwa ni kutokana na upungufu wa askari Polisi, upungufu wa magari, pikipiki pamoja na vifaa vya mawasiliano kama simu za mikononi. Je, Serikali inajiandaa vipi kuwasaidia Askari polisi walipo Karagwe waweze kupambana na majambazi wanaoiba mifugo?

(ii) Kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kulinda Wananchi na mali zao na hawa majambazi wanaoiba mifugo ya Wananchi wa Karagwe wanabakia maskini kiasi kwamba wanashindwa kumudu maisha yao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipa fidia wananchi wa Jimbo la Karagwe wanaoibiwa mifugo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Jeshi la Polisi linakabiliwa na upungufu wa vifaa na vilevile askari. Lakini ukweli ni kwamba kama tatizo hili ni sugu Serikali yetu haitashindwa kulidhibiti hatutatumia upungufu wa vifaa, kama juzi ilivyokuwa pale Rorya baada ya kuona kwamba tatizo ni kubwa Serikali imeji-*mobilise* imepeleka askari wa kutosha na sasa wanalishughulikia kama hali itajulikana kwamba ni mbaya. Sina wasiwasi kwamba Serikali itachukua hatua hizo na kuukomesha uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika sheria ya Tanzania, kama mtu amekuibia, ukamkamata na akahukumiwa ndiyo anatakiwa akulipe mali ulizopoteza. Katika jibu langu la msingi kwamba kuna wezi wengi ambao wamekamatwa na wamefikishwa mahakamani pale ambapo watakapopatikana na hatia pale ndipo watawajibika. Itakuwa vigumu sana kama mali ikiibiwa Serikali ilipe kwa sababu kwa kweli siyo kwamba Serikali imepuuzia ama imezembea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba kunapokuwa na wizi Serikali imekuwa ikifuatilia kwa kasi sana na ndiyo maana mifugo mingi imeweza kukamatwa na kurudishwa na watu kufikishwa mahakamani. Kwa hiyo, wale walioibiwa ni vizuri sana wakadai hao hao waliowaibia ng'ombe ambao wamekamatwa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ningependa kuongezea majibu mazuri sana ya Naibu Waziri kwa kusema yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo la wizi wa Mifugo hapa nchini iko katika harakati za kuimarisha kikosi maalum cha *STPU* ambacho ni kikosi maalum



cha kuzuia wizi wa mifugo, mwezi uliopita ACP Ray Kalama ameteuliwa kuwa Mkuu wa Kikosi hicho na wiki ijayo kwa kutambua tatizo la huko Karagwe ataenda katika ziara maalum Karagwe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimebaini mapungufu kidogo katika majibu ya swali Na. 193 ambalo ni lazima niyatolee mwongozo. Katika majibu Wizara imejibu kwamba inamshauri Mheshimiwa Mbunge akapate majibu ya takwimu kutoka Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge na hii nawaomba Waheshimiwa Mawaziri mzingatie, Mbunge wa Jamhuri ya Muungano anapouuliza swali anataka apate jibu hapa, tunaamini kabisa kwamba Serikali zetu hizi mbili zina mashauriano, mimi sioni kwa jinsi gani Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano anaweza kwenda Zanzibar amtafute Waziri ambaye anawajibika katika Serikali ya Mapinduzi yeye ndiyo amwulize swali.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba tafadhali hata kama lilahusu Wizara nyingine au linahusu sehemu nyinge ya Muungano, takwimu hizo zitafutwe kwa sababu Serikali inafanya kazi kwa ushirikiano ili jibu lipatikane humu ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Na. 195

### **Taratibu za kudhibiti na Kulinda Kazi za Wasanii**

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI K.n.y. MHE. MAGRETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kazi za Wasanii mbalimbali hapa nchini haziwainui kiuchumi wasanii husika kutokana na dhuluma za baadhi ya wasambazaji wa kazi za wasanii:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kudhibiti taratibu hizo ili kuwalinda wasanii wetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margreth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kazi za Wasanii mbalimbali hapa nchini bado haziwainui kiuchumi, tatizo hili linatokana na baadhi ya watu wasio waaminifu kukiuka hakimiliki za wasanii wetu.

Mheshimiwa Spika, zipo haki za aina mbili ambazo hulindwa na haki miliki ya kazi za Wasanii ambazo ni haki za kiuchumi na zile za Kimaadili (*Economic and Moral Rights*).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua tatizo hili tayari inayo sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya Tanzania ya mwaka 99 Na. 7 ya mwaka 1999. Hakimiliki ni ulinzi wa kisheria utolewao kwa muimbaji (*creator*) mtunzi au msanii wa kazi ya asilia.

Aidha sheria hii inasema kuwa hakimiliki ni haki pekee za kisheria za maandishi, kuchapisha, kuonyesha filamu au kurekodi kazi, maandishi, kazi za kisanii na muziki.

Mheshimiwa Spika, Hakishiriki ni Haki za wachezaji, waigizaji, watengeneza kanda za sauti na mashirika ya utangazaji zitokanazo na maonyesho/maigizo, utengenezaji wa kanda za sauti na urushaji hewani wa kazi za sanaa kama vile kwenye redio au *television* (kifungu cha 4 sheria Na. 7/99).

Mheshimiwa Spika, watu ambao hulindwa na Hakishiriki hujulikana kama viungo wa kufanikisha kazi za sanaa. uhusiano wa kati ya wenye Hakishiriki na Hakimiliki unatokana na ukweli kuwa wenye Hakishiriki husaidia katika hatua muhimu ili kuwezesha kazi za sanaa iweze kukamilika na kutangazwa kwa umma na hivyo kupata soko.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwanamuziki anaweza kufanya onyesho au akiimba wimbo ambao hakuutunga yeye, huyu atakuwa na Hakishiriki katika kazi hiyo.

Aidha, tumekuwa tukishuhudia mashirika ya utangazaji yakirusa hewani kazi za wasanii kama vile michezo ya kuigiza ambayo waigizaji si Watunzi wa Mchezo ule, bali ni watu ambao wana Hakishiriki katika kazi hiyo ambayo ni ya Kisanii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria hiyo ya Hakimiliki ya 1999 pia Serikali imeandaa kanuni za uzalishaji na usambazaji wa kazi mbalimbali za wasanii, kazi za muziki na filamu za mwaka 2006, tangazo la Serikali Na. 18 la tarehe 10 Oktoba, 2006.

           Kanuni hizi zimetengezwa chini ya kifungu cha 45 cha Sheria ya hakimiliki na hakishiriki Na. 7 ya mwaka 2006. Kwa mujibu wa Kanuni hizi mikanda na *CD* zote katika soko la Tanzania vitawekwa stika (*label*) zenye namba ziiwazo Haki-grams. Lengo ni kudhibiti ukiukaji wa Hakimiliki na hakishiriki.

Mheshimiwa Spika, Kanuni hizi mpya zinaipa nguvu *COSOTA (Copyright Society of Tanzania)*, polisi au maafisa forodha, kukamata kazi zote zisizo na stika na kuziharibu mbele ya umma baada ya siku 60.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi za wasanii ni ngumu sana na kazi hizo zinahitaji fedha na vile vile vifaa ili kufanikisha kuelimisha jamii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia msaada ama mikopo wasanii wa Tanzania ili kuendeleza vipaji vyao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Bakar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeye kabisa kwamba wasanii wana hali ngumu na wanahitaji vifaa. Lakini kama ujuavyo nchi yetu sasa hivi ina mikakati mingi ningewashauri wasanii katika vikundi ili watengeneze *SACCOS* na hizi *SACCOS* ndiyo zitawasaidia kuweza kutafuta mikopo katika mabenki. Lakini si hilo tu siku hizi kuna mfuko wa JK ambao unatoa fedha ni vizuri na wao pia wakajingiza huko ili waweze kupata fedha za kuwasaidia kuendeleza sanaa zao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wanawake leo wamechangamka kweli kweli. Kwa hiyo, nitawapa nafasi wawili Mheshimiwa Martha Mlata halafu Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri mimi napenda kumwuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *COSOTA* ndiyo chombo pekee ambacho kinaweza kusimamia haki za wasanii hawa. Lakini *COSOTA* hii inashindwa kufanyakazi zake kikamilifu kwa sababu haina fedha za kutosha. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba huu ni wakati muafaka sasa kuwasaidia wasanii kuwezesha *COSOTA* ili iweze kusimamia haki za wasanii? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kabisa kwamba *COSOTA (Copyright Society of Tanzania)* ndiyo wenye haki ya kudhibiti ukiukwaji wote wa masuala ya sanaa katika nchi yetu. Lakini si hivyo tu wao ndiyo wametoa mdhamana wa kuendeleza wasanii katika nchi yetu na wana hali ngumu nakubaliana naye. *COSOTA* wako chini ya Wizara ya Viwanda

na Biashara, Serikali tutajitahidi kuimarisha *COSOTA* ili iweze kusaidia wasanii wetu na kuiendeleza ili iweze kupata fedha za kutosha ili waweze kumudu kazi zao. (*Makofi*)

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa swali la msingi linahusu dhuluma wanayofanyiwa wasanii na kwa kuwa siku za karibuni kile kikundi maalum cha *Ze Comedy* wamezuiwa kuonyesha usanii wao hapa Tanzania na mmiliki wao wa *EATV*. Je, Wizara inasema nini kuhusu hilo kwa sababu wapenzi wengi wa kundi hilo kwa kweli wamekosa fursa muhimu ya kuangalia kundi hilo. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kuhusu *Ze Comedy*. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo kama ifuatavyo:-

Ni kweli liko tatizo kati ya *Ze Comedy* na *East African Television* pamoja na *TBC* suala hilo Serikali tunalifahamu. Tatizo hilo sisi kama Serikali tunaachia chombo chetu cha *COSOTA* tumewaambia wakae ili waweze kutafuta muafaka kwa sababu kama nilivyosema katika swali langu la msingi kuna kitu kinaitwa hakimiliki na kitu kinaitwa hakishiriki. *Ze Comedy* wana haki haki ya hakimiliki, *East African Television* wana haki ya hakishiriki kwa sababu wao ndiyo wanao-*produce*.

Sasa kuna mgongano hapo na ndiyo maana chombo chetu kinalifanyia kazi suala hili *COSOTA* ili mtafaruku huu uishe. Lakini napenda Bunge lako lifahamu kwamba *Ze Comedy* wameshamaliza mkataba wao na *East African Television* kihalali. Kwa hiyo, sasa hivi ni kwamba wanatafuta mtu mwingine wa kuweza kuwa-*promote* ndiyo wamekwenda *TBC*. Lakini nina imani baada ya muda mfupi suala hili litakwisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu mazuri kabisa. Swali linalofuata linauliza na Mheshimiwa Benson Mpesya wa Mbeya Mjini ambaye kwa jina maarufu ni Askofu. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 196

### Ahadi ya Umeme Itende

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kupeleka umeme wa njia tatu (*three phase*) eneo la Itende – Jijini Mbeya, tangu mwaka 2004.

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo?

(b) Je, ni sababu zipi zilizocheleweshwa utekelezaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Chuo cha Biblia cha Itende kuna *transfoma* ya njia moja (*single phase*) inayohudumia Chuo cha Biblia na wateja walio karibu na chuo. Ili kuboresha umeme wa eneo hilo inabidi mfumo wa umeme ubadilishwe kutoka *single phase* kwenda *three phase* kwa kujenga njia ya umeme wa msongo wa *KV 11* yenye urefu wa kilomita 1.8 kujenga njia ya kuzambaza umeme kwa wateja yenye urefu wa kilomita 1 pamoja na kuweka *transfoma* ya *KVA 50*. Gharama za kukamilisha kazi hizo ni shilingi milioni 87.92.

Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme wa Chuo cha Biblia cha Itende utatekezwa kwa kutumia fedha za *MCC*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpeya lenye sehemu 9a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kutimiza ahadi ya kupeleka umeme kwa njia tatu eneo la Itende katika muda wa mwezi mmoja baada ya kazi kuanza kutekelezwa mara tu fedha za *MCC* zitakapokuwa zimetolewa.
- (b) Mheshimiwa Spika, sababu zilizocheleweshwa utekelezaji wa mradi wa huo ni ukosefu wa fedha za kutekeleza mradi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya kutoka kwa Naibu Waziri na yanayotia faraja, nina swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ni takribani miaka 4 sasa eneo hili halijapatiwa umeme na kwa kuwa Serikali imeonyesha dhamira ya wazi katika bajeti yake ya mwaka huu kwamba eneo hili limeingizwa katika mpango wa kulipatia umeme, swali dogo la nyongeza kwa sababu kazi itatimizwa ndani ya mwezi mmoja je, ninaweza nikahakikishiwa ni mwezi upi huo kazi itaanza rasmi ili na wananchi wa Itende wasikie waliopata tabu karibu kwa miaka minne ni mwezi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Kama tunavyofahamu fedha za *MCC* zimekuja zote kwa pamoja, sasa tunasema hizi fedha zitakapopatikana na tukizifanyia *allocation* kwa hizi milioni 87.92 utekelezaji wake utakapoanza tunataraji kwamba kwa sababu siyo mradi mkubwa sana utatumia

muda wa mwezi mmoja baada ya ku- *re- lease* ya hizi *funds* mpaka kukamilika kwa hiyo *project*. Kwa nyongeza tu nataka nimwondolee kila aina ya wasiwasi Ndugu yangu Askofu Mpesya ni kwamba hapa nilipo leo tu asubuhi nimetoka kuzungumza na Engineer mmoja anaitwa Stella M. Hiza ambaye ni meneja wa Mkoa wa Mbeya na ambaye amenihakikishia kwamba utekelezaji huo utakamilika kwa wakati. (*Makofi*)

Na. 197

### **Hali ya Barabara ya Uhuru**

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH (K.n.y. MHE. MUSSA AZAN ZUNGU)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Uhuru ina historia ya Kitaifa na kwa sasa ipo chini ya Halmashauri ya Ilala, na kwa kuwa uwezo wa Manispaa ni mdogo na kwa kuwa barabara hiyo hutumika kwa ugeni wa kitaifa:-

Je, Serikali haioni sababu ya kuichukua na kuifanyia matengenezo na kuipunguzia msongamano na kuiweka katika sura ya kitaifa?

**WAZIRI WA MAENDELEO MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tunatambua umuhimu wa barabara ya uhuru ambayo inahudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Barabara hii imekuwa ikitumika kwa shughuli za kupitisha viongozi wa Kimataifa tangu tulipopata uhuru. Nakiri kuwa kwa sasa babara hii inahitaji kukarabatiwa na ikiwezekana ipanuliwe.

Mheshimiwa Spika, barabara kuwa chini ya mamlaka ya Halmashauri siyo kigezo cha kutopewa fedha za matengenezo au fedha za ujenzi. Mamlaka zote zinapewa fedha za ujenzi na matengenezo kutokana na mipango iliyokubaliwa kati ya mamlaka husika na Serikali. Halmashauri hasa za Jiji la Dar es Salaam hivi sasa zinajitahidi kujipanga vizuri, kinachotakiwa ni kuziwezesha kitaalam na kifedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itashauriana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ili watenge fedha za kutosha kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Ilala katika migao yao kutoka Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) iliyoongezeka ili waweze kuipa kipaumbele barabara ya Uhuru ifanyiwe matengenezo ya uhakika na pale uwezo wa Serikali utakaporuhusu, basi ipanuliwe na kuwa njia nne.

**SPIKA:** Samahani nitakuja kwako Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani lakini tuanze na aliyeuliza swali la msingi.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa sasa hivi Serikali inataka kufanya mashauriano Manispaa ya Ilala lakini na kwa kuwa barabara hiyo kwa hivi sasa ni mbaya sana hasa katika maeneo ya Shule ya Uhuru na maeneo ya Bungoni kuelekea Buruguruni hasa pale kwa Buguruni Malapa. Je, wakati tunasubiri mpango huo na ushauriano huo kwa nini sasa hivi Serikali isiamue kukarabati maeneo yale ambayo sasa hivi yanasababisha msongamo mkubwa sana wa magari na kuleta adha hasa kwa magari ya wagonjwa yanayotoka katika Hospitali ya Amana kuelekea katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili.

(b) Serikali kwa nini haioni umuhimu kwa hivi sasa kujiandaa na kuweza kuitanua barabara hiyo ili iwe njia nne na kurahisisha wapitao na kuunganisha kutoka *keep left* cha Msimbazi kwenda Buruguruni kwa Malapa kuungana na barabara ile inayotokea Buruguruni pale kwa Rozana?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abdulkarim Shah kama ifuatavyo:-

Moja ukarabati wa dharura kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba Serikali itafanya mashauriano na Halmashauri husika ili katika mgao wa fedha ambao umetengewa katika mwaka huu wa 2008/2009 waweze kutenga fedha nyingi zaidi kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii. Tutajitahidi kufanya hivyo ili kwa dharura na kwa haraka barabara hiyo ifanyiwe matengenezo.

Kwa swali dogo la pili, pia kama nilivyojibu katika swali la msingi Serikali ina nia ya kuhakikisha kwamba barabara hii inafanyiwa matengenezo ya uhakika na ikiwezekana kuipanua. Hii barabara ilishawahi kuombewa kupandishwa daraja kuwa barabara ya Wilaya chini ya Halmashauri ya Manispaa kuwa barabara ya Mkoa ili iweze kuhudumiwa na *TANROADS*. Kinachosubiriwa hivi sasa Serikali iko katika harakati za kukamilisha Kanuni ya sheria mpya Namba 13 ya mwaka 2007 ambayo itatoa vigezo vya kupandisha daraja. Tunatarajia kwamba baada ya kukamilisha Kanuni basi tutaifikiria barabara hii ili iweze kuhudumiwa na *TANROADS*.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la fedha kwa ajili ya miradi ya miundombinu limekuwa ni tatizo sugu na kwa kuwa Serikali imepata watu mbalimbali ambao wanahitaji kuingia ubia na Serikali kwa ajili ya kuendeleza miundombinu. Lakini Serikali yenyewe imekuwa nzito katika kutatua matatizo haya. Je, kwa nini Serikali inalimbikiza matatizo haya ambayo tayari ufumbuzi umepatikana lakini hawataki kutekeleza kwa mfano zile kampuni iliyotoka Australia ambao walikuwa tayari kuwekeza bilioni tatu kwa ajili ya miundombinu. Lakini Serikali ikataka kipindi cha miaka miwili lakini mpaka leo haijatoa maamuzi. Ni kwa nini wanandekiza mambo kama hayo ambayo ufumbuzi upo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kama ifuatavyo:-

Serikali ina nia sana na thabiti kabisa kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya nchi hii na hasa miundombinu ya barabara. Tuko katika taratibu za

kukamilisha sera ya ushirikishwaji wa sekta binafsi. Hii sera itatoa mwongozo na namna ambavyo tutaweza kulitekeleza jambo hili kwa ukamilifu na katika taratibu za kisheria mara tutakapokuwa tumekamilisha taratibu hizo bila shaka tutawakaribisha siyo hawa wa Australia bali Marekani, Ulaya nchi zingine zote na hata sekta binafsi ndani ya nchi yetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Naomba nijisahihishe kwa kusema kwa kutambua kwamba nilimwona Mheshimiwa Rita Mlaki swali la nyongeza la mwisho. (*Makofi*)

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona kuuliza swali la kwanza, tangu nimeondoka katika nafasi yangu ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali langu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam lina msongamano mkubwa sana wa watu na biashara nyingi ambazo zinachangia katika uchumi wa nchi yetu. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuanzisha mfuko maalum kwa Jiji la Dar es Salaam tu ambao utasaidia katika ukarabati wa barabara za Jiji la Dar es Salaam? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rita Mlaki kama ifuatavyo:-

Ushauri huo tumeupokea na tutaufanyia kazi kama vile ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli hapa Bungeni kwamba suala la Jiji la Dar es Salaam ni suala zito, ni suala la kitaifa halitatosha tu kuachiwa mamlaka za Halmashauri hizi tatu bila Serikali Kuu kuliingia na kuliwekea mkakati maalum. Tunapata changamoto kutoka mwendelezo wa Jiji la Nairobi kama ambavyo Serikali ya Kenya imeufanya hivi karibuni na tutachukua mafunzo hayo na ushauri huu wa Mheshimiwa Mbunge kuufanyia kazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa sasa ni zamu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Swali linalofuata ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o ambaye yuko safarini amepangiwa kuuliza Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge.

Na. 198

### **Umuhimu wa Wataalam wa Kilimo kwenye kila Kijiji**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE (K.n.y. MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inakiri kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu; na kwa sababu hiyo imeona umuhimu wa kuwa na wataalam wa kilimo kila kijiji kwa kutumia wataalam kutoka kwenye vyuo vya kilimo vya Nyegezi, Uyole, Ukiriguru ambao wana Cheti au Stashahada:-



(a)Je, ni kwa nini vyuo hivyo pamoja na kutoa vyeti na Stashahada, haviruhusiwi kutoa pia Stashahada za juu kama ilivyo kwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru na Kivukoni hasa ikizingatiwa kuwa Chuo Kikuu cha Kilimo kiko kimoja tu nchini?

(b)Je, Serikali haioni kwamba kuwapa fursa finyu wataalam wa kilimo kujiendeleza kunasababisha wabadilishe fani zao?

(c)Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuviongezea vyuo hivyo uwezo wa kutoa Stashahada za juu na Digrii ili kuwawezesha walimu wa kilimo kujiendeleza badala ya kutegemea chuo kimoja tu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ledian Mafuru Mng'ongo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Madhumuni ya kuanzishwa vyuo vya kilimo tangu awali miaka ya 1939, ilikuwa kutayarisha Maofisa Ugani wa kati wenye uwezo wa kuwaelimisha wakulima kuhusu Kanuni za Kilimo Bora.

Kwa hiyo, elimu ya kilimo ambayo imekuwa ikitolewa ni ile ya ngazi ya astashahada (Cheti) na Stashahada (*Diploma*) ambayo ndiyo inastahili kwa wataalam wa ugani Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, endapo vyuo hivi vitapandishwa hadhi na kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu pamoja na shahada havitaweza tena kutoa wataalam wanaohitajika vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2006 vyuo vyote vya kilimo vilisajiliwa *NACTE (National Council for Technical Education)* na hivyo kukidhi masharti ya sheria iliunda *NACTE* No. 9 ya mwaka 1997 ambayo imeipa *NACTE* uwezo wa kisheria kusimamia na kudhibiti ubora wa mafunzo yatolewayo na vyuo vyote nchini vinavyopokea vijana waliomaliza kidato cha nne na cha sita kwa mafunzo ambayo siyo ya Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya vyuo vyote vya kilimo kusajiliwa na *NACTE*, milango imefunguliwa kwa wanafunzi, watumishi kujiendeleza hadi kupata shahada za ufundi wa kilimo kupitia vyuo vya kilimo (*Technical Agricultural Degrees*).

Mafunzo ya kilimo yatolewayo sasa yameandaliwa kwa kuzingatia ngazi za uwezo wa kujiendeleza kimafunzo *National Technical Awards (NTA)* kama ifuatavyo:-

- *NTA level 4* na *5* ni ngazi ya Astashahada (Cheti)
- *NTA level 5* na *6* ni ngazi ya Stashahada (*Diploma*)
- *NTA level 7* shahada ya kwanza (*BSc.*)
- *NTA level 8* shahada ya Uzamili (*MSc.*)
- *NTA level 9* shahada ya Falsafa (*Ph.D.*) – Uzamilifu.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu walimu wa vyuo vya kilimo wanayo fursa kubwa ya kujiendeleza kadri ya uwezo wao kumudu masomo katika *National Technical Awards* husika.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, mafanikio makubwa katika Sekta ya Kilimo ni pamoja na kuwa na wataalam katika ngazi zote za kilimo kama kwenye Wilaya, Kata mpaka Vijijini; na kwa kuwa Serikali kupitia Bunge lako Tukufu mwaka jana iliahidi kuajiri wataalam 2500 wenye *Degree* ili waende kwenye vijiji wafanye kazi za utaalim wa kilimo. Ni kiwango kipi cha mkakati huo kimetekelezwa kwa mwaka 2007/2008?

(b) Kama kuna idadi ya wataalam ambao walijajiriwa, Wizara itakuwa tayari baadaye kutuonyesha mgawanyo wa hao wataalam ambao wameajiriwa katika Halmashauri zetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali ina programu ya kuelimisha na kuajiri wataalam wa ugani ili kufikia mwaka 2011 tuwe tumekwishapata wataalam wa ugani 15,000. Kwa sababu mwaka jana wakati tunaleta programu hii tulikuwa na wataalam wa ugani 3,479 waliopo kwenye ngazi za Vijiji, Kata mpaka kwenye Wilaya. Kwa kiwango ambacho tumekwishajiri mwaka huu nitaweza kutoa hizo takwimu hapo baadaye kwa kila Wilaya. Lakini sasa hivi tuna wanafunzi zaidi 2,000 ambao wanasoma kwenye vyuo vyetu vya kilimo nchini kwa *level* ya *Diploma*. Ila mwaka huu tunategemea kuongeza wanafunzi wale waliomaliza *form four* badala ya wale waliomaliza *form six* kwa sababu wanakuwa ni wachache, mwaka huu tutachukua wale wa *form four* pia ili waweze kuchukua *certificate* katika vyuo hivyo ili tuweze kuongeza ile *speed* ya kuongeza wataalam wa ugani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Godfrey Zambi, kwa swali la mwisho la nyongeza kwenye swali hili.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, hata tukiweza kuwapeleka wataalam hao vijijini na huko kwenye Kata bado tatizo linabaki kuwa makazi kwa ajili ya wataalam hao kuishi pamoja na vyombo vya usafiri. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza ni lini wataalam hao wakienda wanaweza wakapatiwa vyombo vya

usafiri pamoja na makazi ya kuishi ili waweze kufanya kazi zao sawa sawa kwa sababu maeneo hayo pia ni makubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba moja ya motisha ya wataalam wetu hao ili tuweze kuwa-retain kule kwenye vijiji na Kata ni kuwapatia makazi. Katika programu ile pia fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea nyumba, na fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwapatia pikipiki kwa wale wataalam wa ugani wa Tarafa na Kata na pia fedha zimetengwa kwa ajili ya kuwapatia baiskeli kwa wataalam wa vijijini.

Na. 199

**Kuzuia Wananchi Kutokutumia Pori  
Kwa Shughuli za Urinaji wa Asali**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi ya wanyamapori ya Moyowosi/Kigosi, wananchi wa vijiji vinavyopakana na pori hilo walikuwa wakifanya shughuli za urinaji asali; kwa kuwa, mara tu baada ya kuanzishwa kwa hifadhi hiyo wananchi hao walikataliwa kuendelea na shughuli hiyo:-

(a)Je, nini tamko la Serikali kuhusiana na wananchi hawa ambao waliwekeza kwenye pori hili kabla ya hifadhi?

(b)Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia wananchi ambao wameharibiwa mizinga yao na askari wa wanyamapori?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Moyowosi lilipandishwa hadhi kutoka Pori Tengefu na kuwa Pori la Akiba mwaka 198. Pori hilo lenye eneo la kilomita za mraba 6,000 liko katika Wilaya ya Kibondo, Mkoani Kigoma. Kabla ya kupandishwa hadhi, wananchi walikuwa wakilitumia Pori hilo kwa shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na urinaji wa asali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya ushirikishaji mwishoni mwa miaka ya 1980, Wizara yangu ilitoa mwongozo wa wafugaji nyuki kujiunga kwenye ushirika na iliweka utaratibu wa kuruhusu wananchi kuingia na kurina asali kwenye pori hilo kwa vibali maalum. Aidha, wananchi hao hupewa ulinzi na askari wa wanyamapori dhidi ya wanyama wakali wakati wa kurina asali zao. Utaratibu huo unaendelea hadi hivi leo. Katika kipindi cha miaka mitatu (2005, 2006 na 2007) jumla ya wananchi, 2,221 walipewa kibali cha kuingia ndani ya Pori la Akiba la Moyowosi

kwa ajili ya kurina asali. Wizara yangu haijapokea taarifa zozote za wafugaji wa nyuki walioharibiwa mizinga yao katika Pori hilo la Akiba.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa. Lakini bado wananchi wa vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo wameendelea kuwa na jitihada za kuendeleza Maendeleo yao na hasa Maendeleo yanayotokana na kilimo ikiwa ni pamoja na urinaji wa asali. Lakini wananchi hao wamekuwa ni wafuataji wa taratibu za Serikali zilizowekwa kwa maana ya kutokuvunja sheria za Serikali kwa kutokuingia katika hifadhi. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kurudisha mpaka wa Hifadhi nyuma ili wananchi hao waweze kupata maeneo ya kujiendeleza kwa kilimo kwa sababu *population* ya wananchi katika vijiji hivyo inaongeza siku hadi siku?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kubadilisha mipaka ya Hifadhi umeainishwa kwenye Sheria ya Hifadhi za Wanyamapori upo bayana na unahitaji maandalizi maalum. Kwa hiyo, nilikuwa naomba niseme kwamba si muafaka kubadilisha utaratibu huo au sheria iliyotungwa hapa Bungeni kwa kutoa tamko tu kirahisi namna hiyo. Ninamwomba Mheshimiwa Felix Kijiko kwamba Serikali ipo tayari kuangalia namna gani tunaweza tukatafuta jibu la pamoja la kutatua matatizo yanayowakabili wananchi lakini kwa kufuata misingi ya sheria iliyopo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza, nilikuona Mheshimiwa Said Nkumba. Eneo lingine lenye asali nyingi.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi kwa mfano maeneo ya Tabora kule hifadhi ya Ugala, ambayo inahusisha Wilaya ya Sikonge na Urambo.

Kwa kweli wanapaswa kufaidika na shughuli mbalimbali za uendeshaji zinazofanyika karibu na maeneo yao. Na kwa kuwa wawindaji wengine wamekuwa wakorofi hawataki kuchangia shughuli za Maendeleo katika maeneo mbalimbali yanayozunguka hifadhi.

Je, Sheria inasema nini kuhusu kuwashughulikia hawa wawindishaji wakorofi na kama wanashindwa watuachie sisi tushughulike nao? (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, utaratibu uliowekwa kwa miongozo mbalimbali ya Wizara ni kwamba huwa zinatolewa asilimia 25 ya mapato yanayotokana na uwindaji yanakwenda kwenye Halmashauri kufanya miradi mbalimbali.

Kinachohitajika zaidi ya hapo kinatoka katika misingi ya *co-operate social responsibility* ambayo ni mahusiano kati ya mwindaji mwenyewe na wananchi jirani. Sheria haimtaki au haimlazimishi kwamba afanye kitu chochote zaidi ya kufuata utaratibu ambao upo na tunapeleka asilimia 25.

Kwa hivyo nilifikiri kwamba kama kuna matatizo ya kipekee kuhusu mwindaji fulani tuiangalie kwa utaratibu huo. Lakini uchangiaji wao unafuatana na mapato ambayo tunayatoa kutoka na lile gawio la asilimia 25. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda kuuliza maswali umekaribia kufika mwisho. Nadhani tuyamalize kwa ufanisi tu maswali haya ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Linaloanza ni la Mheshimiwa Mwambalasa ambalo nimearifiwa litaulizwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe.

Na. 200

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka ulioishia Juni, 2007 inaonyesha kuwa zipo Idara na Taasisi nyingi za Serikali zinazokiuka sheria ya manunuzi Na. 21 ya mwaka 2004 kwa kutokuwa na *Procurement Management Units* kutokuwa na Bodi za tenda na kutokuwa na wataalam wa ununuzi na kadhalika:-

(a) Je, ni Idara na Taasisi ngapi zinazokiuka sheria hiyo kwa kutotimiza hayo yaliyoainishwa kwenye maelezo ya swali hili?

(b) Je, Serikali inachukua hatua zipi dhidi ya uvunjifu wa sheria hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Jimbo la Lupa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma mnamo mwaka wa fedha 2006/2007 na katika kipindi cha kuanzia Julai 20 07 hadi Machi 2008, ilifanya tafiti katika taasisi za Umma 179 zinazojishughulisha na ununuzi. Utafiti huo umeonyesha kwamba taasisi 116 kati ya 179 zina vitengo vya ununuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna taasisi za umma 345, ni dhahiri kwamba takwimu za utafiti huo zinaashiria kuwa kuna taasisi nyingi za umma zinakiuka sheria ya manunuzi kwa kutokuwa na kitengo cha ununuzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo lililopo, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma, imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuzijulisha kwa barua taasisi zote za umma ambazo zimebainika kuvunja sheria na kuzitaka kuwa na kitengo cha ununuzi haraka iwezekanavyo;

(ii) Kutoa mafunzo juu ya usimamizi na utekelezaji wa sheria ya ununuzi ya mwaka 2004 pamoja na matumizi ya nyaraka mbalimbali za zabuni;

(iii) Kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa waliobainika kukiuka sheria ya manunuzi; na

(iv) Kusitisha mchakato wa zabuni kama imeonekana kukiukwa Sheria ya Manunuzi.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa uzoefu umeonyesha kuwa ukiukwaji wa sheria hii ya manunuzi mara nyingi unasukumwa na dhamira za kijinai. Kwa nini basi hatua zinazochukuliwa na Serikali dhidi ya Taasisi za umma zinazokiuka sheria hii ya manunuzi ni za kubembelezana zaidi kuliko kuwajibisha? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 ina mianya mingi bayana inayopelekea uvunjifu wa sheria hii ya manunuzi kwa urahisi sana. Je, ni lini Serikali italeti Muswada wa kuidusuru sheria hiyo Bungeni hapa ili kuziba mianya hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza jana kwamba sheria hii ya manunuzi ina mapungufu na tunatarajia katika Bunge lijalo tulate hapa marekebisho.

Marekebisho hayo yatasaidia vile vile kuondosha ile dhana mzima ya kubembelezana na hatimaye kuchukua sheria za kinidhamu kulingana na kosa ambalo litakalofanywa na taasisi au na mtu yoyote yule ambaye anahusika na manunuzi. *(Makofi)*

**Mapato yatokanayo na Ongezeko la bei ya Mafuta**

**MHE. ALI JUMA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipandisha bei ya mafuta kwa kiwango cha Shs.100/= kwa lita moja kuanzia kipindi cha Bajeti *Cah* 2007/2008 na hatimaye Bunge kuridhia ongezeko hilo kwa lengo ya kupata fedha za kujengea barabara ili kuwarahisishia wananchi usafiri na usafirishaji.

- (a) Je, tangu kuanza kwa zoezi hilo hadi sasa Serikali imekusanya shilingi ngapi?
- (b) Kwa vile lengo la zoezi ni kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Je, ni kilomita ngapi zimejengwa kwa msaada wa Mfuko huo, na zimejengwa wapi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mbunge wa Jimbo la Chaani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2008 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 202 bilioni kutokana na chanzo hiki cha mapato, ambapo ongezeko la shilingi 100 kwa lita peke yake ilichangia shilingi 101 bilioni.
- (b) Mheshimiwa Spika, Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Barabara inaeleza wazi kuwa fedha zitakazopatikana zitatumika kwa mambo yanayohusiana na barabara, mambo hayo ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Ukarabati na ujenzi wa barabara;
- (ii) Kulipia fidia za mali zinazoathiriwa kutokana na ujenzi wa barabara; na
- (iii) Kusaidia kulipia madeni pale ambapo kuna upungufu wa fedha za miradi ya ujenzi wa barabara inayotekelezwa na Serikali Kuu kwa asilimia 100.

Kwa kuwa barabara zilizofaidika na fedha za Mfuko wa Barabara ni nyingi na ziko katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, haitakuwa rahisi kuzitaja lakini nitampatia Mheshimiwa Mbunge orodha ya barabara hizo, hii hapa. (*Makofi*)

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba kumwuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali ina vyanzo vingi sana vya mapato na kwa kuwa mapato ya Serikali yamekuwa yakiongezeka kupitia vyanzo hivyo mbalimbali. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa ama kupunguza au kufuta kabisa kodi hii ya mafuta ili kuwasaidia wananchi kwa sababu ya kupanda kwa bei hii ya mafuta? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, tozo hili ni shilingi 200 kwa lita moja. Kuondoa shilingi 200 au kupunguza kwa kiasi kikubwa sana hatutamsaidia sana mwananchi wetu kwa sababu bei ya mafuta kila kukicha inapanda duniani. Lakini Serikali inaliangalia tatizo hili kwa upana wake. Nataka nieleze tu tunaliangaliaje. Kwanza tunaliangalia katika muda mfupi kwa maana kwamba ile sheria ambayo tumeipitisha Bunge lililopita la kununua mafuta kwa wingi *bulk procurement* itaweza kusaidia sana ku-*stabilize* hii bei ya mafuta.

Lakini vile vile Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi mkakati wa kuwa na *bio fuel* kwa maana kwamba mazao haya ya jetrofa, mazao ya miwa ambayo yatazalisha mafuta, utaweza kutusaidia sana kuzalisha mafuta hapa ndani, na kuweza kuweka bei yetu wenyewe ya ndani ambayo hatimaye tutaweza kumsaidia vile vile mwananchi wetu wa kawaida. Lakini vile vile mkakati wa muda mrefu ni suala hili ambalo tunalizungumzia la gesi kuigeuza kuwa ni *liquid* nalo vile vile Serikali inaliangalia. Haya yote matatu tukiyaangalia kwa upama wake tuna imani kubwa sana tutaweza kumsaidia mwananchi wetu katika suala la mafuta kuliko hata tutakiondoa. Tukiondoa shilingi 200 itakuwa ni ya muda mfupi tu wakati bei ya mafuta inaendelea kupanda. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Matangazo, kama kawaida tutaanza na wageni. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wote wa Mkoa wa Rukwa wana wageni kutoka Manispaa ya Sumbawanga ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri hiyo ya Manispaa wakiongozwa na Mstahiki Meya, Frank Mrema, pamoja na Wataalam Watendaji Manispaa ya Sumbawanga. Ningeomba Waheshimiwa pale mlipo msimame. Alaah! Ni huku. Ahsanteni sana, ahsante. Karibuni sana, karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Mwaghembe, anao wageni wake ambao ni *Maj. General Kisamba* na Kanali Kakili, wote ni Viongozi wa Jeshi. Mmoja *General* yeye ni Mkuu wa Jeshi la Nchi Kavu na Kanali ni *Base Commander* wa hapa Dodoma. Tafadhali, ooh ndiyo wale wawili pale. Ahsanteni sana, ahsanteni. Ahsanteni wapiganaji, tunafurahi sana mnapokuja kuangalia shughuli za Bunge. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ana mgeni wake ambaye anaitwa Agnes Sagara kutoka Musoma. Bi. Agnes, aah yule pale. Ahsante sana.



Mheshimiwa Bujiku Sakila ana wageni wake ambao ni wanae, Ndugu Robert Siyanteni na Ndugu Edward Mbulu wale pale. Ahsante sana. Karibuni sana. Tunawatakia mema katika mafunzo yenu. *(Makofi)*

Wako wageni wa Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, ambao ni uongozi wa Chama cha Mapinduzi, wakifuatana na Katibu wa CCM Tawi la Uzi. Ni Uzi au Uzini. Basi kama Uzi haya. Ndugu Juma Zubeir pamoja na Katibu wa CCM Tawi la Mwanakwerekwe Ndugu Mayasa Kiloko. Naomba wasimame tafadhali. Wale pale. Aaa karibuni sana, karibuni sana. Tunashukuru kuwakaribisha Ndugu zetu kutoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, anao wageni wake ambao ni Uongozi wa CCM jimbo la Magogoni, wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Tawi la Magogoni, Ndugu Riziki Ramadhani Kibwelu. Pia yupo Ndugu Kilefu Khamis Said. Naomba wasimame, wale pale. Karibuni sana, karibuni sana Ndugu zetu kutoka upande wa pili, Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Janeth Kahama, ni Bi. Sauda Mpambalyoto, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Moshi Vijijini. Yule pale, yule pale. Ahsante sana, karibu sana, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma. Ni Mzee Msuha, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Ruvuma. Ah yule pale, karibu sana Mwenyekiti. Tunashukuru sana. Ninaona upande wa kushoto kuna vijana wa shule ambao hawakuorodheshwa hapa. Sasa sijui ni mwendelezo wa vijana wa shule ipi. Lakini ningeomba wao na walimu pia wasimame ili waweze kutambuliwa. Wale pale, wamo katika sare. Ahsante sana. Karibuni sana na tunawatakiwa, sisi Wabunge tunawatakia kheri katika masomo yenu. Mshike masomo, msiingie katika ngono zembe. Eeeh! Msome, tunahitaji wataalam na tunataka muishi maisha mazuri. Ahsante sana na walimu ahsante kwa kuwaleta. Upande wa kulia kwangu, kuna wanakijiji kutoka katika kijiji cha Mpunguzi. Aha ni wanafunzi, alaa ni wanafunzi kutoka Mpunguzi. Naomba msimame. Ahsanteni sana na nyinyi pia rai yangu ni hiyo hiyo. Nadhani mlisikia jana jinsi Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyokuwa anaulizwa kuhusu mimba za kabla ya wakati wake. Kwa kweli inakera sana Taifa letu.

Basi matangazo mengine yanayohusu shughuli za kazi zetu. Mheshimiwa Ndugu Abdulkarim Shah, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Anaomba kutangaza kwamba kutakuwa na Semina ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka, Jumapili tarehe 13, Jumapili ijayo. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili jengo la Utawala saa 5 asubuhi. Saa 5 asubuhi siku ya Jumapili tarehe 13 Julai, Semina kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Semina muhimu na ndiyo semina yenu ya kwanza tangu Kamati kuundwa upya. Waheshimiwa Wajumbe wote semina hii muhimu ya kuelekeza shughuli zenu. Tafadhali msikose Jumapili saa 5 asubuhi. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kukutana leo saa 5 asubuhi katika Ukumbi Na. 231. Saa 5 asubuhi leo ukumbi Na. 231, Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mwisho, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Ameniomba nitangaze kwamba leo saa 5 asubuhi Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kikao ni muhimu sana. Kwa hiyo, nadhani itakuwa pia ni kukutana na wageni wetu kutoka Nigeria.

Kwa hiyo, Wajumbe wote wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama saa 5 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Hayo ndiyo matangazo ya leo. Namwita sasa Katibu kwa shughuli inayofuata.

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 Wizara ya Maliasili na Utalii**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ina wachangiaji 11 ambao wamekwishachangia mara moja na wawili ambao wamechangia mara mbili tu. Shughuli za uchangiaji tutazimaliza saa saba leo mchana.

Kwa hiyo, inawezekana hawa 11 wakaweza kupata nafasi. Ngoja nisome majina yao ili wajiandae. Nitaanza na Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, atafuatiwa na Mheshimiwa Clemence Beatuce Lyamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Abllah Mikidadi, halafu Mheshimiwa Benito William Malangalila,

Waheshimiwa Wabunge, wengine watakaofuata ni Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Thomas Apson Mwang'onda na Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw'.

Kwa hiyo, huo ndiyo mtiririko wa wachangiaji kwa leo. Sasa nitaanza basi na Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo wakati huo huo atafuatiwa na Mheshimiwa Lyamba. Pia ajiandae mchangiaji wa tatu Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ambayo iko kamilifu na inaeleweka. Vile vile nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kushirikiana naye vizuri pamoja na Katibu Mkuu, Mama Blandina Nyoni, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kabla ya yote napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono mia kwa mia pia ningetoa pole sana kwa ajali ya ndege iliyotokea hivi karibuni ambayo imesababisha vifo ya wapendwa watumishi wa Idara ya Wanyamapori. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kujenga nyumba kwa ajili ya Watumishi wa Selou katika Wilaya ya Liwale. Nyumba hizo zimeongeza mvuto wa Wilaya ya Liwale. Nawashukuru kipekee kwa vile waliamua kujenga nyumba hizo Liwale Mjini.

Miongoni mwa nyumba hizo ipo *rest house* ambayo ni mzuri sana. Inatumika kwa wageni wengi wa kitaifa. Ninawashukuru sana, sana, sana kwa kutujalia kwa kipande hicho. Lakini pamoja na hayo, ninaishauri Wizara husika waendeleo kuboresha nyumba hizo na kuzitunza vizuri ili ziendeleo kuwa nzuri na tuweze kuzitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Liwale ina eneo lipatalo *square kilometer 38,000*. Kati ya hizo asilimia 53 ya eneo hilo ni mbuga za wanyamapori. Lakini inashangaza katika kitabu hiki leo hii sikuona mradi wowote ambao umezungumziwa kwa ajili ya Liwale. Sielewi ni kwa sababu gani?

Je, ni katika miradi gani ambayo ipo Liwale hakuna hata mradi mmoja ambao ni endelevu ambao tungeweza kuufahamu katika bajeti hii? Si hivyo tu, inashangaza pia kwa kuwa mwaka jana kipindi kama hiki wakati nachangia baadaye niliahidiwa kwamba Liwale watakarabati Boma lililoko pale Liwale ambalo ni la zamani.

Kazi hiyo ilitakiwa ifanywe na *GTZ* lakini kwa bahati mbaya *GTZ* haiko tena na Wizara ilichukua jukumu la kufanya ukarabati huo, mpaka hivi leo hakuna kitu ambacho kimefanyika. Kwa nini? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, na sivyo hivyo tu. Kuna mambo ambayo yalielezwa katika bajeti iliyopita. Mojawapo ikiwepo pia ujenzi au kufufua barabara inayotoka Ulanga kwa Mheshimiwa Kombani kuja Liwale kupitia Kijiji cha Ndapata.

Kazi hiyo mpaka leo haijaanza. Ningetaka kupata maelezo kulikoni? Ambapo katika bajeti ile mulieleza kabisa kwamba mtashirikiana na Miundombinu ili kuifufua tena barabara ile ili wananchi wa pande zote mbili waweze kutembeleana. Sijapata taarifa yoyote tangu wakati huo mpaka hivi leo. Hakuna kinachoendelea. Naomba Serikali pale inapoahidi kufanya jambo kweli ifanye.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zetu ambazo ziko kwenye Selou hupata asilimia 25. Kiwango hiki cha asilimia 25 kusema kweli kwa sasa kimepitwa na wakati. Nakumbuka bajeti iliyopita Mheshimiwa Laizer aliomba kiongezwe na mimi pia naomba kiongezwe iwe kati ya asilimia 30 na 35 ili tuweze kutumia vizuri kwa maendeleo ya Wilaya zetu.

Hata hivyo, fedha hizi ambazo tunakiwa kupewa katika Halmashauri zetu kwa bahati mbaya zinatolewa kama hisani badala ya kuwa ni wajibu wao kutupatia. Kwa hiyo inahitaji ufuatiliaji wa karaha kabisa mpaka kuja kupata pesa hizi. Sielewi ni kutokana na nini? Naomba utaratibu uboreshwe ili iwe *automatic* kupata hizo pesa wakati muafaka.

Hali ilivyo sasa hivi hatuna uhakika. Kwa mfano 2003/2004 hatujapata pesa katika Wilaya ya Liwale ambazo zinatokana na uwindaji wa asilimia 25. 2006/2007 pia hatujapata. Mwaka 2005/2006 tulipata shilingi 43 milioni. Mwaka 2007/2008 tumepata mwezi Juni milioni 16. Sasa inashangaza kiasi hiki cha pesa, kwa nini kina-*fluctuate* namna hiyo.

Kwa nini tupate mwishoni mwa mwaka kabisa Juni. Nadhani utaratibu uangaliwe upya. Vingenevyo itakuwa hamtusaidii sisi ambao tunaishi na wanyamapori na pia hamtaweza kusaidia maendeleo ya wananchi. Naomba hilo Serikali itilie maani ili tuone marekebisho yake yanakuwa vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na si hivyo tu kwa kawaida hawa wawindaji hulipa au hugharamia ada na ushuru unaotakiwa kabla hata hawajawinda, *whether* wanyama wamepata au hawajapata. Kwa hiyo inaeleweka kabisa kiasi gani kinaweza kupatikana.

Kama hivyo ndivyo basi kwa nini sisi kama tulioko katika Halmashauri au Halmashauri zetu zisipewe *data* hiyo ili tuweze kuweka katika bajeti *system* yetu ya kujua kwamba matarajio yetu au makisio yetu katika Halmashauri kutokana na uwindaji ni kiasi fulani.

Naomba hali hiyo irekebishwe ili tuweze kwenda kisayansi katika mpangilio wa maendeleo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi ya Liwale, wiki iliyopita niliuliza swali la kuomba ilegezwe taratibu za kuajiri ma-*Game Scout*. Lakini kwa bahati mbaya au jibu la Serikali ni kusema kwamba hawawezi kulegeza na kwamba anayetakiwa kwenda kuua mnyamapori, au kufukuza ni yule aliyepata shahada. Jamani Serikali tuko wapi sasa. Mimi sioni umuhimu wa kumpata mtu wa shahada kwenda kufukuza tembo porini. Kwa kuwa kwa vyo vyote vile huyu akipatikana atakachoweza kufanya ni kukaa Ofisini. (*Makofi*)

Hawa wanyamapori, sisi tumeishi nao, babu zetu wameishi nao na walikuwa wanaweza kufanya mbinu mbalimbali za kuweza kuwafukuza. Leo hii mbinu mnayotupa kwamba tutumie pilipili, kwa nini? Wakati *Game Scout* tunaweza kuwapata, kama *game scout* hatuwezi kuwapata wa *qualifications* hizi zinazohitajika tunao wana mgambo ambao kusema kweli wanaweza wakafundishwa vizuri sana na Idara husika ili tuweze kuwatumia katika maeneo yetu ambayo wanyamapori ni tishio kubwa kwetu sisi wenyewe na maisha yetu pia kwa mazao ya wananchi. Inaelekea Wizara hii ina Idara ya Wanyamapori, hii Idara ya Wanyamapori, kusema kweli inaangalia tu upande wa wanyamapori haiangalii upande wa wananchi wapiga kura. Hili nalo ni tatizo. (*Makofi*)

Mimi niko hapa kuwatetea wananchi wa Liwale. Siko hapa kuwatetea wanyamapori. Utaratibu uliopo sasa hivi inaonekana kama Idara ya Wanyamapori siyo Idara ya Wanyamapori bali ni Idara ya Usalama wa Wanyamapori. Kwa kuwa kila kitu kinachozungumzwa, kinazungumzwa *research* iliyofanyika, wanyamapori wanaumwa. Wana magonjwa. Lakini hakuna takwimu yoyote iliyotolewa katika kitabu hiki cha kuelezea kwamba mashamba kadhaa ya wananchi yanaathirika kutokana na wanyamapori. Wananchi kadhaa wamejeruhiwa kutokana na wanyamapori, wananchi kadhaa wamepoteza maisha yao kutokana na wanyamapori. Sasa tunakwenda wapi? Ila tu mtuambia tembo anaumwa. Au ndovu anaumwa. Sasa hiyo ni nini, tumefikia mahali ambapo tujaribu kuwa na mabadiliko ya aina fulani. (*Makofi*)

Nadhani Wizara au Serikali inatumia ramani iliyopitwa na wakati katika kugawa vitalu. Kwa kuwa ukija Liwale, kuna Kijiji cha Mirui. Kijiji hiki cha Mirui, wawindaji wanaotoka Kilwa, wanaingia mpaka kijijini kwa madai kwamba Mirui iko Kilwa ambapo si kweli. Sasa kuna migogoro ya mara kwa mara kutokana na wawindaji hao. Ningeomba suala hili lirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, tuliwahi kwenda kumuona Mheshimiwa Katibu Mkuu wa wakati huo, alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, Ndugu Severe, kwa suala hili hili lakini hakuna marekebisho yoyote yaliyofanywa. Naomba angalieni ramani ya hivi sasa ili muweze kuona kitalu kile kiko wapi na mipaka ya uwindaji inakwenda wapi? Sababu hali ilivyo sasa hivi inaleta matatizo sana katika kijiji cha Mirui. Naiomba Serikali, ifuatilie kwa karibu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, ninaomba masharti ya upatikanaji wa *games scout* ilegezwe ili tuweze kuwatumia wanamgambo wetu ambao watapata mafunzo ya ziada, waweze kukabiliana na matatizo ya wanyamapori katika maeneo yetu. Hilo ni la msingi mno kwa upande wetu kwa kuwa mazao yetu yanaendelea kuharibiwa na pia maisha ya wananchi yanaendelea kuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ku-*wind*, ninapenda pia Waziri, aeleze leo hii kwa nini boma la Liwale ambalo tuliahidiwa kwamba lingekarabatiwa mwaka jana, halijakarabatiwa pamoja na ahadi zote tulizopewa?

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu, kwa nini barabara ile ambayo tulihitaji ifufuliwe kati ya Ndapata kwenda Ulanga, haijaanza kushughulikiwa? Haya yote ni muhimu kwa jamii zote mbili, za upande wa Ulanga na Liwale.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye misitu, tunashukuru sana sisi pia tumebahatika kuwa na misitu mizuri na inatumika vizuri lakini pia makusanyo ambayo yanendelea kukusanywa katika misitu hiyo kwa bahati mbaya yote huwasilishwa Serikali Kuu au Makao Makuu lakini hakuna hata chembe ya hela tunayopata. Hakuna *retention scheme* katika *project* ile ambayo itawezesha wanavijiji kuendelea kutunza misitu ile, sijui Serikali kwa suala hili mnaliona vipi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, asante. (*Makofi*)

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliyo mbele yetu asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kama ilivyo ada kwa kutoa pole kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na timu yote katika Wizara hiyo pamoja na watendaji, kwa msiba mkubwa uliowapata na tunaomba Mwenyezi Mungu, azirehemu roho za waliofariki na walazwe mahali pema peponi kwa amani, Amina.

Mheshimiwa Spika, naanza pia kwa pongezi, kama ilivyo ada na kama walivyotangulia kusema Wabunge wenzangu, kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Bodi ya Utalii na watendaji wote kwa ujumla, kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya kwa Taifa letu. Hotuba yao imejionyesha kwamba, sekta ya utalii imezidi kuongeza mapato kwa Taifa letu na kuendeleza uchumi na maendeleo katika Taifa na kwa wananchi kwa ujumla. Tunaomba jitihada hizi ziendeleo na watendaji wapate moyo zaidi wa kutenda kazi kwa bidii na kwa uadilifu ili kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, imependeza kutambua kwamba moja ya dhana iliyotumika kuleta mafanikio haya, ni ile dhana ya kuondoa hofu ya kusema “chema chajiuzua kibaya chajitembeza”. Kuondoa hofu hii, kumefanya sisi tuweze kujitangaza kuhusu vivutio vingi vilivyomo katika nchi yetu na mafanikio ndio haya ambayo yameongeza mapato yanayotokana na utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika, tuna kila sababu ya kuongeza jitihada za kutangaza vivutio vya utalii katika nchi yetu ili tuendeleo kuwavuta watalii wengi ili kusudi tuweze kupata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, saikolojia ya binadamu mara nyingi inahitaji kukumbushwakumbushwa. Sisi wote tunajua *Cocacola*, *Pepsi*, tunajua mitandao ya *Voda*, *Tigo*, *Zantel* na kadhalika, lakini kila kukicha kuna matangazo ya *Tigo* kama vile hatuyajui. Yote hii ni kutufanya binadamu wakati wote tukumbuke vitu vinavyoweza kutupa manufaa, kama ni burudani au huduma za msingi. Kwa maana hiyo, kwa upande wa utalii, tusichoke kujitangaza Kimataifa ili kuendeleza dhana ya kupata mapato na kuvuta watalii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda nitoe pongezi maalum kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa haiba yake, matamshi yake na uongozi wake. Kokote anakokwenda duniani anaipa sifa nchi yetu Tanzania na hata watalii na wananchi katika nchi nyingine, wanatamani kuja kuona nchi hii inayoongozwa na kiongozi mwenye haiba na mvuto na karisma ya namna hii na wanajiuliza nchi hii iko vipi na Watanzania hawa ni watu wa namna gain, wenye amani isiyoisha? Kwa hivi, ni lazima tumpe pongezi Mheshimiwa Rais, kwa kazi anayoifanya ya kutangaza nchi yetu na kutuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya faraja, sina budi kuingia katika masuala ya uwakilishi wa kero ambazo wananchi wa Jimbo la Mikumi wamenituma nizitamke.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza kabisa, wananchi wanapenda kujua kwa nini Wizara ya Maliasili na Utalii, imetelekeza Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kwa kipindi cha miaka yote hii? Wizara ina mpango gani kuiendeleza hifadhi hii ili kuvutia watalii?

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma, nafikiri na wewe utakuwa ni shahidi, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ilikuwa *very famous*, ilikuwa inasifika na ilikuwa inavutia watu wengi wa nje na wa ndani. Naamini baadhi yetu na wengine waliokuwa vijana zaidi kipindi kile, walipochoka kusoma vitabu au kufanya kazi, waliweza kuendesha gari mpaka Morogoro, kwenda Mikumi ku-*spend weekend* na unarudi Jumapili yake. Ni karibu na pana vivutio vya kila aina vilivyomo katika hifadhi nyingine za Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali, kwa sababu ambayo haiieleweki na haijulikani, ni kama imepuza hifadhi ya wanyama ya Mikumi. Au pengine kwa sababu njia ya Kitaifa inakatiza pale, kwa hiyo kuna kubweteka kwamba wanaona wanyama bure, sijui wanakuja kuwasalimia wasafiri? Lakini pale kuna kila kivutio, kuna wanyama wote wanaopatikana Serengeti, kuanzia simba, chui, tembo, ngedere, nyani, viboko, mamba na kadhalika, kuna tatizo gani hapo?

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba, katika miaka michache iliyopita kulikuwa na ubinafsishaji uliofanyika na ninafahamu kulikuwa na kesi iliyomhusu mwekezaji fulani ambapo kulikuwa na utata wa masuala ya umiliki wa hoteli inayoitwa *Mikumi Wildlife Lodge*. Ninafahamu kwamba kesi hiyo ilimalizika na uamuzi ukatokea kwamba Serikali inatakiwa kumlipa fidia mwekezaji huyo shilingi bilioni tatu, kwa taarifa nilizonazo. Ninachotaka kujua, Serikali, imeweza kulipa fedha hizo kwa huyo mwekezaji aliyeshinda kesi hiyo? Au hiyo ni sehemu mojawapo ya kikwazo katika kuhamasisha wawekezaji wengine kuja kuwekeza kwa kujenga hoteli katika mbuga hiyo?

Mheshimiwa Spika, moja ya tatizo ninaloliona pale, pengine ni hilo suala la kutokuwa na mahali pa kufikia pazuri. Sasa hivi pana *camps* mbili tu, Kikoboga na *Vuma Hill* lakini nafasi na fursa za kuwekeza hoteli zaidi ambazo ni nzuri na zenye mvuto ili kuvuta watu katika eneo lile ambalo ni *hospitable* kabisa, zipo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini Serikali haichukui jukumu la kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza katika eneo lile? Hili bado ni swali ambalo tunashindwa kupata majibu. Ni sawa na mtu unakalia utajiri, kama tunavyojua utalii unaingiza fedha nyingi, tunakalia utajiri siku zinakwenda; sasa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye suala la msingi nililouliza, kama Serikali imemlipa mwekezaji yule zile fedha na kama bado, Serikali haioni kwamba riba inazidi kuongezeka kama hilo halifanyiki sasa hivi? Basi ni maswali ambayo kwa kweli yanatuchanganya vichwa kwa kutoelewa nini hasa kinachoendelea kuhusu jambo hili.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anajibu hoja mbalimbali za Wabunge na hili aweze kutufahamisha.

Mheshimiwa Spika, nataka nitaje kivutio kingine ambacho ni *special* ambacho kipo katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Maeneo jirani na hifadhi hiyo, kuna vijiji maarufu vitatu wanavyoishi wenzetu wanaolinda tamaduni zao, makabila mengine yote yamekwishapoteza tamaduni zao, Wamasai.

Mheshimiwa Spika, kuna kijiji cha Ngaite, kiko jirani kabisa na Kilosa, Kiduhi na Twatwatwa, katika Jimbo la Kilosa. Ndugu zetu hawa Wamasai wana sifa ya kulinda utamaduni na utamaduni wa Wamasai ni moja kati ya vivutio ambavyo watalii wengi na hata wananchi nchini hupenda kuangalia na kushuhudia. Naamini hii ni sehemu moja ya kivutio cha mvuto kuweza kuunganisha na ujenzi wa hoteli nzuri ili watalii waweze kuufurahia na pia wananchi, kwa utalii wa ndani kuweza kufurahia matunda haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninapaswa kuliwasilisha, ni suala la mahusiano. Kuna kero kubwa ya mahusiano mabaya baina ya walinzi wa hifadhi za taifa kwa maana ya *TANAPA* na wanavijiji wanaoishi au wanaopakana na hifadhi hizo. Kwa upande wa Kata ya Mikumi, wananchi wanapata adha kubwa sana kwa Askari wa *TANAPA* kutoheshimu mipaka ya hifadhi. Wananchi wanathamini sana umuhimu wa hifadhi, wananufaika na misaada mbalimbali na kwa maana hiyo ninapenda kwa namna ya pekee nitoe shukrani sana kwa *TANAPA* kwa misaada mingi ambayo wameitoa kwa baadhi ya Kata kama Ruhembe, Mikumi na Ulaya, kwa ujenzi wa madarasa. Lakini tunapokuja katika masuala ya kuheshimu mipaka, si tu kwamba Askari hawathamini, maana wao wana-*assume* kila wakimuona mwananchi ana baiskeli amebeba mkaa, kuni au mbao, moja kwa moja wana *conclude* amevuna katika Hifadhi ya Taifa. Kwa hiyo, watachoma matairi yale na kukata na kutoboa matairi au kuyapiga teke ma-*rim* ya baiskeli ili yule mwananchi ashindwe kuendelea kuchukua zile mali zake na wakishafanya hivyo, wanachukua mali zile wanazifanya zao. Sasa hii ni unyanyasaji uliokithiri kwa kweli, ambao unastahili kupigwa vita.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inajirudia pia katika maeneo ya Kata ya Ruhembe, katika vijiji vya Lumango, Kitete, Kielezo, Kidogo-basi, Gombati na Matambiko.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeashiria kuleta uhasama mkubwa sana baina ya wanavijiji na Askari kiasi kwamba haipendezi, wakati tunategemea wanavijiji walio jirani wawe ndio kama Askari na walinzi wa hifadhi hizi za Taifa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, afanye utaratibu unaostahili ili kuwepo na mikutano ya mara kwa mara ya ujirani mwema baina ya uongozi wa hifadhi za Taifa na vijiji vinavyopakana navyo ili kuweza kuleta suluhu na mahusiano mema baina yao, la sivyo kwa hakika uhasama huu hautasaidia kuhifadhi hifadhi zetu na maliasili ambayo wote sisi tunaitegemea kwa kuwa ina thamani kubwa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni suala la uharibifu wa mashamba na mazao. Kifupi, Wabunge wengi, wamezungumza juu ya suala hili. Ushauri wangu, unahusu fidia



kwa vifo vinavyosababishwa na wanyama waharibifu. Pengine ingekuwa ni wazo zuri, Kamati inayohusika na Wizara hii, iangalie, itathmini matukio haya na kutoa mapendekezo juu ya namna bora ya kutoa fidia kwa wanaoathirika kwa vifo na mazao yanayoharibiwa mashambani ili mapendekezo hayo yapelekwe katika ngazi husika za Serikali na kugeuzwa au kuwekwa kuwa Kanuni. Maisha ya binadamu huwezi kuyathaminisha kwa fedha ya Sh.200,000/=, haitoshi kabisa, si kitu si chochote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, ashughulikie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa mazao, kama walivyozungumza Wabunge wengine, ingekuwa ni busara kungeza idadi ya Maaskari wanaolinda katika maeneo ambamo mashamba ya wanavijiji mengi yanapakana na hifadhi la sivyo urudishwe utaratibu uliokwishatumika zamani.

Mheshimiwa Spika, wako Maaskari wastaafu, wazee wastaafu ambao kwa utaratibu maalum wa uchunguzi na kuratibu, wanaweza kupewa vibali vya kuweza kupiga au kuwauwa wanyama ambao wanaleta madhara katika maeneo wanamoishi. Nasema, kwa utaratibu maalum unaozingatia hali ya usalama kwa ujumla wa matumizi ya vifaa hivyo. Wapo wenye leseni au Wanamgambo katika vijiji vinavyopakana na hifadhi; wangetumika ingesaidia sana kupunguza adha ya uharibifu wa mali na pia kupunguza *chance* za vifo vinavyosababishwa na wanyama wakali katika maeneo jirani na vijiji hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, natamani sana ningesema siungi mkono hoja hii lakini kwa sababu napenda kuweka rekodi ya kuwa Mbunge Mstaarabu na kuelekea kwenye kuwa *Parliamentarian*, naunga mkono hoja hii nikiamini Mheshimiwa Waziri, atajibu hoja nilizozielezea, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lyamba. Sote tunatambua jinsi ulivyo Mstaarabu na hata wapiga kura kule Mikumi wanafahamu hilo.

Sasa namuita Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, atafuatiwa na Mheshimiwa Benito William Malangalila, wakati huo ajiandae Balozi Dr. Getrude Mongela.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuchukua nafasi hii, kupongeza Wizara kwa kupanga bajeti ambayo imegusa wananchi. Nilikuwa naisikiliza kwa makini kabisa bajeti hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma, ametoa vipengele 138 ambavyo vimegusa mambo mbalimbali, lakini mimi nitazungumzia vipengele vitano (5) tu, ambavyo ni matangazo ya biashara, utalii wa utamaduni, mjusi (*Dinosor*), mfuko wa wanyamapori na ununuzi wa magogo, kama muda utaruhusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matangazo ya biashara.

**SPIKA:** Kile cha tatu umetaja nini, Mjusi?

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, eeh, mjusi (*Dinosaur*).

Mheshimiwa Spika, nianze sasa na matangazo ya biashara. Kwa kweli mimi nimefarijika sana kwa matangazo yale ambayo yamepita sehemu mbalimbali kutangaza utalii wetu. Kwa kweli, biashara ni kujitangaza. Biashara yoyote ni kujitangaza. Matangazo haya yamefanya kazi nzuri na kazi imeonekana.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimeshuhudia ndege nzima ya *KLM* ya tarehe 5, imeshusha watalii karibu 800 pale Kilimanjaro, wanashuka ndani ya ndege wametoka Marekani na *Netherlands*, kwa kweli matangazo yale yamefanya kazi sana.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa sasa pale Kilimanjaro, kile kiwanja inabidi kifanyiwe utaratibu wa matengenezo kwa sababu walipokuwa wanashuka wale watalii pale, wengine walikuwa wanaogopa kushuka pale chini kwa sababu hawajakanyaga (udongo) ardhi ya Tanzania. Yale mawe yalikuwa yanawasumbua sana kukanyagakanyaga, kwa hiyo kama kungekuwepo na lile bomba la kupitishia watu kwenda ndani ingekuwa ni vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maandalizi ya kuwakaribisha watalii nchini sasa yafanyike kwa sababu wameshahamasika sana kuja nchini Tanzania. Kioo ni matangazo na ninaunga mkono suala la kutangaza utalii wetu. Biashara ni kujitangaza na wasanii wanasema:-

*“sema na watu upate ya watu ili uwe mtu mbele ya watu”*

Mheshimiwa Spika, hii ina maana ya kujitangaza, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la utalii wa utamaduni. Hili kwa kweli, nililizungumzia wakati nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu, kwamba sasa hivi watalii wamegeuza kibao badala ya kuuangalia tu Mlima Kilimanjaro, kila siku sasa hivi wanataka mambo ya utamaduni.

Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anazungumzia masuala ya utalii wa utamaduni alitaja maeneo ambayo utalii wa utamaduni upo ambapo ni Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya, Manyara, Pwani na Tanga. Halafu akalizia kutaja Ukanda wa Kusini na Ukanda wa Pwani. Mimi ninamuomba sana, ule Ukanda wa Kusini na Ukanda wa Pwani, afafanue zaidi ni sehemu zipi hizo? Kwa sababu tunapenda kujua hasa maeneo yale na miji ile ili tusije tukasahauliwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nasisitiza kwamba Mkoani Lindi na Mkoani Mtwara, utalii huu upo, wasije wakatusahau kwa sababu, utalii wa utamaduni sasa ndio uliobaki. Watalii wengi wanaokuja kutembelea katika maeneo haya, hao wanaoshuka kwenye ndege kuja Kusini, kuja maeneo mbalimbali, wanafuata hilo hilo, utalii wa utamaduni.

Mheshimiwa Mbugge hapa wa Liwale, alikuwa anasema majengo ya Boma yamesahauliwa kujengwa, lakini ni pamoja na utalii wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kusini kuna utalii wa utamaduni, umejaa kibao, wasije na sisi wakatusahau, ninaomba sana. Kuna boma hilo la Liwale ambalo Mbunge amezungumzia, kuna Viboko wale 500, mimi kila siku nazungumzia suala hili kuna viboko wengi sana, utashangaa. Kuna kilimo, kuna mikoko ya Lindi, kuna *beach* ya bahari ya Lindi na Mtwara ambayo unaweza kuendesha gari juu ya *beach*, kuna bahari nyeupe nzuri sana kutoka Lindi hadi Mtwara. Kuna mambo mengi tu, magofu ya Waarabu na mambo mengine mengi ya kuangalia kama utalii wa utamaduni. Wakati ule nilionyesha senti ya Kiarabu lakini leo nitaonyesha mjusi (*Dinosor*).

Mheshimiwa Spika, niendeleo na suala la mjusi. Mwaka juzi nilizungumzia suala la mjusi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jana alipoisoma sikuona sehemu yoyote ambapo imezungumzia utalii wa mjusi. Sasa nataka kuuliza hiki kitu kipo au hakipo? Mbona mitaani kinazungumzwa lakini sijaona Wizara kuzungumzia popote suala hili? Lakini ninazo takwimu, ninazo picha na watu wanasema wametembea na kumuona mjusi huyo kule Ujerumani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nitaonyesha hapa picha ya mjusi huyo. Nataka niseme tu kwamba ili kuongeza wigo wa utalii, inabidi mambo haya yaongezwe. Suala la huyu mjusi ambaye amepelekwa Ujerumani wakati wa vita, sisi tunaambiwa yuko mmoja lakini nataka niseme hivi kwamba mijusi hii iko mitano. Mijusi hii ilichukuliwa zamani mwaka 1909 na sasa ipo Ujerumani na ni warefu sana na kila mmoja ana urefu wake na ana uzito wake. Mmoja ana uzito karibu tani 80 na urefu wa kwenda juu kama urefu wa mnazi, leo nakutajia tu, ungeniruhusu lakini muda, ningeweza kusema kila mmoja na urefu wake na kimo chake lakini muda hauruhusu na majina yao yako hapa.

Mheshimiwa Spika, mjusi wa kwanza ni huyu hapa, amejengewa nyumba Ujerumani na amewekwa kwenye chumba cha utalii, huyu hapa, mjusi wa kwanza.

(*Hapa picha husika ilionyeshwa*)

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, mjusi wa pili, yupo, mzuri tu ambapo watalii wanafanya *booking* mwezi mzima hawapati nafasi ya kwenda kumuona. Huyu ni mjusi wa pili.

Mheshimiwa Spika, mjusi wa tatu huyu hapa, yupo Ujerumani, wamemjengea kwenye vyumba vya vioo na huwezi kumuona huyo, *booking* yake ni miezi kadhaa, ni utalii wao sasa.

Mheshimiwa Spika, mwingine huyu, halafu sijui wangapi? Mwingine huyu. Kwa hiyo, walichukuliwa baba, mama, mtoto, mjukuu, mjomba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa huu ni utalii, sisi Lindi tumekubali kuwatengea eneo hata kama ni mmoja mmoja kwa kuja Tanzania, maeneo tunayo ya kuwaweka mijusi hii. Tuombe wafadhili, angalau kwa mmoja mmoja kila mwaka kumrudisha Tanzania kwa ajili ya kuongeza wigo wa utalii Tanzania. Huu ni utamaduni, huu ni utalii wa

kiutamaduni. Tunaomba sana, angalau Wizara, ingesema tu kuna kitu kama hiki. Tunaomba Wizara mtuambie kama kipo na waseme basi. Hilo linahusu mjusi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa, hebu mkabidhi Mhudumu alete Mezani ili Spika aweze kuona.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu Mfuko wa Wanyamapori...

**SPIKA:** Tutakuongezea kidogo muda wako, maana... (*Kicheko*)

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Wanyamapori. Mfuko huu ni mzuri sana ...

**SPIKA:** Mhudumu, chukua picha ya mjusi uniletee. (*Makofi/Kicheko*).  
(*Hapa picha husika zilipelekwa kwa Mheshimiwa Spika*)

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Wanyamapori. Mfuko wa Wanyamapori, ni mfuko ambao ungesaidia kutunza wanyamapori. Mara nyingi, majangili wanakuja kuuwa wanyamapori lakini kama mfuko huu ukitumika kuwapa utaalumu na elimu, wananchi wanaozunguka wanyamapori, kwa kweli hakungekuwa na ujangili. Semina zinatakiwa, uelewa unatakiwa, mafunzo yanatakiwa kwa wananchi ambao wanazunguka eneo la pori husika.

Mheshimiwa Spika, nadhani mfuko huu vilevile utumike kwa masuala ya elimu, kuwaelimisha wananchi wanaozunguka mapori haya kwa ajili ya elimu kwa wananchi badala tu ya kutumika vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sisi mfuko huu, tunauhitaji kule Mkoa wa Lindi kwa sababu kuna mapori ya *Selou*. Hii *Selou* imetambaa mpaka Lindi jamani, haipo tu Morogoro peke yake, imekuja Lindi, Liwale na Kilwa. Kwa hiyo, huu mfuko tunaomba na sisi tusaidiwe ili tuweze kufanya masuala ya semina kwa wananchi ambao wanazunguka pori la *Selou*.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ununuzi wa magogo. Magogo mengi sana yanakatwa na kusafirishwa kama inavyozungumzwa na watu wengine, hii ni kweli kabisa. Sisi Mkoa wa Lindi, kuna pori linaitwa *Selou*, sijui kama wanaruhusiwa au vipi, yale magogo yanakatwa sana tena wanakata hovyoyote. Wanakata sehemu ya kati, mwanzoni wanaacha, mwishoni wanaacha, wanachukua kipande tu cha kati. Utakuta magogo mengi yamelala tu, kwa kweli hii tunasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, kama watu hawa wangeruhusiwa kuyapasua magogo haya ndani ya Mkoa wa Lindi, sisi tungefurahi badala ya wao kuruhusiwa kutoka nayo.

Wakifanya upasuaji Mkoani, sisi tunapata ajira vilevile na wananchi wote watapata ajira vilevile kulikoni kuruhusiwa kwenda nayo kwao.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara waangalie nasuala ya kubeba magogo kwenda nayo kwao wanakokwenda kupakia katika meli, kwa kweli yanatisha, ni afadhali yanakotokea magogo basi hukohuko kuwe na viwanda vyao, wafanye shughuli zao, wasafirishe yakiwa yamefanyiwa kazi ili wananchi wetu waweze kupata ajira kuliko sasa ambapo magogo mengi tu yanakwenda kwa sababu kuna wizi ndani yake tumeshaonyesha kwamba ndani ya gogo mtu anaweza akapekecha, akafunika kitu kingine badala ya gogo, anaweza akaweka pembe ya ndovu, bangi au madawa ya kulevya ndani ya gogo akafunga vizuri tu likawa gogo, wewe unafikiria gogo kumbe mwenzako ameweka vitu vingine. Tunaomba masuala ya kusafirisha magogo yaangaliwe sana badala ya kusafirisha, basi yachanwe hukukuku na zipelekwe mbao tu.

Mheshimiwa Spika, naona muda uliniongeza naweza nikautumia, niendeleo?

**SPIKA:** Ndio unautumia hivyo!

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, yapo masuala mengi ya utalii ambayo sisi kwa kweli tunayahitaji katika Mkoa wa Lindi. Mtwara na Lindi ni mtu na nduguye. Mtwara kuna eneo moja ambalo Dr. Livingstone alipita. Maeneo yale yametupwa tu mpaka leo hayafanyiwi kazi yoyote. Sisi tunaomba sana utakapoanza utalii wa utamaduni, suala la maeneo ya Dr. Livingstone, pale alipochukuliwa Susi na Chuma, yaangaliwe upya. Waziri mmoja alikuja kutembelea pale akaahidi kwamba atasaidia ujenzi wa majengo yale pale Susi na Chuma, ambapo walimpokea Dr. Livingstone na alifikia pale kwenye majengo yale. Wizara iliahidi itasaidia kuyakarabati yale majengo iwe kama kumbukumbu. Sasa ile imekuwa kero mpaka sasa, tunaomba Wizara waliangalie suala hilo upya ili waweze kusaidia kukarabati majengo yale yawe sasa utalii wa utamaduni, kwani Boma tayari limeshakarabatiwa yamebaki yale majengo pale pembeni ambayo bado hayajafanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *MANCEP*, walipokuja Kilwa Kivinje, kwa kazi zao tu waliahidi kujenga daraja moja katika kijiji kimoja. Sasa hilo daraja mpaka sasa hawajajenga kwa hiyo imekuwa kama ni kero pale, kila mtu akienda analalamikiwa kuhusiana na suala hilo. Sasa tunaomba *MANCEP* kama waliahidi kweli basi warudi wakaseme kwamba tumeshindwa na kama hawajaahidi basi waende waseme kwamba sisi tulikuwa tunaongea tu na tunafuta suala hilo kwa sababu imekuwa ni kero. Kwa kweli kule kuna upinzani mkali sana kuhusu hilo daraja na mengine mengi lakini hilo limekuwa sababu tu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, hiyo ilikuwa ya pili na ndiyo uliyoongezewa.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimeona picha za hawa mijusi, kwanza nilidhani ni hai, kumbe ni mifupa ya mijusi wa zamani lakini pia kama ni rasilimali iliyotoka nchini kwetu nadhani hapo una hoja.

Basi namwita sasa Mheshimiwa Eng. Benito William Malangalila, atafutiwa na Mheshimiwa Dr. Getrude I. Mongella na ajiandae Mheshimiwa Riziki O. Lulida.

**MHE. ENG. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai mimi pamoja na Wabunge wenzangu pamoja na wananchi wa Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu wake na pia Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuzungumzia Mbuga ya Wanyama ya Ruaha. Mbuga ile takribani miaka kama 20 iliyopita ilikuwa na Nyati wengi sana. Nyati waliokuwepo pale wanakadiriwa walikuwa wanafikia 25,000 lakini hivi sasa Mbuga ile ina Nyati wasiozidi 4,000. Nyati hawa wanapungua kwa sababu ya simba ambao wamekuwa wengi sana katika Mbuga ile. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara hii ifanye uamuzi wa makusudi kabisa kuhakikisha kwamba inavuna simba kwa wingi kabisa ili angalau Nyati waweze kuongezeka katika ile Mbuga ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali iliongeza sana viwango vya uvunaji wa wanyamapori pamoja na Simba, lakini kwa sababu simba wale ni wengi sana pale Ruaha, ninapenda Serikali itoe punguzo la makusudi kabisa ili wavunaji wengi wa simba waweze kuvuna simba waliopo pale Ruaha.

Mheshimiwa Spika, simba wakiwa wengi na simba huwa hapendi sana kupata shida katika utafutaji wa wanyama, sasa kwa kadri watakavyokuwa wanaendelea kuvuna wale simba, uko uwezekano kabisa wakaenda kuwavamia wananchi au ng'ombe au mbuzi walio katika vijiji jirani. Kwa hiyo, ili jambo hili lisiweze kutokea, naiomba Wizara inayohusika ihakikishe kwamba inavuna simba katika ile Mbuga ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Wabunge wenzangu wanailaumu sana Wizara hii kwa kupunguza gharama za vitalu vya uvunaji wa wanyama, binafsi nawapongeza. Lakini nina ushauri kwamba punguzo hilo liwe la ina mbili yaani liwe punguzo kwa wazawa wa nchi hii na liwepo punguzo dogo sana kwa wavunaji wageni. Wavunaji wageni, tozo lao litozwe kama tulivyosomewa jana nchi nyingine zinavyofanya za Botswana, Swaziland na nchi zote ambazo jana tulisomewa hapa ili tuweze kwenda sambamba lakini kwa sisi wavunaji wenyeji. Tunapenda punguzo hili liendelee. Napenda sana kula nyama ya nyati, sasa kama nyati atauzwa dola 900, ni dhahiri kwamba sitaweza

kumvuna. Lakini kama nyati atauzwa dola 500, nitajipigapiga angalau niweze kuchangia hizo pesa nikaweze kuwinda nyati, mimi ni mwindaji pia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, napenda kuzungumzia juu ya misitu ya kupandwa. Sisi kule Mufindi, tumejitahidi sana. Zipo Kata nyingi tu katika Jimbo langu la Mufindi Kusini, nianze na Kata ya Luhunga, Kata ya Mtwango, Kata ya Mninga, Kata ya Igolole, Kata ya Kasanga, Kata ya Mtambula, Kata ya Mnyololo na Kata ya Bumilainga, kwa kweli sisi tunajitahidi sana kupanda miti na mimi kama Mbunge wa eneo hilo huwa nawaambia pandeni miti muhifadhi ardhi yenu. Linakuja Shirikisho la Afrika Mashariki, watakuja watu kutoka nchi jirani, watakuja kunyang'anya ardhi yenu kwa sababu yataonekana mapori kwa sababu watu wamepanda miti kwa wingi. Sasa mimi nawaambia wananchi wa Mufindi Kusini na Watanzania wote tupande miti kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe, nina ekari 70 za PIME na Mwenyezi Mungu akinipa uhai nitakwenda kupata ekari 60 mwaka huu za PIME kwa hiyo nina shamba la ekari 130 lakini ni kiasi kidogo sana, watu wakisema una shamba kubwa nasema nini ekari 130, ni kiasi kidogo mno huwezi ukasema una shamba kubwa ekari 130 wakati mapori yamejaa kila mahali. Kwa hiyo, kila Mtanzania ajitahidi kupanda miti kwa wingi kwa sababu miti ni utajiri, miti ni pesa na miti ni mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapenda niombe Wizara hii ya Maliasili na Utalii, kuhakikisha kwamba inajitahidi sana, inatumia wataalamu wake walioko katika Halmashauri kuhakikisha kwamba wanatembelea kila kijiji kuhamasisha wananchi wapande miti kwa sababu miti ni mali.

Mheshimiwa Spika, tunahangaika sana kwamba ooh, sisi maskini, lakini Tanzania siyo maskini hata kidogo, sisi tuna mali nyingi, kuna nchi zinaitwa nchi za mbao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nalo nitakwenda kulisema kwa ufupi, ni kutunza historia ya maeneo ya wapigania uhuru. Jambo hili ni zuri sana kwani wapigania uhuru walilelewa hapa, wapigania uhuru wa Afrika Kusini, Angola, Msumbiji na hata Namibia, tuliwatunza hapa lakini maeneo haya ni heri yawekewe heshima.

Mheshimiwa Spika, kule Mgagau, Jimbo la Kilolo, wameweka gereza, hivi ni heshima kweli kumbukumbu ya wapigania uhuru kuweka gereza pale? Ni heshima kweli? Mimi binafsi naona siyo heshima.

Mheshimiwa Spika, ili kutunza historia ya wapigania uhuru, pale Morogoro wametengeneza sehemu ya Chuo Kikuu, hiyo ndiyo heshima, pale Mgagau tuweke Sekondari ya Wasichana, hii ndiyo heshima na siyo gereza, hii ni kudhalilisha kabisa kumbukumbu za wapigania uhuru.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine dogo ni kumbukumbu za Malikale. Sisi pale Iringa kuna Hifadhi ya Watu wa Kale yaani Zama za Mawe panaitwa Isimila lakini

sidhani kama eneo hili limetangazwa sana. Tunasoma tu kwenye Vitabu vya Historia *Isimila Stone Age*, tena pembeni pale kuna kaburi moja la ajabu sana. Lile kaburi, barabara ilishindwa kupita na nyaya za umeme zilishindwa kupita juu ya kaburi lile, mimi sielewi kwa nini? Nadhani Serikali itupe majibu kwa nini barabara ilishindwa kupita wakapitisha pembeni na kwa nini nyaya za umeme zimeshindwa kupita juu ya kaburi lile, ni jambo la ajabu sana. Kijiji kile kinaitwa kijiji cha Wenda...

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli.

**MHE. ENG. BENITO W. MALANGALILA:** Ni kweli eeh! Waheshimiwa Wabunge waliopita pale wanasema ni kweli. Sasa ni moja ya maajabu katika Taifa letu hata Mbunge wa Manyoni anajua.

Mheshimiwa Spika, lakini tutapenda Serikali itupe majibu, hivi ni kweli umeme ulishindwa kupita juu ya kaburi lile? Lakini ni kweli kwamba nguzo zilikwenda zikapiga 90, 90, 90 zikaendelea mbele, kuna nini pale cha ajabu? Tunataka Serikali itupe majibu leo na kama ni kitu cha miujiza basi itangaze kwamba ili iwe ni sehemu ya utalii pia. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Hivi Mheshimiwa ulitaka wafukue kaburi? Endelea! (*Kicheko*)

**MHE. ENG. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho. Nimeipongeza sana Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kupunguza kwa 38% gharama ya vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka jana sikupata nafasi ya kuzungumzia juu ya gharama za misitu ya kupandwa ya Serikali pale *Sao Hill*, Mufindi. Mimi mwenyewe nilishiriki kupanda ile misitu pamoja na Shangazi na Wajomba zangu walishiriki kupanda ile misitu. Serikali inadai kwamba imepunguza gharama ya msitu ule lakini mbona bado gharama ile ni kubwa? Mbona bado wenyeji wa Mufindi wanashindwa kununua ile miti kwa sababu ni gharama kubwa?

Mheshimiwa Spika, ninavyojua watu wanaovuna pale ni watu wa Kilimanjaro na wenyewe hawauzi mbao hizo Tanzania wanapeleka nchi za nje, hata hapa Dodoma bei ya mbao ni gharama sana, hata Jimboni kwako Mheshimiwa Spika bei ya *soft wood*, ni gharama sana. Ninyi wenzetu mna Mninga kule lakini *soft wood* yaani ubao unaotumika kupaulia nyumba, ni gharama sana. Sasa mnasema maisha bora kwa kila Mtanzania, maisha bora maana yake ni pamoja na nyumba nzuri. Utakuwa na maisha gani wakati unakaa katika tembe? Hayo siyo maisha bora hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara hii, tena Mheshimiwa Waziri tunafahamiana sana, ni Waziri ambaye ni mwelewa, anajua kabisa hili ninalolizungumza, atalitilia maanani, watapunguza kwa kiasi na ili kupata suluhu ya jambo hili, ninamwomba Mheshimiwa Waziri aende Mufindi akaongee na wadau. Mheshimiwa Zakhia Meghji alikuwa anafanya sana kazi hii. Kuna wakati tulisikia fununu kwamba



walitaka kuuza robo tatu ya ule msitu, nilisema hii haiwezekani na Mheshimiwa Zakhia Meghji alikwenda kule Mufindi.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, aende akaongee na wadau kule Mufindi ili kutafuta suluhu ya bei ya msitu ule ili angalau na wenyeji akina Shangazi, Wajomba na hata mimi mwenyewe, niweze kumudu kwa kweli kununua ule msitu angalau na mimi mwenyewe niweze kupasua mbao.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, ninapenda kuzungumzia mgogoro wa ardhi uliopo katika kile kijiji cha Ihomasa. Wananchi wa Kijiji cha Ihomasa wako katika Kata ya Kasampa. Wananchi wale kwa miaka mingi wamekuwa na mashamba yao wanalima kabichi na hata njegere, lakini juzi juzi wamefukuzwa na Wizara hii eti wamevamia eneo. Sasa nataka Wizara hii ituambie mtu amekaa pale, analima shamba lake zaidi ya miaka 15 lakini anaambiwa toka, hili ni eneo la Serikali, hutakiwi kulima hapa tena, wanafukuzwa na Mgambo. Sasa naona hii siyo haki. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha, atupe ukweli na atupe jibu kwamba hivi ni kweli mtu amekaa katika eneo lake analima, maisha yake yanategemea pale, uje umfukuze, uje umwambie aondoke, si sahihi.

Mheshimiwa Spika, maeneo yetu ya Mufindi yana uhaba mkubwa sana wa ardhi, ni maeneo ambayo watu wanayapenda yana, mvua nyingi pia miti na watu wanasema ni *Switzerland of Africa* na hali ya hewa safi. Sasa wakitoka pale wanakwenda wapi? Hili ndiyo swali ambalo nitapenda Mheshimiwa Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Spika, halafu pale Ihomasa kuna pango moja zuri sana. Hilo pango inasemekana Wajerumani walikuwa wanajificha humo wakati wanapambana na akina Mkwawa. Ni pango zuri na mimi mwenyewe nimewahi kuingia humo ndani yaani ni pango la kuvutia. Sisi kule Mufindi, kwa kweli hatuna vivutio vingi sana vya utalii, ni vichache tu kama miti, mashamba mazuri ya chai ambapo watu wa nje ya nchi, wanapenda sana kututembelea kuona hayo na kule Luhunga kuna Mzungu mmoja anaitwa Foxy, ana hoteli yake nzuri kule yeye ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Benito W. Malangalila.

Namwita sasa Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, atafutiwa na Mheshimiwa Riziki O. Lulinda na Mheshimiwa Peter J. Serukamba, ajiandae.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ambayo na mimi niliwahi kuwa Waziri wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana na kama tutataka kusonga mbele, nadhani hii ni miongoni mwa Wizara ambayo itatusaidia katika nchi yetu kwa sababu kwa lugha ya Maliasili na Utalii, inasema *products* yaani mazao ambayo katika dunia hii hayana ushindani tukianza na fukwe zetu na ukiangalia vivutio vingine vya asili na vya kihistoria, kwa kweli Tanzania haina mshindani. Tukiweka mkazo katika maendeleo ya Wizara hii, hii ni biashara ambayo hatutapaswa kuwekewa vigezo kama tunavyowekeka katika maeneo mengine ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, napenda kumpongeza Waziri, mwanafunzi wangu ambaye kwa kweli najivunia kwamba kumbe kazi niliyoifanya wakati nafundisha, nilipokuwa Mwalimu wa Walimu, ilikuwa ni kazi nzuri sana. Najisikia vizuri kumuona amekaa pale na anaendesha Wizara hii vizuri, amerithi nyayo za Mama yake, Mwalimu Getrude I. Mongella, UTS Na. M6390. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kumpongeza Katibu Mkuu, nimemwona wakati wa Sabasaba alivyoweza kuinadi Wizara hii kwa ujasiri kabisa. Nawapongeza wafanyakazi wote wa Wizara hii ambayo wengi wao ninawafahamu.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi, kwa mara ya kwanza, tuna Wizara ambayo inaendeshwa na wanawake watupu kutoka Waziri mpaka ngazi ya Wakurugenzi. Napenda nimwambie Waziri kwamba *you can make it, it can be done*. Kwa hiyo, hakuna kutetereka, msije mkatuaibisha, wakasema Mama Mongella aliomba katika Wizara ya Nishati, wanawake waangaliwe, haya, ngoja tuone kazi, naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Katibu Mkuu wakisaidiana na wataalamu wao, waifanye kazi hii vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nataka tu niseme haya yafuatayo. Moja, katika suala la utalii, kuna uhusiano mkubwa kati ya Wizara hii na Wizara nyingine, kama Wizara nyingine zisipotekeleza majukumu yake, Wizara hii inapata vikwazo vingi. Kwa mfano, Wizara hii inategemea usafiri na mawasiliano kwa hali ya juu kama alivyokwisha sema Mheshimiwa Fatma Mikidadi, ukiangalia viwanja vyetu hasa kiwanja cha Mwanza, Kilimanjaro na hata Dar es Salaam havijafikia kiwango cha kuvutia watu kwa sababu utalii katika maeneo ya usafirishaji ni suala muhimu sana. Mtu asipopata usafiri wa kuaminika, asipohakikishiwa kwamba atakuwa na usalama wa kutosha wakati akiwa katika maeneo ya utalii mpaka kuondoka, inapunguza sana idadi ya watalii wanaoingia nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, viwanja vya ndege ni kitu muhimu na hata viwanja vidogo vidogo kama kile cha Kabingo, Ukerewe ni kiwanja muhimu sana kuleta watalii katika maeneo kama hayo na viwanja vingine vidogo katika maeneo ya *Selou*. Kwa hiyo, ni vizuri sana Wizara hii ifanye kazi kwa karibu sana na Wizara nyingine ili tuweze kuwa na usafiri unaoaminika katika upande wa barabara na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, hapa ninapenda kusema kwamba suala la kueneza *ICT* yaani *Information Communication Technology* katika maeneo ambayo watalii wengi wanakwenda, ni la kuangalia kwani ni muhimu sana kwa sababu watalii wasingependa kufika huku na kuachana na dunia iliyoendelea na hakuna sababu kuendelea kuonyesha umaskini wetu. Ni lazima tuweze kuendeleza hii mifumo ya *ICT* ili watalii wanapokuwa huku waendeleo kuwa na mawasiliano ya uhakika na kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoteli. Katika hoteli, ninasema utalii si hoteli kubwa tu hata hoteli ndogo ndogo zinawafaa sana watalii. Bahati nzuri, mimi nimesafiri sana katika dunia hii, namshukuru Mwenyezi Mungu na nimeona mahali pengine sehemu zinazovutia siyo zile hoteli kubwa ambazo ni za gharama kubwa isipokuwa ni hoteli ndogondogo na hili ndilo ningeomba Wizara itilie mkazo katika hata kuwafundisha watu wa kawaida wanaoendesha biashara mbalimbali za hoteli ili mtalii anapofika aweze kupata chakula safi na aweze kupata mahali pazuri pa kulala na wakati huohuo sehemu hizo ziwe zinaandaliwa katika hali ya kuvutia.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu niseme usafiri mwingine ambao kila mara tunausahau ni usafiri wa majini kwa ajili ya utalii. Maji tunayo mengi na tungeweza kuimarisha utalii wa majini tungeweza kuendeleza utalii wa majini na mashindano yake ni makubwa sana kwa mfano kupiga makasia na sisi ambao tuko katika visiwa kwa kweli kupiga makasia ni kazi mojawapo ambayo tunaifahamu ni kuongezea tu vifaa ambavyo vinaweza kutusaidia katika kujenga utalii wa kupiga makasia. Ukiangalia kwenye *television* michezo ya kupiga makasia ni kati ya michezo maarufu sana duniani na inavutia sana. Kwa hiyo, ukiangalia Ziwa Nyasa, Tanganyika, Victoria na Pwani, tungeweza kabisa kuendeleza aina hiyo ya michezo ambayo inavutia watalii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia niseme kwamba nchi yetu hii imebarikiwa kuwa na hali ya hewa nzuri. Juzi juzi tulikuwa Misri katika Jangwa, mahali panaitwa Harmashek na pale ni jangwa yaani ni mchanga mtupu lakini niliona maajabu. Jioni mmoja kati ya Wabunge wa Bunge la Afrika wa Misri, akasema anatupeleka *Harmshek by Night*, nikaona maajabu. Tukaingia kwenye mchanga ule na *Guides* walikuwepo kwa sababu ni rahisi kupotea ndani ya mchanga, tulikuta ni miamba tu lakini ilivyotengenezwa hiyo miamba na taa zilivyopandishwa kwenye ile miamba tulikuwa tunaona ni maajabu kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama hawa watu waliopo Jangwani, wanaweza kutumia mazingira yao vizuri na sisi tunaweza kutumia yetu vizuri zaidi yakapendeza kwa miti na misitu lakini Wizara hii inapaswa kusaidia katika kuleta maarifa mapya ya kutumia mazingira siyo haya ambayo tumeyazoea na kwa sababu natumaini kwamba Waziri pamoja na wataalamu wake wa utalii wachukue nafasi kabisa ya kuangalia na kusafiri duniani, mimi nitaongeza shilingi kama kuna kuongeza ili muweze kusafiri kuona jinsi utalii unavyoimarishwa kwa mambo madogo madogo tu ambayo huku kwetu tunayapuuza.

Mheshimiwa Spika, katika aina za utalii *cultural tourism*, iko katika *paragraph* ya 96, ukurasa wa 51 imeelezwa, ninapenda kusema Mheshimiwa Waziri na Wizara yako, niwakaribishe katika visiwa vya Ukerewe, pale mtakuwa mmeweza kuanzisha mfano wa *cultural tourism* yaani utalii wa kiutamaduni kwa sababu vigezo vyote tunavyo. Tuna ngoma mbalimbali zisizopungua 15 katika visiwa hivyo, tuna muziki wa kila aina kama Zeze, Marumba na ngoma zote hizo zinapigwa katika visiwa vya Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, tuna mila na desturi nzuri tu ambazo zinavutia hasa ukiangalia mahusiano ya watu kwa watu na jinsi tunavyoendesha shughuli zetu. Tuna mila nyingi ambazo zinavutia ambazo zinaambatana na kazi za kilimo pamoja na kazi za uvuvi. Ngingekuwa na muda ningeeleza zaidi ila siku nyingine nitaeleza lakini nitawakaribisha wataalamu waje, nilishawaona wataalamu waliovuka akiwemo Mtaalam mmoja aliyeitwa Pamba, wakati huo alikuwa amekwenda Ukerewe kutazama namna ya kuendeleza Ukerewe lakini sijapata jibu na mkakati ambao Wizara imefikia.

Mheshimiwa Spika, tuna pia sanaa mbalimbali, tuna mapango makubwa mengine ukienda nayo unatokea ndani ya Ziwa, ni maeneo mazuri tu ambayo yangeweza kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, pia tuna mawe ya maajabu kama Jiwe la Blebeka Ukawe ambalo linacheza likiamrisha na wenye jiwe lenyewe, wakiliambia salimia wageni, Mheshimiwa Waziri nakukaribisha uje ili jiwe hili liweze kukupa saluti maalum watakapokuwa wenyeji wake wameliamrisha na ni la maajabu ningeomba sana mkaribie wote mlione.

Mheshimiwa Spika, nimetoa tu mfano wa Wilaya ya Ukerewe, lakini maeneo mbalimbali yana vivutio. Bila kuweka juhudi maalum tunaweza tusiendeleze utalii. Kwa sababu sio jambo la mtu mmoja mmoja, wakati mwingine miundombinu ambayo ndiyo inasaidia utalii haiwezi kuendelezwa na mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Wilaya ya Ukerewe, usafiri wetu ni wa maji, barabara na wa anga lakini ukiangalia kiwanja cha Kabingo, hakijaendelezwa, ukiangalia majini watu wengi wanaogopa maji kwa hiyo lazima tupate *speed boat* na mambo mengine ambayo yatamfanya mtalii aweze kufurahia.

Mheshimiwa Spika, nimetazama kwa mfano katika Mto Nile, unakuta mara nyingi watu wanapewa nafasi ya kula melini, lakini sasa mitumbwi yetu hatuwezi kula melini lakini kwa kushirikiana na Wizara tunaweza kupata meli moja, nzuri ambayo watalii wanaweza kukaa majini wakala *dinner* huku wanasafiri, wanaangalia mandhari nzuri za visiwa vile na tunaweza kufanya hivyo katika visiwa vya Mafia na sehemu mbalimbali zenye maji ambazo kwa kweli ndiyo msingi mkubwa wa utalii.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingine kumetokea kitu kinaitwa *medical tourism*. Kama India sasa hivi watu wanafanya utalii ili akatibiwe India, acha tunaokwenda tupo mahututi lakini kuna watu wanasafiri tu wanakwenda kufanya *medical*

*tourism*. Anaweza kwa mfano, katika hospitali ya *Apollo* mtu anapata uchunguzi wa mwili mzima kwa dola chini ya mia mbili ambazo ni ndogo kuliko hata unavyoweza kupata uchunguzi wa mwili mzima hapa na watu wameitumia hiyo kama *medical tourism*.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nibadilishe kidogo, hapa tuna waganga wa kienyeji, wapo wale matapeli wanaodanganya watu, wanaoingiza na ushirikina ndani, lakini kuna wale ambao ni watu tu, wanafahamu namna ya kutibu watu na tungeweza ku-*develop* ikawa imetoa motisha kwa waganga wetu ambao wanajua dawa asilia lakini hazina ushirikina ndani yake na Tanzania tunao wengi katika maeneo mengi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wakati fulani nilipata *fracture* ya mkono, nilitibiwa tu Ukerewe kienyeji na nikapona, hiyo ingeweza kuwa *medical tourism*. Tunapaswa tu kuwahamasisha na kuhakikisha kwamba wana mazingira mazuri, hiyo itasaidia kuuwa wale walaghai ambao wanadanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna *education tourism*, naisemea hii, nimeianzisha kimya kimya kwa sababu ya mahusiano yangu na watu mbalimbali nikaona kwamba kwa nini nisiwe natoa fursa kwa watu kutembelea nchi yetu na visiwa vya Ukerewe kwa ajili ya elimu. Kwa hiyo, nilianza kwa kikundi cha akinamama kutoka New York ambao wanaitwa *the Girls Talk* na wakawa wanakuja kwenye visiwa hivi na wanabadilishana, kuna *exchange program*, wanabadilishana na wasichana kutoka katika visiwa vya Ukerewe ambao nao walikuwa wanapata fursa ya kwenda Marekani.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa pia na kundi lingine la *Georgia University*, wakija kwa muda wa mwezi mmoja wanapata pia na *points* na tunawawekea *syllabus* zinazowasaidia kuongeza *points* katika masomo yao. Kwa hiyo, wanajifunza wakati ule...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ohoo, Naunga mkono hoja kwa masikitiko kwamba sijamaliza maelezo yangu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Pole sana Mheshimiwa Balozi Dr. Mongella.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa na afya njema na leo naweza kuchangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi zangu za dhati, kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Maige na Katibu Mkuu, Mama Blandina Nyoni na wataalamu na

wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Pia napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa leo sina mengi sana ya kuongelea lakini nimeona niangalie Mkoa wa Lindi umepata nafasi gani katika kutangazwa katika utalii na rasilimali zake ili Serikali izidi kupata pato kubwa na kuweza kuleta changamoto ya utalii Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hii *Selous*, kila siku ninapochangia hoja najaribu kulizungumzia kuwa ni pori na ni mbuga kubwa sana, inabidi ifanyiwe kazi kama ilivyopewa kwa *TANAPA* au Ngorongoro, nafikiri *Selous* itaweza kutoa mapato makubwa zaidi kuliko hizo taasisi mbili. Kwa nini nasema hivyo? Nazungumza hivyo kwa sababu mpaka sasa hivi nimeangalia katika hiki kitabu nimeona *Selous* ya Kaskazini angalau wameitaja, Behobeho, Matambwe, Kingupira lakini *Selous* ya Kusini, imeachwa kama ilivyo, imekuwa kama shamba la bibi maana shamba la bibi mtu yeyote anaweza kwenda na kuvuna.

Mheshimiwa Spika, leo Kilwa kuanzia Nangurukuru, Njinjo, Migelegele mpaka Liwale ni pori kubwa sana lakini katika kitabu hiki, Liwale haikuguswa kana kwamba hawana umuhimu wa maendeleo, ndiyo maana imenibidi nisimame niombe Serikali iiangalie Liwale. Liwale sasa hivi kuna uwindaji mkubwa lakini inahitaji kupewa msukumo wa hali ya juu ili kuleta maendeleo ili na wao waweze kufaidika na maendeleo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza Mbunge mwenzangu kuwa kwa muda mrefu hawajapata asilimia ishirini na tano ya pato la uwindaji, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwanza yeye ni mwenyeji wa huko huko, amekulia Nachingwea, hivyo anaifahamu Liwale vizuri sana, aiangalie Liwale, Kilwa kwa jicho la huruma ili na wao wapate maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza wakati nikichangia katika hotuba ya bajeti kuwa Kilwa ina urithi wa dunia namba ishirini na moja lakini Serikali bado haijaona umuhimu wa kuitangaza Kilwa kikamilifu ili kuleta maendeleo. Kama dunia iliiona Kilwa ipo katika urithi wa dunia basi Tanzania ilibidi itoe kipaumbele zaidi kuitangaza Kilwa. Kwa mfano, leo Kilwa ina fukwe kubwa sana za bahari lakini katika ukurasa namba 45, wameitaja Tanga tu kama ina fukwe na inabidi iendelezwe, hizi fukwe za Kilwa nimezizungumza kwa muda mrefu, itafikia muda mpaka Serikali ikianza kuziangalia, zimeshakamatwa na wajanja na wababaishaji, wamo, wanachukua fukwe kwa bei ndogo sana, naomba Serikali ione umuhimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa heshima yako Waziri au Naibu Waziri, wawe tayari wakaziangalie hizi fukwe kuanzia Mtwara mpaka Lindi, waone umuhimu wa hizo fukwe ambazo hazijaandikwa humu ndani na kuona kama zina umuhimu. Leo ukienda Mtwara, kuna fukwe za Msimbati, Kela na Kijiweni.

Mheshimiwa Spika, wakati nimekwenda kuhudhuria mkutano wa *African Travel Association*, Balozi Mwakawago aliniuliza je, hivi ile fukwe ya Kijiweni imeendelezwaje na Serikali?

Mheshimiwa Spika, ile fukwe kwa mara ya kwanza nakwambia ndege hizi ndogo zinaweza kutua, kwa mfano *caravan* au helikopta inatua ndani ya *beach* na ndiyo maana kile kijiji wanakiita Jiwe la Mzungu, Wazungu walikuwa wanatua pale na ndege zao na kufanya utalii.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuongea sana lakini hawajatoa nafasi wala umuhimu. Mkoa wa Lindi peke yake inao uwezo wa kuchangia pato la utalii ambalo ni 17.2% ikaongezea lile la Taifa la Ngorongoro na Serengeti na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, sio Lindi tu, tukienda Rukwa ni hivyo hivyo, wana vivutio vingi ambavyo bado havijapewa mwendelezo. Serikali iangalie sehemu moja ile waliyoendeleza warudi nyuma wafanye *promotion* ya juu sehemu hizi ili nazo ziweze kufaidika. Tutakaa kila siku tunaangalia sehemu moja tunaridhika na asilimia 17.2 lakini bado tuna uwezo wa kuweza kuendeleza na kufanikiwa zaidi na zaidi na kututoa katika umaskini ambao ni endelevu sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili ina taasisi zake ambazo zinafanya kazi mojawapo ni Ngorongoro na kuna *TANAPA*. Kwa kweli hizi taasisi lazima tuzipongeze, zinafanya kazi kubwa sana za ujirani mwema kujenga shule, hospitali, barabara na kuleta huduma za maji. *TANAPA* vilevile imepewa hifadhi zingine iziendeleze lakini Serikali inataka fedha zake nyingi zilizobaki ziingie katika Mfuko wa Serikali, je, Rukwa itaendelezwaje katika Mbuga zake za Katavi bila *TANAPA* kuwa na fedha? Gombe itaendelezwaje na *TANAPA* bila kuwa na fedha? Ruaha, mbuga kubwa kama hii mnataka iendelezwe bila kuwa na fedha, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, tufikie mahali tuseme taasisi zetu tuziendeleze na tuone kuwa zinahitaji msaada wa hali ya juu, Serikali isianze kuwa yenyewe inataka kumuua mwanawe wakaachiwa wawekezaji wanakaa katika hizo mbuga, wanaweka hoteli katika hizo mbuga, barabara imejengwa na Serikali, maji yameletwa na Serikali, miundombinu yote imeletwa na Serikali, wao kazi yao pale kuja kufyonza fedha zetu na kuzipeleka kwao na tukabaki maskini. Hawana huruma na nchi yetu hata kidogo, wao wapo pale kila siku kutaka kulalia waweke bei ndogo ili wafaidike kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Spika, tupo hapa sasa hivi kuulinda Tanzania yetu iwe na utalii endelevu na itutoe kutoka katika umaskini itupeleke mbele. Saa nyingine unafika mahali

unajiuliza baadhi ya hao wawekezaji ni Watanzania lakini hawana huruma na nchi hii. Wamekaa pale wanashirikiana na wawekezaji kuhakikisha kuwa Tanzania katika suala la utalii isiwe endelevu, jiulize kwa nini Botswana wanaweza kupiga hatua, Namibia wanapiga hatua, Swaziland wanapiga hatua mpaka Kenya hapa wanatuzidi tukiacha South Africa lakini wao wapo pale tu, kwa kweli ni waharibifu na wabadhirifu sana na wameamua kutufanyia makusudi. Kila kitu wao wanataka kiwe chini wafaidike wao ili waache Tanzania ikiwa inasemwa tu kuwa ina utalii lakini hauendelezwi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba hao Watanzania ambao wamejiingiza katika shughuli hizo wawe na uzalendo. Bila kuwa na uzalendo, wataendelea kuwa na chuki na wananchi kuwaona wao wamekaa pale kutufanyia fujo na kuhakikisha hii nchi haiendelei.

Mheshimiwa Spika, narudi tena kama alivyozungumza mwenzangu kuhusu suala la *cultural tourism*. Mkoa wa Lindi tuna *cultural tourism* za kutosha ambazo zinabidi ziendelezwe. Kwa mfano, Kilwa Kipatimu, tuna mapango arobaini, yale mapango ndiyo walikuwa wanatumia katika Vita vya Majimaji, Serikali ikiangalia yale mapango yamekaa vilevile hayajapata msukumo wowote wa kuendelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivyo viboko vinavyozungumza, mimi ni shahidi, hata wewe ukipata nafasi uende kuona hao viboko maana tunavyoongea hapa isije ikaonekana kama ni uzushi, hapana, wale ni viboko ambao wanatumia utamaduni wa wenyeji kuwaamrisha, inukeni wanainuka, fanyeni hivi wanafanya vile, sasa matokeo yake pamekaa hapajaendelezwa na tumejaribu kusema kila kitu inakuwa mwisho wake kama si kweli lakini ni kweli kuna utalii endelevu Kusini.

Mheshimiwa Spika, hata hiyo mijusi anayoizungumza Mama Mikidadi, nam-*support*. Tendeguru imetolewa mijusi ya *dinosaur* kupelekwa Ujerumani lakini Wajerumani wanafaidika na kumtangaza yule mjusi duniani kote, je, Tanzania tunapata nini? Ninaomba Serikali ilifuatilie suala la mjusi huyu, itafute pesa angalau mapato yanayopatikana *twenty five percent* irudi itusaidie kuendeleza sehemu iliyotoka mijusi hiyo kama vile kujengewa shule, hospitali, barabara bora sio wao wamtumie yule mjusi sisi wenyewe tukiwa katika hali ngumu ya kimaisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kulisisitiza sana suala la fukwe. Fukwe za nchi nzima zinamalizika kuchukuliwa na wajanja, wale wale ambao wapo Serengeti, Ngorongoro wanazivamia hizi fukwe kwa bei ya chini, baadaye Serikali itakapokuwa tayari kutaka kujenga mahoteli watakuwa hawana nafasi. Watakapotaka kuleta utalii endelevu wa fukwe za bahari hawatapata nafasi hiyo, wajanja wameshafika kule na wanazichukua kwa wingi.



Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yangu sasa hivi barabara ya Lindi kimebakia kipande kidogo ambacho kitakuwa tayari hivyo Lindi tutakuwa na lami kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi halafu ni kipande kifupi sana hivyo utalii utakuwa endelevu katika Mkoa wa Lindi. Kwanza, tuna bandari kubwa ya Mtwara hivyo hata kusema tutumie utalii wa meli, uwezo tunao, tuna fukwe nzuri ambazo naweza kusema Tanzania hakuna fukwe nzuri kama zile lakini hazijatumiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nazungumzia upande wa magogo, Mkoa wa Lindi, Kama alivyozungumza Mama Mikidadi, ni kweli bado kuna biashara za panya za kutoa magogo. Magogo mpaka sasa hivi yanasafirishwa, wajanja wanatumia njia za bahari kutoa magogo maporini kama vile kuyasafirisha katika majahazi na biashara ya mkaa sasa hivi Lindi imekuwa biashara kubwa.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam hivi sasa wanasema ukitaka mkaa mzuri nenda Lindi kwa sababu mkaa wao unatumia *hard wood*. Sasa je, ile miti ya asili ambayo iko pale karibu miaka mia moja, watu wanaivuna kwa ajili ya mkaa, je, Serikali inasema nini kuhusu suala hili? Naomba tukimaliza Bunge hili, Waziri tufuatane naye, twende Lindi akaangalie hilo ninalolizungumza ili litupe faraja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina mengi zaidi ya hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lulida, kama kawaida mchango wako umeupanga vizuri sana. Anayefuata ni Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia. Napenda nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuangalia hali ya dunia katika utalii. Kwenye ripoti ya dunia inasema mwaka 1980 duniani kulikuwa na watalii milioni mia mbili themanini na saba. Itakapofika mwaka 2020, duniani kutakuwa na watalii bilioni moja pointi sita. Inakadiriwa asilimia ishirini ya *population* ya dunia hii itakuwa kwenye utalii.

Mheshimiwa Spika, nikawa najaribu kujiuliza, sisi kama Watanzania, tunajiandaa je ili tuweze kuwa kwenye hii hesabu kwamba utakapofika mwaka 2020,

tutakuwa na watalii bilioni moja pointi sita duniani, *about twenty billion people* watakuwa wanasafiri duniani. Ukiangalia hesabu kwenye kitabu cha Waziri, ukurasa wa 50, Mheshimiwa Waziri anasema utakapofika mwaka 2012, tunatarajia tutakuwa na watalii milioni moja na laki mbili.

Mheshimiwa Spika, ukifanya hesabu za kawaida kwa kuanzia mwaka 2007 ambapo tuko laki saba na ishirini na nne, unaona tunakwenda mpaka 2012, tutakuwa mia moja laki mbili utaona watakaokuwa wameongezeka ni watu laki nne na sabini na sita pamoja na vivutio vyote vilivyoko nchini, hesabu zetu ni hizo. Kwa hiyo, ina maana ukiongeza kwa idadi hiyo tutakapofika mwaka 2020 tukiwa na watalii wengi milioni moja na laki nane. Hii ni idadi ndogo sana kama kweli tunataka utalii uwe na maana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nasema sasa hivi *trend ya experience economy* imeanza ku-*override* hii *physical economy*, ndiyo *trend* ya sasa. Kwa hiyo, lazima tujiandae ili hao watalii wengi wa mwaka huo niliousema waje Tanzania. Tunafanya nini ili waje Tanzania? Lazima tubadilishe *mindset* zetu, tusipobadilisha tutabaki hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza sana, Watanzania, sisi viongozi, tunatembea sana duniani lakini tunachofanya huko zaidi ni kufanya *shopping*, napata wasiwasi, hatujifunzi na kuleta hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda India kule chini kabisa maana ndiyo nchi ya *third world*, Mji wa Kerara, kuna mto mkubwa, ukiangalia watalii wanaokuja kutembea na huo mto unajiuliza, hivi ni mto upi Tanzania tunafanya hivyo, hakuna hata mmoja. Mito Mungu ametupa, tunaangalia, Mungu ametupa mbuga za wanyama, fukwe na kila kitu, *mention any in* Tanzania tunacho lakini najiuliza tatizo ni nini. Nadhani sasa lazima *mindset* zetu zibadilike kama kweli tunataka *figure* hizi katika utalii au *industry* hii ziwe na maana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikawa nafikiria unaangalia yanayoendelea Botswana, Namibia, unajiuliza vinchi vidogo vile ambapo hawana vivutio vingi kama sisi bado wanapata zaidi kwenye *tourism* maana yake ni nini? Kwa hiyo, lazima lipo tatizo *somewhere* tufikirie vizuri namna ya kwenda.

Mheshimiwa Spika, kuna mwanazuoni mmoja anasema:-

*“Clever marketing seeks to turn the most mundane activity into an experience economy”.*

Mheshimiwa Spika, anaweza, *you will turn to be a clever marketing*. Kwa hiyo, nasema tunalo tatizo la *marketing* katika sekta yetu hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nikawa najiuliza lazima tufanye kazi moja, tuvitambue vivutio vyote vilivyopo kuanzia Wilaya, Mkoa, kwa *zone* zetu. Nikawa najiuliza ipo *zone* ya Magharibi ambako natoka, ukienda *zone* ya Magharibi kuna Gombe, Mahale, *Lake Tanganyika* yenyewe, Katavi, Livingstone Memorial Ujiji, Ugala *Game Reserve*, *River Malagarasi* *mention any* hujaweka mapori mengine. Tunafanya nini kwenye hii *zone* ili ziweze kuwa na maana. Napenda kushauri lazima wenzetu wa Wizara waanzishe *zone* hizi ili sasa tunapokuwa tunafanya *marketing* yetu ziende kwenye *zone* hizi ili tuweze kufanya vizuri zaidi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika  
kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, hii siyo kengele ya kwanza, nadhani ni ya yule ambaye alikatiza katikati.

**SPIKA:** Mmh ya kwanza hiyo. Mazungumzo yamekolea endelea tu, bado dakika tano.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaangalia, wenzetu wamesema jana hapa, kwenda kuona *gorilla* Rwanda kwa mtu mmoja ni dola mia tano. Kuangalia *chimpanzee* waliopo Tanzania peke yake kule Gombe ni dola hamsini, unajiuliza sisi tuna matatizo gani na kuweka bei, tunamwogopa nani kuweka bei? Nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri anafanyaje na lazima apandishe bei ya hawa *chimpanzee*, kwa sababu wenzetu dola mia tano kwa *one hour*, sisi dola hamsini mpaka utakapochoka uondoke, hii ndiyo Tanzania yetu. Kwa hiyo, lazima tu-*package* utalii wetu lakini lazima tufanye kazi ya kujenga viwanja vya ndege na barabara zetu ili tuweze kwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, *tourism* ni *export* lazima *export* hii ituletee pesa. Naomba leo nipendekeze yafuatayo. Ninaomba kwenye sekta ya utalii tuachane kuweka *bill* zetu kwa dola tuweke kwa shilingi, maana yake ni nini? Hii habari tuliyonayo kwamba Wazungu wote wanapotaka kuja kutalii Tanzania wanalipia Ulaya ukiweka hapa sheria kwamba ukitaka kwenda Tanzania lazima ulipe kwa hela yao, hawatachukua hela kule kwao watakuja na dola zao watachenji kwenye *bureau* zetu na kwenye benki zetu ili wapate shilingi ya kulipia za kulipia hiyo *tourism* yetu. Kwa kufanya hivyo, tutapata dola nyingi sana lakini pia hatutaibiwa na hao wajanja ambao wanalipia huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ukienda duniani kote hata Uganda ukikaa hotelini unapewa *bill* kwa pesa yao ya Uganda lakini sisi tuna tatizo gani na dola? Naomba tubadilike, tu-

*bill* kila kitu kwenye *tourism* yetu kwa kutumia pesa yetu ya Tanzania. Tukifanya hivyo, tutapata dola nyingi zaidi na uchumi wetu utafaidika zaidi katika *industry* hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la fukwe, wenzangu wamelisema sana. Jamani Watanzania kuanzia Tanga unateremka unakwenda mpaka Mtwara kuna *beautiful beaches*. Ukienda Kigoma *Lake Tanganyika*, ukienda Nyasa, Lake Victoria, lakini angalia hapa Mheshimiwa Waziri ameongelea suala la fukwe katika ukurasa wa 45, ameongelea kidogo sana *paragraph* moja.

Mheshimiwa Spika, ukienda Madagascar, Mauritius, biashara ya *tourism* ni fukwe, sisi tunazo fukwe nyingi lakini Waziri anaongelea habari za fukwe katika *paragraph* moja tu. Kwa hiyo, kwake yeye fukwe si jambo la msingi sana. Naomba tukubaliane kabisa kwamba, kama kuna watu wamepewa viwanja kwenye fukwe zetu wanyang'anywe kwa faida ya Watanzania na uchumi wa nchi yetu *otherwise* tutakuwa tunasema hapa mambo hayabadiliki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niseme habari ya leseni za biashara ya utalii kwa maana ya utalii wetu wote. Naomba sana kama tumesema tuamue, hakuna atakayekuja ku-*invest* Tanzania bila kuwa na *local shareholder*, ndiyo namna ya *empowerment*. Tukifanya hivyo, tutafaidi sana katika hii *tourism* lakini wanaokuja kujenga hoteli kwenye mbuga za wanyama tuwaambie TANAPA na Ngorongoro, yeyote anayejenga hoteli kwa sababu hawapewi *occupancy* basi TANAPA iwe na *share* ishirini na tano mpaka thelathini kwenye hoteli hizo. Kwa kufanya hivyo, ndiyo tutafaidi kama nchi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Kenya wana kitu kinaitwa *brand*, *it is high time* na sisi tufanye *branding* ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, najua Wizara ya Fedha, inataka kuchukua fedha TANAPA pamoja na Ngorongoro. Leo TANAPA wanasimamia *National Parks* karibu kumi na tano na zinazoleta faida au ambazo wanapata *surplus* hazizidi nne, ukisema unachukua zile *surplus* maana yake utaua *National Park* moja baada ya nyingine. Kazi tuliyonayo ni kuwaambia watu wa TANAPA wahakikishe wana-*invest heavy* kwenye mbuga zetu zote ili mbuga zetu ziweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, tukishafika hapo, tutapata fedha nyingi na Serikali itapata fedha lakini kabla hatujafika hapo, tusipokuwa waangalifu ndiyo kama ile biashara tulifungua ofisi nyingi sana, makampuni yakaanza kufa moja baada ya nyingine, tukaona *solution* ni kwenda kwenye ubinafsishaji. Tukizubaa wakaanza hiyo *move* wanayotaka kufanya, tutaanza kubinafsisha mbuga moja baada ya nyingine na sisi ni wepesi kutafuta majibu rahisi kwenye mambo magumu.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni la msingi sana, wenzetu Kenya wanafanikiwa, narudia tena kusema *mindset* zetu zibadilike kama wenzetu. Mungu ametupa kila kitu, hatuna maelezo yoyote katika nchi hii kwa nini *tourism sector* isiweze kuchangia kwa kiasi kikubwa kuliko inavyochangia kwenye pato la Taifa, maelezo ya kweli hayapo.

Mheshimiwa Spika, naomba leo nitoe maelezo kuhusu kwa nini hatujafanikiwa, tatizo letu ni namna tunavyoendesha mambo yetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kwenye hesabu hapa tunatarajia kupata dola karibu bilioni thelathini kutoka Mlima Kilimanjaro lakini kwenye uwindaji tunatarajia kupata bilioni ishirini na nane, unajiuliza Mlima Kilimanjaro tutapata bilioni thelathini lakini mlima utabaki, huku ambako hivi vitu vinaisha kwa sababu ukiwa unawawinda wanyama wanaisha hawarudi, tunapata kidogo namna hiyo, maana yake ni nini? Haielezeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje na mkakati hapa kwamba tunafanya nini kwenye fukwe zetu ili tuweze kufanya nchi yetu ifanane kama ilivyo ili kila *zone* iweze ku-*benefit* kwenye suala hili. Nasema haiwezekani tutegemee *tourism* katika *North Circuit* peke yake, matokeo yake *North Circuit* itakufa na utalii utakufa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba. Mchango wako umefikia viwango ambavyo Spika anapenda, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mpesya.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Maliasili na Utalii.

Kwanza, nianze kwa kuzungumza kwamba, tutazungumza mengi sana, lakini lengo letu la mwisho ni kuhakikisha tunampunguzia umaskini wa kipato Mtanzania huyu. Hilo ndilo lengo letu, ndiyo *ultimate goal* yetu, kumpunguzia Mtanzania umaskini wa kipato. Kila Wizara inayoleta hoja ya bajeti hapa lazima lengo liwe ni kumsaidia Mtanzania kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze tu na hili ambalo lipo mbele yangu juu ya upandaji wa miti. Tumekuwa na kampeni nyingi sana za kupanda miti katika nchi yetu na moja kati ya maeneo ambayo yameitikia vizuri sana katika upandaji miti katika nchi hii ni Mkoa wa Iringa na Mbeya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna watanzania wamejitolea kupanda miti, sote tunajua miti inatusaidia kwa ajili ya ku-balance hali ya hewa, hali ya joto, miti inatusaidia kuvuta mawingu ili tuwe na mvua za kutosha, miti ni muhimu kwa sababu ya mazao

yanayotokana na miti hiyo, tuna kuni, tuna mbao, tuna magogo, tuna nguzo na kadhalika. Miti mingine hii kama miwati inatumika katika kutengeneza lami.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya jambo moja. Wenzetu nimesikiliza wazungumzaji wengi wakisema Watanzania tuna matatizo, labda tubadili *mindset* yetu.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni *mindset* kubwa ambayo inatakiwa tubadilike ni kuingiza uzalendo kwa kila jambo tunalolifanya. Tuingize uzalendo, tuingize utaifa, tuitetee nchi yetu kwa hali na mali, tuwatetee waliotuleta Bungeni kwa hali na mali. Hiyo ndiyo *mindset* peke yake inayoweza kuitoa nchi hii kwenda kwenye maendeleo na sio vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwa nini nazungumza hili. Maliasili pamoja na kujua kwamba tuna miti mingi sana, pamoja na kujua kwamba kuna Watanzania wamejitolea kupanda miti, tujiulize wanalilindaje soko la wananchi hawa ambao wameamua kupanda miti. Wanatumia uzalendo gani kuhakikisha watu hao ambao wamepanda miti kwa ajili ya soko la ndani linalindwa na wanapata faida na wakapunguza umaskini wa kipato ili mwaka 2025 wote tuonekana kwamba tunafaidika.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nataka niseme ambalo linahusiana na mambo ya uzalendo. Mbeya na Iringa wana miti mingi sana ambayo ni mizuri kwa nguzo katika Bara la Afrika lote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninafikiri hapa ni mahali pake. Wizara ya Maliasili na Utalii wanaruhusu mtanzania mmoja huyo achezee fedha zetu za kigeni kwenda kuagiza nguzo Afrika ya Kusini kwa kisingizio kwamba bei ya kule ni nafuu. Hakuna uzalendo hapo hata kidogo! Tunapotakiwa kwamba tuzilinde fedha zetu ndogo za kigeni, wenzetu wanasema kule kuna bei ndogo. Sio kweli! Hakuna zaidi ya kusema kule kuna *ten percent!* Hakuna uzalendo hapo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninataka nijue hiyo nguzo inayotoka *South Africa* kuileta hapa nchini na kusafirisha na kuitengeneza, wakati mti wa kawaida wa mtu wa Mbeya na Iringa hawapewi zaidi ya Sh. 10,000/= kwa mti mmoja. Sasa ukiukata mti huo ukau-*treat* ukawa tayari kwa nguzo utauzwa kwa shilingi ngapi? Bado utakuwa umefanya la maana, umelinda fedha za kigeni tulizonazo kwamba ziwepo ndani hapa.

Mheshimiwa Spika, nataka niwambie wenzangu angalieni makampuni yote yanayoendeshwa na wenzetu wa kutoka India, gari utakayoina ni TATA wanayoitumia kwa shughuli zao, gari utakayoina ni Mahindra inayotumika katika shughuli zao huo ni uzalendo, wana *market* kile ambacho kinatoka kwenye nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama kutakuwa na kampuni itaanzishwa na Muingereza, gari lake kila wakati utaikutani *Land Rover, Range Rover*, huo ndiyo uzalendo kwamba kitu cha kwake lazima akithamini zaidi. Mimi ninawashangaa wenzangu, miti imekaa Iringa

watu wanakosa soko, wanasema kwamba wanaagiza Afrika Kusini kwa sababu kuna bei nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi Wizara ya Maliasili na Utalii wanalindaje soko la ndani kuhakikisha watu wetu hao wanaopanda miti ambao mmewahamasisha wanakuwa na soko la uhakika la ndani ili nje tupate faida zaidi.? Wanalindaje hili soko? Hilo ni jukumu lao kwa sababu huyo akiuza miti yake tayari mmemsaidia kupunguza umaskini wa kipato. Kwa nini Watanzania tunakuwa hatuna mapenzi? Hatuna huruma na wenzetu, tunatapanya tu hela! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kukiwa na njaa wanakwenda kuagiza mahindi India, mahindi ya watu wa Mbozi, mahindi ya watu wa Sumbawanga wanayaacha, kisa ni nini? Wakiyaleta yale mahindi ya kutoka nje, *quality* yake ni ndogo na ni membamba. Yote hii ni *mindset* tunayoizungumza, ni kukosa uzalendo wa kuitumikia nchi hii. Kukosa uzalendo wa ukweli kabisa kwamba tunataka tuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika ninakwambia nchi hii kama tutasema kwamba sasa tumeamua uzalendo kuuweka mbele, ninaamini kabisa muda mfupi tutabadilika kabisa. Lakini watu zaidi wametanguliza ubinafsi mbele. Matakwa binafsi yamewekwa mbele kuliko maslahi ya Taifa hili na maslahi ya nchi hii. Hatuwezi kwenda kwa namna hii. Kwa hiyo, lazima tuelezeni ukweli, hakuna *mindset* wala haziko nyingi wala nini, ni kukosa Utaifa tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba niwapongeze sana wenzangu, wanamazingira pamoja na kikundi cha *JET* pamoja na rafiki yangu Felix Mwakyembe aliyepo pale Mbeya, wanaandika sana juu ya eneo la Ihefu. Hilo eneo tengefu la Ihefu na kwa kweli katika mchango wao ule maji katika eneo lile la Ihefu yameongezeka, uoto wa asili umerudi katika eneo lile, ndege wale ambao walikuwa wanapatikana, ndege wazuri wamerudi tena kwenye eneo lile, wanyamapori wameongezeka kwenye eneo lile, Bwawa la Mtera limepata maji ya uhakika na matokeo yake ni kuwa na umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu hao wanamazingira pamoja na *JET* waliamua kuweka maslahi ya Taifa mbele na ndiyo maana hali hii imebadilika kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ninasema Watanzania tukiamua tutakwenda mbele. Wakati wa Mkutano ule Sullivan, Mmarekani mmoja alisema amepolekwa Serengeti, aliyokwenda kuyaona Serengeti akasema hawa watu sio maskini na sielewi kwa nini tunawapa misaada, Serengeti tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mungu ametupa kila kitu! Kaskazini, maji; Kusini, maji; Mashariki, maji; Magharibi, maji; tatizo letu ni namna ya kutumia rasilimali hizo, maliasili ambazo Mwenyezi Mungu ametujalia na kutupatia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiri wakati tunazungumzia suala la Ihefu lilikuwa ni tatizo la Kitaifa na nguvu yote na kampeni zote tulilikabili tatizo la Ihefu

kwamba ni tatizo la Kitaifa. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, sisi kama RCC tuliridhia kwamba pamoja na eneo hilo la Ihefu, wananchi wa vijiji saba wa Ikoga, Idunda, Upagama, Sololwambo, Msiangaji, Kiwale na Ukwaheri wanayaacha maeneo hayo wahame ili kupisha eneo hilo ambalo litakuwa ni mbuga kuu ya Ruaha kwa mapenzi kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika mkutano huo, tulikubaliana kwamba wakati tunawahamisha wananchi hao, cha kwanza, barabara, maji, kuna visima vilichimbwa vya gharama kubwa sana pale, shule, zahanati hivyo vyote viwe vitu vya kwanza vitangulie kule wanakohamia wananchi kuwe na mashule, kuwe na visima vya maji. Kwa kifupi, miundombinu ipelekwe kule tunakowahamishia Watanzania hao wazalendo, walioamua kuiunga mkono Serikali yao, wahame kwenye maeneo yao ya asili. Kwa masikitiko makubwa, wawaache wapendwa wao waliolala kwenye makaburi, wahamie maeneo hayo ili kulinda maliasili ya nchi yetu. Hayo ndiyo makubaliano.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika kipindi kile, Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa John Mwakipesile alishangaa sana kutuona Waheshimiwa Wabunge wote tumekwenda, tukasema usishtuke, tumekuja kukuunga mkono. Tunataka hao wananchi wahame kwenye maeneo ili kufungua *corridor* ya utalii upande wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu, tunapozungumzia maendeleo, maendeleo lazima yawe ni ya watu. Eneo hili nililolitaja ni eneo la Mheshimiwa Estherina Kilasi. Matukio makubwa matatu yamemkuta. Kwanza, wametaifisha mashamba makubwa ya mpunga ya Kapunga na Mbarali. Pili, tunawaondoa wananchi katika vijiji saba, kijiji kimoja kule kwetu hakipungui watu 16,000, 17,000. Matukio hayo yanatokea katika muda mfupi. Ninamwonea huruma sana! Jana alivyokuwa anachangia alikuwa anatamani kulia kwa sababu ya mzigo aliotwishwa ni mzito mno! Jamani na huyu ndiye dada yetu pekee tuliyenaye wenzenu wa Jimbo. Tusingependa tumpoteze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme, pamoja na lile la kuwaondoa wafugaji kutoka Ihefu, yote hayo yanamkumba na wapiga kura wote wanaondoka pamoja na matatizo yote. Lakini hili la mwisho la kuhamisha vijiji saba ndiyo limetuletea simanzi na kero ya hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niliseme hili na Serikali isikie kama tuliamua kuiona Ihefu ni suala la Kitaifa kwa nini tunapowahamisha wale wananachi wa vijiji saba tusilione ni la Kitaifa. Mimi nilitarajia kwamba Serikali hapa ingekuwa *proactive* ikasema vikosi vyake vya Jeshi, vikosi vyake vya Magereza hebu nendeni kwenye maeneo yale ambapo wanahamia wananchi hao wawatengenezee shule zao, wawatengeneze visima vyao vya maji, wawatengeneze zahanati wananchi hao wahamie. (*Makofi*)

Ninasema ukiwaona wananchi hao na zile kambi za wakimbizi tunazozungumza kule Muyowosi na wapi wale wana nafuu kuliko hao. Tunawafanya wananchi wanakuwa wakimbizi ndani ya nchi yao wenyewe. Inatia simanzi na uchungu. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, nasema Mheshimiwa Estherina Kilasi ana moyo mgumu sana, maana hata familia yake baba na mama na wajomba na shangazi na wenyewe wameondoka, angalau yeye ana nafuu kimapato. Lakini wale Watanzania wamekusanyika mahali ambapo hakuna vyoo, watoto wa shule Mheshimiwa Waziri Mkuu toka mwezi Agosti, 2007 wengine hawasomi na mnajua wale wanakuwa kama *stray animals* na watakuwa *vulnerable* kwa mimba maana hawana shughuli ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingekwenda pale ikasema *intervention* yake ni kuwasaidia hawa, kwa nini mnawafanya watu wanasikitika na kulalamika na kulia bila sababu? Tukiacha wale ambao ng'ombe zao zilikuwa zinakufa kila njia, mimi nilibahatika kupita katika ile njia ya Songea kwenda Namtumbo mpaka Tunduru, mizoga mitupu njia nzima na wengine walikuwa wananyang'anywa na wenyeji wanachukua ndama! Yote hayo wamevumilia na kwa hili waende wapi sasa hawa? Walijenga shule zao, sasa kitu cha kushangaza mnaiachia *TANAPA*, *TANAPA* inajitahidi, lakini *TANAPA* sio Serikali. Tunataka kuona *intervention* ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hebu fikiria Msangaji wamejenga shule kwa gharama ya shilingi milioni karibu 400, fidia waliyopewa shilingi milioni 17. Zahanati waliyojenga ni karibu shilingi milioni 120, fidia waliyopewa shilingi milioni mbili. Hii shilingi milioni mbili hata choo itajenga kweli! Kwa nini tunawafikisha wananchi mahali hapo? Ilikuwa ni suala la kujipanga. Wako wapi wale watu zamani ambao walijua hili la vijiji saba ni vijana wetu wa *JKT* na wapi wanakaa, wanapiga kambi zinatengenezwa. Fedha ndogo hizo ambazo zipo *TANAPA* na zipo wapi, zingetosha kuwalisha wanajeshi wetu na wananchi wasingekuwa na malalamiko, wangepata shule zao, wangepata visima, wangepata amani na makanisa yangejengwa, misikiti ingekuwepo, wangemtukuza Mungu na kipato kingeongezeka. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Safi sana.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu ahsante sana. Kwa kweli kwa mimi ninayekaa hapa kwa muda wote, michango ya leo ni bomba kweli kweli! Ahsante sana. Tunakwenda sasa kwa Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda na tutamaliza na Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw'.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia nampongeze sana Mheshimiwa Benson Mpesya, jirani hapa, alivyozungumzia tatizo la Ihefu kwa sababu na mimi watu wangu, Wabena wenzangu, walikuwa pale wameteseka sana halafu wamenyang'anywa mashamba. Kwa kweli amenisemea na Wabena wenzangu kule wananisikia.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kumpongeza Mheshimiwa Mpesya, nawapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Naibu wake mdogo wetu Mheshimiwa Ezekiel Maige na Katibu Mkuu ambaye tunatoka sehemu moja, Blandina

Nyoni Mjomba wetu na watendaji wote wa Wizara. Vilevile, nichukue nafasi ya kipekee kuwashukuru Mawaziri waliopita wa Wizara ya Maliasili na Utalii na Katibu Mkuu Kiongozi Bwana Luhanjo aliyekuwa pale.

Mheshimiwa Spika, wakati nasoma hiki kitabu, kwa kweli wamejitahidi kutengeneza vizuri. Lakini ninachoelewa ni *theory*. Lakini *practically*, mambo hayako hivi. Mimi niseme kwamba hela zinaonekana zinapatikana nyingi, lakini hazina *impact* kwa wananchi. Wenzangu wamezungumza suala la uzalendo, lakini kwa kweli sisi uzalendo ni mdogo sana. Mimi nilikuwa naangalia maeneo ambayo utalii upo. Utalii kwa haraka haraka upo maeneo ya Kaskazini (*Northern Wildlife Areas*) tukimaanisha Arusha kidogo na Mwanza, halafu kuna Jiji la Dar es Salaam.

Halafu kuna visiwa vya Zanzibar kwamba kuna utalii. Kwa bahati nilipita kule Zanzibar, mahoteli ni mazuri sana. Lakini nikiangalia wazalendo waliowekeza pale, yaani Wapemba au Wazanzibar ambao wanawekeza pale, nimeona waliowekeza pale karibu ni ngozi nyeupe kabisa. Sasa wale wazalendo wa pale hata kazi za ufagizi zenyewe hazipo pale. Sasa tutasema ni uzalendo huo!

Mheshimiwa Spika, lingine, nizungumze suala la chanzo cha watalii. Chanzo cha watalii kwa haraka haraka wanatoka sehemu za Ulaya, wanatoka sehemu za Amerika Kaskazini. Lakini najiuliza, kwa nini kuna sehemu nyingine kama Asia, Korea, Japan, naona kule watalii hawatoki wengi sana. Sasa najiuliza, tatizo ni nini? Bahati nzuri nilikwenda kule Japan, tatizo kubwa nafikiria ni usafiri kwamba safari ya kutoka Ulaya kuja Dar es Salaam *Airport* ni rahisi sana kwa ndege. Safari ya kutoka Canada kwenda Ulaya kuja Dar es Salaam ni rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini safari ya kutoka Japan naona kuna tatizo sana la usafiri. Lakini hata hivyo ukitaka kuangalia, ukipiga mahesabu, wenzangu wameeleza, kwa nini huku Kusini kabisa tumesahaulika, utalii haupo? Sababu zipo za msingi, kama miundombinu, barabara za lami hazipo, viwanja vya ndege hatuviboreshi. Kwa mfano, pale Ilembula kuna kiwanja kizuri tu cha ndege. Yaani tungetengeneza ule uwanja wa ndege pale Ilembula ungesaidiana na uwanja wa Songwe Mbeya.

Kwa hiyo, mtalii akitoka Dar es Salaam anapanda ndege anashuka pale Ilembula *Airport*, ni rahisi kwenda hata Songwe, ni rahisi hata kwenda sehemu nyingine. Sasa ukiangalia usafiri wa kutoka Ulaya kwenda Dar es Salaam - *Airport* ni masaa nane, usafiri wa kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya ambayo ni jirani zangu, pale ni masaa 12. Gari likienda haraka sana ambalo linaweza likasababisha ajali ni masaa 11. Sasa mtalii gani aanze kusumbuka asitumie ndege aende kwa barabara ambazo tena zina mashimo? Lazima tujiulize sana. Kwa hiyo, nilichokuwa nazungumza hapa, hoja ni kwamba tuimarishe viwanja vyetu vya ndege, tuimarishe barabara zetu miundombinu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuchangia ni upande wa wawekezaji. Utalii ni utajiri. Ni muhimu Watanzania wakapewa kipaumbele uwekezaji uwe 50% *sharing*. Maeneo yapo ya kuwekeza, Kusini, wapewe Watanzania. Lingine huko *National Park* sasa hivi zaidi ya asilimia 80 ya wawekezaji ni watu wa nje. Hii ni hatari kiuchumi na kisiasa. Ni kweli tunafurahia sana wawekezaji wengi, lakini Watanzania wengi

wanakuwa watazamaji kama wakiangalia kama kombe hili tunaliangalia la mpira. Kwa hiyo na Watanzania katika huu uwekezaji ndiyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma kwenye vitabu vyangu, kuna mtafiti mmoja alisema kwamba kama tungewekeza vizuri, ukiwekeza kama milioni moja unaweza ukapata 1.8 yaani unapata Sh. 1,800,000/= yaani kama mara mbili hivi. Lakini sasa kwa Tanzania hatufanyi hivyo! Sehemu nyingine zipo *under utilized*, zipo chini sana. Kama tunawekeza, basi tunawakaribisha wageni ndiyo wanachukua utajiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, lingine, nizungumze kuhusu hizi *package tours*. Hizi *package tours* sehemu kubwa, hawa wenzetu wanakuja huku kwenye utalii, sehemu kubwa wanalipia malipo yote nje. Kwa hiyo, wanakuja hapa hawana hela, hela zetu wanalipa kwa hela za kigeni. Sasa uzalendo, mimi nasema hivi kwamba ni vizuri tubadilike kwamba sawa watalipia kule lakini tuangalie: Je, Wizara ya Maliasili na Utalii ina uhakiki vipi kuhusu suala la *package tours*? Je, wananchi wa kawaida wanafaidikaje? Kwa sababu inaweza ikawa tunasema tunapata hela nyingi, lakini wanaofaidika ni watu wa nje, watu wetu wanateseka sana. Kwa hiyo, hilo nalo nafikiri tuliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumze kuhusu suala la kule Jimboni kwangu. Kule Jimboni kwangu Njombe Magharibi, sasa hivi wanasikiliza wanasema Mbunge wao Yono anasemaje? Kuna kilio kikubwa sana kule, kuna suala la kuhamishwa. Wanahamishwa mpaka Kipengele, Mpanga *Game Reserve*, watu tulipokuja walishangilia sana. Lakini sasa hivi ni mzigo mkubwa sana kwa maana ya kwamba wananchi wanatishiwa. Unaona watu wanapita wanaweka kama wana hesabu wanaweka alama, watu wa Malangali wanapata shida sana. Watu wa pale Mpanga Mpya walihamishwa na bado wanaambiwa kwamba watahamishwa tena.

Sasa watu wa Luduga wanapata shida sana, wanakuwa na wasiwasi. Wanakuwa kama watumwa kwenye nchi yao. Sasa kwa vile wananisikiliza hapa, kwa kweli naomba Wizara ijaribu kuliangalia. Wenzangu walikuwa wanaomba kwamba Waziri waongozane naye ili waangalie kilio cha wananchi wa kule. Kwa sababu sasa hivi imegeuka kama siasa kwamba watu wakimbilie kwenye vyama vingine, lakini ukweli watu wanateseka sana, wanatishwa tishwa. Halafu mbaya zaidi ni kama walitapeliwa, waliambiwa kwamba wahame watajengewa zahanati, watajengewa barabara nzuri, shule zitajengwa pale, maji yataletwa, pale itakuwa kama Ulaya ndogo, lakini siyo kweli. Sasa hivi kwa kweli watu wametelekezwa pale. Halafu mbaya zaidi wanasema ile mipaka waliyohama, tena wanataka warudishiwe, sijui nini! Kwa kweli hilo Serikali iliangalie, wananchi kwa kweli wamenituma wanalalamika hawataki kabisa wanaona kwamba wanaonewa sana.

Mheshimiwa Spika, halafu mbaya zaidi, kule hakuna wanyama, sasa labda Serikali, Wizara inayohusika inieleze ni lini wanapeleka kule Simba, lini watapeleka Twiga, lini watapeleka pale sijui wanyama ambao wanaweza wakawezesha watalii wakafika pale. Kwa sababu wanyama pale hawapo. Nashauri kwamba ingewezekana badala ya kuwasumbua wananchi tuanze kupanda miti pale. Watu wanapata shida sana, wana wasiwasi, wanakuwa watumwa kwenye nchi yao. Tunafurahi wanyama ambao ni wa kuhesabu, pale pana digidigi, vipaa vidogo vidogo. Sasa wananchi ambao wana uhai

wanasumbuliwa. Sasa mimi sielewi mnataka watu waende wapi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara kwa kweli isiwasumbue wananchi, waende pale, twende na Waziri tuwaeleze kwamba hilo tatizo halipo, hawatahamishwa tena. Wamehamishwa mara ya kwanza, inatosha. Sasa hivi waendeleo na shughuli zao za kilimo kusiwe na tatizo kabisa.

Mheshimiwa Spika, lingine, nataka niwatete watumishi walioko pale Ilembula. Kulikuwa kuna nyumba zinajengwa pale Wanging'ombe za Mpanga Kipengele *Game Reserve*, zile nyumba zimetelekezwa haziishi, wanafanya kazi pale, wako wachache sana. Yule meneja anafanya kazi nzuri sana Bwana Hamis, lakini mazingira ambayo anaya-face pale, hana ofisi nzuri, hana wafanya kazi wa kutosha, hana gari nzuri, maisha ni taabu, anafanya kazi vizuri sana. Lakini aangaliwe, pale, zile nyumba wazimalize mapema, tena wapeleke umeme pale kwa sababu umeme upo pale Wanging'ombe Sekondari. Lakini Kijiji cha Wanging'ombe, pale umeme haujapelekwa. Zamani kulikuwa kuna tatizo la *transforma*. *Transforma* iko pale, sasa kuna sababu gani umeme usipelekwe pale Wanging'ombe au tuseme nalo ni tatizo la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba sana, Wizara inayohusika ya Maliasili na Utalii iangalie ipeleke umeme pale Wanging'ombe na zile nyumba ziishe mapema, wale watumishi wasipate taabu, wasipange, wanatutulia aibu sana. Kwa kweli naomba sana Wizara ikamilishe yale majengo.

Mheshimiwa Spika, lingine niseme kuhusu suala la utalii, nasema utalii mwenzangu Malangalila alizungumza utalii kwa sababu huyu tunapakana kule Njombe Magharibi na Idenyimambe Mufindi. Utalii pale upo, Saja pale barabara hazipitiki sasa utasemeje kuna utalii? Idenimembe pale hali ni mbaya.

Sasa Wizara inayohusika waongee na Wizara ya Miundombinu wale Idenyimambe na lile daraja litengenezwe liunganishwe kati ya Malangali, Mufindi na Njombe ili watu wanapokwenda Makambako iwe ni rahisi. Wamedanganywa kidogo kwamba inajengwa barabara kutoka Idofi kwenda Saja, lakini barabara imeishia pale Igomba Shule ya Msingi na hiyo barabara siyo nzuri, ni nyembamba, ni mateso matupu! Inawezekana Halmashauri haina hela, basi ni vizuri *TANROADS* waingilie kati. Wananchi wa pale, suala la utalii pale Saja ingekuwa ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie kuhusu suala la *Five Stars*. Tunazungumza kwamba utalii Kusini hakuna, lakini tuulize: Je, *Five Stars* zipo kule? Nashukuru kwa Mikoa ya Kusini, kuna mwekezaji mzalendo anataka kuweka *Five Stars* pale Iringa Mjini *Peacork Hotel*, lakini naye alitaka kuwekewa mizengwe kibao. Tumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa pale, alileta *RCC* kwa kweli tunashukuru kwamba *Five Stars* inajengwa katikati ya mji pale na *Five Stars* huwa hazijengwi nje ya Mji kwa sababu lazima watalii tuwaangalie usalama wao. Kwa hiyo, tukijenga *Five Stars*. Hata wenzetu wa Mbeya watatumia *Five Stars*, wa pale na Rukwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kule. Kwa hiyo, wakifikia pale watakuja na ndege na uwanja wa Nduli ule naelewa utaimarishwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nalo nilitaka nilizungumzie kwamba *Five Stars* zinatakiwa zijengwe kwenye maeneo husika. Kwa kuanzia, hiyo *Five Stars* inaweza ika-*save* Mikoa kama minne ya Kusini Ruvuma, Mbeya na Iringa.

Mheshimiwa Spika, lingine nilitaka nizungumzie kuhusu suala la Utalii wa Mazingira. Kule Imalilo, Wangama, Kipengele kuna utalii wa mazingira, kuna hali ya hewa kama Ulaya, baridi sana. Sasa naipongeza sana Halmashauri ya Njombe, imekumbuka kutengeneza barabara ya Wangama kwenda Imalilo karibu shilingi milioni 300 zimetumika pale. Kwa hiyo, usafiri wa kwenda kupeleka watalii kwenye maeneo ya mandhari ya Kipengele itasaidia sana. Kwa hilo ninaipongeza sana Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ila tunachoomba ni uwezekano wa kuwekeza pale viwanda vidogo vidogo. Kwa sababu pale pana ulanzi mzuri kabisa, tukiweka kiwanda cha ulanzi pale itakuwa ni *tourist* nzuri kabisa. Sasa watu wanacheka, lakini kwa kweli ile ni *juice!* (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, utalii ni pamoja na vinywaji na vyakula. Kwa hiyo, naipongeza Serikali na mwisho niseme naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yono, wamesikia na watakuja huko. Namwita sasa Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda. Hayupo, ooh! Basi nadhani Mheshimiwa Omar Kwaangw' upo tayari?

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Nipo tayari.

**SPIKA:** Tafadhali!

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwanza, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango kidogo juu ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kwa niaba ya wananchi wa Babati Mjini, naomba niungane na wenzangu wengine katika kutoa pole na rambirambi kutokana na ajali ambayo wataalamu wa Wizara hii walipata. Kukosa wataalamu kwa njia hii ni pigo kubwa kwa Wizara kwa sababu kumtayarisha mtaalamu mwingine au kupata wengine itatumia muda mwingi sana, basi tumwombe Mwenyezi Mungu alaze roho zao pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, mengi yamekwishasemwa na mimi niwatakie Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wenzake wote ufanisi katika kazi yao na nawatakia kila la kheri.

Naomba tu nianze na mambo machache kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwenye kitabu cha hotuba ukurasa ule wa 17 kwa ruhusa yako Mheshimiwa Waziri amezungumza suala la kuongezeka kwa watalii na mimi nawapongeza sana na kwamba

watalii zaidi ya laki sita, kwa kweli wametembelea nchi yetu katika kipindi kilichopita na kwamba hii ni kama asilimia 10.8 ya ongezeko ya kipindi kilichopita. Tunawapongeza kwa juhudi hiyo na kwa ongezeko hilo japo ni dogo, lakini vile vile kwa kukusanya karibu shilingi bilioni 61.7 ambayo ni ongezeko la asilimia 6.1, tunawapa hongera.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na wenzangu wengine waliosema badala ya kurudiarudia kwamba bado kabisa utalii nchi nyingi ukisafiri bado hawajui Tanzania, bado wanauliza Tanzania iko wapi? Sasa nilidhani ni vizuri tujitahidi tutengeneze vipeperushi vya kutosha, watu wanaposafiri hata Wabunge wanasafiri sana, wapeni vipeperushi waende kule, wanakutana na watu mbalimbali watangaze utalii wa Tanzania na wasafiri ni wengi sana kutoka nchi yetu. Hii itakuwa namna nyingine au itakuwa njia tofauti najua mnamtuambia Balozi zetu na maeneo mengine, lakini nadhani ni vizuri kwa kweli tuone hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limesemwa na mimi sitaki kulirudia ni lile la kuuza huduma zetu za utalii kwa dola. Nadhani limesemewa vizuri, sina sababu kwa kweli, ni vizuri ushauri uliotolewa uzingatiwe sana. Kwa sababu yamesemwa mengi mazuri na mimi naungana na yale mazito yaliyokwishasemwa, basi naomba nirudi kwenye mambo ambayo pengine yanahusu katika maeneo tunakotoka au katika maeneo mengine mambo yanayofanana.

Mheshimiwa Spika, moja, nianze pengine na takwimu. Hapa limezungumzwa suala la asilimia 25 la pato linalotokana na uwindani wa Kitalii. Katika miaka iliyopita, tulikuwa tunapata takwimu kwenye hotuba ya Waziri, huku nyuma kwenye kitabu tunapata takwimu ambazo ziko humu, kuna takwimu za kimkoa tu ambazo zinaonyesha mambo ya kupanda miti, makusanyo ya maduhuli, ziara za maonyesho, idadi ya watalii na kadhalika. Lakini tungependa kuona takwimu vile vile za asilimia 25 ya pato ambalo Wilaya zetu zinapewa. Kwa kawaida tunapata takwimu hizi, tena zinaandikwa kwa dola. Kwa miaka iliyopita ilikuwa inawekwa kwenye kitabu cha Waziri. Naomba takwimu hizo ziwekwe. Ni muhimu sana, kwa sababu tungependa na sisi kujua kwamba fedha hizi zinapokuja kule Wilayani zinafanya nini na tuweze kuzifuatilia, tunaomba hizi takwimu hizi ziwekwe.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ninahitaji takwimu vile vile ni suala la ujirani mwema, nataka nipongeze hifadhi za Taifa kwa kutenga asilimia 7.5 mpaka karibu 10 ya bajeti yao kwa ujirani mwema. Kipindi kilichopita wametuonyesha hapa shilingi bilioni 3.7 na vile vile shilingi bilioni 2.8 kwenye miradi ya maendeleo sasa vile vile tungependa kupata takwimu, kwenye ujirani mwema, Wilaya zipi zimepata nini, nini wamejengewa. Kama ni zahanati, kama ni shule, tupate hizi takwimu ili tuweze kujua. Kwa hiyo, tunaomba hizo takwimu, hilo litakuwa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nihamie tu kwenye eneo lingine ambalo limesemewa na Wabunge wengi sana ni tatizo hili la wanyama waharibifu, wanyama ambao wanaharibu mazao ya wananchi. Tumesikia habari ya tembo na kule kwangu tembo ni wengi sana. Ukitaka kujua tembo wengi wako wapi katika nchi hii, wewe nenda pale Tarangire, utakuta tembo ni wengi sana. Ni hifadhi ambayo ina tembo wengi sana.

Samahani, wale ambao wataona tembo sio jina sahihi, lakini basi wanisamehe kwa sababu halijabadilishwa hilo jina.

Mheshimiwa Spika, tumesikia vile vile habari ya simba na habari ya mamba. Sasa naomba vile vile basi na mimi niseme habari ya viboko ndani ya Ziwa Babati. Ziwa Babati ni ziwa ambalo kwa kweli ukubwa wake lina kilomita za mraba 18. Sio ziwa kubwa sana, lakini ziwa muhimu kwa sababu kuna rasilimali za asili ambazo tunazitumia pale. Kuna samaki, kuna perege, kuna kambale, kamba maji na wengine vile vile kuna ndege, kuna maeneo ambayo vile vile na mfumo wa bioanuwai pamoja na hao viboko. Sasa tunalo tatizo kubwa sana. Viboko kwa historia ya Ziwa Babati wameanza kuingia kwenye ziwa mwaka 1930 wakitokea kwenye maeneo ya Mto Bubu pamoja na Ziwa Manyara. Idadi yao sasa imefikia viboko 400 kwa ziwa dogo kama lile. Kwa vyote vyote vile usalama wa raia na matatizo ya wananchi kujeruhiwa sasa ndiyo yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, sisi kwa kawaida huwa tunafunga ziwa Januari mpaka Juni, halafu tunafungua Julai mpaka Desemba kwa ajili ya wananchi kwenda kujipatia vitoweo na vile vile kwa ajili ya kujiongezea vipato. Sasa viboko hawa 400 kama nilivyosema, kwa vyotevyote vile sasa wameongezeka.

Kwa hiyo, watakuwa na matatizo ya malisho ndani, wanatoka ndani ya ziwa wanakwenda kutafuta malisho nje kando kando ya ziwa na hata wakati mwingine kwenda kwenye mashamba ya wananchi mbali zaidi kabisa kutoka ziwani. Vile vile mfumo wa viboko, viboko dume kwa kawaida wana *tendency* ya kuwa na kundi la majike. Sasa wanapokutana na madume wengine huwa wanapigana. Kwa hiyo, wanajeruhiwa, wakijeruhiwa wanakuwa wakali sana. Kwa hiyo, ni tabia ya viboko.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimejitokeza pale Babati, yako matukio ya vifo ambayo kwa kweli sasa vimeongezeka sana. Muda mfupi katika kipindi kifupi tu wiki iliyopita kwa masikitiko, wako vijana wawili ambao walikwenda kujitafutia riziki kwenye ziwa hilo na ni jirani zangu kabisa kwenye kijiji cha Singe, bahati mbaya mtumbwi wao ulipinduliwa na kiboko, mmoja aliweza kuogelea akasalimika lakini amejeruhiwa, lakini mwingine kwa kweli alipoteza maisha. Kijana aliyepoteza maisha anaitwa Hamisi Juma Sinda. Naomba nitumie nafasi hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi vile vile wa Babati, nitoe pole pamoja na rambirambi kwa familia ya kijana huyo na Mungu ailaze roho yake pema peponi. *Amina*

Mheshimiwa Spika, kijana huyo alikwenda kutafuta riziki pamoja na mwenzake na huyu mwenzake kwa kweli ambaye amejeruhiwa jina lake anaitwa Karim Hassan Senge. Vile vile, namtakia kila la kheri aweze kupona ili aweze kuendelea na harakati za kujitafutia maisha. Ni tatizo! Tatizo hili la viboko Halmashauri ya Mji imefanya juhudi, tumepata kibali cha kuajiri Afisa Wanyamapori, lakini kwa bahati mbaya sana katika ajira hii kwa taarifa nilizonazo imetangazwa karibu mara mbili kwenye gazeti la Majira tarehe 15 Februari, 2008 tumetangaza ajira hii, hakupatikana mtu. Tarehe 6 Aprili, 2008 imetangazwa hakupatikana mtu. Sasa kwa kweli tunaomba Wizara mtusaidie

hawapatikani hawa Maafisa Wanyamapori na viboko wale sasa wamekuwa wengi, tunahitaji kuwa na Afisa Wanyamapori ili wapunguzwe.

Kule kwetu kwa kawaida kama heshima ya mtu ni kuwa na ng'ombe wengi, lakini lazima ifike mahali uweze kuwapunguza. Sasa Serikali punguzeni hawa viboko kwenye Ziwa Babati. Ziwa lile ni dogo, viboko hawa wamekuwa wengi sana. Wataalamu wanakisia wako 400, lakini pengine ungeniambia mimi mtu wa kawaida ambalo nafahamu ziwa lile, wako zaidi ya hao pengine. Sasa ni hatari sana. Wanatoka na unakutana nao mara nyingi mjini.

Hata mimi nimekutana nao wakati narudi kwenda kijijini, inabidi usimame uwapishe wanatembea mjini wakati mwingine. Ni hatari na sasa wameshasababisha vifo vya watu na sasa hivi ni mmoja hapa wiki iliyopita, lakini katika kipindi cha nyuma mmoja aliuawa kwa kweli kwa namna ambayo sio vizuri, maana walimchanachana kabisa na wengine wamejeruhiwa. Kwa hiyo, ni matatizo kwa kweli. Ombi langu lilikuwa ni hilo kwamba Wizara itusaidie, hatuna Afisa Wanyamapori na tunaomba kwa kweli hatua za kupunguza ziweze kufanyika. Hao viboko ambao inasemekana idadi yao wako 400 ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, basi kwa dakika zilizobaki tano hizi nitumie nafasi hii kueleza machache juu ya migogoro kati ya wananchi na Hifadhi za Taifa. Tumesikia hapa migogoro mingi kweli kweli, vijiji vinavyopakana na hifadhi, mimi nadhani migogoro hii Wizara naomba turudi kwenye historia, tutafute historia ya migogoro hii ni nini. Mimi nimekuwa Mbunge pale Babati Mashariki kwa miaka 10, migogoro tuliiona, lakini wakati mwingine vijiji vimeishi pamoja na hifadhi kwa miaka mingi bila migogoro, kwa nini inajitokeza leo?

Hifadhi ya Tarangire kwa mfano ilianzishwa kwa *GN* mwaka 1970, lakini kwa nini migogoro inatokea katika miaka hii. Ni moja tu, tatizo ni baada ya *GN* kuanzisha hifadhi kilichotakiwa ramani ya hifadhi ingechorwa. Sasa tatizo, ramani hizi hazikuchorwa mapema, mimi nafahamu sana utaratibu huu kwa sababu muda hautoshi, sina muda wa kueleza kwamba matatizo yalikuwaje kwa sababu nimetembelea sana maeneo haya, nafahamu matatizo yaliyoko kwenye Kata zile za Mamire na Galapo, kijiji cha Gijedabung kwa mfano Kata ya Mamire, Ayamango, Galapo na Gedimar wamepata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna migogoro kati ya vijiji hivi na hifadhi na katika ukanda ule mzima. Migogoro iko mingi tu! Turudi kwenye historia tukumbuke kwamba Serikali mwaka 1974/1975 vile vile iliweka vijiji kwenye maeneo ambako wanyama wapo kwenye maeneo ya hifadhi na vijiji vikachorwa. Kwa Babati, kwa mfano ramani zote za vijiji vya Babati ilichorwa kwa kutumia picha ya ndege. Zipo na vijiji vimepewa hati, sasa unakuta hati juu ya hati. Kwa hiyo, ni lazima vile vile Serikali ione kwamba hifadhi zilichelewa kuchora hizi ramani na vijiji vikagawa kabisa maeneo yale ikawapa watu kihalali. Sasa tunapowaondoa bila ya kuwa na utaratibu na kuzua migogoro, jambo hili sio zuri na hakuna sababu ya kugombana na wananchi. Hebu tukae chini. Kama



tunategeneza muafaka kwenye vyama inashindikana nini muafaka katika migogoro ya wananchi na Hifadhi za Taifa na hifadhi ni zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kumshauri Mheshimiwa Waziri, aunde timu ambayo itakuja izungumze na wananchi juu ya migogoro hii na nafahamu hifadhi wamekuwa wakiwasiliana. Lakini wakati mwingine unawasiliana na watendaji au Mkuu wa Wilaya peke yake, jamani eeh, dhamana ya ardhi ipo kwa Halmashauri za Wilaya tusiishie tu kwa watendaji, twende kwa wananchi, kuna vyombo vyao Serikali za Vijiji kuna Halmashauri za Wilaya, twende huko hebu tukae na sisi wengine tupo ambao tunafahamu matatizo hayo kwa muda mrefu sana. Tusigombane kwa ajili ya kutunza hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kweli ikitokea kwamba watu hawaeleواني, basi lazima utafutwe utaratibu, lakini ni vizuri kwanza tuanze mazungumzo, majadiliano halafu tufike mahali tuseme tumekubaliana kutokukubaliana. Hapo itaeleweka nini kinafanyika. Lakini yasiwe mazungumzo ya upande mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri, tafadhali kabla ya maamuzi yoyote hata kabla hujaleta jambo lolote katika kupanua hifadhi, tafadhali sana hakikisha kwamba Serikali za vijiji na wananchi wao wamearifiwa vizuri na Halmashauri ya Wilaya Madiwani wamezungumza halafu ndio ije Wizarani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nitumie nafasi hii kumtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na sisi tuko tayari. Tunajua sasa hivi kuna kesi ambazo wananchi wamepeleka Mahakamani na kadhalika, lakini tuma watu tukae kwa pamoja tuelewane tuondoe migogoro kati ya wananchi na Hifadhi za Taifa badala ya kufukuzana kila siku. Kwa sababu wananchi hawa wamewekwa na Serikali za Vijiji, mimi sisemei wale ambao wamevamia wenyewe mmoja mmoja, hapana, hawa waliowekwa na Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Omar Kwaangw'. Kwa bahati njema naona Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda ameingia, kwa hiyo nampa nafasi yake na naona atakuwa ndiyo msemaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Samahani *I am still catching my breath* kidogo, ilibidi nikimbie, nilikuwa hospitali tangu asubuhi ndiyo maana kidogo nimechelewa. Lakini nakushukuru sana kwa kunipa nafasi japo kwa dakika chache zilizobaki ili na mimi nitoe mchango wangu kuhusiana na hoja iliyopo mbele yetu.

Awali ya yote, naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Wizara hii - Mheshimiwa Shamsa Mwangunga ambaye mimi namwita kama *aunt* yangu. Lakini nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, maana tangu Bwana Maige amechaguliwa kuwa Waziri, nimekuwa nikipata pongezi nyingi sana za kuwa na mimi ni Waziri. Kwa hiyo, labda ndiyo Baraza zenyewe za baadaye. Nawapongezeni sana

kutokana na hotuba ambayo mmeiandaa kwa umakini mkiangalia zaidi faida au maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali yangu, nadhani nitakuwa *very brief*, lakini nitajitahidi nieleweke na niwe kidogo nikitoa maelezo ya ufasaha. Pamoja na kuwa Mbunge wa kuteuliwa ninayetoka Mkoa wa Mbeya, lakini nataka kuligusia, nina hakika linagusa Taifa letu kiujumla.

Mheshimiwa Spika, unapokwenda nchi za nje na mimi kwa bahati nzuri nilishawahi kufanya kazi kwenye *industry* ya *tourism* nikiwa kama mtu wa mauzo. Lakini kila unapopita katika matangazo utasikia Serengeti, Manyara na mbuga zile kubwa kubwa. Ingawa sasa hivi sio Waziri, lakini naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu Naibu Waziri aliyepita - Mheshimiwa sana Zabein Mhita.

Nakumbuka mwaka jana tulipata nafasi ya kufuatana naye na Naibu Waziri mwingine - Mheshimiwa Mwananzila nikaweza kujionea mbuga ya Kitulo ambayo niliona aibu, maana yake mimi mwenyewe niko jirani pale pale Mbeya, lakini nilijifunza kitu cha ajabu sana. Kama Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka tulitoka kwenye *TV* tukiimba wimbo wa Taifa tulikuwa tumeshika viuaviua hivi, mwaka jana tukachekesha kidogo, lakini *the message was sent*.

Mheshimiwa Spika, Mbuga ya Kitulo ni mbuga nzuri sana. Ziko mbuga za namna hii nyingi, lakini hazipati *promotion* inayostahili. Ukienda pale, kuna mandhari nzuri sana. Utalii wa pale ni maua na ndege, wageni kweli kutoka nchi za nje wengi wao hawafahamu. Kwa hiyo, ninachokiomba, huo ulikuwa mwanzo mzuri. Tulikwenda Wabunge na baadhi ya viongozi wa Maliasili na Utalii kutoka Mkoa wa Mbeya pale, tulijifunza mengi sana. Mimi sikujua kama maua yanaweza yakafaa kwa utalii, sikujua kama watu wanaweza wakaenda wakakaa wakaangalia ndege tu. Lakini nikaona *there is so much richness, so much wealth, in terms of tourism* ambayo nchi inaweza ika-offer. Lakini *promotion* imekuwa ni zile zile mbuga tulizozioea.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara hii, bado tunaweza kukajitengenezea mapato makubwa na kina Mheshimiwa Kimaro mnalisikia hili, nyinyi wadau, akina Ndesamburo na kadhalika hebu shirikianeni na Wizara hii tuone hizi mbuga ambazo zina utalii tusiozoea zikinyanyuka kwa namna moja ama nyingine. Tafadhalini sana, ombi langu kubwa sana, pamoja na kuwa mwanasiasa na Mbunge, pia kidogo najishughulisha katika mapato madogo kwa maana ya biashara kidogo kwa siku za nyuma ingawa sasa hatujui huko baadaye itakuwaje, tutaendelea kufanya biashara au vipi. Nilichojifunza, hasa katika nchi zile za Uarabuni, mfano Dubai pale au Saudi Arabia, ukienda *Qatar* pale Doha hao wenzetu ukiongea nao wamegundua kuna uwezekano sasa au niseme ziko *challenges* zinazo-challenge vyanzo vyao vya mapato.

Wenzetu msingi wao mkubwa wa mapato umekuwa ni suala la mafuta. Lakini wameliona hili sio la milele, hili sio la kudumu. Kwa hiyo, wame-opt *something else* ambao ni utalii. Saudi Arabia wana mji mmoja, wanaujenga, utatumia miaka 15, jina la Mfalme wa Kiarabu, lakini mwishoni limeishia *Economic City*. Niende kujenga mji ambao utashindana na *Washington, London, Newyork City*, ananikumbusha Mheshimiwa

Mbunge. Kwa hiyo, *point* ninayotaka kuweka hapa au nichukulie mfano mwingine kuhusu *Dubai* pale *UAE*. *UAE* wamejenga *Man made Island*, visima vilivyojengwa na wanadamu. Kwa mfano, kuna kile kisiwa kina alama ya mnazi, kina Ndassa mnajua mnasafiri sana nyie. Kuna kisiwa kile kinafanana na ramani ya dunia, lakini yote hii ni kwa ajili ya kuendeleza utalii. Wanajua ipo siku watakwama kwa upande wa vyanzo vya mafuta.

Sasa nikikaa nikiangalia nchi yetu ya Tanzania, wale Waarabu kule pamoja na mimi kuo Mwarabu, lakini lazima niseme tu, nitajibu mwenyewe nyumbani huko. Lakini wale Waarabu kule hawana mbuga za wanyama zaidi ya wale ngamia. Yale majangwa wanaweza wakayatangaza, watu wanakwenda wanafanya *basic tours* na kadhalika. Sisi bahari tunayo, wawekezaji wenye uroho kwa ajili ya kuwekeza kwenye nchi yetu wapo, tumeona kwenye madini. Swali ninaloomba niulize Wizara hii, kwa nini na sisi tusiige mfano huo? Sekta ya utalii tumeifanya kama *by the way sector* tu, ipo tu. Lakini nchi nyingine kama *Mauritius* au *Madagascar* ndio njia pekee ya kupatia mapato, kwa nini sisi hatufanyi hivyo? Tunazo mbuga, tuna visiwa, tuna mito, tuna bahari, ingawa nilikuwa hospitali nilikuwa namfuatilia Mheshimiwa Yono pale amenifundisha leo mpaka Ulanzi tunaweza tukaufanya kwa watalii, sijui kama inawezekana, ndio nimeisikia hiyo leo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *point* yangu nataka niseme ni kwamba, hebu tufikirie upya suala zima la utalii kama njia mojawapo kubwa sana. Bahati mbaya sikupata nafasi ya kuchangia Wizara ya Nishati na Madini, niseme sisi tuna bahati sana, maana bado *oil* yetu hatuja-*explore* na bado utalii hatuja *explore*. *We can still do so much better* kwenye sekta ya utalii.

Mimi nilikuwa naomba hebu kama tuliweza tukatafuta uwekezaji, waka-*invest* kwenye hoteli, kwenye madini na sasa hivi tumefumbuka, tuna Kamati zetu zinatubana kila sehemu, hebu tuwaite tena kwenye sekta hii. Bahari wanayojengea visiwa kule Dubai ni hii hii wanaita *Land reclamations*, wanafanya sana Holland kule, ndio wataalamu. Bado kuna *a lot of potential!*

Tanzania katika dunia ya wenzetu, inatazamika lugha yake ya Kiswahili itanishinda kidogo, labda mtaalamu atanisaidia, inatazamika kama *an exoctic place*, sio ambayo ya kawaida, utapata vitu vya asili zaidi *natural*. Sasa hii ni faida kubwa sana ambayo tunaweza tukaitumia na tukapiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, *Dubai is doing that*, wanajua wataishiwa mafuta, njia pekee wanaweza kujikwamua kama kuna mtu alikuwa anakwenda Dubai miaka miwili iliyopita, akiingia leo hii Dubai ni bora upande daladala wangukuwa nazo. Teksi ni ugomvi, watalii wameongezeka sana *purely* ni kwa sababu ya *promotion* ya *tourism* ni vitu vya kawaida tu. Pana maduka yanayotoka nje kama *NEXT*, *Benans* na kadhalika. Kuna hizi *man made* na kadhalika, hebu tu-*review* hii sekta tunaweza tukafanyaje?

Mheshimiwa Spika, ahadi kuu ya msingi ya Chama cha Mapinduzi na mimi naongea kwa fahari kabisa, nikiwa sauti ya Umoja wa Vijana wa CCM. Ahadi kuu ya

msingi ya Chama cha Mapinduzi ni maisha bora kwa kila Mtanzania. Naomba niwahakikishie Wapinzani marafiki zangu mliomo ndani ya Bunge hili, ahadi ile haijapoteza muda hata kidogo. Hatujapoteza dira bado, tunakwenda vizuri na maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana. Lakini sekta hii tunaweza tukaitumia vizuri sana, akina Aloyce Kimaro hata wale Wapinzani kina Ndesamburo wanajua hili, lakini kuna kitu tumekuwa hatufanyi.

Mheshimiwa Spika, kuna watu hawa tunawaita *tour guides*, sijui Kiswahili chake mtanisaidia kidogo. *Tour guides* mojawapo ya kupata maisha bora kwa kila Mtanzania ni kuongeza kiwango cha ajira kwenye nchi hii. Tutengenezeeni nafasi za kazi kwa kupitia *tour guides*.

Naiomba Wizara kutaneni na wadau wengine, tunao humu Bungeni, majina yao nimeyatajataja, hebu fanyeni *round table, discussion* ya namna gani hii Wizara pia inaweza ikakuza kiwango cha ajira. *Tour Guides* ni *essential* kama daladala wanaweza wakatengeneza wapiga debe, kwa nini sisi tushindwe kuwa na *tour guides* ambao ni *official* kabisa?

Mheshimiwa Spika, kama mtu amekwenda pale *New York* nilikwenda pale mwaka 2006 nikakuta tena Waafrika wenzetu wa Ghana, Wa-Nigeria na kadhalika wanatuongoza mle, wanakatisha tiketi, wanapata *commission*, kuna hizi *tour buses* zimeandaliwa za kuufahamu mji wa *New York* wanapata ajira kwa wingi tu. Wakaniambia, *brother, my brother we are not here to stay, after this we will make money, we go back home.*

Mheshimiwa Spika, hatukai kwa ajili ya *tour guiding*, wale watu wanatengeneza fedha za kwenda kujenga familia zao nyumbani kwao Waafrika wenzetu. Sisi utalii una nafasi kubwa, kwa nini hatutengenezi ajira kwenye *tour guides*. Serikali naomba ifanye changamoto hiyo tuhakikishe tunatengeneza ajira kwenye *tour guides*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali niliyoisema hapo mwanzo ya kiafya niliyonayo, leo nadhani nitakuwa ndani ya muda, naomba Wizara iyapokee hayo machache niliyoweza kuyasema. Leo ningependa niseme zaidi kama ningekiandaa vizuri, lakini *inshallah* Bunge haliishi leo. Naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tom Mwang'onda kwa niaba ya sisi Wabunge wote nakutakia uweze kupata afueni haraka kutokana na hali hiyo ya kukohoa na mafua.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RICHARD MGANGA NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba niwakumbushe ilani yetu hasa kwenye Ibara 34 inayohusika na wanyamapori, misitu na Ibara 112 inayozungumzia Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, bado baadhi ya Idara za Wizara ya Maliasili na Utalii zinalalamikiwa kufuatana na utendaji wao usioridhisha. Bado umangimeza unatawala, hauendani na wakati.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Wanyamapori bado hatujajitangaza vya kutosha, juhudi zifanyike kutangaza hifadhi za wanyamapori wetu. Serengeti itangazwe zaidi kuliko kuangalia zoo zinazotengenezwa na Waarabu kule Dubai. Nawaomba sana changamoto kubwa ni kuhifadhi wanyama waliopo wasitoweke.

Mheshimiwa Spika, siyo vibaya sana kuiga mfano wa Akavango ya Botswana au *Kluger National Park* kwani hifadhi zinafanana na za kwetu. Tukae na tujadili pale Serengeti/Ngorongoro wanyama watamudu vipi kuishi

Mheshimiwa Spika, tishio kubwa ambalo linawakabili wanyama wetu ni la ujangili kwenye hifadhi zetu hasa Ikoma na Ikizu. Kama majangili hayo yataendelea na utaratibu mbaya unaokisiwa wa kuwa zaidi ya wanyama 50,000 kwa mwaka, kwa utaratibu huu tukijipa miaka 10 ijayo tutakuwa hatuna wanyama tena, sisi badala ya kwenda kuangalia au watalii kuja Tanzania, sisi tutakuwa watalii nchi za wenzetu. Lakini tunaweza kwenda Dubai kwenye Zoo za Seng'enge kwenda kuangalia wanyama ambao walikuwa kwenye mbuga zetu. Pia tuangalie namna ya kutokuwabugudhi wanyama hawa kwa kuingiliwa kwa hifadhi, wanyama wakishakosa njia, hawana maji watakufa. Nashauri mbuga/hifadhi zisiingiliwe kisiasa, hii ni kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii, sekta hii bila ubishi hutoa mchango mkubwa kwa uchumi wa Taifa, naomba tusrudi nyuma, tunavyo vivutio vingi, tunazo mandhari za fukwe za bahari, historia na wanyamapori, tunaomba viendelezwe hasa ule Utalii wa fukwe.

Pamoja na mambo mengine, kwa muono wangu, watalii wengi wanapenda sana bahari kuliko wanyama, hii ni kutokana na hali ya hewa ya kwao. Wanataka ngozi za miili yao wakirudi makwao iwe tofauti na wale ambao hawakwenda kwenye fukwe. Tujikite kwenye kuendeleza maeneo ya Pwani. Barabara za mbugani ziimarishwe, gharama za hoteli zetu ziangaliwe, ninalalamikiwa sana, usalama wa watalii ni suala la muhimu. Tukisimamia vizuri sekta hii nina uhakika itaongeza sana pato la Taifa. Pia tukisimamia vizuri hifadhi ya wanyamapori, wanyama wataongezeka kwenye mbuga zetu ili vizazi vijavyo vikute wanyama kama sisi tulivyowakuta.

Mheshimiwa Spika, upandaji miti ni suala la msingi sana. Karibu asilimia 10 ya misitu inapotea kila mwaka, tutawezaje kupanda asilimia 10 ya misitu? Miti mingapi? Vitalu vingapi? Nashauri siku ya upandaji miti isiwe Januari Mosi ya kila mwaka iwe kila msimu wa mvua, iwe vuli, unyevu, kila Mkoa uwe na siku yao ya kupanda miti. Mvua zinatofautiana kila Mkoa. Lakini unapopanda, je, unakatwaje? Labda hili ndilo swali la kujuliza. Pamoja na kwamba umepanda miti wewe, iwepo sheria ya kutokata ovyo miti.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kuona mlima Kilimanjaro kwa mbali, nenda Kenya ukitaka kupanda mlima Kilimanjaro na kuuona kwa karibu zaidi njoo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, nahitaji kueleza utaratibu wa uvunaji wa mazao ya misitu kama mbao kwa wavunaji wadogo wadogo. Imekuwa ni kero kwa wavunaji hawa wanapofuata taratibu zote za kisheria, kulipia, kusajili, kodi zinazostahili na hata sheria Na. 14 pamoja na *Social Support* zote, Wizara hupeleka taarifa Wilayani ya kuzuia uvunaji wa mbao. Wavunaji hawa huwa wameshagharamia kwa ajili ya uvunaji na wakati mwingine hata leseni.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapositisha ghafla wakati wavunaji hawa wameshalipia gharama zote, watarejeshewa gharama zao?

Je, Wizara (idara ya Misitu) itawaruhusu kuvuna msimu ujao au mwingine kwa kutumia gharama hizo walizokwishatoa?

Mheshimiwa Spika, nahitaji maelezo ambayo yatawafariji wavunaji hawa wadogo wadogo waliopoteza fedha zao.

Mheshimiwa Spika, fedha yoyote inayoingia Hazina ni fedha ya kila Wizara na inatumiwa kwa kipaumbele chochote ambacho Serikali itapendekeza na inachooni ni muhimu. Vipaumbele vya *TANAPA* na Ngorongoro inawezekana visionekane kwa Hazina, hivyo basi, nashauri kwamba fedha za *TANAPA*, Ngorongoro na wengineo wanaohudumia misitu zisiende Hazina. Kufanya hivyo ni kuu maeneo haya ya misitu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, asilimia 25 inayotolewa katika Halmashauri ni ndogo, kwa sababu hazielezi mtiririko mzima wa mapato ya uwindaji na mengineyo. Tunaomba iongozwe, na fedha ambazo mwisho wa miaka mingine hazitolewi kujumlishwa kwa mwaka unaofuatilia? Kama si hivyo zinawekwa wapi?

Mheshimiwa Spika, wanyama waharibifu wanawaletea njaa na vifo wananchi walio katika maeneo jirani ya hifadhi, hasa vijiji vya Miguruwe, Njinjo, Zinga Kibaoni na kadhalika. Naomba hatua zichukuliwe za haraka. Nakiri kuona mpango katika Kitabu cha hotuba, lakini naweka msisitizo, kwani hizi ni kero za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nampa hongera Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri.

**MHE. MARYAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuandaa hotuba hii ambayo imeonyesha kazi ambazo zitatekelezwa katika kipindi cha mwaka mzima. Sio hivyo tu, bali imeonyesha na utaratibu wa kukusanya maduhuli.

Vile vile, nawapongeza Mheshimiwa na Naibu Waziri wanavyosimamia kazi za Wizara kwa kushirikiana na Katibu Mkuu wa Wizara hasa kuwa kufanya mabadiliko makubwa ya kuwahamisha watumishi wa Wizara kwa manufaa ya nchi na wananchi kwa ujumla. Hili limewasaidia hata waliohamishwa kujifunza mazingira ya maeneo mengine na kuondoa yale mazoea.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nichangie machache, kwanza nianze kusema Wizara hii ni muhimu katika suala muhimu la kuongeza mapato ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba niikumbushe Serikali kuhusu Utalii wa Malikale ambayo kama ulivyooleza kwamba mtaendelea kutambua maeneo mapya ambayo kwa Kondoa yapo, kuna michoro katika maeneo ya Kijiji cha Itundwi. Boma lilijengwa na Wajerumani, Daraja la Mneso na Chemchemi viliyoko Wilaya ya Kondoa mjini.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba michoro iliyopo Mnenia Kondoa imeingizwa kwenye urithi wa Dunia. Hivi faida ambazo tungepata au tuliotegemea kupata mapema, mbona hazionekani? Hata hivyo haikuelezwa kwenye hotuba maeneo yote yaliyoingizwa katika urithi wa dunia tutakavyonufaika. Hivyo ningepomba kujua ni jinsi gani tutanufaika na ni nani aulizie kama ni Wizara, basi ni vizuri tukafahamu na Serikali ifuatilie.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kuhusu utunzaji wa ndege aina ya *heroe* ambao wanapatikana katika ziwa *Natron* ambako ndio maeneo pekee wanakozalia katika dunia na Afrika kwa ujumla. Naishauri Serikali isiruhusu mradi wowote ujengwe karibu na ziwa hili, kwani manufaa yake ni kidogo sana, badala yake liendelee kutunzwa ili liweze kujengewa miundombinu kama barabara ili watalii waendelee kuja. Kiwanda kikijengwa, matokeo ni magadi, yakiisha kiwanda kitafungwa na wale ndege watahama na hivyo vyote vitapotea.

Mheshimiwa Spika, kifuta jasho cha binadamu walioliwa na simba na mazao yanayoliwa na wanyama kiangaliwe upya kwa maana binadamu kufa na kulipwa ndugu zake Sh. 200,000 sio halali, kwani haziwezi kusaidia chochote hata kama ni kumaliza msiba wa Marehemu na yale mazao yanayolimwa ndio yameshapotea na mtu huyu atakuwa hana chakula tena hivyo Serikali ione thamani ya binadamu aliyepoteza maisha angalau zifanye hesabu za kipato chake angalau alipwe kwa miaka kumi na mazao yathaminishwe ndio Serikali ilipe.

Mheshimiwa Spika, suala la kuharibu mazingira kwa kukata miti, limeathiri sana sehemu kubwa ya Wilaya ya Kondoa na maeneo mengi ya nchi hii. Naomba Kitengo cha Mbegu kingekwenda kufanya utafiti juu ya aina ya mbegu zinazofaa na kuwaelimisha wananchi waweze kupanda aina ya miti itakayofaa.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa juhudi inayofanya ya kuendeleza wafugaji nyuki. Hivyo naiomba iongeze juhudi za mafunzo na hasa kuboresha ukamuaji na utunzaji ili kuwa na asali bora iwawezeshe kupata masoko. Naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mara zote Wizara ndiyo imekuwa ikilipwa fedha za uwindaji katika vitalu na wawindaji na Wizara kurejesha asilimia 25 ya mapato katika Halmashauri: Je, hivi Wizara huwa inapeleka taarifa za hali halisi ya mgao huo wa mapato kwa Halmashauri kwa maana uwiano halisi wa mapato na asilimia 25 inayopelekwa? Halmashauri ya Wilaya ya Songea imekuwa ikipata taabu sana kupata na kufuatilia mapato hayo. Kwa kuwa wamiliki wengi wa vitalu hivyo huwanyanyasa sana wananchi, mfano kufunga barabara, vitisho na kadhalika: Je, Serikali inasaidiaje masuala ya usimamizi wa mahusiano kati ya wananchi wanaozunguka vitalu hivyo?

Mheshimiwa Spika, kuna mwelekeo gani wa kushirikisha jamii katika umilikishaji wa vitalu kwa wawindaji? Nashauri kwamba ni muhimu sheria sasa ikatoa ushirikiano wa wanavijijiji katika umiliki wa vitalu na utalii uhamishie nguvu Miko ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na wasaidizi wake wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na hotuba nzuri waliyoiwakilisha hapa Bungeni. Kutokana na kuwa hotuba hiyo nzuri na ya wazi kabisa, basi natanguliza kutamka kwamba ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa inayofanywa katika kuwatunza kuwalinda wanyamapori wetu lakini bado kumejitokeza wimbi kubwa la wawindaji haramu ambao bado wanapora vibaya sana wanyama wetu kama chui, Kifaru, Sala na kadhalika. Ninaomba kushauri sana askari wetu wa wanyamapori waongezwe, wazidishiwe mafunzo mazuri kupitia silaha zenye uwezo wa kupambana na maharamia hao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna utajiri mkubwa katika sekta ya utalii. Naomba kuzidi kushauri kwamba jukumu la kuutangaza lizidishwe, tutumie Balozi zetu za nje kwa vipeperushi na mabango mbalimbali ndani ya nchi na nje ya nchi yetu tujenge uhusiano wa matangazo ya utalii katika vyombo vya habari hasa katika zile nchi zinazotoka watalii wengi kama Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Ugiriki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara kwa juhudi kubwa ya upandaji wa miti na utunzaji mzuri wa mapori yetu, lakini ninazidi kuiomba Wizara izidishiwe ulinzi mzuri wa ulinzi, kwani bado ukataji wa miti kwa ajili ya mbao umekithiri, aidha, uchomaji wa mkaa kwa ajili ya nishati bado unaendelea kwa nguvu. Katika kuendeleza



uharibifu huo, vyanzo vya maji vinakauka. Vile vile baadhi ya wakulima wanavigema kwa kufanya mifereji isiyo ya kitaalam na kusababisha kukauka vyanzo hivyo. Jambo lingine la kuangaliwa ni uchomaji moto ovyo wa misitu yetu na kusababisha kuuwa viumbe vingi vya porini na hata pia kusababisha ukame wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ninamaliza kwa kusema tena kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CASTOR RAPHAEL LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara kwa maana ya Waziri mwenyewe, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa idara mbalimbali kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu imepakana na Hifadhi ya Taifa ya *Selous*, ambako vitalu vingi vimegawiwa kwa makampuni mbalimbali. Moja ya Kampuni hiyo ni *Miyombo Safari Tours* ambayo wanamiliki vitalu kadhaa katika Wilaya yangu. Mara nyingi kampuni hii imekuwa katika mgogoro wa wananchi wanaozunguka mbuga hii. Hivi karibuni pametokea kutoelewana kati ya Kampuni hiyo ambayo ilipewa ardhi katika Kata ya Utengule na Wapandamiti (yaani Kampuni ya *Tree Planting*) ambao walipewa ardhi katika Kata ya Taweta Masagati. Kampuni ya *Tree Planting* walichomewa makambi yao kwa kugombania ardhi. Naomba Wizara ichunguze jambo hili.

Pamoja na faida nyingi za kuhifadhi wanyamapori, wananchi nao wana haki ya kutumia rasilimali hiyo kwa kupata kitoweo. Siku hizi maeneo mengi ambayo ni *game controlled areas* ambazo zinaruhusu uwindaji nazo zinagawiwa kwa wenye vitalu, kiasi cha kuwafanya wananchi wasiofaidi rasilimali yao hata katika kipindi cha uvunaji cha kuanzia Julai mosi hadi Desemba 31.

Katika Kata ya Mangula kuna kijiji cha Kayenje, kuna tatizo la muda mrefu la Tembo kula mazao ya wananchi.

Ingawa Wizara ilichukua jukumu la kuwa-*train* vijana pale kijijini jinsi ya kulinda wananchi, lakini hawakupewa nyenzo za kufanyia kazi hiyo, yaani bunduki na risasi. Je, Wizara itakuwa tayari kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo kwa kuwapa nyenzo hizo?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa watumishi katika Idara ya Wanyamapori. Je, Serikali ina mpango gani katika kutatua tatizo hili kwa kuajiri wafanyakazi wapya?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna mwamko mkubwa wa wananchi kupanda miti. Katika Wilaya yangu Kata ya Uchindile, Utengule na Taweta wamepata wawekezaji wa kupanda miti kama *tree planting company*. Kata ya Uchindile, iko karibu na kiwanda cha *Mufindi Paper Mill* na wamealikwa rasmi na Kampuni/Kiwanda hicho cha karatasi kulima miti ili wao wawe wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, hii Kampuni ni ya Kitanzania au ya Kigeni? Je, taratibu za kupata ardhi zimefuatwa kama ikibainika ni Kampuni ya Kigeni?

**MHE. ALHAJ PROF. JUMA ATHUMANI KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wake na Watendaji wote, Wakuu wa Wizara kwa kutuletea bajeti safi sana na kwa sababu hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba kuwasilisha shida za wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la kutokuwa na askari wa wanyamapori katika maeneo ambayo yanapakana na mapori ya wanyama yaliyohifadhiwa kama vile Ukumbi, Siganga na Uyowa. Matokeo yake, wananchi wanadhuriwa sana na wanyamapori hawa hasa Tembo, Simba, Chui, tunaye askari mmoja tu anayekaa Makao Makuu ya Wilaya – Urambo.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ya Ukumbi, Siganga na Uyowa kwa muda mrefu wamekuwa wakijitajidi nao waanzishe *WMAs* lakini mpaka leo hatujafanikiwa. Tatizo ni nini? Hali hii inawanyima fursa zinazotokana na uwepo wa *WMAs*. Tunaomba msaada wako. Iwapo tatizo ni namna tunavyoanzisha mchakato mzima wa utaalim, basi tunaomba kusaidiwa ili tufanikishe azma hii kwa faida ya wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, narudia kupongeza na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DK. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, naomba chonde chonde kero ya mashambulizi ya mamba kwenye jimbo la Songwe lishughulikiwe mapema pia ile ahadi ya kutoa kifuta machozi, nashauri litekelezeke. Orodha ya waathirika ilikiwshaletwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja tajwa hapo juu. Kwanza kabisa, napenda kuongelea Wawekezaji na hasa wenye Mahoteli ya *VIP*. Kwani mzungu huyu sioni sababu ya yeye kuwepo hapa ndani ya nchi na kuamua kuwafanya Watanzania kuwa watumwa ndani ya nchi yao. Ni mkubwa gani anamlinda mwekezaji huyo, hata akawa na kiburi kiasi hicho? Je, Katibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii hajui hili? Kama analijua, ni kwa nini asichukuliwe hatua? Au mkataba wake ndio unasema hivyo? Naomba maelezo wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivyo ni pamoja na kuwinda maeneo ya wazi, pamoja na kuwazuia wenyeji kupita karibu na eneo hilo, pia kutuma askari wake kufanya msako kwa wenyeji ambao huchukua jukumu la kumwaga hata vitoweo vya wanakijiji, ili mradi awe amepika nyama, huu ndio utawala bora au ndiyo maisha bora kwa Watanzania?

Tunaiomba Wizara ieleze Bunge hili, hatima na uhalali wa mwekezaji huyo ayafanyayo hapa nchini. Tunaomba uwazi wa Mwekezaji huyo na afuate mkataba aliofunga na Serikali. Kama mkataba ndiyo unasema hivyo, pia tuambiwe.

Pili, naiomba Wizara hii iliangalie suala la Kisiwa cha Sanane ambacho kipo Mwanza. Kwani kuwa na Chuo cha Maliasili hapo Mwanza kuende sambamba na uboreshaji wa Kisiwa cha Sanane. Kisiwa hiki tunaomba kiwe mfano, kwani hapo awali kilifurahisha na kuvutia sana. Tunaomba uangalifu katika Kisiwa. Huo ni Utalii wa mwanzo, wa ndani.

**MHE. ELIZABETH A. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba nzuri yenye maelezo ya kina kuhusu bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia au kifuta machozi kwa wananchi wanaouawa na wanyama wakali au kuumizwa, aidha, uharibifu unaofanywa na wanyama hao kwenye mashamba linastahili kuangaliwa na kutekelezwa kisheria badala ya kufanya kisiasa au kulingana na maoni ya mtu. Uhai wa binadamu ni wa thamani isiyopimika, hivyo kifuta machozi cha Sh.200,000/= ni mzaha.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikawasikiliza wadau wakiwemo Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Migodi *Lake Natron*. Serikali ithamini maoni ya wadau na kupima hasara itakayopatikana iwapo ndege (*flamingo*) wataathirika au kupotea kabisa. Mwekezaji atapeleka faida yote kwao. Nashauri kiwanda kisijengwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpa pole Mheshimiwa Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajali ya ndege iliyotokea majuzi na kusababisha vifo vya wafanyakazi watatu wa Idara ya Wanyamapori. Aidha, naomba nitumie fursa hii kutoa salam za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu.

Mheshimiwa Spika, hakika utakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga - Waziri wa Maliasili na Utalii, aliwasilisha Bungeni Makadirio ya Matumizi ya Wizara yake kwa ustadi na ufasaha mkubwa. Anastahili pongezi na ninalazimika mapema kabisa kutamka kuwa naunga mkono hoja yake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara ilituarifu Bunge juu ya zoezi la kutambua maeneo ya fukwe na kuyatangaza kwa ajili ya uwekezaji. Katika hotuba ya Waziri kwa mwaka wa fedha 2008/2009, suala hili linaelezwa tena ukurasa wa 45. Msisitizo ni maeneo ya fukwe za bahari.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iharakishe zoezi hili ambalo linakwenda pole pole sana na vile vile zoezi hili lihusishe fukwe za maziwa kwa mfano fukwe nzuri za Matema, zilizoko Ziwa Nyasa, ambazo bila hata kutangazwa zinavutia watalii zaidi ya 1,000 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Bunge lilielezwa kuhusu programu ya Taifa ya uendelezaji Utalii. Ningependa kufahamu utekelezaji wa programu hii utaanza lini ili sehemu za pembezoni zenye vivutio vizuri vya kitalii kama Kyela ziweze kufaidika zaidi na sekta hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, ningependa kujua maendeleo ya maandalizi ya Sera ya Malikale ili Taifa lisipoteze urithi wa utamaduni wetu ambao sehemu nyingi unaondolewa kupisha ujenzi wa nyumba za kisasa na matumizi au shughuli nyingine. Thamani ya historia yetu ni kubwa kwani uzoefu umeonyesha sehemu nyingine duniani kuwa sio rahisi kusonga mbele bila kujua ulikotoka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyojaa matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia niseme, utalii ni muhimu katika kuliongezea pato Taifa letu. Ni vyema tujitahidi kuimarisha *ECO – Tourism*, watu wengi wanafikiria utalii ni kupanda tu mlima. Kuna baadhi ya watalii wanakuja kutazama utamaduni wa Watanzania (*cultural tourism*) katika hili Watanzania wa aina ya Wamasai ambao Watalii huangalia utamaduni wao.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya kusini itengenezwe ili wageni waweze kwenda Ruaha, *Selous* kuna watalii wengi wameshatembelea *Northern circuit* sasa wanataka ku- *explore southern circuit* lakini kikwazo ni miundombinu. Pia kuna ukosefu wa mahoteli ya kutosha. Hivyo nashauri Wizara iangalie upande huo.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yanapotolewa katika chombo hiki cha Bunge lako, ni vyema yaheshimiwe. La kusikitisha, Wizara iliweza kufuta maamuzi ya Bunge juu ya sheria za gharama za uwindaji. Kitendo hiki hakikuwa sahihi, kwani Wizara ililazimika sheria hii irejeshwe Bungeni kwa njia ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali iimarisha uwanja wa ndege wa Mwanza ili watalii waweze kutembelea *Lake Victoria* kwa urahisi. Tufahamu kuwa kuna watalii wanakuja kufanya Utalii wa *fishing*, vile vile Mwanza kuna *dancing stone*, wimbo ukiimbwa yale mawe hucheza, hiki ni kivutio cha kipekee.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, nasema ahsante.

**MHE. DR. SAMSON MPANDA:** Mheshimiwa Spika, ni lini tutapewa askari wa wanyamapori wa kutosha pamoja na risasi ya kutosha ya kupambana na wanyama

waharibifu wa mazao kama vile Ndovu, ambao sasa hivi wanaingia hadi majumbani? Pia Mheshimiwa Waziri, kumezuka balaa la mamba wala watu katika mto Matundu Kilwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kifupi watu wanne wameliwa na mamba hao. Nimejitajidi kutoa risasi kwa ajili ya kufukuza mamba, lakini bado tishio linazidi hasa wakati wa masika. Pia kuna wanyama wasumbufu kama vile nguruwe, nyani na tumbili. Tunaomba kungeletewa nyavu ili tuwatokomeze waende kwenye mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Misitu imetunga sheria Na.14 kama mwanga katika shughuli zote za uvunaji endelevu ambao mwananchi anapaswa kuzifuata.

Pamoja na wadau kufuta sheria hiyo, lakini Idara ya Misitu yenye dhamana yote ya usimamizi na uendelezaji wa misitu haiwatendei haki wananchi wa Kilwa. Idara ya misitu inaongeza umaskini, badala ya kuondoa. Lini Serikali na Idara ya Misitu itatoa leseni kwa wakati sheria inavyotaka?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilwa kuna vivutio vingi sana vya Utalii, kuna magofu, mapango zaidi ya 22 ambayo ni kivutio kikubwa cha watalii kama Serikali itatolea tamko rasmi. Mapango hayo yaliyopo Tarafa ya Kipatimu yaitwayo Nangoma, Namaengo ni kivutio kikubwa kwani wakati wa vita ya Majimaji Wajerumani walichemka kuwapata Wamatumbi katika vita hivyo.

Mwisho, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, narudia pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wakuu wote wa Wizara na Taasisi/Mashirika yake kwa kazi nzuri wanazozifanya. Nawatakia kila la kheri. Ningependa kuongezea hoja yangu hapa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kuwa na *WMAs* ni zuri katika maana ya uhifadhi na kuendeleza biashara kwa kutumia rasilimali zilizomo katika maeneo hayo. Sasa tuna takriban *WMAs* 16. Ni vyema Serikali ikaharakisha *WMAs* zote kuweza kuendeshwa na kusimamiwa na wananchi kama inavyotarajiwa. Inatarajiwa kuwa mara “*Authorized Association*” (*AA*) kuandikishwa na mamlaka ya kutumia (*user right*) kutolewa, wananchi waache kujiamulia matumizi endelevu ya maeneo hayo kama vile uwindaji, Utalii wa picha na mengineyo. Cha msingi ni kuwa, matumizi ya rasilimali yafuate miongozo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji wa *TAWIRI* katika utafiti, itapendeza na ni muhimu kutafuta njia endelevu za mapato ya fedha za utafiti. Napendekeza sheria mpya ya wanyamapori ijayo itamke wazi kuwa *TANAPA* na *NCAA* (chombo kingine chochote cha usimamizi – *management* wa wanyamapori) zina wajibu wa kuchangia *TAWIRI* kwa asilimia fulani ya mapato yao kwa mwaka. Sambamba na *TAWIRI*, pia uchangiaji wa *CAWM* – Mweka na Pasiansi utamkwe kwenye sheria.

*TAWIRI* waharakishe kuanzisha nafasi ya *Research Associateship* ili kuimarisha utendaji wa utafiti. Sioni sababu kwa nini hili lichelewe wakati rasimu imekuwepo tangu mwaka 2005. *Research Associates*, hawatakuwa watumishi wa kudumu wa Taasisi, bali wanatumiwa kwa kazi maalum tu za utafiti. *Research Associates* watatoka ndani na nje ya nchi kwa kufuata vigezo fulani, hawa watakuwa ni pamoja na wastaafu, walio vyuo vikuu na taasisi nyingine stahili au *freelance but qualified people*.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanazozifanya. Nashauri wawekeze katika ujenzi wa Mahoteli wakianza na Arusha Mjini, kwani viwanja vikubwa wanavyo (Njiro). Hii itachangia kuongeza nafasi ya makazi bora ya wageni katika eneo hili lenye *Conference tourism* ya juu. Hawatakuwa na sababu ya kuziendesha, wanaweza kukodisha kwa kampuni mahiri au kuajiri menejimenti bora kutoka popote duniani.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha soko letu la ndani, napendekeza tufikirie kuanzisha *Tourism Development Fund*, mfuko utakaokuwa chini ya *TTB*. Hii itawezesha wadau wengi kuchangia fedha za kuitangaza nchi yetu kitalii kuliko kuitegemea Serikali pekee. Kazi inayofanywa na *TTB* ina nufaisha wadau wengi zaidi ya Serikali, hivyo wachangie kwa utaratibu huu. Nchi nyingi zinazoendelea kwenye Utalii zina mifuko kama hii.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyowasilishwa kwa ufasaha sana na Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga - Waziri wa Maliasilia na Utalii. Nampongeza tena kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii. Nampongeza vile vile Mheshimiwa Ezekiel Maige kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya wakisaidiwa na Bibi Blandina Nyoni - Katibu Mkuu ambaye nampongeza pia kwa kazi ngumu, lakini kazi anayoimudu vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa mfupi tu. Nitagusia suala la hifadhi ya mazingira asilia ya Mlima Rungwe. Msaada wa *TANAPA* kwa jamii, Wilaya ya Rungwe na upanuzi wa hifadhi ya Kitulo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika mchango wangu wa maandishi nilielezea umuhimu wa kuipandisha hadhi hifadhi ya msitu ya Mlima Rungwe, kuwa hifadhi ya Taifa. Baada ya uamuzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kupata ridhaa ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya, suala hili sasa liko mikononi mwa Wizara. Tutaendelea kushirikiana na Wizara katika nia na uamuzi wake wa kuhakikisha kwamba hifadhi hii inapandishwa hadhi kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia. Katika kufanya hivyo, naamini tutajifunza kutokana na uzoefu wa hifanyi nyingine za namna hii kama vile Amani, ili hifadhi hizi ambazo ndio ngazi ya juu ya uhifadhi, zinakuwa na fedha za kutosha na zinazotabirika ili ziwe endelevu kwa faida ya Tanzania, ulimwengu/dunia yote na vizazi vinavyokuja.

Kuhusu ushirikiano kati ya *TANAPA* na Wilaya ya Rungwe. Napenda kuushuruku uongozi wa *TANAPA* kwa misaada mbalimbali inayotolewa kwa jamii inayozunguka hifadhi ya Kituo/Mlima ya *Livingstone*, upande wa Magharibi. *TANAPA*

imesaidia ujenzi wa madarasa matatu katika shule ya sekondari ya Mwasisi, Kata ya Kandete. *TANAPA* imepokea vile vile ombi la msaada kutoka Kamati ya Ujenzi wa Sekondari ya Luteba na wamekubali kimsingi kutoa msaada. Nawashukuru, kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi, marafiki wa mlima *Livingstone*, Taasisi zisizo za kiserikali zikiongozwa na *CEEST Foundation*, Halmashauri za Wilaya ya Rungwe na Makete na wananchi wanaozunguka milima ya *Livingstone* (safu za mlima) walikuwa na tukio la kupanda milima hiyo kutoka Kipangamansi/Lumakali, Kata ya Lufilyo, Wilaya Rungwe, mpaka madihani, Wilaya ya Makete. Wanasanyansi toka Vyuu Vikuu walihusika pia. Lengo lilikuwa ni kueneza uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutunza misitu, vyanzo vya maji, *bioanuai* na utunzaji wa mazingira asilia.

Tunashukuru *TANAPA*, ilihusika pia na walichangia kufanikisha zoezi lile. Tutashukuru kama *TANAPA* watashirikiana na *CEEST Foundation* na Wilaya hizi mbili ili kulifanya zoezi hili liwe la kudumu na lihusishe mafunzo kwa vijana wa shule zetu. Ikiwa itakuwa *annual event*, naamini tunaweza tukaanzisha Utalii wa kupanda Milima ya *Livingstone*. Nikiwa Mbunge wa eneo hilo, kwa kushirikiana na Mbunge mwenzangu wa Makete tutakuwa tayari kushirikiana na Wizara na *TANAPA* kuhusu suala hili.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, ni suala la uhusiano ulioharibika au ambao sio mzuri kati ya *TANAPA* na wananchi wa Lutega, Kata iliyo Rungwe mashariki ambayo inapakana na Hifadhi ya Kitulo upande wa Magharibi kwenye mtemremko wa safu za milima ya *Livingstone*. Wananchi wamelalamika kuhusu *high handedness* (ubabe?) walinzi wa *TANAPA*. Naamini tunaweza tukarudisha amani na uhusiano mwema kupitia majadiliano, elimu na kuongeza ufahamu wa wananchi kuhusu mipaka ya hifadhi, wajibu wa wananchi walio mipakani na kujibu maswali wanayouliza bila kiburi au jeuri. Naamini hili linawezekana. Uvumilivu unahitajika kwa kila upande.

Mheshimwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, anapokwenda nyumbani kwake Kyela, achepuke pale Tukuyu ili atembelee eneo hili na kuzungumza na wananchi. Mheshimiwa Spika, uhalali wetu kama Serikali unatokana wananchi na ridhaa yao. Nimemwalika Ndugu Bigurube - Mkurugenzi Mkuu wa *TANAPA* atutembelee. Naamini atapata nafasi mwaka huu 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, namalizia kama nilivyoanza kwa kuunga mkuono hoja hii na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hii na wakuu wa Sekta.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nimeomba kuchangia kwa kuzungumza, ni dhahiri sasa sitapata nafasi hiyo. Kwa hiyo, naleta mchango wangu kwa muhtasari. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mwangunga, Naibu wake, Katibu Mkuu - Mama Nyoni na timu yenu yote kwa hotuba fasaha na kazi nzuri mwaka uliokwisha.

Mheshimiwa Spika, natoa pole sana kwa maafisa wa Wizara hii waliofariki kutokana na ajali ya ndege.

Mheshimiwa Spika, Mchango na Mapendekezo kwa ufupi, Mkoa wa Iringa umevalia njuga kukuza Utalii. Tuna vivutio vyote (isipokuwa mlima Kilimanjaro), hifadhi za Taifa, mbuga za uwindaji, utamaduni na mambo ya kale/historia. Tuna uwanja wa ndege wa Nduli na uwanja mwingine mdogo wa *Ruaha National Park*. Barabara inayopitika japo sio ya lami.

Mheshimiwa Spika, miundombinu mingine mfano Mahoteli, ni hafifu, lakini mlango ukifunguliwa, haya yote yatasahihishwa, *after all* nini hutangulia? Yai au kuku? Kwa hiyo, narudia ombi langu nililotamka katika bajeti ya Waziri Mkuu kuwa namkaribisha Mheshimiwa Waziri Naibu na/au wataalam kuja Iringa kuona *potential* iliyopo na kusaidia *Steering Committee* jinsi ya kuendeleza azma yetu.

Mheshimiwa Spika, Makumbusho ya Kalenga, jengo letu ni dogo sana (futi 10 kwa 10) halitoshi kuhifadhi historia ya Wahehe na utamaduni wao. Isitoshe, hivi karibuni tumebaini kuwa Wizara hii imeweka mpaka kuzungushia eneo hilo ambalo tayari ni kitovu cha utalii. Je, Wizara ina mipango gani ya muda mfupi na mrefu ya kuendeleza eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, suala la ujirani kati ya Hifadhi na vijiji, nilipokuwa Mwenyekiti wa *TANAPA* miaka ya nyuma, nilianzisha sera hii. Lakini hali ya sasa ni kwamba *TANAPA* husaidia maendeleo ya jamii kwa hisani au maelewano na wanakijiji. Maoni yangu ni kwamba, hivi sio hisani bali ni haki ya wanakijiji kutegemea namna fulani ya msaada kwa matumizi ya raslimali zao.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi asilimia 25 inayolipwa na Serikali ni kidogo mno na ni kwa uwindaji tu. Upande mwingine nimevutiwa na *formula* ya Tume ya Jaji Bomani kuhusu madini kwa kuwa kimsingi tunazungumzia ushirika wa vijiji na wanaotumia raslimali zao, nashauri *formula* ya Bomani itumike, yaani kwanza malipo yawe rasmi kiasilimia na pili, viwango tofauti vilipwe kwa wanakijiji jirani na Halmashauri ambayo ndiyo *custodian* wa raslimali zote Wilayani.

Kwa maana hiyo, isiwe uwindaji tu, bali hifadhi pia. Kwa hiyo, nashauri kwamba namna fulani ya mrahaba ilipwe kwa wanakijiji jirani kwa upande mmoja na Halmashauri za Wilaya kwa upande mwingine. Ichukuliwe kwamba ni haki yao na sio hisani.

Mwisho kuhusu utangazaji, nashauri kwamba zinapojitokeza fursa kama za *Sullivan Foundation Fund*, ni vyema na haki, fursa kama hizo zielekezwe *Southern Tourism Circuit* na siyo kila mara Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, naunga Mkono hoja.



**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri, Katibu Mkuu - Mama Blandina Nyoni na wataalam wote kwa hotuba yao nzuri waliyowasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu kutokana na ajali ya ndege iliyopelekea vifo vya watumishi wa Wizara hii. Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la mbuga za Wanyama eneo la Simanjiro Mkoani Manyara ambalo lina *hunting Blocks* nne na eneo hili lina ukubwa takriban kilometa 20,000 na zote zimeenea wanyama. Hivyo, watalii wanapokuja kuwinda hawapati shida yoyote kwa sababu wanyama katika eneo hilo hawabugudhiwi na wameenea kuanzia Kata ya Embaret mpaka Kitwai. Lakini Halmashauri yao, Wilaya hainufaiki kabisa kwa sababu asilimia inayotolewa ni asilimia 25 inayogawanywa kwa Halmashauri nyingine zilizoko jirani na eneo la uwindaji. Hakika ni kwamba asilimia 25 hailingani na mapato yanayovunwa. Ni vyema basi tupatiwe angalau asilimia 40 kama maeneo mengine yanavyopewa. Naomba Serikali iangalie upya kiwango hicho kwa sababu wananchi hawaridhiki kabisa.

Mheshimiwa Spika, vile vile, hao askari wanaolinda vitalu hivi wawe watu wenye uwezo wa kutumia silaha na ikiwezekana wawe wanapewa mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kutumia silaha hata kama ni mgambo ni vyema waweze kukabiliana na hali yoyote inayojitokezwa wakiwa kwenye maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Spika, suala hili la kuvuna magogo na kupeleka nchi za nje, suala hili limekuwa likipigiwa kelele na Wabunge wengi.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini mwangu eti rasilimali, miti mizuri tuliyopewa na Mwenyezi Mungu tu tunaziachia hivi kwa wageni. Madini tunaachia bure, magogo tunaachia bure bila faida yoyote, hivi mwishoni itakuwaje? Ie miti mizuri yote ikishavunwa tutabaki hatuna kitu, tunabaki kununua samani kutoka nje (China) tena kwa thamani kubwa na vina ubora. Wametudharu kuwa hatuelewi kitu. Serikali ichukue hatua mara moja kusimamisha uagizaji wa samani nje ya nchi. Tuna viwanda vingi nchini hapa wanatengeneza samani nzuri kuliko hizo za nje. Ningeomba Serikali ichukue hatua mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu raslimali kale za Tanzania ambazo zinahifadhiwa katika jumba la Makumbusho ya Taifa Kenya – Nairobi. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Wizara pia kujenga jumba la Taifa la Makumbusho ili tuweze kurejesha raslimali zetu zote zilizoko kwenye Jumba la Makumbusho la Kenya. Lakini je, ni nini hatima ya Serikali kuhusu vyura walioko Marekani ambao Serikali ya Tanzania inayalipia hifadhi tena kwa dola vyura hao? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, linaongoza kwa kipindi cha miaka mitano na baada ya hapo, Mbunge akirudi kijijini amesahaulika kabisa. Lakini Mabunge mengine yanawajali na kuwaenzi wanasiasa hao.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Denmark wana utamaduni mzuri. Kuanzia waasisi waliopigania Uhuru, Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Wabunge, Jaji Mkuu na wengi picha zao zimewekwa ukutani kwenye jengo la Bunge. Picha ya kila Mbunge aliyemaliza muda wake. Hivyo wageni wanapotembelea kule wanaona picha zao na huo ni ukumbusho hata kwa vizazi vijavyo, wajukuu na vitukuu watakapotembelea Bunge wanaweza kuona picha za Wabunge Wahenga. Ni utamaduni wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba na sisi tuwe na utamaduni kama wa wenzetu ni jambo zuri sana. Isiwe kwamba Mbunge akimaliza muda wake kazi yake imekwisha na anasahaulika na kubaki kwenye vitabu vya *Hansard*. Tunaomba litengwe eneo maalum kwa ajili ya picha maalum za viongozi Wakuu na Wabunge.

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Mheshimiwa Spika, napongeza shughuli zote za Wizara hii. Pamoja na mambo makubwa ya kuongeza uchumi wa nchi bado ninao ushauri kama ifuatavyo:-Miundombinu ya nchi ni muhimu ikawa ni Agenda ya Wizara hii, wasiachiwe Wizara ya Miundombinu peke yake.

Miundombinu ya barabara, umeme, mabenki, *Bureau de change*, viwanja vya ndege, baadhi ya maeneo mazuri ya utalii hayafikiki kama Kalenga kwenye fuvu la Mkwawa, Kitulo, Milima ya Livingstone Ludewa, umbali wa usafiri wa barabara unakatisha tamaa lakini pia viwanja vya ndege kila Mkoa ni lazima viwe *vina-operate*.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali ituonyeshe ni jinsi gani ina *control* suala la *leakage*. *Leakage* yaani watalii wanaokuja, lakini malipo yote yanabaki nje. Malipo kama *Air tickets agency* wa *Hotels* na malipo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya hoja tajwa hapo juu, nitakuwa tayari kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. DAVID MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, *Mkomazi National Park* imechukua baadhi ya makazi na mashamba ya Kata ya Kizungo. Je, wananchi hao ni lini watalipwa fidia zao?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kata ya Kisiwani imepakana na *Mkomazi National Park*: Je, vijana wa Kata hiyo watakaotaka kuajiriwa na hifadhi hii watapewa Kipaumbele?

Naunga Mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji kwa hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kupatiwa ufafanuzi katika hoja zifuatazo:- Jumla ya wananchi 328 waliokuwa wanaishi Ikovo, walilazimika kuondoka kutokana na kuachia

nafasi *Mpanga - Kipengere Game Reserve*. Wananchi hawa wanadai fidia ya jumla ya Sh. 221,608,548/=. Taarifa ya Mdhamini Mkuu wa Serikali ilikamilika Januari, 2008. Napenda kupata ufafanuzi kama Wizara imetenga fedha hizi katika bajeti yake ili kuwalipa wananchi hawa ambao tayari wamekwishahama.

Mheshimiwa Spika, ukipitia vitabu vyote pamoja na bajeti, hakuna mahali popote panaponyesha mkakati wa kuendeleza hifadhi hii mpya ya Kitulo iliyopo Makete. Serikali ifafanue. Pia tunaomba Serikali ijenge miundombinu ya kuwawezesha watalii kufika kwenye hifadhi hii bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa juhudi kubwa wanayoichukua katika kukamilisha majukumu yao na Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake katika ukurasa wa 32 amesema Tanzania inazalisha asali bora ambayo inakubalika katika soko la Jumiuya ya Ulaya na kuiwezesha Wilaya ya Manyoni kupata medali ya dhahabu. Hili ni jambo la kupongezwa, lakini Wizara lazima iwe macho na wajanja wachache wanaotengeneza asali ya kupika.

Mheshimiwa Spika, suala hili lipo na Watanzania wengi wamepata hasara kwa kununua asali hiyo iliyopikwa kwa kutumia mazao ya asali.

Mheshimiwa Spika, suala hili kama halikuchukuliwa hatua za kufaa litaharibu ubora na sifa ya asali ya Tanzania kwa hiyo, naishauri Wizara ifanye ukaguzi wa awali hasa kwa kuwa asali ya namna hiyo ipo sokoni inauzwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utangazaji wa utalii, katika sekta hii juhudi kubwa imechukuliwa kwa kutangaza vivutio vingi vilivyoko nchini lakini masikitiko makubwa sikuona vivutio vilivyoko Tanzania Zanzibar wakati kuna vivutio vingi na fukwe nzuri za kuvutia utalii Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba si jambo zuri kuitangaza Tanzania na kuiacha Zanzibar kwa sababu Zanzibar ni sehemu ya Tanzania katika Jamhuri ya Muungano hasa ukizingatia Zanzibar hivi sasa hali ya uchumi ni mbaya na inategemea Utalii ni sehemu ya kupatia mapato.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni kitu kimoja haina haja kunyimana. Ndugu si kufanana bali kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja

**MHE. MCH. DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maliaasili na Utalii. Hii inaonyesha Rais na Serikali iligundua vipawa vilivyo ndani yako, hongera sana. Naomba pia nitoe pongezi za dhati kwa hotuba nzuri inayokidhi malengo ya Taifa.

Naomba nichangie kwenye eneo la utalii. Tunashukuru jitihada za kuitangaza nchi yetu na vivutio vilivyo ndani ya Tanzania. Juhudi inatakiwa iongezwe kwa kasi ili tutahamike. Balozi zetu ziongezewe pesa ili watangaze kwa bidii tuvutie watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, vivutio vyote viboreshe, viwekwe kwenye vipeperushi ili vitangaze raslimali tulizonazo. Tujivunie Mlima Kilimanjaro, wanyama na mbunga.

Mheshimiwa Spika, hoteli na mazingira yanayozunguka yawe safi. Tuboreshe usafi kwenye vyoo ili watalii wavutiwe. Wazungu wanajali sana usafi wa vyoo kwa usalama wao. Hoteli iliyoungua Mikumi itengenezwe. Mbunga zinazopendwa na wengi. Tuzingatie utalii wa ndani, tuhamasisha shule, vyuo na Watanzania wote ili waone vivutio vya nchi yetu, utalii ni Baraka za Mungu kwa watu wote kila Mtanzania atakiwa azifaidi.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napenda kuishauri Serikali kwamba iwe makini zaidi na umegwaji wa maeneo ya Hifadhi ya Taifa kumilikiwa na wageni. Mfano halisi ni ule wa Mbuga za Serengeti. Inatisha sana kusikia mgeni anauziwa na kijiji zaidi ya ekari 5,000 ndani ya mbuga za Serengeti! Hapa hakukuwa na umakini.

Je, ni Watanzania wangapi wanaweza kwenda nchi kama Amerika na Uingereza na hata Arabuni akakubaliwa kununua kipande cha ardhi kikubwa hiyo akiwa peke yake? Hii inadhoofisha maisha ya vizazi vijavyo. Si vizuri kila wakati kuwepo malalamiko ya kunyanyaswa kuonewa, kunyimwa haki kwa wananchi wazawa na wageni wanatanua, haifai, mbaya! Irekebishwe kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia iangalie Mkoa wa Kagera, nao una vivutio vyipya vingi ambayo havijatangazwa. Naishauri Serikali iwasiliane na uongozi wa Kiroyeru Bibi Mary Kalikawe, ni mfano wa ubunifu huu na amesaidia kuweka Kagera katika ramani.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali hasa Wizara hii husika iwe karibu na Wizara ya Miundombinu ili kazi ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Bukoba ikamilike haraka maana usafiri wa ndege unarahisisha utalii. Kwa sasa ndege za *Presicion* zimesitisha usafiri wa kwenda Bukoba, hali ambayo inatudhoofishia sana kiutalii, maana wengi hawapendi kutumia muda mwingi katika kusafiri. Nawasilisha.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nikawa mzima na kuweza kuchangia hoja hii ilioko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kivuli Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa hotuba yake nzuri na nampongeza Waziri wa Maliaasili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Mwangunga kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii, kwa kuanzia napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri ilikuwaje tumepitisha sheria hapa Bungeni ya bei za uwindaji ghafla Serikali ikabadilisha bila hata kuleta taarifa hapa Bungeni, hii si inaonesha dharau?

Mheshimiwa Spika, kuna habari za kusikitisha sana kwa mfano kama hizi Hoteli za *Sope lodge* ambazo *booking* yake huwezi kuipata mara moja yaani ina wateja wengi kwa mwaka jana mtu mmoja analipa dola 60 – 100 sijui mwaka huu wanalipa ngapi na Serikali inachukua dola 1 hadi 3 sasa kweli hii ni haki?

Mheshimiwa Spika, hili jambo halitaki hata mwenyewe unahisi kuna mkono wa mtu kwa sababu haiwezekani Serikali inashida kubwa kuhusu maendeleo ya nchi hii mpaka inawachangisha wananchi, wakati wawekezaji wanapeta.

Mheshimiwa Spika, katika hoteli nyingi Zanzibar hasa zile za Kitalii, hoteli hizo zina ubaguzi sana hata ukitaka kunywa soda unaambiwa ufanye *booking Italy*, hivi ni Mzanzibar gani atakayefanya *booking* ya hoteli Italy? Huu ni unyanyasaji ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wamiliki wa hoteli hizi *package* zote zilipwe huko huko Italy na fedha zinazoletwa nchini ni ndogo sana, je? Idara ya Mapato wanakusanyaje mapato kutoka katika hoteli hizi?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iyafanyie kazi mambo hayo ili unyayasaji huu uondoke katika nchi yetu, vile vile na mapato ya uhakika yapatikane. Ningeshuri fukwe za Dar es Salaam ziimarishwe kwa kuzijali, mazingira mengine ni machafu sana, haziwezi kuvutia watalii kwa hali ile, kivutio kingine ni lile soko la Dar es Salaam liwe safi kama ilivyo kabidhiwa na Wajapan, watalii wameacha kwenda pale kwa sababu pananuka hata magonjwa ya mlipoko yanaweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi za dharti kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara hii.

Kuhusu kuendeleza utalii na fukwe, nimevutiwa sana na zoezi lililofanywa Mkoa wa Tanga – Muheza na Pangani. Napenda kuuliza ni kwa nini Wizara haisaidii kuendeleza *Beach* za Oysterby (*Coco beach*) ili kuzuia mmomonyoko unaoendelea na bahari ambayo karibu itafika barabani. Pia eneo lililobaki kati ya *Golden Tulip* na *Sea*

*Cliff*, ile sehemu nzuri sana kama ikiendelezwa, baada ya kuacha pori na kuwa sehemu ya kutupa taka. Wizara isaidie Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutoa ushauri wa mfano maeneo kama yale sehemu mbalimbali duniani mfano Durban, *South Africa*. Kinachoendelea sasa ni mabishamo makubwa ambayo hayana maana katika kuendeleza utalii wa fukwe za Dar es Salaam.

Pia kuna matatizo makubwa ya Hoteli zilizopo ufukweni mwa bahari upande wa kata za jimbo la Kigamboni, hoteli hizi zinazuia wananchi kufika kwenye fukwe za bahari kinyume na sheria ya ardhi. Tafadhali zifuatilieni.

**MHE. EUSTANCE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa Bajeti iliyoandaliwa vizuri na kuwakilishwa vizuri pia uendeshaji mzuri wa shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wanyama wenye madhara Karagwe, tunashukuru hatua zilizochukuliwa kuhusu makundi ya tembo waharibifu. Tunaomba Wizara ijiandee vizuri ili kila mara uvamizi wa tembo utokeapo *response* ije haraka zaidi ili kupunguza madhara.

Kuhusu utangazaji wa vivutio vya nchi yetu. Napongeza Wizara kwa hatua za kutangaza vivutio vya nchi yetu nchi za nje. Nashauri mkakati huu uendelee, pamoja na ughali wake kwa kuwa bado tunakutana na watu wengi wasiojua vizuri vivutio vyetu, hata wengine hawajui Tanzania iko wapi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu Ndugu Blandina Nyoni pamoja na wakuu wa Idara wote (Wakurugenzi).

Awali ya yote nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kukubali ombi la kurudisha Chuo cha Nyuki Tabora. Pia niwashukuru sana Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa kuona umuhimu huo wa kurudisha mradi huo. Ningependa pia kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa juhudi zake za kuhakikisha mpango wa ukarabati wa Chuo hicho unaendelea vizuri kama alivyoeleza kwenye hotuba yake. Wananchi wa Mkoa wa Tabora watakuwa bega kwa bega kuhakikisha kwamba wanakitumia chuo hicho kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie suala la kuanza chuo liwe mapema mara ukarabati utakapokamilika. Hata hivyo ningeshauri pia mafunzo ya muda mfupi yaendelee kutolewa kwa wafugaji kwa vikundi mbalimbali hapa nchini kuliko kuendelea kupeleka Olomotonyi, Arusha.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wadogo wapewe mizinga ya kisasa ili waendeleze soko zuri na ubora wa asali ndani na nje ya nchi. Pia Tabora kuna vivutio, kuna suala zima la biashara ya utumwa huko Kwihara na safari ya Stanley pamoja na Livingstone. Naomba litangazwe kwenye maeneo au Mataifa kuliko toka wazungu na waarabu ili

wajue historia ya watu hao kwa vizazi vyao na kuongeza Pato la Taifa na maendeleo ya Mkoa wa Tabora ili waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikupongeze kwa kazi nzuri unayoifanya. Hakika Waziri anao uzoefu na amekomaa. Tunamtegemea.

Pamoja na pongezi naomba niwasilishe matatizo na malalamiko ya wachimbaji wadogo eneo la Matabe. Matabe ilikuwa chini ya kampuni ya *Barrick*, baadaye *Barrick* waliruhusu wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo wakatuma maombi Wizara ya Nishati na Madini na Waziri wakati huo alikuwa Mheshimiwa Nazir Karamagi akaiandikia Wizara ya Maliaasili na Utalii barua hiyo haikujibiwa hadi leo. Cha kusikitisha *DC* wa Biharamulo akaenda na *FFU* akawafukuza wachimbaji wadogo kama vile ni majambazi, waliobaki pale ni wachoma mkaa na wakulima wa viazi na mahindi ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ushauri naomba eneo la Matabe wapewe wachimbaji wadogo, wawekewe mipaka na masharti ya kutunza mazingira. Wachimbaji wapo tayari kufuata masharti hayo. Nashauri wasiliana na Kamishna wa Madini Dr. Kafumu atawapa maelezo juu ya mateso ya wachimbaji wa Matabe.

Mheshimiwa Spika, Geita kuna misitu ya hifadhi ambayo haina wanyama ila inaathiriwa sana na wachoma mkaa na wapasua mbao. Nashauri kwa kuwa kuna wafugaji ambao wangependa kuishi humo na mifugo yao bila kukata miti au kulima chochote wakae humo kwa mkataba wa kuwa walinzi wa misitu hiyo. Wafugaji wakipewa kazi ya ulinzi wa misitu wataweza na msitu utadumu na kuendelea.

Katika Ziwa Victoria eneo la Bukondo na Kasamwa mamba wamezidi, wanakula watu sana, naomba wawindaji wa mamba waende Geita sehemu za Bukondo na Kasamwa wakapunguze mamba hao ni wengi na ni hatari kwa wakazi hao. Hili sasa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba mradi wa ufugaji nyuki katika maeneo ya misitu yangu.

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwanza kwa kuteuliwa kushika Wizara hii muhimu, nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri. Imani yetu ni kuwa kwa bidii na uadilifu wenu nchi inaweza kupata faida au kunufaika na sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie wataalam wa mambo ya hoteli waje Njombe ili watoe semina kwa wahudumu wa hoteli zetu. Njombe mjini tunavyo vihoteli vingi, vidogo, lakini vizuri sana kwa usafi na ujenzi. Tatizo letu kubwa huduma ni za chini sana na mbaya. Wenye hoteli hawana ujuzi wowote na wala hawana

*standard* za hoteli. Hivyo tukipata wataalam wakaja tukawa na semina au mafunzo kwa muda wa wiki moja kwa kuanzia naamiani sekta hii itakuwa imefika mahali pake.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kukaribisha wageni wengi lakini huduma ni mbaya kiasi cha kufanya wageni wasiwe na raha. Ikiwa ombi hili litakubalika basi tutawaandaa wasimamizi wa hoteli hizo na wasaidizi wao kupata mafunzo hayo. Makadirio ya watakaohusika kwa awamu ya kwanza ni kama wahudumu mia moja.

Mheshimiwa Spika, nipo tayari kueleza zaidi nikipewa nafasi ya kuongea ana kwa ana na wataalam hao. Naomba kuunga hoja mkono.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na wenzangu kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Maliaasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inalenga kuonyesha utalii endelevu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na uongozi wa *TANAPA* kwamba magari mengi ya mizigo yanayoenda Mara, kwanza yanaharibu barabara na vile vile yanaleta adha kwa watalii kwani ni kweli yanaongeza msongamano. Ushauri wangu kama njia ya kumaliza tatizo hili, ile barabara ya kutoka Musoma – Mugumu – Loliondo hadi Mto wa Mbu kwenda Arusha, kwa kuwa imeshapimwa naiomba *TANAPA* ipitishe greda ili njia hiyo ifunguliwe na *TANAPA* waweke katika barabara hiyo vituo vya kukusanya fedha ile wanayolipa wanapopita Ngorongoro na Serengeti na fedha hiyo itasaidia kuendelea kukarabati njia hiyo mpya wakati Serikali inatafuta fedha za kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo ile adha inayotokana na barabara iliyopo sasa itapungua kwa kiasi kikubwa na pia wananchi wa Mkoa wa Mara tatizo la mfumuko wa bei litapungua kwani mizigo mingi sasa toka Arusha itatufikia pasipo matatizo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana kwa Bajeti nzuri. Naomba kuchangia kidogo sehemu mbili ili kuongeza utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya kujenga hoteli, kuna maeneo mengi jijini Dar es Salaam ambayo watu wamehodhi yachukuliwe kisheria na kugawiwa *investors* wa ndani na nje. Mkaribishe *big chain – Hilton Hyatt Regency, Inter-continental* na kadhalika na kuwaomba wajenge. Uwe mkakati wa Serikali. Halafu nimeona mtafufua ofisi za *Marketing* nje ya nchi. Naomba mzingatie *market* ya Asia – Dubai, Japan and *Far East, Europe* na *America*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja sana.



**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake mahiri. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Wizara hii kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa hotuba hii na ushauri wao wa kitalaam.

Mheshimiwa Spika, kama walivyokwisha sema Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, kama Wizara hii itazidisha juhudi za kuhakikisha Maliasili zetu zikiwemo misitu, wanyamapori na maeneo mengine muhimu ya vivutio kama fukwe na bahari, mapango ya michoro ya watu wa kale na makumbusho mengine, sekta hii ingeweza kuchukua hatamu katika kuliingizia Taifa letu pato kubwa la fedha. Kwa sasa misitu mingi inateketezwa bila utaratibu na kwa kiasi kikubwa watuhumiwa hudai wenye kuruhusu au wadau wakubwa ni maafisa Maliasili wa maeneo husika. Pia bei ndogo ya wawindaji wa wanyamapori wetu ikilinganishwa na nchi zingine inapunguza Pato la Taifa, bila kusahau utaratibu usiokubalika wa watalii kulipia gharama za utalii wao hapa kwa mawakala walioko kwenye nchi wanazotoka, ambao huishia kuwasilisha kiasi kidogo tu cha fedha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naomba sasa nielekeze mchango wangu mfupi Mkoani Mbeya, Wilaya ya Mbozi hususan Jimbo la Mbozi Magharibi. Mkoa wa Mbeya una maliasili na vivutio vingi vya utalii ambavyo mpaka sasa havijaweza kuchangia hata kidogo Pato la Taifa. Kati ya hivyo ni misitu mikubwa ya asili na ya kupandwa, maziwa juu ya vilima (*creater lakes*), maji moto, maporomoko ya maji, vimondo vya Mbozi Ivuna Wilaya ya Mbozi, nyayo za binadamu kwenye mawe na wanyama pori kwenye mbuga mbalimbali. Wilaya ya Mbozi hususan Jimbo la Mbozi Magharibi, lenye uwanda wa juu na Ukanda wa Bonde la Ufa, kuna vivutio vifuatavyo:-

Kwanza, unyayo wa binadamu kwenye jiwe katika kijiji cha Nkangamo, kata ya Nkangamo, kilimeta zipatazo 20 kutoka Tunduma kwa barabara ya Sumbawanga, pamoja na jiwe hilo kuwa na unyayo huo, pia kuna michoro ya binadamu au zamadamu hao. Kana kwamba hilo halitoshi, mara nyingi juu ya jiwe hilo watu wanaotembelea eneo hilo huona joka kubwa pale likiwa limejipumzisha juu yake.

Pili, mbonyeo mkubwa wenye upana wa takribani kilometa 20 na urefu wa zaidi ya kilometa 100 wa Bonde la Ufa la Rukwa (maarufu kama *Msangano trough*) ambao una ardhi yenye rutuba isiyohitaji mbolea ya aina yoyote kwa kilimo cha aina yoyote kwa kilimo cha mazao mbalimbali na ufugaji. Pia kutokana na mito iliyopo eneo hilo wanyamapori kutoka uwanda wa juu huteremka kutafuta maji na malisho. Eneo hili huanzia kilometa chache kutoka barabara kuu ya Zambia karibu na Tunduma hadi Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kingo za Bonde la Ufa la Rukwa (*Msangano trough*) zimepambwa na misitu mikubwa asilia yenye miti ya mininga, mininga maji, mipilipili,

miyombo na kadhalika ambayo huonekana kama vile imepandwa. Miti hii ina maliaslili za aina mbalimbali kama mbao, asali na wanyamapori wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nne, Ziwa Rukwa lenye viumbe hai mbalimbali wakiwemo viboko, mamba na samaki wa aina mbalimbali wa maji baridi. Pia kando kando yake huonekana kwa nadra siku hizi wanyama wa aina ya swala ambaye hapatikani sehemu nyingine yoyote ya dunia aitwaye Sheshe au *greater Puku* ambaye miaka ya hivi karibuni kwa utaratibu wa ulinzi maalum ameanza kuonekana Mahenge.

Tano, kKimondo cha Ivuna, kata ya Ivuna, tarafa ya Kamsamba ambacho kwa bahati mbaya sana kutokana na miundombinu duni ya kufikia sehemu hiyo hakijatanzwa kama ilivyo kwa kimondo kingine kilichopo Wilayani Mbozi, maarufu kama Kimondo cha Mbozi.

Mheshimiwa Spika, kwa uchache tu hiyo ndiyo hali halisi ya Jimbo la Mbozi Magharibi na vivutio vyake vya Maliaasili na Utalii. Naomba Wizara ya Maliaasili na Utalii ipanue wigo wake wa utendaji ili kuweza kuvuna utajiri mkubwa uliopo eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda kusema naunga mkono hoja.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliaasili na Utalii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa ujumla kwa kuwasilisha Bajeti yao nzuri yenye mwelekeo mzuri kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema kuwa kuna tatizo kubwa sana katika Wilaya ya Maswa, ukataji miti kwa ajili ya matumizi ya kuni Gereza la Maswa, ni kweli kwamba umekuwa ni tatizo kubwa kupata kuni kwa ajili ya matumizi ya wafungwa ndani ya Gereza na hii imesababisha kuongezeka kwa jangwa kwa kasi kubwa.

Nilikuwa naomba Wizara inisaidie ni njia gani mbadala itumike ili kuokoa miti hii ya Maswa na nilijaribu kuwasiliana na Mkuu wa Gereza, nikamuuliza ni kweli kuwa hampati fungu maalum kwa ajili ya manunuzi ya kuni alisema hakuna fungu la namna hiyo. Nadhani ipo haja ya kuangalia upya suala hili ili tuweze kunusuru miti hii ambayo wakati mwingine imevunwa ikiwa midogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kuchangia utaratibu mzima wa vibali vya uuzaji wa mikaa kwa wananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize au nipate ufafanuzi kwa Serikali, utaratibu gani unatumika ili wananchi hawa waweze kupata vibali vya kuuza mikaa? Kwani wananchi wa kawaida wamekuwa wakipata taabu sana kupata vibali jambo ambalo limekuwa likiwatesa sana wananchi hawa. Lakini pia wamekuwa wakikamatwa ovyo na kutozwa faini kubwa kuliko mzigo walionao wakati mwingine mwananchi ana debe mbili au tatu tu, kweli inatia huruma sana. Lakini pia wananchi hawa wamekuwa wakizungushwa kupata vibali. Naomba Serikali ijariibu kuwasaidia Watanzania hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu wafanyabiashara wa uuzaji wa mbao kwa kweli wamekuwa wakifanya biashara hizi wengi wao wanafanya kinyemela (hawana vibali) au leseni za biashara wakikamatwa wanatoa pesa kidogo na kuendelea na safari zao. Naomba Serikali ifuatilie kwa karibu ili Serikali iweze kupata ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu viwanja vya ndege vilivyopo ndani ya Mbuga. Ndege hizi hutua na kuondoka nchini bila kukaguliwa na mtu yeyote yule je, Serikali haioni kuwa watu hawa au wawekezaji wanaweza kabisa kuwasafirisha wanyama wetu bila mtu yeyote kujua? Naomba Wizara iweke utaratibu wa ukaguzi wa ndege hizi mara zituapo na kuondoka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ambayo kwa kiasi ina lengo la kuiongezea mapato Serikali yetu. Kwa muda mrefu mchango unaotokana na sekta hii haulingani na makadirio/matarajio wa wananchi wa Tanzania. Ni imani yangu kuwa kwa hotuba hii ya leo pamoja na uongozi imara uliokuwapo katika Wizara hii kwa sasa, Serikali yetu itapata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu watumishi wa Wizara hii walio wengi hukaa katika kituo kimoja. Si ajabu kumwona mtumishi amekaa katika kituo cha kazi kwa zaidi ya miaka kumi. Kitengo hiki huwafanya watumishi hao kujiona ndio wenye mamlaka na maamuzi yote hivyo kuingia kwenye migogoro na wananchi. Mfano ni meneja wa Mikoko Kanda ya Kati ambayo makao yake makuu yapo Kibiti. Meneja huyu amekaa kwa muda mrefu katika kituo hiki na kuwa ni mojawapo ya chanzo cha migogoro baina ya wananchi wa Idara ya Mikoko.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali imhamishe kiongozi huyu ili Serikali pamoja na wananchi waweze kupata tija kutokana na misitu inayowazunguka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni uvunaji wa Mikoko. Katika ukanda wa *Delta*. Kwa zaidi ya miaka mitano uvunaji wa miti ya Mikoko umezuiliwa na hakuna kibali kilichotolewa ili wananchi wa maeneo hayo waruhusiwe kuvuna. Jambo la kushangaza ni kuwa miti hii inapita njia za panya na kujaa katika masoko ya kuuzia huko Zanzibar na Mafia. Je, hao wanaosafirisha wanapata wapi vibali hivyo? Je, kwa nini wananchi wanaozungukwa na miti hiyo hawaruhusiwi kuvuna?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe vibali vya uvunaji wa Mikoko kwa wananchi wa maeneo hayo kwanza ndipo watoe kwa waombaji wengine. Pia ikumbukwe kuwa miti hii huota na kukomaa si zaidi ya miaka kati ya mitano hadi kumi, hivyo kuendelea kuvunwa itakuwa ni bora zaidi ili miti mingine iweze kuota. Pia ni vizuri vibali hivi vya uvunaji Mikoko viwe vinatolewa na Mkuu wa Wilaya kwa niaba ya Serikali Kuu kwani wananchi wengi wanashindwa kwenda Wizarani.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia suala la Wajasiriamali wadogo wadogo wanaofanya kazi ya useremala. Vijana hawa waliungana na kukata leseni ndogo

wanapata adha kubwa pindi wanapotaka kusafirisha mazao yao (samani) kwenda nje ya Wilaya ya Rufiji ili kwenda kuuza. Mara kwa mara wajasiriamali hao wanateremshiwa samani zao na hatimaye kuuzwa bila ya wao kupewa taarifa. Huu ni unyang'anyi wa dhahiri. Unyang'anyi huu upo hasa katika kituo cha ukaguzi maliasili pale Kibiti. Kwa nini hali hii inatokea Rufiji wakati maeneo mengine ya nchi hii samani hizo husafirishwa bila ya matatizo. Hali hii huwakatisha tamaa sana wajasiria mali hao ambao wanafanya shughuli hizo kihalali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuwa sheria au utaratibu huu unaowakandamiza wajasiriamali wa Rufiji uondolewe au utumike kwa nchi nzima kila mmoja aweze kuguswa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, suala la uvujaji na usafirishaji wa magogo nje ya nchi (isipokuwa miti aina ya mitiki pamoja na *cyprus*) miti mingine yote ya asili ilizuiliwa na hadi leo ndiyo tunavyofahamu. Ni kwa nini bado biashara hiyo inaendelea kinyemela? Magogo yanapita wapi kutoka mashambani/misituni hadi kufika bandarini wakati kila *check point* kuna ukaguzi wa mazao ya misitu? Maafisa misitu wa ugani zote kuhamia kata, Wilaya hadi Wizarani wanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai, 2008, Katibu Mkuu wa Wizarani alitoa habari kwenye vyombo vya habari kuhusu magogo mengi yaliyokutwa bandarini na kiasi cha fedha zilizookolewa. Kwa muono wangu kilichookolewa ni kidogo sana ukilinganisha na kiasi kinachopotea kwa magogo yanayotoroshwa kinyemela.

Mheshimiwa Spika, tunataka tuendeleo kupiga siasa kwa maeneo yasiyo na utekelezaji hadi nchi yetu iwe jangwa? Naomba Wizarani ieleze Bunge sasa nini hatma ya biashara hii ya magogo?

Mheshimiwa Spika, kuna habari ambazo hazijathibitishwa kwamba Serikali iko mbioni/imeanza kujadili suala la kufungua tena/au kuruhusu biashara ya mbao/magogo hapa nchini. Nina wasiwasi kama kweli hili lipo Serikali inaitakia mema nchi yetu? Tunakwenda wapi? Ni juhudi gani zimefanywa na Serikali kupanda na kukuza miti kwa muda huu mfupi na hivyo kufungua biashara hiyo? Miti/magogo yanavunwa yametunzwa kwa haraka zaidi ya 100 leo sisi uchu na uroho wa fedha tunataka kumaliza yote! Kama wazo hilo lipo tujulishwe Bungeni ili nasi tutoe michango yetu.

Mheshimiwa Spika, viwango vya ada za uwekezaji zinazotolewa na hoteli kubwa za kitalii ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wageni wanaoingia, idadi ya vitanda na huduma nyingine zinazotolewa hapo. Mfano hoteli ya *Moven Peak* inalipa ada kiasi cha dola 1000 kwa mwaka kwa Serikali, fedha hii ni ndogo sana na hailingani na kile kinachokusanywa na wawekezaji wenye hoteli kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mwongozo utakaoweka wazi hoteli za hadhi fulani/daraja fulani kulipa kiasi kadhaa kulingana na madaraja ya hoteli hizo. Hili litasaidia nchi kupata pato linalostahili na hivyo kuweza kunufaika na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni utaratibu unaotumiwa na hoteli/wawekezaji wa hoteli kukwepa kulipa fedha na kuwekeza hapa nchini kwa kubadili majina na hoteli hizo pamoja na kubadilisha majina ya wamiliki wa hoteli hizo. Serikali imeweka utaratibu ambao siyo mzuri wa kuwasamehe wawekezaji wasilipe kile wanachotakiwa kwa muda wa miaka mitano kwa madai kwamba wanajiimarisha! Hapa ni kuwanufaisha wawekezaji tu. Wanachofanya hawa ni kwamba wakiona miaka mitano inakaribia wanabadili jina la hoteli, jina la mmiliki, wakati wamiliki ni wale wale. Mfano *Movern Peak Hotel* ilanza na *Sheraton* kwa ujanja huo sasa ni *Movern Peak*. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kuhusu jengo ambalo lilikuwa *Embassy Hotel* limekaa tupu, linaozea pale kwa miaka nane sasa bila kufanyiwa chochote. Hii ni mali ya Watanzania kwa nini liachwe hivyo? Ni kweli Serikali imeshindwa kulipangia mipango mizuri ili liweze kuzalisha? Kwa nini jengo hili ambalo lipo karibu na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*) wasikodishiwe wakawa wanalipa japo kidogo kuliko kuliacha liendelee kuharibika?

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpanda, asilimia 63 ya eneo lake ni misitu ambayo inazo rasilimali nyingi na pia napongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kuhifadhi maeneo mengi na kuwepo kwa *National Park* ya Katavi, *game controlled area* na *Forest Reserves* kwa maslahi ya leo na urithi kwa vizazi vyetu.

Lakini Mheshimiwa Spika, eneo hili pamoja na kuwa na rasilimali hizo nilizotaja Wizara hii haitowi kipaumbele na huduma stahilki kwa kuendeleza na kutunza rasilimali hizi kwa kuwapa vitendea kazi stahiki, magari, silaha na hata malipo ya masurufu na motisha ili kuongeza ari kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo, ofisi ya maliasili wanyamapori hawana gari wanategemea magari ya idara nyingine ama misitu, *TANAPA* au Rungwa/Lukwati au Halmashauri jambo ambalo wakati mwingine linakwamisha ufanisi wa shughuli zao na hasa kama unavyofahamu hali ya ujangili ilivyo katika Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko ya kuchelewa kulipwa kwa madai ya masurufu kwa wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi, nashawishika kuamini kwamba kwa uzembe huu kunaweza kuwashawishi wafanyakazi hao kupokea vizawadi au vipesa kidogo kutoka kwa wawindaji wa kitalii na kutotimiza wajibu wao ipasavyo lakini chanzo ni Serikali kutotimiza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo pia sasa la usafiri kwa wafanyakazi wa Rungwa/Lukwati *Game Reserve* hasa baada ya wafadhili kupitia *GTZ* kukamilisha

mikataba yao na makambi hayo yapo mbali sana msituni hakuna huduma na kama zipo hazitoshelezi hata elimu kwa watoto wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na uvunaji holela na uharibifu wa misitu na sehemu kubwa ya uharibifu huu imefanywa na wakimbizi ambao ama wataondoka au kuendelea kuwepo. Hasara hii na uharibifu huu uliofanywa nani analipa? Napenda kukiri wenyeji pia wanafanya vitendo hivyo lakini idadi ya wingi wa wakimbizi na uharibifu wao. Wenyeji ingawa wanachukua zaidi ya miaka 50 kuharibu kiasi kilichoharibiwa naomba utafiti wa kina ufanywe juu ya uharibifu wa wakimbizi vs wenyeji na tunahitaji fidia toka katika Jumuiya za Kimataifa ya kuboresha na kuendeleza eneo hili lililoathirika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata maelezo ya kina juu ya ufugaji na uvunaji wa asali ambayo inapatikana kwa wingi Mpanda na kwa nini zao hili linaendelea kushuka mwaka hadi mwaka na kama zipo takwimu sahihi za zao hili au ni takwimu za kufikirika tu pia wapo watumishi wachache sana na kama Wizara itakuwa tayari kusaidia idara hii ili kuongeza Pato la Taifa. Kadhalika ni lazima tufanye tathmini ya kina juu ya mizinga inayotumika kwa maana mizinga ya kisasa vs mizinga ya asili ni ipi ambayo huvutia makundi ya nyuki kuweka makazi.

Aidha, masharti magunu kwa warina asali yaangaliwe hasa maeneo yote yanayofaa kwa kufuga nyuki ama ni *game reserves* au *forest reserves*. Kibaya zaidi maeneo ya *game* yamepewa na kugawiwa kwa wawindaji wa kitalii ambao wanawapa usumbufu mkubwa wananchi ambao hawaoni hata hicho kinachopatikana kutokana na kuwepo kwao miaka nenda miaka rudi na kuyafanya maeneo hayo kuwa mali yao na haki zaidi kuliko wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho sitakuwa nimetenda haki kama sijasema kuhusu *Katavi National Park*. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa michango yao kwa jamii na vijiji vinavyozunguka hifadhi naiomba Serikali iendelee kuboresha mazingira ya hifadhi na miundombinu ili kujenga mazingira bora kwa utalii na kuendelea kuitangaza duniani, lakini si vibaya kupitia kwako Mheshimiwa Spika na Waziri wa Maliaasili na Utalii kuiomba tena *TANAPA* kutusaidia kujenga wodi ya watoto na kina mama wajawazito katika *Town Clinic* ili kupunguza msongamano katika hospitali ya Wilaya ambayo hata watumishi wa hifadhi wanategemea kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupata maelezo ya ziada juu ya totauti ya mishahara ya watumishi wa Idara ya Wanyamapori, ambao wote kwa ujumla hupata mafunzo yao katika vyuo ama Pansiasi Mwanza au Mweka, Moshi na kupewa ajira ama Serikalini Idara ya Wanyamapori au *TANAPA*, mazingira ya kazi, athari na usalama katika maeneo hayo yanafanana, inakuwaje mishahara ya askari wa kawaida (*game*) na askari huyo huyo (*TANAPA*) inapishana, jambo hili linapaswa kuangaliwa ili kupunguza malalamiko ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upungufu wa askari wa wanyamapori, watumishi wa misitu na nyuki ni wachache sana Mpanda ukilinganisha na eneo ambalo wanalismamia.

Lakini tatizo pia lililopo na uhaba wa maeneo ya kuwindia wananchi ada zake ambazo nahisi ni kichocheo cha kuendelea kwa ujangili.

Katika Wilaya ya Mpanda maeneo yote yenye wanyama wamepewa wageni ni vitalu vya kuwindia, wananchi hawa wameachiwa maeneo ya wazi ya misitu isiyokuwa na wanyama kabisa, hivyo basi wananchi hawa watalazimika kuingia katika maeneo ambayo yana wanyama ni vema basi wananchi hao wakapewa maeneo mazuri ya kuwindia. Pia ni lazima tuangalie ongezeko la watu na kutoa maeneo kiasi cha mahitaji ya maendeleo na ustawi wa watu kwa kupunguza maeneo ya *forest reserve* iwapo mahitaji hayo ya wananchi ni lazima ustawi wao pia ni muhimu ili wasionekane kila siku ni wavamizi wa hifadhi za misitu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nitapenda kushauri na kupata maelezo ni juu ya hizi hifadhi ambazo zinakuzwa sasa kama Katavi na nyinginezo ni lazima sasa fursa zote za kuendeleza wapewe wazawa (Watanzania) kwa maana ya hoteli na huduma nyingine ili kupunguza haya malalamiko ya kutoa maeneo yetu kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya mambo ya Kale. Taifa lolote ambalo haliwezi kutunza, kuhifadhi na kulinda historia yake Taifa litakufa bila kuacha athari. Tunayo maeneo mengi ya kihistoria na mambo ya kale lakini hayatunzwi ipasavyo. Nimetembelea Kaole inasikitisha sana.

Juhudi za makusudi zinahitajika kuboresha na kutunza maeneo yote, hata Tabora tembe la Kwihara au magofu ya Kilwa na mapango au Michoro ya Kondoa haiwezekani tukaacha yanaharibika, na fedha zinazotengwa kwa eneo hili hazitoshelezi kabisa. Urithi huu tusikubali ukapotea, leo Misri wanapata watalii kwa ajili ya *Pyramids* tu ambazo zimejengwa karne na karne zilizopita lakini waliwekeza na kuzitunza nasi tunaweza.

Mheshimiwa Spika, kwa makusudi kuongeza maeneo ya vivutio vya kitalii katika Mkoa wa Rukwa zaidi ya hifadhi ya Katavi yapo pia maporomoko ya Kalambo (*Kalambo falls*) pia samaki wa mapambo katika Ziwa Tanganyika na fukwe zake nzuri na kwa sababu ya umbali na miundombinu hafifu zingetenenezwa taratibu mahsusi na ada za kuvutia ili kuwashawishi watalii kuja kutembelea hifadhi ya Katavi ni hifadhi pekee yenye misitu minene na Nyanda za wazi na kila aina ya wanyama.

Mheshimiwa Spika, mwishoni ni vitalu vya kuwindia Watanzania wanaweza kusimamia na kuendeleza biashara hii basi na wananchi hususan wa maeneo yenye wanyamapori hata kampuni moja iwe *resident company* ya Wilaya husika. Nadhani Wizara itazingatia na kutoa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, *Ngorongoro Crater* kuna yale malori makubwa ya *over land* yanayoleta wageni wanaendeshe kutoka Ulaya mpaka *South Afrika* kupitia Tanzania magari haya ni mazito na huwa yanateremkia *Crater*.

Ushauri wangu magari haya yasiteremke kule *Crater* yana-park pale juu halafu wakodishe magari madogo kuteremka *Crater* ili kuzinusuru zile barabara ndani ya *Crater* ambazo zina uwezo wa kubeba magari madogo.

Mheshimiwa Spika, kuna *NGO* iliyopo pale mjini Moshi inayoitwa *Kilimanjaro Porters Project* hawa ni wazungu kutoka Marekani tangu wazawa wawe ndio wenye kupeleka wageni mlimani wameanza kuhujumu *Local Town Operator* na kusema hawajali ma-porter. Wanapeleka habari mbaya sana kwenye *internet* hata zile habari zilizotoka kwenye magazeti. Hawa hawalitakii Taifa letu mema. Swali watu hawa wachunguzwe na Idara ya Uhamiaji wanafanya kazi pale kwa sheria ipi na kibali gani? Na je, fedha wanazopata kutoka kwa wafadhili hao kwa ajili ya kusaidia *porters* hawa ni nani anazichunguza? Kwa kuwa hata vifaa vyenyewe hawavitoi kwa ma-porter na huku wanadanganya wanajali mavazi ya ma-porter lakini *porters* wakienda pale hawana vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, watu hawa nakuja kujitafutia ajira na kutufanya sisi wajinga. Tayari kuna vyama vya ma-porter na operators wapo hata *KINAPA* wapo, wanafanya nini?

Kuhusu kutangaza Tanzania katika maonyesho ya Kimataifa, maonyesho ya utalii mjini London yanakaribia *World Travel Market (WTM)*.

Naomba yasije yakatokea yaliyotokea *ITB, German* kwa Zanzibar kuwa na banda lao wenyewe. Tuuze nchini moja kama matangazo yetu yanavyosema *The Land of Kilimanjaro, Zanzibar and Serengeti*. Kwa kweli ikitokea mkanganyiko mkubwa sana pale *German* wakati sisi Tanzania Bara tunaiuza Zanzibar bila ubaguzi wowote, naomba sana hili liangaliwe katika maonyesho yote.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Mheshimiwa Ezekiel Maige kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri na Naibu Waziri, nawatakia kila la heri kuongoza Wizara hii muhimu. Nawapongeza pia kwa kuleta hotuba hii ya Bajeti ya Wizara yao, ikiwa ni mara ya kwanza kwao kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa wamefika wakati mabadiliko makubwa ya uongozi yamefanyika karibu katika sekta zote za Wizara hiyo na hasa katika sekta za misitu na wanyamapori. Bila shaka huu umekuwa mwanzo mzuri kwa uongozi wa sasa wa Wizara, ni wakati mzuri kuongoza Wizara baada ya dhoruba.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri Wizara iangalie upya kuhusu utoaji wa lesini za kusafirisha na kuvuna miti. Sasa hivi kuna vurugu kwenye *road blocks* hasa kati ya Masasi na Dar es Salaam. Maafisa Misitu Wilaya wanaogopa kutoa leseni hivyo biashara ya mbao nchini ni ngumu kweli.

Mheshimiwa Spika, nashauri uwepo utaratibu mzuri utakaotenganisha baina ya biashara ya mbao nchini na wale wanaopeleka nje. Biashara ya mbao ndani ya nchi iwekewe taratibu zake zinazoeleweka na ziwe tofauti ya zile za nje.



Mheshimiwa Spika, naunga mkono suala la kuongeza thamani katika mazao ya mbao kabla ya kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya wanyamapori, naona kuna maendeleo makubwa yanayoonyesha utulivu katika idara hii. Mabadiliko ya watumishi waandamizi yaliyofanywa yataleta matunda mema. Mipango ya maendeleo ya sekta bila shaka yatakuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii, inaendelea kukua kwa kasi hasa katika ongezeko la watalii na kadhalika. Mkutano wa Sullivan nao ulikuwa tangazo la pekee kuhusu utalii wetu.

Lakini bado tuna matatizo pale *Airport* sehemu ya kufikia wageni, eneo lile linatia aibu hasa wanavyojazana watalii wakitokwa majasho katika foleni ndefu. Kwa nini mpango wa kufanya *Terminal I* ishushie *Domestic passengers* ili *Terminal II* itumike kwa wasafiri wa nje?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja, mpaka nipate ufafanuzi wa kina na wakati ukifika nitatumia kifungu cha 103 (2) cha kuondoa shilingi katika Makadirio.

Naomba ufafanuzi mambo yafuatayo, kwanza ni lini wananchi wa vijiji vya Semu, Bugayabahya, Lubiga, Nyanza, Mwanindwa, Malwilo, Tindabuligi, Ming'ongwa, Butuli, Matale, Mwamhongo, Mwasengela na Nghanga vilivyoko kando kando ya pori la akiba la Maswa, jimbo la Kisesa Wilaya ya Meatu vitatengewa eneo la uwindaji wa ajili ya kitoweo na shughuli zingine za kijamii? Serikali kupitia maswali yangu ya msingi na nyongeza imekuwa ikiahidi kutenga eneo hilo *Hansard* shahidi. Pia Naibu Waziri alitembelea vijiji hivyo na kujionea mpakani mlivyokaa vibaya ni mateso kwa wananchi.

Pia kama ni makosa yalifanywa na Serikali kwa kuwa haikutenga eneo la shughuli za jamii (*controlled area*), aidha, ifahamike kwamba eneo ninaloliomba si kwa matumizi holela mbali kwa utaratibu wa *WMA* nina pendekeza kutoka mpakani kuingia ndani ya pori la akiba kama mita 200 au itakavyoonekana inafaa. Hii ni haki ya wananchi Kikatiba na matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Kama Serikali itaendelea kupiga danadana na kupuuza haya madai ya msingi basi tuwaruhusu waende mahakamani kudai haki zao.

Pili, naomba ufafanuzi juu ya mgawo wa asilimia 25, kwa nini fedha hizi haziletwi katika halmashauri kwa wakati? Kwa nini Halmashauri 13 kati ya 44 zimelipwa gawio, je, zinazobaki zitalipwa lini? Kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Meatu katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 imepokea shilingi 12,100,000 kati ya 50,000,000 stahili ya 25% lini fedha hizi zitakamilishwa kwa kuwa upungufu umeathiri miradi iliyopangwa?

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya maliasili na utalii. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo, kwanza ni kuhusu sekta ya utalii, kwa kuwa sekta ya utalii ni muhimu sana na inachangia Pato la Taifa na kwa kuwa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya utalii ni kidogo, je, Serikali itakubaliana nami kwamba ipo haja ya kuongeza Bajeti ya sekta ya utalii ili sekta hii iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mfuko wa utalii ili kuwezesha Watanzania wengi kuweza kushiriki katika shughuli za utalii kwa kuwa utalii sio wageni kutoka nje ya nchi lakini Watanzania wapewe elimu ya kutosha ili washiriki katika sekta ya utalii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundomibu na hasa mawasiliano ya barabara ili kuvutia watalii wengi kutembelea mbuga zetu za wanyama bila matatizo wakati wa mvua (masika) na kiangazi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma mbalimbali na hasa katika hoteli yetu ili kuvutia watalii wengi zaidi. Je, Serikali imeweka mikakati gani wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na ulinzi wa usalama wa kutosha kwa watalii wanapoingia katika nchi yetu. Bila usalama na ulinzi wa kutosha watalii wataogopa kuja Tanzania kutembelea nchi yetu na Taifa litakosa mapato kutoka sekta ya utalii. Je, katika mwaka 2006/2007 na 2007/2008 sekta ya utalii imeliingizia Taifa letu mapato ya shilingi ngapi, asilimia ngapi ya Pato la Taifa.

Kuhusu sekta ya wanyamapori, kwa kuwa sekta ya wanyamapori ni muhimu sana na watalii wengi huja Tanzania kuona wanyama katika mbuga zetu za wanyama, je, Serikali imeweka mikakati gani wa kuwapatia vitendea kazi vya kisasa ili kupambana na ujangili katika mbuga zetu? Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi yao na kuwaendeleza kitaaluma.

**MHE. MRAMBA B. PESAMBILI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naishukuru Wizara kwa kushughulikia tembo wanaosumbua Rombo kutoka Kenya. Mwaka jana nilibahatika kuzungumza na Rais Kibaki, kuhusu hatua gani zichukuliwe na Kenya na Tanzania, kudhibiti tembo na kufidia wananchi wanaoathirika. Rais alishauri Mawaziri husika wakutane na kushauri. Napendekeza Mheshimiwa Waziri aanze mjadala huo na Kenya (wenye mali). Nipo tayari kushiriki ikibidi, kama mdau muhimu. Pindi tukisubiri, naomba tutimize ahadi za Wizara na maelekezo ya Makamu wa Rais ya Januari, 2008 kuhusu suala la tembo Rombo.

Watalii hufika kupanda Mlima Mawenzi (*Loitoktok Route*), wakitokea Arusha – Moshi – Dar es Salaam – Mombasa – Nairobi na Mbuga za Kenya za Tsavo na Amboseli. Hivi sasa barabara ya lami kuunganisha Marangu – Tarakea – Loitoktok hadi Emali kuelekea Nairobi inatengenezwa kama Barabara ya Afrika Mashariki pande

zote mbili. Watalii wataongezeka zaidi itakapokuwa tayari na hasa kama mpango wa barabara ya kuzunguka Mlima Kilimanjaro utakamilika.

Tuna tatizo la hoteli muafaka. Tulielezwa kuwepo kwa Mfuko wa Ufaransa kukopesha wenye nia ya kujenga hoteli. Naomba maelezo vipi Rombo tutumie fursa hiyo? Aidha, nashauri Wizara ione namna ya kusaidia wawekezaji kwenye miji na maeneo ya pembezoni kama Rombo ili kutumia fursa zao za kuvutia watalii. Kwa mfano, kutafuta wawekezaji wadogo au wa kati kuingia ubia na Halmashauri za Wilaya au wajasiriamali wa kati, kudhamini mikopo kama vile ya vyombo vya fedha kwa mfano, *NSSF*, *PPF* na kadhalika.

La tatu ni ufugaji wa nyuki wa asali na nta Wilayani Rombo. Wilaya imeamua kukumbatia Mradi wa Nyuki kwa utaalumu wa kisasa. *Honey care* wapo tayari kushauri na kununua mazao hayo. Tutahitaji Serikali itusaidie mafunzo na fedha za kufanikisha Mradi huo unaokusudiwa kuwa zao la biashara la Wilaya hiyo.

La nne, linahusu ujenzi wa *airstrip* kwa ajili ya watalii wanaotaka kupanda Mlima Mawenzi na wale watakapata ajali barabarani au wakipanda mlima. Hawa wataweza kupelekwa hospitali kubwa kama KCMC au za Nairobi. Wilaya haina hata kiwanja kimoja cha aina yoyote. Tusiubiri ajali zitokee! Ardhi ipo. Halmashauri haina uwezo. Nitashukuru kujibiwa hata kwa barua.

Mheshimiwa Spika, namalizia tena kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kusema naunga mkono hoja hii na pia nazipongeza juhudi za Wizara hii katika kukuza utalii na pia uendelezaji maliasili. Hata hivyo, ninayo maoni yafuatayo:-

(a) Kutokana na Wilaya ya Manyoni kuwa na *Game Reserves* za Rungwa, Mukesi na Kizigo, wanyamapori huishi katika mapori hayo na kuua watu (Simba) na kuharibu mazao (tembo) takriban kila mwaka. Maafisa wa *Game* wa Kata na Tarafa inabidi wapewe mafunzo kwani hivi sasa sio effective. Aidha, Wizara iwe karibu na maeneo kama yetu, kwa kuhakikisha wanakuwepo *Game Officers* wenye uwezo pia zana hasa silaha na risasi.

(b) Tunaomba ushirikiano wa hali na mali kutoka Wizarani kuhusu uendelezaji wa kupanda miti hasa ukuzaji wa miche katika *nurseries*. Katika Halmashauri ya Manyoni, upandaji miche katika vitalu umefifia, tuna mpango wa kufufua. Wizara inakaribishwa kushirikiana hasa katika upatikanaji wa mbegu na utaalumu. Aidha, utafiti wa mikaratusi tuleteeni matokeo yake hasa ile inayovumilia hali ya ukame (*semi arid areas*) ili tupande katika maeneo hayo.

(c) Hotuba ya Waziri imetambua ubora wa asali ya Manyoni, ambayo ilipata nishani ya dhahabu kwa ubora. Wizara ije tushirikiane kuli-*promote* zao hili kupitia vikundi vya vijana na wanawake ili Tanzania tuwe namba moja katika zao la asali duniani.

Maeneo ya kufuga nyuki tunayo makubwa, tatizo letu ni utaalamu na vifaa. Wizara inaweza kusaidia. Ahsante.

**MHE. SIGFRID S. NG'ITU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Tatizo la kwanza, wapiga kura wangu kule Nanganga, Ruangwa wanaliwa na mamba wa Mto Lukuledi. Tatizo hili litakwisha lini, tangu mwaka juzi tanalalamika lakini bado lipo?

Tatizo la pili, mbona askari wetu wanaolinda mapori ya wanyama hawana usafiri? Tangu mwaka 2006 nalamikia hili; wanalinda vipi kwa kutembea kwa miguu au baiskeli?

Tatizo la tatu, sisi kule hatuna kitoweo labda toka kwa wafugaji wa Kimasai wanaouza ng'ombe wao eneo la Rufiji Mkoani Pwani. Nao ni bei kubwa ikilinganishwa na nyati, swala walio katika eneo la Selous ambao huwa wanaonekana. Je, hatuwezi kupata msaada wa bwawa la samaki mkishirikiana na Idara ya Uvuvi na sisi tuwe walinzi wazuri wa wale wanyama kule Selous? Ahsante.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, mara baada ya Bajeti afanye ziara Wilayani Mtwara kwenye Mradi wa *Marine Park* katika Vijiji vya Nalingu, Msangamkuu, Kitongoji cha Mnazi na Ruvula, Msimbati na Kilambo ili kuzungumza na wananchi na kusikiliza kero zao juu ya maendeleo ya *Ruvula Marine Park*.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalamu wa Wizara na Taasisi za Wizara kwa hotuba nzuri. Bila kusita, naunga mkono hoja.

Kuhimiza upandaji wa mashamba makubwa ya miti: Mwaka 1987 nilipokuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, tulibaini umuhimu wa kuhimiza mashamba ya miti ya kupandwa yanayomilikiwa na Serikali Kuu. Serikali za Mitaa, Makampuni, Watu Binafsi, Vijiji na mashule kwa lengo la kuongeza kipato na kuokoa misitu yetu ya asili isitoweke. Je, hali ikoje sasa? Ibara ya 44 ukurasa wa 24 inaelezea mashamba ya Serikali tu na hata hivyo, nashauri maeneo ya mashamba ya Serikali yapanuliwa na mapya yaanzishwe. Wizara itafakari hoja ya kutoa miche kwa wananchi vijijini hasa wanawake kwa bei ndogo au bure ili wapande miti kwa wingi.

Barabara za utalii Wilayani Lushoto: Utalii hasa *nature tourism* ni sekta inayoleta matumaini Wilayani Lushoto. Tatizo kubwa ni hali mbaya ya barabara na njia za miguu. Wizara itasaidia vipi eneo hili?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nauanga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Ni matarajio yangu, Wizara inatambua vivutio vya utalii vinavyopatikana katika Jimbo la Nkenge Wilaya ya Missenyi. Vivutio vya utalii vinavyopatikana katika Jimbo la Nkenge Wilaya ya Missenyi ni pamoja na mapango ya mambo ya kale ya Mugano, Bwanja, Tarafa ya Kiziba. Msitu wa Minziro wenye vipepeo visivyopatikana sehemu nyingine duniani; Kumbukumbu za Vita ya Kagera; Msitu wa Mukyamo – Kantare ambao ni chimbuko la mibuni na kuna nyoka ambao hawapatikani sehemu nyingine duniani; Mapango ya Nyakijoga pamoja na Vivutio vya Utamaduni (*Cultural Based Tourism*); na mabaki ya Kambi ya Wajerumani, pamoja na Reli (njia za reli), ambayo inasemekana ilitumika wakati wa Utawa wa Wajerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie kutangaza vivutio tajwa hapo juu ukiwa ni pamoja na kutambua uwepo wa vivutio nilivyovitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Wizara kwa kuandaa taarifa nzuri na wanavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali na hasa Wizara, inifahamishe kuhusu Sikonge kupandishwa hadhi maeneo ya Hifadhi na Rais Mkapu na mpaka sasa wananchi hawamiliki maeneo hayo kama Sheria inavyostahili. Wananchi wana haki yao kama *WMAs* inavyoelezea Sheria zinazostahiki kufanywa.

Mheshimiwa Spika kuna shida kubwa sana ya Serikali kuleta Sheria ya Wanyamapori hapa Bungeni. Kuna nini Sheria hiyo inachelewa kuletwa na shughuli za wanyamapori kufunya kazi zake katika muundo wa Sheria na kuacha minong'ono ya ucheleweshaji wa Sheria hiyo?

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri anijibu; je, kumeshafanyika utafiti kila mkoa kufahamu mambo ya kale yaliyopo katika mikoa hiyo na yanahifadhiwa vipi; na yanaongeza kipato kutokea mikoani humo kwa kiasi gani?

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa uteuzi wake kuwa Waziri kamili. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Maige, kwa kuteuliwa nafasi hii. Nampongeza pia Katibu Mkuu, Ndugu Blandina Nyoni, Wakurugenzi, Viongozi wote na Wafanyakazi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi nitachangia sehemu chache:-

(i) Kwa muda mrefu Mapango ya Amboni yamekuwa kivutio kikubwa na kitega uchumi kwa Mkoa wa Tanga. Miaka ya karibuni, mapango haya yamekuwa

yanapoteza sifa na kutokusikika, hasa baada ya kupata tatizo la mafuriko kule maeneo ya Amboni Wilaya ya Tanga. Je, Wizara inasemaje kuhusu kupungua kwa umaarufu huu na ina mkakati gani kurudisha heshima ya mapango haya, yenye historia kubwa sana ya kina Cekello ambapo vizazi vyetu vinakosa?

(ii) Je, Wizara inajua kuwa kule Tanga Mjini maeneo ya Chumvini karibu na maeneo ya Amboni kuna chemchemi ya maji moto yenye *sulphur* na kwamba, watu wengi wakiwemo watalii wanavutiwa kwenda kuona na hasa pale kinaposemekana kuwa maji hayo ya uvuguvugu na yenye *sulphur* ni dawa pia ya Magonjwa ya Ngozi? Kama ndiyo, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa imeangalia vipi eneo hili ambalo limeachwa ovyo, ili kuweza kupahifadhi na kuweza kupatumia kama sehemu ya kitalii na utafiti kwa faida ya nchi hii?

(iii) Maeneo ya uwindaji (vitalu) Wilaya ya Kilindi sehemu za Saunye na Mkindi: Kwa vile watu kutoka nje ya Wilaya ya Kilindi na Handeni, wamekuwa wakipatiwa leseni za kuwa na vitalu vya uwindaji; ni kiasi gani wananchi wa maeneo yale hususan ya Mkuidi, Saunye na maeneo ya Jaila wanafaidika? Mbona hali za wananchi ziko hoi pamoja na ushuru au fedha wanazolipia hawa waliopewa leseni; ni nini kimaendeleo na kijamii wamefaidika wananchi hawa?

(iv) Handeni na Kilindi ni Wilaya miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Tanga zinazozalisha sana asali wa nyuki wanaouma na wasiouma. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuongeza zao hili katika maeneo haya, kwani ingawa wapo maafisa ugavi wanaoshughulikia nyuki, bado hakujawa na tija kwa vile wengi wanaorina asali bado wanatumia njia za *ki-primitive* za kurina kwa kuchoma moto, matokeo yake kusababisha mioto na uharibifu wa mazingira?

Nataraji mtanipatia ufafanuzi vinginevyo, nawapongeza kwa maandalizi yenu mazuri katika Banda la Maliasili na kuwa kivutio kikubwa kwa Watanzania wakati wa Maonyesho ya Sabasaba (*DITF*). Nami najipanga nikatembelee na kupumzika katika maeneo ya Kitalii. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri sana na aliyoisoma kwa ufanisi mkubwa. Aidha, hotuba yake inakamilishwa na takwimu muhimu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Kwa upande mwingine, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri, Bibi Blandina Nyoni, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Mashirika, pamoja na Wasaidizi wote chini yao, kwa kazi nzuri na yenye ufanisi, iliyomuwezesha Waziri kutoa hotuba inayoeleweka na yenye kiwango cha juu humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, natamka tena kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pili, ninatoa pole kwa kifo cha wafanyakazi waliofariki kwa ajali. Tatu, hongera kwa bajeti nzuri iliyogusa wananchi.

Lakini pia nilulize swali; katika Bajeti hii sijaona sehemu yoyote iliyotaja kuhusu mjusi (*Dinosaur*) aliyechukuliwa Tanzania kwenda Ujerumani. Je, suala hili kwa nini halipo na kwa Serikali hata haitaji *skeleton* ya mjusi (*Dinosaur*) aliyetoka Lindi, Kijiji cha Mipingo kwenda Ujerumani ambaye hadi leo yupo huko? Sisi Lindi tupo tayari kumpokea na eneo la kumuweka tumemtenga mleteni tu.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuiunga mkono hoja ya Waziri kwa asilimia mia moja, kutokana na jinsi ilivyoandaliwa na kugusa maeneo karibu yote. Nawapongeza Wataalam wote wa Wizara hiyo, kwa ushirikiano mzuri ambao matunda yake yamekuwa ni hotuba nzuri ya Waziri aliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa ufupi katika vipengele vifuatavyo:-

Hifadhi ya Pori ya Moyowesi/Kigosi, mipaka yake inapakana na Vijiji Kifura, Busunzu, Kitahana, Rusohoko, Murungu, Kakonko, Muganza na Kiyobera. *Population* ya Vijiji hivi imeongezeka kuanzia wakati ulipowekwa mpaka. Kwa mantiki hiyo, ipo haja ya makusudi mazima ya kurudisha mpaka nyuma ili wananchi wa vijiji hivyo waweze kupata maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kurumbanga kipo karibu na mto mkubwa ambao unayo madini na pia ipo chumvi ambayo hutumiwa na wananchi wa vijiji vipatavyo vitano. Ili wananchi waweze kufaidi matunda yatokayo katika mto huo ni budi mpaka urudi nyuma ili kutoa mwanya wa uchimbaji wa chumvi, chokaa na chumvi bila kukiuka ama kuvunja sheria .

Mheshimiwa Spika, lipo agizo ambalo llinawabana wananchi kupasua mbao. Hali hii inawagusa wajasiriamali wanaoishi kwa kutegemea kazi za mikono kama vile mafundi seremala na wajenzi. Sheria hii ilegezwe kwa kutenga maeneo maalum ambayo wajasiriamali hawa watakuwa wakipata malighafi hiyo bila kuingiliana na kitendo cha kukiuka taratibu ama kuvunja sheria.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, baada ya Pori la Kimisi na Burigi kutangazwa kuwa Hifadhi ya Taifa, wanyamapori hasa tembo wamezaliana kwa wingi Wilayani Karagwe. Tembo hao wanaingia kwenye mashamba ya wananchi na kuharibu mazao yao na wakati mwingine kusababisha vifo. Maeneo yanayoshambuliwa mara kwa mara ni ya Kata za Nyakakika, Nyaishozi, Nyakasimbi, Nyabiyonza, Kihanga, Rugu na Ihembe. Ni jambo la kawaida kukuta kundi la tembo kuanzia 100 – 300 katika makazi ya watu. Tatizo lililopo, Wilaya ya Karagwe haina Watumishi wa Maliasili; hivyo, tunaomba watumishi wa kutosha Wilayani na vifaa vya kutosha mfano risasi, bundiki, magari, fedha na kadhalika.

Akijibu swali langu hapa Bungeni, aliyekuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zabein Muhita, aliahidi kuwa tayari Serikali imetenga fedha za

kujenga Ofisi ya Wanyamapori Jimboni Karagwe ili kuondoa kero ya wanyamapori kwa Wananchi wa Jimbo la Karagwe. Ajabu, Bajeti hii haionyeshi hata kidogo dalili ya kujenga ofisi hiyo!

Napenda kuifahamisha Serikali kuwa, kutojenga ofisi hiyo Karagwe ni dhahiri kuwa Serikali haithamini maisha ya wananchi wangu na mali zao. Tembo wameua watu wengi, hakuna hatua za makusudi za kuondoa kero hii. Ninashauri fedha zitengwe katika Bajeti hii na ziende kujenga ofisi hiyo Karagwe haraka iwezekanavyo, kwani hivi ninapoandika wananchi wangu wanaendelea kupambana na tembo kwa kutumia mawe na vijinga vya moto. Hii ni aibu kwa Wizara na jeuri ya Watumishi wa Wizara hiyo kutotusikiliza sisi wawakilishi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yaani Naibu Waziri na Waziri waliopita, wamekuwa wakiahidi kwenye bajeti zilizopita kuitembelea Wilaya ya Karagwe na kujionea hali halisi lakini hawafanyi hivyo.

Wilaya ya Karagwe hasa Jimbo la Karagwe lina matatizo mengi, ikiwemo kuuwawa na majambazi toka nchi jirani na kama hiyo haitoshi, tembo nao wameendeleza mauaji kwa Wananchi wa Karagwe. Hili halihitaji wafadhili, Serikali yetu inaliweza.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii hadi ofisi ijengwe.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, maoni yafuatayo ni muhimu:-

Kwanza, *TAWIRI* Wawezeshwe na Dr. Simon Mduma amekaimu kwa muda mrefu sasa, kwa nini hathibitishwi kwa nafasi hiyo; kama hatoshi kwa nini hateuliwi anayetosha?

Pili, tumeambiwa siku nyingi sasa kuwa Chuo cha Wanyamapori Mweka kilianza kutoa mafunzo maalum kwa kada ya *Profession Hunters*. Je, ni kwa nini mafunzo hayo hayajaanza kutolewa hadi sasa?

Tatu, hoteli zilizo ndani ya hifadhi zetu; *GRs, NPs, NCAA* na kadhalika, zinalipa fedha kidogo sana kama *concession fees* na malipo mengine kama *bed fees*. Kwa nini kila Bodi za *TANAPA* na Ngorongoro wanapoamua kuboresha mapato ya hifadhi kwa kuwataka wenye hoteli walipe, Wizara inachelewa kuunga mkono Bodi zake yenyewe?

Nne, Hifadhi zetu zipangwe upya nchi nzima ili tuwe na *an Ecosystem Based Protected Area System* na pia zichambuliwe ili kuona endapo ni lazima *GR* iendelee kuwa hivyo, *FR* iendelee kuwa hivyo, *NP* iendelee au zibadilishwe hadhi. Pili, Hifadhi za Bahari – *Marine Parks and Reserves* zirudi kwenye *Protected Area System* chini ya *TANAPA* baadhi na baadhi ziende katika shirika jipya ambalo Kamati ya Bunge inapendekeza lianzishwe. Tatu, *Amani Forest Reserve* ihamishiwe *TANAPA* kwa uhifadhi bora zaidi na kuvutia watalii zaidi.

Tano, baadhi ya hoteli zilizo nje ya hifadhi hasa huko Wilaya za Ngorongoro, Monduli, Longido, Simanjiro, Serengeti na kadhalika; hayalipi chochote cha maana kwa



Wizara, pia hoteli hizi zina mikataba feki na Halmashauri za Wilaya ambapo Halmashauri hizo hulipwa kiwango fulani kwa kila mgeni anayelala kwenye *Tourist Camp* hizo. Hali hii ni vyema ikabadilika.

Sita, Dr. Kilahama alikuwa Morogoro; pale kuna Kiwanda cha Polyester cha Mohamed Enterprises, ambacho kinakwepa kutumia umeme badala yake kinatumia kuni na kuharibu mazingira kwa kiwango cha ajabu; kwa nini wanaruhusiwa kuvuna miti ovyo kiasi hicho?

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri, yenye kuleta mwelekeo mpya wa kutuletea maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Katika changa moto zilizo mbele yenu, kubwa kuliko yote ni kuhakikisha kuwa, maliasili yetu tunapata fedha stahili kuliko mapato yanayopatikana sasa. Tunaomba sana watalii wote walipe fedha hapa Tanzania, wala tusikubali watalii kulipia gharama zote huko Ulaya/Amerika kwa mpango wa *Pre-paid Tourist Packages*.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuzingatia maslahi ya nchi yetu, kwa kutenda haki katika mgao wa vitalu vya uwindaji. Aidha, asilimia ya fedha inayolipwa kwa vijiji vinavyozunguka hifadhi iongoezwe, ili wananchi waone faida ya kuhifadhi na kuilinda maliasili yao.

Hifadhi ya Selous, sehemu ipo Wilaya ya Rufiji; naomba kuishukuru Serikali kwa kukarabati Viwanja vya Ndege (*Airstrips*) vya Kingupira na Mtemele (Mloka). Hakika Hifadhi ya Selous inapendwa sana na watalii/wawindaji.

Tunaomba Wizara ichukue hatua ya kuinyanyua hadhi ya Hifadhi hii ya Selous na kuitangaza kwa nguvu zote ili kuongeza namba ya watalii na wawindaji wawe wengi.

Tunaomba Serikali ijenge barabara za kuifikia Selous kwa njia ya Dar es Salaam – Kibiti – Mkongo – Mloka (Selous). Ni barabara ya *TANROADS* Mkoa wa Pwani. Wizara iimarisha barabara ndani ya Selous. Kwa kweli barabara za ndani ya Selous hazipitiki hasa wakati wa masika.

Hatua za kuitangaza Selous kwa nguvu zote, itawafanya watalii/wawindaji kuja kwa wingi. Hatua ya kuongezeka kwa watalii itawafanya wawekezaji wajenge hoteli katika Mbuga ya Hifadhi ya Selous. Serikali lazima ikubali kujenga miundombinu bora ya kuifikia Selous na miundombinu ndani ya Selous ili iwe rahisi kwa wawekezaji wengi kujenga hoteli nyingi ndani ya Selous na hatua hii itanyanyua biashara ya nchi yetu.

Tunaendelea kuishukuru Serikali kwa kutuwekea minara ya Celtel katika Hifadhi ya Selous yote. Sasa tunazungumza kwa simu ya mkono bila wasi wasi. Asante sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja lakini naomba Wizara ifanye *Forest Audit* ya kujua miti iliyofyekwa kwa ajili ya magogo na mbao hasa katika Wilaya ya Rufiji na Kilwa. Kisha kuwe na *National Programme* ya kurudishia upandaji wa miti katika sehemu zote za misitu iliyofyekwa kwa ajili ya uroho wa kuuza magogo na mbao na wameacha nusu jangwa sehemu ya Wilaya yetu. Ahsante sana.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa Hotuba nzuri ya Bajeti.

Napenda kuipongeza Wizara hii kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana; watalii wameongezeka kwa sababu ya matangazo yanayoeleza vivutio vilivyopo hapa Tanzania. Ongezeko la watalii limeongeza pia Pato la Taifa. Hongera sana. Idadi hii ya watalii inaweza kuongezeka sana kama yafuatayo yatafanyika:-

Naikumbusha Serikali kuwa, vivutio vya utalii vipo kwenye sehemu nyingi hapa Tanzania. Tatizo ni kuwa Wizara inapotangaza vivutio, inatangaza Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Zanzibar tu na kusahau sehemu nyingine kama Kagera.

Kagera kuna *Game Reserves* zenye wanyama wengi, kuna misitu mikubwa, minene, yenye bioanuwai ya kupendeza na kuridhisha; kwa nini sehemu hizi hazipandishwi hadhi, zikatambuliwa kama Hifadhi ya Mazingira Asilia?

Kwenye Hotuba ya Waziri, Serikali imesema itaendelea na mchakato wa kupandisha hadhi ya maeneo mengine ili yatambuliwe kama Hifadhi ya Mazingira Asilia, lakini hakuna eneo hata moja la Mkoa wa Kagera linalotegemewa kuingia katika mchakato. Utalii unaongeza Pato la Taifa na kuinua kipato cha wakazi wa eneo hilo, hivyo kupunguza umaskini. Naomba Waziri anieleze; ana mpango gani wa kukuza utalii Mkoani Kagera?

Mheshimiwa Spika, nchi jirani ya Kenya inafanya vizuri katika Sekta ya Utalii kwa sababu pamoja na maliasili ya mbuga za wanyama, misitu, milima na kadhalika, vilelvile wameweka miundombinu inayovutia.

Juzi nilisafiri na ndege ya KLM kutoka Amsterdam, tulipofika KIA, Wazungu wengi waliteremka hapo wakielekea kwenye maeneo mbalimbali ya utalii nchini. Hii ni hatua ya kujivunia, kwani huko nyuma wengi wa watalii hawa, walikuwa wanateremkia Nairobi.

Naishauri Serikali ifanye yafuatayo ili wale watalii tuliokwishawavutia wasikate tamaa, wakahamia nchi jirani kama Kenya: Uwanja wa Kilimanjaro ukarabatiwe vizuri; *Arrival, Departure Longe, Duty Free Shops* vyote virekebishwe na vipendezeshwe ili vililingane na kukidhi viwango na ubora wa kimataifa; na tuendeele kujenga hoteli nzuri kubwa mfano Kati ya *Three* na *Five Star Hotels* tuweke viwanja vya *golf* na hivyo kufikia kiwango kizuri cha kimataifa, kitakachowavutia watalli wengi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, bila kuzingatia mambo hayo juu, hata watalii tulioanza kuwapata watatutoroka.

Nahitimisha kwa kumkumbusha Waziri wa Maliasili na Utalii kuwa, Kagera kuna *Game Reserves* za Kimisi, zenye tembo wakubwa kuliko sehemu yoyote Tanzania. Pia kuna chemchemi za maji ya moto, kuna miti iliyotumika kumtibu Livingstone, kuna Ziwa kubwa la pili duniani (Ziwa Victoria), kuna Mto Kagera, kuna Bonde zuri la Mto Ngono na kuna watu wenye tamaduni za kuvutia. Naomba Waziri anieleze kwa nini vivutio hivi havijaingizwa; je, ana mpango wa kuja Kagera kuviona; na ni lini?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, ndugu na jamaa wa familia za Marehemu Bi. Miriam Onesmo Zakaria, Ndugu Godfrey Mahinya na Rubani Pius Elisha Ng'walali. Msiba huu siyo wa Idara tu ni wa Watanzania wote. Mimi nawafahamu sana; ni wachapa kazi Marehemu Mariam alikuwa mwalimu hodari wa kuendeleza *WMAs* zote nchini. Mungu awalaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kupendekeza kuanzishwa maeneo mengine mapya ya *WMAs* ikiwemo Longido, pamoja na maeneo mengine ya Rufiji, Kilombero, Kigoma, Urambo na Monduli. Kutokana na matatizo yaliyotokea, naomba elimu juu ya matumizi ya wanyamapori itolewe. Wananchi watajua Sera na Kanuni za Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya uwindaji yanayomilikiwa na wawindaji, kuna uwindaji haramu unaoendelea. Wawindaji haramu wanatoka Kenya, Mjini Arusha na Moshi. Kwa mfano, mwanzo wa mwezi huu, Twiga watatu wameuwawa hapo Longido; cha kushangaza watuhumiwa wameachiwa wapo huru! Nategemea kwamba, uwindaji haramu utaendelea kwani Wizara peke yake bila kusaidiwa na Mahakama ujangili utaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia 25 inayorudishwa kwenye Halmashuri zinazozunguka maeneo ni Sheria iliyopitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo ni haki kila mwaka wanapewa fedha hizo. Nategemea tutapewa mgawanyo wa fedha hizo kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelewa kuhusu eneo la Lake Natron, ambalo mara nyingine Wizara ya Viwanda na Biashara wanatangaza kwamba ni eneo ambalo linajengwa Kiwanda cha Soda Ash huku Wizara ya Maliasili na Utalii wameweka kwenye eneo la ardhiouevu. Sitegemei kama kuna uwezekano wa kufanya mambo yote mawili kwa wakati mmoja kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Waziri, naomba kueleza kwamba, endapo Serikali itakubaliana na mapendekezo ya Kamati, eneo la Ziwa Natron litengwe liwe chini ya *Ngorongoro Conservation Area Authority* au Mamlaka nyingine.

Kwanza, ikumbukwe kuwasiliana na Wilaya ambazo Mlima Lengai na Lake Natron zinapakana nayo. Eneo hilo lipo kwenye eneo la Wilaya ya Ngorongoro na Wilaya ya Longido. Kwenye eneo la Longido wamependekeza WMA inayoanzishwa, ichukue maeneo yote ya Ziwa Natron WMA. Maana yangu ni kwamba, ushirikishwaji uwepo kwa jamii zinazozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba Longido inapakana na eneo kubwa la Kenya, majangili huingia kuwinda bila kizuizi chochote. Naomba Wilaya ya Longido wapewe gari ili waweze kupambana na majangili toka Kenya.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja hoja hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa masikitiko makubwa, natoa rambirambi zangu kwa niaba ya Wananchi wa Mfenesini, kwa msiba mkubwa uliosababishwa na ajali ya ndege ambayo ilipoteza maisha ya ndugu zetu wote muhimu waliokuwemo ndani ya ndege hiyo ndogo. Zaidi ya hayo ni kwamba, Bwana ametoa na Bwana ametwaa. Hivyo, kwa uwezo wa Muumba awapumzishe mahala pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Wizara kwa utendaji wake mzuri, ambao umeonyesha matumaini makubwa katika mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ambayo ndiyo kiungo kikubwa cha nchi kutokana na kuitangaza nchi, siyo ya Muungano lakini mimi nashauri ushirikiano mkubwa uongezwe baina ya Wizara hii na ile ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwani kufanya hivyo kutaboresha kuitangaza Tanzania katika mazingira mazuri ya kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, pili, nashauri Wizara hii ishirikiane sana na *UNICEF* katika kupata ushirikiano wa kifedha katika kuboresha magofu ya kale, ambayo ni rasilimali iliyotukuka katika ulimwengu huu na ujao, yaani vizazi vitakavyokuja badala yetu; mfano yale ya Bagamoyo, Kilwa, Lindi, Mangapwani – Zanzibar, Maruhubi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ilipoundwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne, tulielezwa kwamba, Mheshimiwa Balozi Sharrif ameteuliwa kuwa ni Mtangazaji Mkuu wa nchi yetu ya Tanzania nchi za nje. Bila shaka atakuwa na kitengo chake, lakini hadi hii leo hatujasikia *impact* ya taasisi hii juu ya mafanikio ya hasara.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara hii kuelekeza na kuhamasisha uwekezaji katika bahari ya uzamiaji (*Diving*) katika Bahari Kuu, kwani huko kuna bustani za ajabu ambazo duniani hazipo; hivyo, hii itaingiza fedha nyingi kuliko hata mbuza za wanyama.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara hii kupitia Bunge hili Tukufu, kukusanya vivutio vilivyopo katika Wilaya mbalimbali za nchi hii baadae kutungiwa kitabu ambacho kitaambukiza ushawishi wa kutembelewa na kuweka kumbukumbu za vivutio vilivyopo nchini vikiwemo vile vya mizimu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara hii kwa dhati kabisa, iangalie maliasili za kudumu hasa miti adimu nchini hasa mpingo na kadhalika, kwani imekuwa kwa muda mrefu sana ikikatwa na kusafirishwa nje. Mimi sina hakika, lakini hofu yangu kubwa ipo hapo kwani mpingo na mvule huchukua zaidi ya miaka hamsini ili uwe mti wa kuvunwa. Kwa mtazamo huu, vijana wa sayansi ya leo hawahamasiki na kuingia katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza sana Katibu Mkuu, Mama Nyoni na timu yake, kwa usaidizi mzuri kwa Waziri, lakini ipo dosari ndogo ya upotoshaji katika utendaji irekebishwe kabla Wizara hii yenye sifa kupoteza imani kwa Bunge na wananchi kwa jumla.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Wizara muhimu kama hii. Najua kuwa uwezo na juhudi za Mheshimiwa Mwangunga, zitamuwezesha kumudu Wizara hii hongera.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kwenye baadhi ya mambo ya utalii mkoani Dodoma.

Michoro ya Kale ya Mapango Wilayani Kondoa; huko Kondoa kuna michoro ambayo inadhaniwa kuwa na zaidi ya miaka milioni moja. Michoro ya aina hii ni michache duniani na Mkoa wa Dodoma tumebahatika kuwa nayo. Michoro hii ni kivuvito kikubwa sana kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Waziri ni kuomba Wizara iboreshe mazingira ya sehemu muhimu duniani; ifanye juhudi kutangaza duniani michoro hii ili kuvutia watalii; iishirikishe *UNESCO* katika jambo hili maana ndiyo wataalam wa jamii hii; na iboreshe miundombinu kwenda kwenye michoro hii.

Mheshimiwa Spika, huko Mbozi kuna *meteorite* kubwa sana iliyoanguka kutoka angani miaka mingi iliyopita na ni mojawapo ya *meteorite* kubwa sana duniani. Ombi langu kwa Wizara ni kulitangaza kwa makini duniani, maana ni kitu adimu daniani.

Pili, kuna umuhimu wa kuboresha miundombinu ya kuifikia na kuboresha mazingira ya mahali ilipo hiyo *meteorite*. Lazima niseme ni Watanzania wachache wanaojua kuwepo kwa *meteorite* (kimondo).

Barabara kutoka Dodoma hadi *Ruaha National Park*: Kutokana na kukua kwa haraka kwa Mji wa Dodoma, tunahitaji mahali pengi pa utalii ili wageni wanaokuja Dodoma wawe na mahali pa utalii pa kutembelea. Kinachohitajika hapa ni uboreshaji wa barabara kutoka Mpunguzi – Mwitikila – Naguki – Huzi – Manda – Ilangali – Mbuga ya Ruaha. Nija hii ndiyo fupi kuliko zote za kwenda *Ruaha National Park*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iwasiliane na *TANAPA* wasaidie barabara hii. Kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri ya Chamwino, haiwezi kuitengeneza barabara hii kufikia kiwango cha kupitika wakati wote. Tunamwomba Waziri kwa juhudi zake atusaidie.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atufikishie shukrani zetu kwa *TANAPA*, kwa msaada wao mkubwa wa kutujengea madarasa ya Shule ya Sekondari ya Kata ya Mpwayungu. Wananchi wanatoa shukrani nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunamtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri. Tunampa Hongera na kumtakia maisha marefu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa hotuba na mpango endelevu wa kukuza utalii na kulinda maliasili nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mapendekezo na maombi kama ifuatavyo:-

Kwanza, matokeo ya ukaguzi uliofanywa na Wizara hivi karibuni kwa Mkoa wa Dar es Salaam, umeonyesha mafanikio makubwa na pongezi kwa walioshiriki. Matokeo yameonyesha bado wapo watu wengi wanafanya shughuli za utalii bila kulipia ada ya leseni kisheria. Serikali itenge fedha ili kuwezesha ukaguzi kufanyika katika maeneo muhimu kama Moshi, Arusha, Tanga, Mwanza, Musoma/Serengeti/Manyara, Kusini mwa Tanzania. Hata katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, inaonyesha ukweli huo kama vile Manyoni, Singida na kadhalika.

Pili, tuongeze ubunifu katika kuwezesha watalii kupata vionjo vingi vya utamaduni wetu na vivutio wakati wanaposafiri kutoka sehemu moja ya eneo la utalii kwenda sehemu nyingine. Mara nyingi watalii wana uelewa wa maeneo machache hivyo wangetumia muda wao vizuri kwa kuona vivutio vingi zaidi.

Tatu, tuboreshe na kuongeza hadhi ya karatasi za leseni. Vipeperushi vilingane na vile vya kimataifa ambavyo tumeanza kwa kuwa na mhuri wa kisasa katika karatasi za leseni za utalii hivi sasa. Nawapongeza kwa hilo.

Nne, tuboreshe lugha na kuongeza uwezo wa wahudumu katika Sekta ya Utalii kuweza kuzungumza lugha tano na zaidi (Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kichina na Kiswahili sanifu). Ni dhahiri vyuo vyetu vilivyopo na chuo kipya kinachojengwa sasa, vitazingatia umuhimu huo.

Tano, kumetokea vitendo vya uhalifu hasa wizi dhidi ya watalii. Suala hili liliulizwa hata katika Mkutano wa Sullivan uliofanyika Mjini Arusha hivi karibuni. Wizara isaidiane na kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani (Polisi) ili kuongeza ulinzi na usalama kwa watalii. Njia moja na ziada ya Wizara na *TANAPA* kusaidia kujenga Vituo Vidogo vya Polisi katika maeneo muhimu kama ambavyo wananchi wanafanya katika maeneo ya vijijini.

Sita, kuboresha barabara ndani ya hifadhi ili watalii waweze kuvinjari katika maeneo makubwa zaidi na kuweza kuona vivutio vingi zaidi. Inatokea mara kadhaa, hasa wakati wa mvua, magari yenye watalii kushindwa kwenda mbali kutokana na tope hivyo kuwarudisha watalii katika hali ya kutoridhika.

Mheshimiwa Spika, nilifanikiwa kumtambulisha *TANAPA* mgeni mmoja (Mtanzania), Mr. Benston Mwakalinga ili awape teknolojia iliyopo sasa hivi inayotumika kuimarisha barabara za vumbi, changarawe na tope ziweze kupitika bila matatizo kwa wastani wa miaka mitano. Matumaini yangu ni kuwa, Wizara na *TANAPA* wataitathmini fursa hiyo na kufanya maamuzi ya kujaribu kuanza kuitumia.

Maonyesho ya Saba saba 2008, Wizara ya Maliasili na Utalii imefanya vizuri sana, kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa biashara na huduma za utalii katika Banda la Wizara. Mmewapa wadau heshima kubwa na nafasi ya kuwajulisha wananchi huduma zao na hata kutambua fursa zilizopo kwa Watanzania kuweza kufanya kazi za huduma kwa watalii. Nawapongeza sana kwa hatua hii.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani ni muhimu sana kwa utalii unaokua sana. Pia yapo mashamba manne, makubwa ya chai inayozalishwa na kuhitaji kusafirishwa toka Amani hadi Masoko ya Mnada, Moshi na Mombasa.

Tumefanya kikao cha pamoja mwezi Juni, 2008 katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kuwashirikisha Viongozi wa *Amani Natural Reserve*, *TANROADS* na Mdiwani na kukubalina Idara ya Misitu iruhusu *TANROADS* kupunguza kivuli cha miti inayozuia barabara hiyo kukauka hata baada ya mvua na hivyo kuathiri usafiri. Naomba Wizara ya Maliasili na Utalii itoe idhini hiyo katika ngazi ya juu. Matawi na miti hiyo michache ikatwe kwa kusimamiwa na Maafisa Misitu lakini gharama ziwe za *TANROADS*.

*TANROADS* watahitaji kifusi kidogo kuimarisha ujenzi katika kona mbaya 11 za barabara hiyo ili kuwezesha kuweka zege na mifereji. Eneo hilo ni dogo na haliwezi kuathiri mazingira. Mtaalam wa Misitu Amani, Bwana Sawe, aliridhia katika kikao hicho lakini sasa amesafiri kwenda Canada na mgeni ambaye yupo amezuia kazi kufanyika, tunaomba Wizara itusaidie kuiboresha barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jitihada kubwa anazofanya katika anga za Kimataifa za kuitangaza nchi yetu na kubwa zaidi kukubalika kwake katika anga hizo, hali ambayo imeleta hamasa kubwa kwa watalii wengi kuja Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu nzima ya Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayoifanya bila kusahau Bodi ya Utalii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna aina nyingi za vivutio vya utalii, kwa mfano, kuna visiwa vidogo vidogo kama Kisiwa cha Mbudya; Fukwe nyingi zenye kuvutia kama Kigamboni; Utalii wa Bahari wa kutumia boti kuwatembeza watalii; historia nzima na makabila ya Mkoa wa Dar es Salaam; Pugu Sekondari aliyofundisha Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere; Makumbusho ya Taifa; Kijiji cha Makumbusho – Mwenge; Wachonga vinyago vya mpingo walioko Mwenge; Soko la Kariakoo likiboreshwa litakuwa na mvuto kwa watalii.

Viwanja vya Mnazi Mmoja ni baadhi tu ya vivutio vya utalii vilivyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam, ambavyo vikiboreshwa vitasaidia sana kuinua uchumi wa wananchi na pia Serikali itaongeza pato lake.

Serikali iwe na mpango madhubuti wa kuvitambua vivutio vya utalii vya aina mbalimbali kwa kila mkoa na kuboresha *Centre* hizo ili mtu akitaka kuona utamaduni wa mkoa husika, aweze kufika bila wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe na Mkakati Maalum wa kuwaandaa wadau wote wa Sekta ya Utalii ili waweze kutoa mchango katika sekta hii. Mfano, taxi dereva: anampokeaje mtalii au yule dereva akimwona mgeni ni kana kwamba amemaliza matatizo yake yote ya mwezi huo? Utakuta anamtoza mahali pa Sh. 5,000 anamwambia ni Sh. 50,000; je, huu ndio ukarimu? Eneo hili ni muhimu wakapata mafunzo ya utalii na takrima (*Tourism and Hospitality*). Pia wajengewe uzalendo waipende nchi yao. Je, wafanyabiasha na wahudumu wa hoteli wana ukarimu unaokidhi haja ya huduma hii ya kitalii?

Katika kufikia matarajio hayo, kunahitajika ushirikiano wa Sekta mbalimbali na hasa Sekta ya Habari, Elimu, Jeshi la Polisi na kadhalika ili ziweze kuwaelimisha wananchi kuhusu ukarimu na utalii salama.

Mheshimiwa Spika, hoteli zilizoko Mbugani (*Wildlife Lodges*), Wizara izisimamie kwa karibu zaidi ili waweze kuboresha hoteli hizo kama *Lake Manyara, Ngorongoro Wildlife Lodge* na *Mikumi Lodge*, ambazo zinahitaji kuboreshwa ili ziwe katika kiwango cha Kimataifa na kuleta watalii wengi. Matatizo makubwa ni kama ifuatavyo: ukarabati; kuboresha huduma; maslahi ya wafanyakazi; na huduma ya umeme kwa saa 24, hasa *Ngorongoro Wildlife Lodge*.

Mheshimiwa Spika, naomba pia ufafanuzi juu ya hatma ya *Mikumi Wildlife Lodge*. Hali ikoje? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, *Cultural Tourism* siyo tu itatangaza utamaduni wa kila mkoa, bali pia itasaidia kutoa ajira kwa wananchi waishio vijiji ambao watashiriki kutangaza utamaduni wa mkoa husika. Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la watalii hapa nchini, Wizara ishirikiane na Jeshi la Polisi kutoa mafunzo kwa askari wengi zaidi wa wanyamapori na pia kuwalinda watalii wote wa ndani na nje ya nchi.



Mwisho, Wizara itie nguvu katika kutangaza utalii wa ndani; soko lipo ni ubunifu, uamuzi na utekelezaji kwa muda uliopangwa. Viongozi wabunifu wapo, tena wachapakazi, tunawaamini sana tena ni akina mama wawili wanaoiongoza Wizara hii nyeti sana kwa uchumi wetu. Mungu awasimamie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya bajeti na kazi nzuri wanazozifanya kwa maendeleo ya Sekta hii muhimu kwa maendeleo ya uchumi wetu.

Utalii ni Sekta ambayo maendeleo yake yanategemea uhusiano wa karibu sana na Sekta nyingine katika nchi yetu hususan Sekta za Miundombinu, Kilimo, Usafiri na Mawasiliano. Kilimo na Viwanda zina nafasi muhimu sana katika harakati za kuendeleza utalii wa nchi hii.

Sina haja ya kusisitiza umuhimu wa maingiliano ya karibu ya Sekta hizi kwa maendeleo mazuri ya utalii. Mipango yetu isisitize umuhimu huo ili kuhakikisha kwamba, kuzorota kwa mahusiano yanayosaidia maendeleo ya Sekta ya Utalii ni hatari kwa uchumi wetu.

Aidha, utalii wetu umejikita zaidi sehemu ya Kaskazini ya nchi wakati nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii katika sehemu nyingine za nchi. Maendeleo ya hizo sehemu nyingine za utalii (Magharibi, Kusini na kadhalika), yanakwazwa na ubovu wa miundombinu.

Shirika la Ndege lenye ufanisi ni muhimu sana katika kukuza utalii na kuhakikisha kwamba, uchumi wetu unafaidika zaidi na safari za watalii nje na ndani ya nchi. Hali ya Shirika letu la Ndege haisaidii sana maendeleo ya utalii wa nchi yetu. Tulirekebishe Shirika letu la Ndege.

Mheshimiwa Spika, misitu yetu ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wetu. Inatupatia nishati, dawa, mbao, asali na kadhalika. Nashauri tuisitize utunzaji wa misitu yetu ili iwe endelevu. Turuhusu uvunaji kwa mipango mizuri. Aidha, tuisitishie kabisa mauzo ya magogo nje. Tuhimize ujenzi wa viwanda vya mbao hapa nyumbani kwa utengenezaji wa samani (*furniture*) mbalimbali.

Vumbi za randa zitumike kutengeneza *chip* na *ceiling boards*. Vilevile tunaweza kuwa na viwanda au kiwanda cha uhakika cha karatasi, pamoja na *boxes*.

Nazipongee juhudi za kukirejesha Chuo cha Nyuki Tabora. Wananchi katika maeneo yenye nyuki wengi waelimishiwe ufugaji bora pamoja na urinaji mzuri unaozingatia upatikanaji wa asali yenye ubora mzuri na itakayokubalika katika Masoko ya Kitaifa tena kwa bei nzuri. Aidha, warina asali watengenezewe mfano mzuri wa masoko ya asali na nta.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina hazina kubwa ya wanyama wa kila aina katika mbuga zetu. Naishukuru jamii ya Kimataifa, inayoisaidia nchi yetu kumudu gharama za kuilinda hazina hii ya wanyama chini ya *World Wildlife Conservation*.

Uwindaji wa Kitalii ni eneo linalotuingizia fedha nyingi za kigeni toka kwa wawindaji wa kitalii. Tatizo letu ni utaratibu mbovu/usioridhisha wa jinsi vitalu vya uwindaji vinavyogawiwa na hasa kwa kuwapendelea wageni zaidi kuliko Watanzania Wazalendo. Naisisitiza Wizara, itekeleze Maazimio ya Bunge kuhusu hoja binafsi ya Mheshimiwa Mzindakaya.

Hali kadhalika, kuna haja na kuainisha bei za wanyama mbalimbali wanaowindwa ili ziwiane na bei zinazotowwa katika sehemu nyingine Barani Afrika. Mwaka jana, Wizara ilileta mapendekezo ya bei mpya kwa wawindaji na Bunge liliidhinisha. Kwa sababu zisizoeleweka, Wilaya ilishindwa kuzisimamia bei mpya na badala yake ziliteremshwa bila idhini ya Bunge. Naomba maelezo ya kuridhisha kwa nini Wizara ilifanya hivyo?

Idadi ya hoteli zenye hadhi ya kitalii na zenye Madaraja ya Kimataifa hazitoshi. Tunahitaji Mkakati Maalum wa kuendeleza ujenzi wa hoteli za kitalii, hususan kwa kukaribisha wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, nazipongeza jitihada za Serikali za kuutangaza utalii Duniani. Tuendeleze juhudi hizi tena kwa utaratibu wa mipango mizuri.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, na Wataalam wao wote, kwa kuandaa Hotuba nzuri ya Bajeti. Hata hivyo, napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanasayansi wanatuambia kwamba, Kimondo cha Mbozi (*Mbozi Meteorite*) ni jiwe kubwa ambalo lilianguka miaka mingi iliyopita. Kimondo hicho, kama nilivyosema ni jiwe kubwa na la aina yake. Kuna mambo mengi ya kujifunza kutokana na jiwe hilo. Kimondo hicho ni utalii tosha kabisa na kama kingetangazwa na kutunzwa vizuri, kingeliingizia Taifa pesa ya kutosha. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana kimondo hicho kimetelekezwa.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kimondo cha aina hiyo hiyo kingekuwa katika nchi za Ulaya, Marekani, na Asia, kingekuwa kivutio tosha kabisa kwa wanasayansi na wananchi wa kawaida. Kwa maana hiyo, nchi ingefaidika sana na kimondo hicho kutokana na mapato.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

- (i) Wizara ikitangaze kimondo hicho ndani na nje ya nchi;
- (ii) Kujenga jengo zuri na kuweka samani mahali kilipo kimondo;

- (iii) Kuwepo na machapisho ya kutosha kuhusu kimondo na zipatikane mahali kilipo na kadhalika;
- (iv) Kuweka Mtaalam wa Masuala ya Sayansi anayeweza kutoa maelezo fasaha kuhusu kimondo hicho kwa hasa kutoka nje ya nchi; na wageni
- (v) Kujenga barabara nzuri kutoka Kijiji cha Mahenje *Tanzam Highway* hadi Kijiji cha Ndolezi kilipo kimondo hicho.

Mheshimiwaa Spika, naishukuru Wizara kwa kuona umuhimu wa kukiboresha kimondo hicho. Hata hivyo, naomba maboresho yazingatie ushauri wangu na mambo mengine, ambayo Wizara itaona yanafaa. Aidha, nitapenda kujua maboresho hayo yamelenga maeneo gani na kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa maboresho hayo.

Mheshimiwa Spika, bado inaonekana mbuga/hifadhi zetu za wanyamapori si salama sana hii inatokana na ukweli kwamba, nyara za Taifa kama vile meno ya tembo, ngozi za chui, simba, pundamilia na kadhalika, zimekuwa zikikamatwa kwa uwindaji haramu. Hivi tatizo ni nini? Je, askari wa wanyamapori ni wachache au askari hao pia hushirikiana na wawindaji haramu katika kulihujumu Taifa?

Kama tatizo ni uchache wa askari, basi Wizara iajiri askari wengi zaidi ili kukabiliana na vitendo hivyo viovu. Kama tatizo ni askari wetu kushirikiana na wawindaji haramu, basi wale wote watakaobainika kufanya hivyo, wachukuliwe hatua kali za kinidhanmu na kisheria.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mkoani Iringa ilikamatwa shehena kubwa sana ya meno ya tembo, iliyokuwa ikisafirishwa kwenda Dar es Salaam na bila shaka nje ya nchi. Meno hayo ya tembo yanasadikiwa kusafirishwa kutoka Mkoani Mbeya, Wilaya ya Mbarali. Aidha, inasadikika kwamba, biashara hiyo haramu inamhusisha kigogo mmoja wa Chama cha Mapinduzi Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, namtaka Waziri awaeleze Watanzania ni kiasi gani cha meno ya tembo kilikamatwa na yana thamani (pesa) kiasi gani? Aidha, namtaka Waziri atueleze waliokamatwa katika tukio hilo ni akina nani; wako wapi na hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba, wale wote watakaopatikana na hatua/makosa, wachukuliwe hatua kali. Aidha, gari lililotumika litaifishwe na fedha zitakazopatikana ziende kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasisitiza Waziri ajibu hoja zangu ili nisilazimike kusimama kwenye vifungu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kumshukuru Mheshimiwa Ngeleja aliyepitisha bajeti yake jana tarehe 9/7/2008 kwa kutenga fedha kupitia Mfuko wa Usambazaji Umeme Vijijini (*REA*) za kupeleka umeme Ihanja na Sepuka Wilaya ya Singida na kupeleka umeme Mgongo kata ya Shelui Wilaya ya Iramba. Kwa niaba ya wananchi wa Singida, ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, sasa nianze kutoa mchango wangu kwa kuwapongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, rafiki yangu mpenzi, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Naibu Waziri, mwanangu Mpendwa Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mama Blandina Nyoni, Mpendwa wangu wa karibu sana, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri sana ambayo imeanisha wazi vitengo vyote ndani ya Wizara na utekelezaji wake kwa kuinua pato la Taifa kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Mwenyezi Mungu awe nao katika kutekeleza yote waliyoyainisha kwa ufanisi mkubwa na kuleta tija kwa Taifa hili maskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuainisha upya vivutio vya watalii, napenda kuishauri Serikali kupitia upya vivutio vya watalii kwani nina imani ipo Mikoa mingi ambayo ina vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, asilimia ya uwindaji kuwa wazi, naipongeza Serikali kwa kuanisha wazi asilimia inayotolewa kwenye Halmashauri zetu zenye mapori ya uwindaji kuwa ni asilimia 25. Vile vile ninashauri kuwa Idara ya wanyamapori kuainisha kila mwaka aina ya wanyama watakaovunwa kwa idadi yake na gharama yake. Ili kutoa mashaka ya asilimia inayotolewa na Hazina, bora mchanganuo huo, nakala ziwe zinapewa Halmashauri zetu za Wilaya kuwawezesha kujua mgao wao wa asilimia 25 ni shilingi ngapi. Nategemea Waziri atanjibu ili nisimsumbue wakati wa majumuisho yake hasa kwenye vifungu.

Mheshimiwa Spika, natambua wazi mbuga za Hifadhi za Rungwe, Kizigo, Mhesi na Chaya kuwa kuna makampuni karibu kumi huwa yanawinda lakini asilimia inayorudi ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, mbung'o walioko kwenye hifadhi za Rungwa Kizigo, Mhesi na Chaya, napenda kufahamu kama Serikali inafahamu kuwa kuna mbung'o wengi kwenye hifadhi tajwap hapo juu. Je mbung'o hawa hawana madhara kwa wanyama na watu? Nitahitaji ufafanuzi wa Waziri kama wana madhara, Serikali inakabiliana vipi na tatizo la mbung'o? Nitashukuru sana kupata maelezo kutoka wa rafiki yangu Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Waziri.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya vitalu vya uwindaji, ni kweli wakazi wanaoishi karibu na vitalu vya uwindaji vya Wilaya ya Manyoni, wananchi wanapata shida sana

kwa kuingiliwa na wanyama. Napenda kujua Serikali inasema nini kusogeza mipaka hii ili kunusuru watu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu simba wala watu, naipongeza Serikali kutambua tatizo la simba wanaokula watu maeneo mbalimbali nchini pamoja na Singida vijijini, Manyoni Magharibi Mkoani Singida. Vile vile natambua jitihada zilizofanyika hadi sasa ingawa tatizo bado ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile naishukuru Serikali kuamua kujenga vituo vya Askari wa Wanyamapori kwa jinsi nilivyomsikia Waziri kwamba bajeti hii watajenga vituo vitatu na Singida haipo. Napenda kuelezwa kero hii kubwa ya watu kuliwa na simba na idadi ya watu walioliwa na simba sasa ni kubwa, wanaisaidiaje Singida kuondokana na kero hii kubwa ambayo sasa Watendaji wameacha kazi zingine wanawinda simba wakisaidiana na Wanamgambo kwa silaha duni hata usafiri hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji maelezo ya kina kwani sasa ni tatizo, wanashindwa kwenda hata mashambani kuchunga mifugo, kusafiri kwa miguu, baiskeli, au pikipiki. Haya ni maafa yanahitaji mkono wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbao zinazokamatwa, ninafahamu kuwa zipo mbao zinazokamatwa kisha wahusika hushindwa kuzikomboa, naiomba Serikali iziuzie vijiji na kata kwa kujenga Zahanati, Vituo vya Afya, shule za msingi na sekondari kwa bei nafuu ili ziweze kukamilisha miradi hii ya maendeleo kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoteli za kitalii, naiomba Serikali ili kila Mkoa uwe na hoteli hizi nzuri za kitalii litolewe agizo kila Mkoa kujenga hoteli mfano tano kwa kipindi fulani. Kazi ya kutafuta wawekezaji iwe ya Mkoa wenyewe. Kwa kufanya hivi Mikoa itaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nimalizie kwa kuunga mkono hotuba hii nikiwa na mategemeo kuwa hoja zangu zitajibiwa ili nisishike mshahara wa Waziri ambaye ni rafiki yangu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vyema hotuba yake. Nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Maige, kwa mchango wake mzuri na kwa kujibu maswali vizuri Bungeni na ushirikiano anaotoa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja hii, ni kuiomba Serikali katika kazi inayofanya ya ugawaji wa *quarter* za wanyama kwa walio na miliki ya vitalu kwa msimu, iwe inatupatia *copies* katika Halmashauri zetu yenye idadi ya wanyama na thamani zake kwa msimu watakaovunwa katika vitalu vinavyozunguka Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia kwanza Halmashauri kufahamu *percentage* inayotakiwa kisheria na kupata thamani kifedha hivyo kuweza kuingiza katika bajeti yake

kama mapato yatakayopatikana msimu husika. Kwa maana nyingine kuingia katika vitabu kama *income projection* ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, pili ni njia bora ya kutekeleza sheria inayoelekeza mapato yanayopaswa kwenda katika Halmashauri yatokanayo na uvunwaji wa wanyama na uwindaji wa kitalii. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJ DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Ndugu Blandina Nyoni, Katibu Mkuu na viongozi wengine pamoja na watumishi wa Wizara kwa maandalizi na uwasilishaji mzuri hapa Bungeni hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, pili, naunga mkono hotuba na hoja ya Waziri Mwangunga, hoja imekamilika na namtakia Waziri na Wasaidizi wake, mafanikio katika utekelezaji wa malengo na shabaha zilizomo katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, tatu, suala la kuhifadhi maeneo ya ardhioevu la Bonde la Mto Kilombero ambalo liko katika Wilaya za Ulanga na Kilombero, halijitokezi vizuri katika hotuba wala mipango ya Wizara. Hali hii hairidhishi kwa sababu bonde la Mto Kilombero, ni eneo muhimu la ardhioevu hapa nchini. Nadhani kwa sasa ni eneo pekee lenye wanyama “sheshe” (puku) ambaye anapatikana hapa nchini kwetu na yuko katika hatari ya kutoweka kutokana na uvamizi wa wafugaji. Wafugaji wengi waliofukuzwa katika Bonde la Ihefu, Mbeya, wameingia kiholela katika bonde la Kilombero, hususan Wilaya ya Ulanga na Kilombero.

Wafugaji wameingia Ulanga na Kilombero kwa kupitia njia ya Reli ya Tazara kwa treni au kwa miguu kuanzia vijiji vya Uchindile, Matema, Mlimba, Mpanga, Ngombo na Ngalimila. Tarafa za Mlimba, Wilayani Kilombero na tarafa za Malinyi, Mtimbira na Lupiro (Jimbo langu la Ulanga Magharibi), Wilayani Ulanga ndizo zilizoathirika zaidi na uvamizi huu wa wafugaji na mifugo. Uvamizi huu ni kero kubwa kwa wana-Ulanga na wana-Kilombero hasa wakulima wadogo wadogo lakini athari kwa mazingira na uhifahi wa wanyamapori hasa Sheshe, Nyati, na Viboko ni ya kiwango cha kutisha.

Mheshimiwa Spika, inaelekea Wizara haitambui kuwa eneo la Bonde la Mto Kilombero, (Wilaya za Ulanga na Kilombero), ni pori tengefu, yaani “*game controlled area*”. Sisi na hasa Wizara ya Maliasili na Utalii, ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa hifadhi na mapori tengefu za wanyamapori na misitu tumeshindwa/imeshindwa kusimamia eneo hili la ardhioevu na kumlinda sheshe (puku) wa eneo hili? Ntoa wito kwa Wizara kulisimamia eneo hili la ardhioevu vizuri na ukamilifu zaidi sasa kuliko huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, nne, iko kero kubwa inayosababishwa na watumishi wa *Selous Game Reserve* kutoka kambi ya mbuga na kambi za kampuni za uwindishaji za

*Wild foot prints* (Shallom) na *Bushman* (*Abood group of companies*) za Mpunguso na usumbufu kwa wananchi Jimboni kwangu.

Moja ya nyanyaso hilo ni kuwabambikizia nyara za Serikali hasa ngozi ya chui, nyama mbichi au kavu ya wanyamapori, kuingia katika nyumba za wananchi na kukamata vyombo vya majumbani kama vile vikaango kwa madai zina harufu ya nyama ya porini, kupiga na kuwaweka mahabusu wananchi wanaowatuhumu kuwa majangalili. Ziko kesi za wananchi wanaoshtakiwa Mahenge kwa makosa ya kukutwa na nyama ya swala, kesi zinazotajwa tu muda mrefu bila kusikilizwa kwa sababu watumishi husika hawafiki Mahakamani kutoa ushahidi. Nyanyaso na usumbufu huu ni kero kubwa, naitaka Wizara ikomeshe kero hii mara moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu huu na naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, mchango huu wa maandishi ni nyongeza ya mchango wangu wa jana nilipozungumza.

Mheshimiwa Spika, bado msimamo wangu uko pale pale, “Siungi mkono hoja” hii hadi hapo nitakapopata ufafanuzi kwa hoja nilizosema jana na hizi zifuatavyo katika maandishi.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa jana, Bunge liliambiwa mara kwa mara mikakati na hatua ambazo zilikuwa zinachukuliwa kutangaza vivutio vya Tanzania katika nchi za nje. Tuliwahi kuletewa hapa Bungeni majarida mbalimbali yaliyokuwa yamebeba matangazo hayo, matangazo katika *CNN* na vyomb vingine vya habari na kadhalika. Lakini pamoja na nia njema ya Serikali kuchukua hatua hizo, yapo maeneo ambayo ninapenda kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, sambamba na Serikali kupeleka Dola 450,000 katika balozi 30 za nchi yetu, hivi tathmini ya matumizi ya fedha hizo na matokeo yake imefanyika? Kama imefanyika nini matokeo yake? Faida gani imepatikana?

Mheshimiwa Spika, tulitangaziwa hapa Bungeni kuwa Tanzania sasa inaranda katika jiji la London – Mabango makubwa ya kutangaza Tanzania yalikuwa yamewekwa pale Heathrow na mabasi karibu 100 yalikuwa yamepambwa vivutio vya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujua, kwa vile pesa zile ni dhahiri ni za Serikali zilitoka katika bajeti gani? Nataka pia kufahamishwa ni kiasi gani cha fedha kilitumika katika zoezi hilo na kama Ubalozi ulishiriki kikamilifu katika kufanikisha matangazo hayo?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hoja za jana, ninaomba kupata ufafanuzi pia juu ya hoja hii ya mwisho, mkakati wa kutangaza vivutio vya Tanzania mjini London – kiasi gani cha fedha kilitumika, mabango mangapi yaliwekwa Heathrow, Mabasi mangapi ya London yalitumika na Ubalozi ulishiriki vipi katika mchakato huo?

Mheshimiwa Spika, ni baada ya kupata ufafanuzi wa mambo haya, nitaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Shamsa Selengia Mwangunga (Mb), Naibu Waziri Ezekiel Maige (Mb), Katibu Mkuu, Ndugu Blandina Nyoni, watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii, ni sekta nyeti sana katika uchumi/pato la Taifa, utalii ukitumika vizuri unachangia vizuri pato la Taifa. Kwa kuwa tunavyo vivutio asilia vingi katika nchi yetu ambavyo tukivitumia vipasavyo, ni kielelzo tosha vitatangaza nchi yetu nje ya mipaka yetu na hatua kwa hatua hivyo tutavutia watalii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, nitoe mchango wangu hasa nikitoa ushauri katika kuiboresha zaidi sekta hii ya utalii ili kuzidisha ufanisi katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara isione utalii katika eneo moja kwa maana ya kuona utalii wa mbuga za wanyama, kama vile Serengeti, Manyara, Ngorongoro, Selous na Mlima Kilimanjaro. Katika hili, naomba Wizara izingatie kwamba urithi wa kale ni moja ya vivutio ambavyo navyo vinaweza kuvutia watalii na kuleta pato kwa Taifa. Vivutio hivyo ni kama:-

- Utalii kama ule wa pango la Mtemi Gelege lililopo eneo la Kisiriri Wilayani Iramba;
- Boma ya Utawala wa Kijerumani iliyojengwa kwa umahiri mkubwa huko Mkakua Iramba; na
- Mawe mazuri ambayo yamepandwa na kuleta mandhari ya kuvutia yalipo Mkoa wa Singida, bado nayo yangeweza kuwa sehemu ya utalii na kuleta pato kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili, tumeyasahau maeneo mengi muhimu yanayoweza kuvutia watalii kwa mfano, visiwa vidogo vidogo vilivyopo karibu na bandara ya Dar es Salaam, visiwa hivi sasa havitumiki kwa shughuli yoyote na badala yake vimetelekezwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, mbinu zinazotumiwa na Wizara kuutangaza utalii wetu nje ya mipaka yetu, mfano mzuri kila Ubalozi lazima uwe na mwambata wa utalii, ili aweze kutangaza utalii huko nje.

Mheshimiwa Spika, nne, utaratibu wa kutangaza kabila moja zaidi kama sehemu ya utalii, makabila yote yatumiwe.

Mheshimiwa Spika, tano, sekta ya misitu, pamoja na juhudi za Serikali kuboresha mazingira, misitu asili imekuwa ikipukutika bila utaratibu na kufanya nchi yetu kupoteza



miti yake ya asili muda wote. Mfano, miti aina ya mpingo inavyotoweka Jimboni Iramba Magharibi. Inasikitisha kuona hali hii inatazamwa bila kuchukuliwa hatua zozote.

Mheshimiwa Spika, pori tengefu katika hifadhi ya Sekenke, hatua za makusudi zichukuliwe na Wizara ili kulinda misitu na vyanzo asilia vya maji pamoja na wanyama waliokuwemo tangu asili katika pori hilo .

Mheshimiwa Spika, nyuki sasa wapo wengi katika Wilaya ya Iramba, elimu ya kuhifadhi nyuki ingetolewa kwa wananchi wa Iramba, ingesaidia kuwe na vyanzo vingine vya pato kwa wananchi na hivyo ingewaondolea wananchi makali ya maisha. Kadhalika elimu pia itolewe kwa wananchi kuhifadhi na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kuona hoja ya kuwa na Maafisa Utalii kwa kila Wilaya ili maafisa hawa wawe na uwezo wa kutembelea na kutoa tathimini ya masuala ya utalii uliopo kwa kila Wilaya. Naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa Bungeni kujadili hotuba hii nzuri kwa manufaa ya Watanzania na wageni wote wanaotuneemesha kwa kutembelea kama watalii.

Mheshimiwa Spika, pili, ninampangeza sana Waziri wetu wa Maliasili na Utalii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zinazohusika. Hotuba ni nzuri na inaatia matumaini. Hata hivyo, ninaomba ufafanuzi kwa mambo kadhaa na pia nitatoa ushauri kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, wanyama waharibifu kama vile tembo. Katika ukurasa wa saba (7), aya ya kumi (10), Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwa kina kuhusu ulinzi wa maisha ya watu na mali zao huko Karagwe, Nunda, Serengeti, Rombo na Pangani na kadhalika. Aidha imeelezwa wazi kuwa vituo vitajengwe katika Wilaya za Rombo, Simanjiro na Bunda – mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi kwa mambo yafuatayo:-

- (a) Ujenzi huo wa kituo cha kudhibiti tembo huko Rombo, utaanza lini na utamalizika lini? (*Time frame*).
- (b) Je, ujenzi huu wa vituo hivyo utahusisha pia nyumba za watumishi?
- (c) Je, Serikali iko tayari kuwatuma Maafisa wa Wanyamapori kwenye kipindi cha December, 2008 – Februari, 2009, endapo nyumba hizo zitakuwa hazijakamilika ili kuchunga mazao yatakayokuwa yameiva tayari kuvunwa?
- (d) Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia waathirika wa mazao kwa kipindi cha nyuma?

(e) Je, kuna mpango gani wa kujenga kituo kingine Wiyala ya SIHA? Kituo cha Siha ni muhimu kwani ndio mkondo/routine ya tembo hao.

Mheshimiwa Spika, matukio ya moto, Mlima Kilimanjaro. Mara kwa mara yamekuwepo matukio ya moto kwenye msitu wa Mlima Kilimanjaro wakati wa kiangazi. Moto huu, husababishwa aidha na warina asali au majangili wawindaji haramu wa wanyama wadogo wa kitoweo kama, paa, sungura, digidigi, swala na kadhalika. Moto ukishawashwa, amani inatoweka kabisa kwa familia zinazouzunguka mlima hususani vijana, kina mama na wanaume wa kaya.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba ieleweke wazi kuwa, wanaojitolea kuzima mlima huwa hawana vifaa wala mavazi rasmi ya kujikinga wala *dry ration*. Je, Serikali haioni kuwa ni muhimu kutoa vifaa vya kurahisisha kazi ya kuzima moto, zikiwemo, *boots*, kofia, *track suits*, vibuyu vya maji na *Biscuouts (dry ration)* ya kula njiani na kadhalika.

**MHE. DR. OMARI O. M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kujiunga na wenzangu kuchangia hoja hii muhimu.

Awali ya yote, napenda saana kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchangia kama ifuatavyo. Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na maliasili, katika nchi hii, Mwenyezi Mungu ametupa rasilimali asilia kama miti na kadhalika. Miti hii hutoa magogo na baadaye mbao kwa matumizi ya wananchi (binadamu) lakini hakuna utaratibu mzuri wa uvunaji wa maliasili hii. Katika uvunaji huo, utakuta sheria zinawabana mno wananchi wazalendo au wananchi wanaozunguka misitu hiyo ambao wao ndiyo wenye haki ya kutumia mali hiyo ambayo wamepewa na Mwenyezi Mungu Muumba. Lakini utakuta wageni wanavuna maliasili hiyo na kusafirisha maliasili hiyo nchi za nje kwa gharama ndogo sana au wakati mwingine hakuna hata gharama yoyote kutokana na ufisadi. Hii inasikitisha sana maana kama tungetumia vizuri utajiri huu tuliopewa na Mwenyezi Mungu Muumba, nchi hii ingeweza kuondokana na umaskini tulionao.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, naomba Wizara hii ijipange upya ikiwa ni pamoja na kupitia upya sheria zilizopitwa na wakati ili tuweze kuboresha ili kuiongezea uchumi nchi hii. Utajiri unawatengemea ninyi mliopewa dhamana na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuzungumzia utalii. Utalii ni jambo la msingi sana hasa katika mbuga za wanyama. Mbuga hizi zina wanyama wengi, wazuri wa kuvutia, jambo ambalo lingeweza kuliingizia Taifa hili pesa nyingi sana. Lakini ili

tupate watalii wengi, ni vizuri tungerekebisha miundombinu kama barabara inayokwenda kwenye mbuga hizo, lakini utakuta barabara chafu, mashimo marefu kiasi kwamba inakatisha tamaa kwa mtu kuingiza gari lake.

Mheshimiwa Spika, pili, viwanja vya ndege vianzishwe ili ndege ziweze kutua bila matatizo na hivyo kuwezesha watalii wengi na kutuwezesha kupata fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, tatu, vitalu vya wanyama, ninaomba Serikali iangalie mambo yafuatayo. Katika ugawaji wa vitalu hivi, kwanza tuangalie wawekezaji ambao wanapendekezwa na wananchi wanaozunguka vitalu hivyo. Lakini pia wawekezaji hawa wawe wanawasaidia wananchi wanaozunguka maeneo hayo waboreshe maendeleo ya wananchi hawa, kama kuwajengea mashule, *dispensary*, visima au maji ya bomba na kadhalika. Lakini pia kuwe na mikataba maalumu kwa ajili ya kuwalinda wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine mtu mmoja au kampuni moja wasipewe kitalu zaidi ya kimoja huu ni ukiritimba. Ni vizuri watu wakagawana maliasili hii.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kukupongeza kwa kusimamia ipasavyo kikao hiki cha Kumi na Mbili, hongera sana.

Pia, napenda kuwapongeza wasimamizi wakuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kuanzia na Waziri mwenyewe akiwa ni Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga (Mb) na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, (Mb), kwa kuiongoza Wizara ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Ngorongoro, imekuwa ni kivutio kikubwa kwa watalii walio ndani na nje ya nchi yetu (Tanzania) kiasi ambacho kutoka kipindi cha Julai, 2007 hadi kufikia Machi, 2008, ni wageni 426,230 waliotembelea Ngorongoro. Kati yao ni 244,379 kutoka nje ya nchi na 181,851 ni watalii wa ndani ya nchi na kupelekea mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kukusanya kiasi cha Shilingi 31,942,989,130.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali kutumia vyombo tofauti vya habari vilivyopo Tanzania na nje ya Tanzania kuweza kuvitangaza vituo vyote vya utalii ikiwemo Ngorongoro na sehemu nyingine za utalii kupitia vyombo kama TBC 1, TBC Taifa, Televisheni ya *CNN – America*, *CNN Headline Neris*, *CNN International* na vituo vingine duniani ili kuweza kuinua pato la Taifa (*National Income*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, bado Tanzania tunahitaji kuelimishwa kuhusu sekta ya utalii kuanzia wananchi wenyewe, wafanyakazi pamoja na wataalam, ili tuimarishwe zaidi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kusimamia vema maliasili zote za baharini na nchi kavu zihifadhiwe, zitunzwe na zitumike vizuri na tuweze kutumia kwa faida ya Taifa letu sio kwa faida binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magogoni na mimi mwenyewe naunga mkono hoja hii ipitishwe, ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Nampongeza vile vile Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja watendaji wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, utalii ili uwe endelevu lazima kuwe na mkakati wa kutangaza. Huko nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa *Brand Tanzania*. Hawa je, wapo na kama wapo wanafanya nini? Je, wako chini ya Wizara gani na wanapata fedha kutoka wapi za kuendesha shughuli zao?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuliwa na matangazo ya Tanzania kwenye mabasi katika jiji la London, naomba kujua ni nani amefanya kazi hiyo na malipo yanatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, Wizara ilisema kwenye bajeti ya 2007/2008, kuwa kuna fedha za kuwakopesha wenye mahoteli madogo ili waweze kuyaboresha. Naomba kujua kama fedha hizo zipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mlima Kilimanjaro, naomba kusikia kauli ya Serikali hapa Bungeni ya kuwa kuanzia Januari, 2009, mishahara ya waongoza watalii, Mlima Kilimanjaro, ni kama ilivyokubalika kwenye kikao cha wadau pamoja na Mheshimiwa Waziri ambapo iliamuliwa kuwa *Guide* atalipwa dola 20 kwa siku, Mpishi dola 15 na *Porter* dola 10 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, pia njia ya Maua ambayo inatumika kama *administration route* sasa iwe njia kamili ya kupandisha wageni kwa kuwa utalii Mlima Kilimanjaro unaongezeka. Njia hii ni muhimu kwa kuwa hata wazee wanaweza kutumia njia hiyo na wakishindwa watachukuliwa na magari kurudi mahotelini.

Mheshimiwa Spika, pia njia nyingine zifanyiwe utafiti ili ziweze kutumika. Lengo kuu liwe kuufanya Mkoa wa Kilimanjaro uwe *Tourist Destination*.

Mheshimiwa Spika, siyo vema kufanya leseni kuwa ni chanzo cha mapato. Leseni iwe ni ya kutambua kuwepo kwa wafanyabiashara. Kodi iwe ndio chanzo cha mapato. Kuna TALA licence zifuatazo:

- |                       |              |
|-----------------------|--------------|
| (1) Kupandisha mlima  | - 2,000 USD. |
| (2) Hoteli ya Kitalii | - 2,000 USD. |
| (3) Safari            | - 2,000 USD. |

Mheshimiwa Spika, leseni hizi ni ghali sana. Leseni hazijali una magari mangapi wala una vyumba vingapi. Nashauri mfumo ufuatao ufuatwe ili hata wale wazawa wanaoanza waweze nao kunyanyuka.

- *Mountain Climbing* - 2,000 USD.

- *Hotel licence - 100 USD + (10 USD X No. of Rooms).*
- *Safari licence - 100 USD + (10 USD X No. of vehicles).*

Mheshimiwa Spika, mimi nazungumzia uzalendo, uzalendo na utaifa. Sisi tumekosa uzalendo na utaifa, tumejaa ubinafsi. Nashauri njia zote kuu za uchumi ziwe mikononi mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, nashauri Watanzania wapewe maeneo yote ya kuwekeza ili kama kuna wageni wanataka waingie ubia, *prime areas*, wanapewa watu wa nje tafadhali kwa hili Wizara na TANAPA wawe na moyo wa utaifa.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wa mahoteli kwenye *parks* hawalipi *concession fees*.

Mheshimiwa Spika, *Sopa Lodges* na Serena ndani ya hifadhi, ni wajeuri sana hawataki kulipa kwa kuwa Wizara inawalinda.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji wa Ngorongoro *Wildlife Lodge*, Ndugu Lobo na Scronera, wameshindwa kazi na wameshavunja masharti ya mkataba. Nashauri wanyang'anywe mara moja. Naunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS P. NAKEL:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mb, Katibu Mkuu na Maafisa wengine Waandamizi kwa kumsaidia Waziri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka, 1970 Hifadhi ya Taifa ya Tarengire ilianzishwa rasmi kwa Tangazo la Gazeti la Serikali – *It was gazetted by Government Notice*, kilichofanyika ni kufanya *Arial Survey* kuweka mipaka. Hata hivyo, mipaka hiyo yaonekana kuwekewa *Beacons* mwaka 1990/91.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1976, vijiji vya Gedamar na Ayamongo, vilisajiliwa kwa taratibu zote za Kiserikali ikiwemo michoro ya mipaka. Baadaye ilionekana vijiji hivyo na kijiji cha Gijedabang mipaka yake ilionekana ku-*overlap* na mipaka ya Tarangire kwa tofauti ya hekta 8,000, sasa kuna mgogoro. Wananchi wanaelekea kutakiwa kufukuzwa, hii si jambo jema. Naomba mgogoro huu tu tafutie muafaka kwa namna ya maelewano. Ili iwe hivyo naomba, Mheshimiwa Waziri, uje Jimboni kwangu mapema iwezekanavyo ili kujionea hali yenyewe (*physically*) ili kulinganisha na nadharia iliyopo, naamini tutafika kwenye maelewano.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala zima la ushirikishwaji wa wananchi katika maendeleo yao hususani katika eneo la utalii. Kule kwangu Babati Vijijini katika Kijiji cha Vilima Vitatu, wafugaji wa eneo hilo wamelazimishwa kuhama

kumpisha mwekezaji wa kitalii ili ajenge hoteli ya kitalii. Hali hii daima huonyesha uonevu wa jamii fulani hususan wafugaji. Jambo rahisi kabisa ni kuwashirikisha tu. Kuna ugumu na tatizo gani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili haya niliyotaja yafanyiwe kazi.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Shamsa Mwangunga (Mb), Naibu wake, Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Katibu Mkuu, Bibi Blandina Nyoni na watumishi wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya hoja hii. Naiunga mkono kwa dhati na ninatarajia mwakani timu hii itatuletea mageuzi makubwa ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, yapo machache ambayo ningeshauri Wizara iyazingatie kuanzia sasa ili kuweka uwiano mzuri wa shughuli za Wizara kwa nchi nzima:-

(i) Utalii kwa sasa uanze kuangaliwa maeneo ya Kusini; Nyanda za Juu Kusini na Magharibi. Hali ya sasa na kuendelea kuweka mkazo maeneo ya Kaskazini, yatafanya maeneo hayo yaharibike haraka na kufanya utalii usiwe na raha inayostahili kwa kulundika watalii eneo hilo hilo.

(ii) Mheshimiwa Spika, naona katika hotuba ya Waziri, mkazo hauonyeshi kuwekwa kwenye “*Southern Highlands Programmes*” ambazo kwa sasa zimeanza kuvutia wawekezaji wengi kwa kutumia maandishi na utafiti unaofanywa na asasi ya “*Wildlife Conservation Society*” chini ya usimamizi wa Dr. Tim Davenport ambaye ameandika kijitabu kiitwacho “*A guide to Southern Highlands of Tanzania*”. Kitabu hiki kama Wizara haina, ikipate ni muhimu sana kuangalia “*potentials*” zilizomo ndani ya Kanda hii ili isukume juhudi za huyu mtaalamu.

(iii) Hifadhi ya msitu wa Mbizi ulioko ndani ya eneo na Manispaa ya Sumbawanga, haizungumzwi hata kwa sentensi moja. Je, Waziri anafahamu msitu huu ndiyo wenye “mbega wekundu” pekee katika upande huu wa Afrika ya Kati, Kusini na Mashariki? Nini azma ya Serikali kuhifadhi msitu huu ambao pia ndicho chanzo cha maji kwa wakazi wa mji wa Sumbawanga.

(iv) Mheshimiwa Spika, suala la uwindaji wa mamba katika Ziwa Rukwa, limesaidia vipi wakazi wa eneo hilo, licha ya hasara ya upungufu wa samaki kutokana na wingi wa mamba katika Ziwa hilo?

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa waliopata vibali vya kuwinda mamba, hawatoi mrahaba kwa wakazi wa maeneo hayo. Je, Wizara inaweza kulifuatilia hilo. Pamoja na hilo, inasadikiwa kuwa maeneo hayo yanayotumika kwa uwindaji wa mamba, kuna uchimbaji wa madini kinyume cha maombi ya wahusika. Naomba hili nalo lichunguzwe.

Mheshimiwa Spika, mbuga na shamba la Katavi, ni muhimu kwa ustawi wa utalii Kusini Magharibi kwa nchi hii na watu wake. Bado miundombinu siyo mizuri na kuna

haja kujenga Hoteli ya Kitalii yenye hadhi kama zilizoko kwenye maeneo mengine ya Kaskazini. Wizara ielekeze wawekezaji huko na siyo waende kule tu ambako kumejaa tayari.

Mheshimiwa Spika, mwisho, suala la vitalu vya uwindaji viangaliwe kwa makini ili tusije tena tukarudi Bungeni kulalamikia utaratibu mwingine. “*Once bitten, twice shy*” Wazungu hunena, hivyo. “*Enough is enough*” tusikubali kuendelea kufanya makosa tena.

Mheshimiwa Spika, naomba apate nafasi ya kuja Mkoani Rukwa, aone tulichonacho ili asaidie kutuweka nasi katika picha ya ulimwengu wa utalii na baadhi yetu tuwe tunachukuliwa kwenda kutangaza utalii, kwa maeneo yetu na Tanzania kwa ujumla. Namuomba Mheshimiwa Waziri alione hilo kama sehemu ya maombi yangu kwa niaba ya wakazi wa Mkoa huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kumtakia Waziri na Wasaidizi wake kila la kheri wakati wote wa kutekeleza majukumu haya ya Kitaifa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha nami niweze kuchangia kwa maandishi katika hoja iliopo mbele yetu.

Pia napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri, wake kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kujikita zaidi katika uvunaji wa mazao ya msitu. Kwa kweli, watu wengi wanavamia na kukata miti tena ile miti mizuri na migumu kama mvule. Miti hii wanaikata bila kibali chochote toka kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, inaelekea kuwa kuna mchezo mchafu unaochezwa katika uongozi uliopo vijijini mwetu. Wanatoa vibali ambavyo sio vibali halisi ila tu ubabaishaji. Hili lisipofuatiliwa, tutajikuta nchi inabaki kuwa jangwa.

Mheshimiwa Spika, Tanga Mjini kilikuwepo kiwanda cha mbao kilichojulikana kama (*Sikh Saw Mills*). Japo kiwanda hicho kilikuwa cha mtu binafsi lakini kilitoa ajira kwa watu wasio na kazi. Kiwanda hiki kimepunguza uzalishaji, je, ni sababu zipi zilizopelekea kupunguza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kuhusu utalii, wengi tunafikiria kuwa ni mbuga za wanyama tu. Katika utalii, Tanga pia kuna vivutio kadhaa ambavyo vikiboreshwa, vinaweza kuingizia nchi fedha nyingi sana.

- (1) Kuna mapango ya Amboni ambayo ni kivutio kikubwa sana kwa watalii;
- (2) Kuna maji moto yenye kibiriti upele (*sulphur*) ambayo yapo Amboni;
- (3) Kuna magofu ya nyumba na misikiti walioishi Waarabu zamani huko Tongoni;

- (4) Katika Wilaya ya Mkinga, Kata ya Kigongoi chini Mlimani kunapita mto, mto huu maji yake yanaharufu ya mafuta ya taa. Hii pia ni sehemu ya utalii na pia ndio mwanzo wa uguduzi wa nishati;
- (5) Milima ya Dahuni kwa chini kuna udongo wa rangi mbalimbali ambayo ukisiriba katika nyumba, nyumba inavutia sana. Hizo rangi ziko katika udongo huo; na
- (6) Katika bandari ya Jiji la Tanga katikati kuna kisiwa. Ndani ya kisiwa kuna kisima kirefu sana ambacho kina maji yasiyokauka pia kuna handaki ambalo lilichimbwa enzi hizo kwa ajili ya watu hujificha . Hivyo vyote ni vivutio ambavyo vingeweza kuingizia nchi fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuingiza pato kwa Taifa, kwa nini kisiwa hiki kilichopo katika bandari ya Jiji la Tanga, pasijengwe hoteli ambayo ingeweza kuchangia katika pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu fukwe zetu, Tanga tunazo fukwe nyingi na nzuri. Je, Serikali inazitumiaje fukwe hizi badala ya kuzitoa kwa wawekezaji? Je, Watanzania hawawezi kuwekeza katika fukwe hizi? Jiji la Tanga lina Chuo cha Utafiti wa Ndorobo, je, nini maendeleo ya chuo hiki?

Mheshimiwa Spika, mwisho, watalii wanaokuja wanakuja na mitindo ya mavazi ambayo hayako katika maadili mazuri. Mavazi haya huigwa na kizazi chetu cha leo kiasi cha kupoteza maadili ya nchi yetu. Je, Serikali inao mpango gani wa kuhakikisha kuwa unadhibiti hata ubora wa mavazi kwa watalii wetu ili isiwe ndio chanzo cha kupoteza maadili yetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la UKIMWI, watalii wanaoingia kwetu, hatuwajui afya zao. Je, Serikali inao mpango gani wa kupima afya za watalii kwa vile kuna wengine wanakuwa na VVU au UKIMWI na kuweza kusambaza kwa baadhi ya ndugu zetu ambao wengine hujiuza kwa watalii hawa.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kusema kwamba kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Kwimba, naiunga mkono hoja hii. Hotuba ni nzuri, inaonyesha uzalendo. Ni hotuba inayolenga kuinua nchi na Taifa letu kiutalii kwa kulinda maliasili yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba hii sina budi kusema wazi kuwa, nampongeza kwa dhati Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika uandaaji wa hotub hii. Wote ninawapongeza kwa ushirikiano wenu unaoonekana dhahiri katika tunda zuri la hotuba hii, hongereni sana.



Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, ninaomba ufafanuzi na maelezo katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, sekta ndogo ya Misitu na Nyuki. Mimi ni mkazi wa Wilaya ya Kwimba, Wilaya ambayo ni kama kwa asili ni Wilaya isiyokuwa na miti mingi. Wananchi wa Kwimba, wamehamasishwa kupanda miti sana. Wamejitahidi kwa kiwango kikubwa na kwa shida kubwa kutokana na ukame huo. Cha kuhuzunisha, maelekezo ya kupanda miti yalikuwa yanaishia kupanda na kuzuia kukata miti bila kuwapatia wananchi faida endelevu za miti.

Vivutio vilivyokuwa vikitumika kuwashawishi wananchi kupanda na kutokukata miti ni vivuli, matunda na mbao vivutio ambavyo kwa kuona kwangu sio endelevu kwa kuwa vingi vinaishia katika kuikata. Hivyo, wananchi bila waelekezaji wao kuelewa walikuwa waikielekezwa kupanda ili baadaye waikate wakihitaji kufanya hivyo. Heri kama kupanda miti huko kungekuwa kupanda na kupata vivuli, matunda na dawa watu wangeweza kuona kuwa miti inazo faida za muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa suala la upandaji miti lilikuwa halihusishwa moja kwa moja na uchumi wa mtu mmoja mmoja unaotokana na uhusiano wa karibu sana kati ya misitu na nyuki. Nyuki na mazao yake yakiwa ni pamoja na viwanda vidogo vidogo ngazi ya kaya. Mazingira, matunda na vivuli vingaliachwa kuwa matokeo yaliyojificha ya kugunduliwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji wa upandaji miti ifaayo kwa nyuki ufanyike katika sehemu kubwa ya nchi yetu hususani zile ambazo ni kame kama Kwimba. Uhamasishaji huo uende sambamba na elimu ya ufugaji wa nyuki, ninaamini hili linawezekana katika maeneo hayo japo katika maeneo machache kwa kuanzia. Naipongeza Serikali kupitia Wizara hii kuliona hili kama Ibara ya 37, 58, 60 katika bajeti ukurasa wa 21,22,23 inavyoonesha. Ni vyema hili likaendeshwa kwa kasi kubwa kidogo kadri bajeti itakavyoruhusu. Hivyo ombi langu ni kuwa Wilaya ya Kwimba hususani Jimbo la Kwimba lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, pili, utalii. Nchini yetu inao utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii. Tatizo nilionalo mimi ni kuwa hatujawekeza vya kutosha katika kuvitambua na kuvitangaza. Naomba Bunge lijulishwe kama mambo yafuatayo yanajulikana kwa kiwango gani katika Wizara na Idara hii. Mambo haya yako Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Waziri aseme yametangazwa wapi na kwa nani. Nasema haya kwa kuwa hata watu wa Jijini Mwanza huenda hawayajui au kutokana na imani ya ushirikina, wanaogopa kwenda huko hata wakisikia, mambo hayo ni:-

(a) Ndani ya Ziwa Victoria kuna visiwa zaidi ya 20 vilivyo na moto wa asili ikiwemo miti mirefu ya mitobo na zaidi;

(b) Maji ya ziwani yanayoruhusu mambo mengi kufanyika kama mashindano ya boti ziendaza kwa kazi, michezo mbalimbali. Kulikuwa na uvumi kuwa maji ya Ziwa

Victoria yana vichocho na kuwa kufanya michezo yoyote katika ziwa hilo watu wangepata kichocho. Jambo hili ni dhahiri kuwa watalii wengi hawawezi hata kuja Mwanza, Musoma, Bukoba kwa kuogopa kupata vichocho.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hotuba yake, aeleze kama uvumi huo ni wa kweli. Kama ulishawahi kuwapo Serikali imechukua hatua gani kukanusha taarifa hiyo? Kama ni kweli, je, upo utaalamu wowote wa kuweza kulisafisha ziwa hilo liondokane na wadudu wa kichocho? Naomba maelezo;

(c) Mapango makubwa katika maeneo ya Igogo na Bwiru. Yapo mapango makubwa na kama yakifanyiwa marekebisho kwa kuzingatia usalama bila kuharibu uasilia wake na kutangazwa yanaweza kuwa vivutio vikubwa vya utalii.

(d) Mashimo ya Wajerumani. Maeneo ya *City Council*, zipo njia za chini kwa chini yanayoenda kwa Kilomita kama tatu hivi yaliyoachwa na Wajerumani. Inasadikiwa kuwa ndani humo zimo mashine zilizokuwa zikitumika kunyongea watu. Mabaki ya mashine hizo zimo katika njia hizo. Njia hizo zikitengenezwa upya kwa kuzingatia usalama zaweza kuwa vivutio kama si kwa watu wa nje angalau utalii wa ndani. Kinachohitajika ni kuvitambua, kuvikarabati vizuri na kuvitangaza. Kama Bagamoyo na Kilindi imewezekana kwa nini Mwanza isiwezekane?

(e) Mawe. Yapo mawe yenye maumbile mazuri mifano ya matofali yenye urefu kati ya futi 45 hadi 60. Pamoja na mawe hayo lipo jiwe kubwa “*The great Stone*” katika sehemu za Igogo na Kitangiri ambalo limekaa kama meza, hapo utakuta mbao zilizokuwa zikitumika katika michezo ya watu wa “kale”.

Mambo haya ni baadhi tu ya mambo mengi unayoyakuta hapo jijini kabla hata hujaingia katika Wilaya zingine. Naomba Mheshimiwa Waziri mambo haya kwa kiwango gani yamefikiriwa katika hazina ya orodha ya vivutio vya kitalii kama si wa nje angalau wa ndani.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni maduhuli kutokana na Filamu za Vivutio vya Utalii. Moja ya vyanzo vya fedha kwa nchi yetu, ni fedha tunayoikusanya kutoka kwa watalii wanaokuja kuitembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, shirika linalojulikana kama *National Geographical Society of England*, kama jina linavyoonesha ni shirika la kigeni. Shirika hili huwa linatuma watu kuja kupiga picha na kutengeneza filamu za vivutio vyetu vya kitalii.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aeleze:-

(i) Je, nchi yetu inanufaikaje moja kwa moja kimapato ukilinganisha na shirika hilo kutokana na filamu hizo licha ya filamu hizo kuitangaza nchi yetu nje?

(ii) Je, nchi ilipata kiasi gani kutokana na filamu ya:-

- (a) *Serengeti Shall Not Die?*  
(b) *The wings of Kilimanjaro?*

(iii) Je, utaratibu wa kuwaruhusu waandaji wa filamu hizo ukoje na ada zao zikoje?

(iv) Je, wanapokuwa hapa wakiandaa filamu hizi kwa kivuli cha *Education Aterials* wanakuwa kama watalii au vipi?

Mheshimiwa Spika, ushauri, wanapokuja watu kama hawa waje na bajeti zao zikionyesha malipo yetu yatakuwa kiasi gani na kwa kuwa wanao uwezo walipe kabisa siyo watengeneze – waende malipo baadaye.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia hotuba ya Wizara ya Miundombinu, ukurasa 84, inathibitisha wazi kuwa ule mradi wa kuvuna magadi (*Soda Ash*), Serikali imeshaamua licha la umuhimu wa eneo hilo la Ziwa Natron kwa Tanzania na kiulimwengu.

Mheshimiwa Spika, eneo la ziwa Natron ambapo asilimia 70 ya ndege *heroe* wadogo ndipo wanapozaliana sana, kwa vyovyote kwa kuanzishwa mradi wa uvunaji magadi, utaathiri mazingira ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Wizara hii ndio yenye dhamana ya ardhi yetu, ipo haja ieleze ina msimamo gani kuhusu eneo hilo la ziwa Natron kuvunwa magadi.

Mheshimiwa Spika, ili uhifadhi wetu uwe endelevu, ni lazima kuwa na utafiti wa wanyamapori. Serikali inavyoonekana, katika utafiti inategemea zaidi wahisani kutoa fedha.

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana hali ya mapori ya akiba, wafanyakazi wake wana matatizo makubwa kimaslahi na vitendea kazi ukilinganisha na (*National parks*) licha ya kuwa kazi zao zinalingana.

Mheshimiwa Spika, mapori ya akiba yaliyo chini ya Idara ya Wanyamapori kwa hali hiyo iliyojitokeza, ni dhahiri ipo haja mapori ya akiba nayo yaundiwe taasisi yenye mwelekeo kama TANAPA badala ya kuwa chini ya Idara ya Wanyamapori, ahsante.

**MHE. JOHN P. LWAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kutokana na kukithiri kwa matatizo ya wanyamapori, namwomba Mheshimiwa Waziri au hata Mheshimiwa Naibu Waziri, atembelee mbuga za akiba za Ruangwa/Kizigo na Nkasi, Chaya, asikilize kilio cha wananchi.

Mheshimiwa Spika, nasihi Serikali ije (kwa makusudi) na sera mpya ya kuwajali binadamu dhidi ya wanyama wakali ili walipwe fidia kwa maisha yao na mazao yao. Ni dhambi kumlipa mtu 200,000/= kifuta jasho. Majibu kwamba huwezi kuthaminisha maisha ya binadamu na fedha, si kweli. Wote tunahangaika kupata fedha, ‘*statements*’

kama hizo ni za kuwahandaa wananchi. Fidia halali pia ilipwe kwa mazao yanayoharibiwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na maelezo kuwa hakuna sera ya fidia nchi zingine. Hivi ni lazima kuiga nchi nyingine wakati Tanzania ndiyo kitovu cha wanyama duniani? Sisi wenyewe tuje na sera hiyo watu wa mataifa mengine waje wajifunze kwetu. Siyo kila kitu tukaangalie nje wanafanya nini. Fidia ihusu pia mifugo inayouawa na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa zao la asali na nta, hatuna Bodi ya Asali na Nta nchini. Naishauri Serikali ije na mchakato wa kuunda Bodi ya Asali, ili kusimamia zao hili muhimu na kuliendeleza kitaalam zaidi.

Mheshimiwa Spika, naisihi Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya doria, risasi, posho, magari na wafanyakazi (*game scouts*) kwa kila Tarafa. Manyoni ilipata Sh.18m/= tu msimu huu na tayari zimeisha. Dawa mojawapo ni hiyo kuwamotisha wafanyakazi hawa wawe na ari na kuipenda kazi yao. Ni maskini sana wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ieleze ina sera gani ya uvunaji mbao kwenye mapori ya Akiba ya Ruangwa/Kizigo na Mukesi. Maana uvunaji umeachwa kwa wavunaji haramu. Mbao za mninga ni ghali na za thamani kubwa sana lakini ulanguzi wake ni wa kutisha, usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, *Mgandu Complex*, ndani ya Pori la Akiba la Mhesi kuna mgodi ulioachwa na Mjerumani. Wananchi wanadai kuwa Maaskari wa Wanyamapori wanashirikiana na wenye *hunting blocks* kuchimba dhahabu kwenye mgodi huo bubu unaoitwa *LITMAN*.

Naomba suala hili lichunguzwe kwa makini na kama ni kweli kuna dhahabu, basi iwe *formalized* ili Taifa linufaike na rasilimali hii na hususan wananchi wa maeneo hayo na Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua hatma ya Bwawa la Ruangwa. Naona kama vile liko mbioni kutelekezwa kabisa. Pamoja na *TWPF* kutenga Sh.100,000,000/= kwa ajili ya kuchimba visima, naona hatua hii ni kama kisingizio cha kuliacha Bwawa hili life kwa kisingizio kwamba halikujengwa sehemu inayostahili. Maisha ya watu wa Rungwa bila Bwawa hilo hayawezi kuwa sawa tena. Naiomba Serikali iwe wazi kuhusu suala hili na ieleze fedha za awali zilizotengwa za Sh.510m/= zitaenda wapi.

Mheshimiwa Spika, naisihi Serikali ije na mpango wa kuwachimbia mabwawa wafugaji wanaoishi kandokando ya mapori haya ya akiba ya Rungwa/Kizigo, Mukesi na Chaya. Mipaka iliposogezwa karibu na vijiji, mabwawa kadhaa kama yale ya Damweru na Doroto, yaliingizwa ndani ya hifadhi na kuwanyima fursa wafugaji kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya hifadhi/mapori ya Akiba yarudishwe nyuma kwenye mipaka ya zamani ili kuwe na “*buffer zone*” kati ya vijiji na mapori ya akiba.

Mheshimiwa Spika, dhana kuwa simba wa Singida ni mbojo (simba mtu), si kweli. Ni simba wazee wasioweza kuwinda wanyama. Tatizo liko Idara husika kwa kutokuwa na *game scouts* wa kutosha, silaha, motisha, usafiri, posho na mishahara duni. Wakati idara ni tajiri lakini watumishi wake wa chini ni hohehahe, ni maskini sana. Serikali ichukue hatua kurekebisha suala hili kwa kutoa magari na motisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, pongezi zangu ni kwa Waziri ambaye ni Mwanamke mwenzangu ambaye ameonyesha ujasiri wa hali ya juu na uzalendo kwa kuiongoza Wizara hii kwa nguvu zake zote, hekima na maarifa ndio maana kumeonekana mabadiliko makubwa ya maendeleo na ustawi katika Wizara hii. Pongezi sana, inaonyesha wazi wanawake tuna uwezo mkubwa sana wa kuiongoza.

Pia pongezi hizo ziende kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii kwani naye ni mwanamke. Hii inaonyesha wanawake ni makini kwani ushirikiano wake kwa Waziri na uongozi wote pia watendaji ndio uliozaa matunda haya ya mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida kuhusu suala la wanyama waharibifu. Suala hili limekuwa ni kero kubwa katika Mkoa huu wa Singida hasa kwenye maeneo yenye wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Spika, watu wamekuwa wakiliwa na simba kila mwaka na Serikali imekuwa kimya tu. Wale Maafisa Maliasili walioko kule, naona wapo tu kazi yao imekuwa ni kukamata watu na kuwatoza faini, basi, lakini ule udhibiti haupo. Sasa naomba Wizara inieleze leo, tatizo ni nini? Silaha au uelewa/ujuzi duni na inawahakikishiaji wananchi wa Mkoa huu usalama wao?

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyopo pembezoni mwa Mbuga za Wanyama/Hifadhi, kuna fedha ambazo huwa zinatolewa kila mwaka, lakini cha ajabu, fedha hizi kwanza haziji kwa wakati na si kwa *percentage* iliyo sahihi. Naiomba Wizara ilianganalie suala hili. Pia iongeze fedha hizo, kwani wananchi wa vijiji hivyo, ndio walinzi wa hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ije itazame vivutio vya Kimataifa Mkoani Singida na kuvitangaza ili tuweze kuongeza pato la uchumi wa Singida. Mkoa wetu una *Game Reserve* za Rungwa, Mukesi na Kizinga. Pia tuna mapango yaliyoko Nduguti, Michoro na Maboma ya Kijerumani Mkalama na pia utamaduni, mavazi na mambo ya kale ambapo ni kivutio tosha.

Mheshimiwa Spika, suala la kutangaza utalii wa Tanzania, lina gharama kubwa na ili kupata faida kubwa ni lazima uwe na mtaji wa kutosha. Hivyo basi, napenda

kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa mwezi April, 4, 2008, vijana wa asili ya Kimasai wapatao sita (6), walifanya kazi kubwa sana ya kuitangaza Tanzania na utalii wake nchini Uingereza, London bila kutumia fedha yoyote toka Serikali ya Tanzania na kwa jinsi ilivyokuwa gharama yake kama ingethamanishwa ni fedha nyingi sana.

Hawa vijana waliekwenda kushiriki *London Marathon* kwa ajili ya kutafuta fedha za kuchimba kisima cha maji safi ya kijiji chao. Lakini walikuwa kivutio kikubwa sana na walivuta watu wengi, vyombo vyote vya habari vilivyo maarufu kama *BBC Television*, magazeti mfano *The Guardian* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara au Bodi ya Utalii, inalijua hilo na je itakubali kuungana nami kwamba vijana hawa tuwatambue kama wachangiaji wakuu wa pato la Wizara hii?

Mheshimiwa Spika, pia kama nilivyoomba kuwa watambuliwe hapa Bungeni na ofisi yako imekubali na Wizara iko tayari kuungana nami na Wabunge wote kuwatambua rasmi vijana hawa kwa ushirikiano na ofisi yako Spika?

Mheshimiwa Spika, je, wako tayari kuwaandikia *NGO* iliyowafadhili kwenda Uingereza barua ya shukrani (*Greenforce* pamoja na *BTS*)?

Mheshimiwa Spika, maelezo mengi juu ya Watanzania hawa, nitayatoa siku ya kuwatambua hawa vijana na ninatoa *copy* kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, matangazo ya utalii London. Imekuwa ni faraja kubwa kwa *promotion* kubwa ya utalii iliyofanywa nchini Uingereza kwani matangazo yale yaliyozinduliwa Ubalozini London, ambayo yapo kwenye mabasi na *underground* pia Heathrow. Lakini nilipata taarifa kuwa matangazo yake ni ya muda mfupi tu, je, Wizara haioni kuwa kutoendeleza hayo matangazo, itakuwa imepoteza fursa kubwa kupata walichokitaka?

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kumpongeza sana Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti na kuiwasilisha hapa Bungeni kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, niwape pole kwa ajali ya ndege iliyotokea hivi karibuni huko Arusha na kusababisha vifo vya watumishi wa Wizara hii. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amin.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe maelezo haraka kwa maandishi kuhusu:-

(1) Ndege iliyoanguka ya Idara ya Wanyamapori ilikuwa na Bima inayofanya idara hiyo ilipwe kutokana na ajali hiyo?

(2) Waliokufa kwenye ajali hiyo nao watalipwa fidia kupitia ndugu na jamaa zao?

- (3) ni kampuni gani iliyotumika kukatia Bima ndege hiyo?
- (4) Ni nini matumizi makubwa ya ndege hizo ikiwemo hii kubwa ya *TANAPA (Caravan?)*
- (5) Ndege hii ya *TANAPA (Caravan)* imenunuliwa kiasi gani? Ni pesa za nani mkopo, ruzuku, au msaada?
- (6) Nini madhumuni ya kununua ndege hii *Caravan* ya *TANAPA*?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapo wazawa wanaotaka kufanya biashara ya utalii (*Tours Operator*) lakini wanashindwa kutokana na masharti au taratibu kubadilikabadilika bila mpangilio maalum. Naomba sana masharti hayo na taratibu za kupata leseni hiyo ya *Tour Operator* ziwe wazi na kwa heshima naomba nakala ya taratibu hizo ili nami niweze kuwapa/kuwafahamisha wale wanaotaka leseni hizo za *Tour Operator*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimeomba majibu haya hata kwa maandishi, ni tegemeo langu Wizara itafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu, Ndugu Blandina S. Nyoni na wasaidizi wake, wakiwemo watumishi, viongozi wa taasisi chini ya Wizara, kwa kazi nzuri na hasa kwa hotuba hii nzuri. Nampongeza kwa jinsi ulivyoiwasilisha hotuba yako ya bajeti ya 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utafuata mpangilio wa hotuba yako, yaani maliasili, utalii na mambo ya kale. Nafasi ikiniruhusu nitagusia utawala na rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, shughuli zinazofanywa na sekta ndogo ya wanyamapori, kama zilivyoielezwa kwenye Ibara za 5 – 36, ni muhimu sana na maelezo yanathibitisha jinsi Wizara inavyosimamia vizuri sekta hii pamoja na malengo yake katika kipindi cha mwaka 2008/2009. Muhimu kwa sekta hii ni kuleta manufaa kwa Taifa, ni hifadhi ya wanyamapori na mazingira yao. Mkakati wa kuwashirikisha wadau mbalimbili, ndiyo mbinu bora ya kuhakikisha kuwa Wizara inalitekeleza jukumu hili kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba haitoshi kulinda wanyamapori na mazingira yao pekee bila ya kujali usalama wa watu na mali zao hasa mazao yao mashambani na mifugo. Katika Ibara ya 10, hili linaongelewa, lakini haitoshi kulifanya kwa dharura. Ni vizuri Wizara ikawa na sera na utaratibu unaoeleweka wa kulinda watu na mali zao. Kwa hiyo, katika Muswada unaoongelewa kwenye Ibara ya 6 ni vizuri kuingiza masuala ulinzi dhidi ya wanyama hatari kwa binadamu na waharibifu wa mazao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa ununuzi wa ndege itakayoweza kubeba Askari kumi na tatu (13) kwa wakati. Lakini, tukizingatia kuwa shughuli nyingi za sekta hii ziko kwenye mapori na kwa kuwa haiwezekani kuwa na viwanja vingi vya ndege (*Air strips*) kwenye mbuga, pia ili kupambana na majangili mbugani, Wizara ifikirie ununuzi wa '*helicopters*' zenye uwezo wa kutua sehemu mbalimbali, magari vumilivu na yaendayo kwa kasi pamoja na silaha za kisasa za kupambana na majangili.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 17 ipo azma ya kuongeza WMAS 10 kwenye Wilaya zilizotajwa pale. Napenda kuikumbusha Wizara kuwa moja ya sehemu za hifadhi ya Selous iko katika Wilaya ya Kisarawe. Naamini kuwa maeneo ya Rufiji na Kilombero ndiyo hayohayo kando kando ya Selous. Nashauri kuwa na Kisarawe iingizwe katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa kama ushauri wangu utazingitiwa, makusanyo ya sekta hii ndogo yatakuwa zaidi ya Sh.42.3 bilioni zinazotajwa katika Ibara ya 36.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya misitu na nyuki ni muhimu sana. Ikisimamiwa vizuri, mchango wake utakuwa mkubwa zaidi ya sekta zote ndogo labda ukiondoa utalii. Hapa nashauri mambo mawili:-

(i) Wizara isimamie upandaji wa miche zaidi ili ingawiwe kwa watu mbalimbali bure au kwa bei nafuu ili kuiongeza misitu, hasa ya mbao ngumu, kwa haraka zaidi.

(ii) Mafunzo ya ufugaji wa nyuki yasambazwe kwa watu wengi vijijini ili kuongeza uzalishaji wa asali na ajira.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya utalii, utalii ni moja ya sekta tatu (3) muhimu za uchumi wa Tanzania nyingine zikiwa kilimo na madini. Lakini, kama ilivyo kwa kilimo, utalii una nafasi kubwa sana ya kuchangia zaidi kwenye uchumi wetu. Uchimbaji wa madini una kikomo, baada ya miaka mingi akiba ya madini itakwisha, lakini kwa utalii, ili mradi tunaendelea kuvutia watalii, mapato yake yatakuwa yanaongezeka. Kwa hiyo, hapana budi utalii usimamiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuunda mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za utalii (*Tourism Satellite Account*); upangaji wa Hoteli katika daraja; kuanzisha mradi wa mafunzo ya utalii na kufaulu kuishawishi dunia kukubali Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Utalii kijengwe nchini Tanzania. Binafsi nafurahi zaidi kuwa Chuo hicho kitajengwa Mkoani wa Pwani kuanzia mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara inastahili pongezi nyingi sana kwa mikakati mipya ya kutangaza utalii wa Tanzania, hasa kwa kutumia njia mbalimbali zilizotajwa katika Ibara za 87 – 91 za hotuba hii ya Bajeti. Napenda kuongeza kuwa kwenye vyombo vya



habari vya Kimataifa tumieni pia mtandao wa *Al-JAZIRA* ambao siku hizi unatishia kuipita *CNN* na *BBC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya Balozi zetu, kutangaza utalii wa Tanzania, mfano wa matumizi ya Dola za Kimarekani 450,000 kuziwezesha Balozi zetu za kununua nyenzo za kutangazia vivutio vya Tanzania, ni mwanzo mzuri. Lakini napenda kukumbusha kuwa miaka ya nyuma tulikuwa tukipeleka Maafisa Utalii kwenye baadhi ya Balozi zetu muhimu ambao walikuwa wakitangaza vivutio vya Tanzania huko. Tuliwaondoa kwa sababu ya ukwasi.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuangalie uwezekano wa Bodi yetu ya Utalii kufungua ofisi ndogo za utalii kwenye miji maarufu wanakotoka watalii wengi kama vile Marekani, Italia, Ujerumani, Ufaransa, Japan na China. Naamini kuwa, ingawa matumizi yetu yatakuwa makubwa, lakini mapato yatakuwa makubwa zaidi kuziwezesha ofisi hizo kujilipia na ziada ikachangia kwenye uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya mambo ya kale. Mambo ya kale ni baadhi ya vivutio vya utalii wa aina yake. Wapo watalii, hasa watafiti wa mambo ya kali, waandishi wa vitabu na makala mbalimbali na kadhalika ambao wanasafiri mbali na kuandika mambo ya kale.

Kwa hiyo, Wizara naipongeza kwa kupitisha sera ya Malikale mwaka huu. Kwa hiyo mambo ya kihistoria kama ujenzi wa Kituo cha Taarifa ya Dr. Livingstone, njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa na vipusa, ujenzi wa vituo vya kumbukumbu za maeneo mbalimbali na utunzaji wa historia ya mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Kusini mwa Bara la Afrika ni mambo yatakayoweza kuwavutia baadhi ya watalii wasomi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, nashauri Wizara ishirikiane na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wakamilishe vituo vya kumbukumbu za maisha ya Mwalimu Julius K. Nyerere na Mzee Abedi Amani Karume.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni saa 11.00 Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wana dakika zao 75. Kwa hiyo, watatueleza mezani wamejipangaje ili anapoanza Naibu Waziri halafu atafuatiwa na mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zilizopangwa kwa asubuhi sasa tumefikia mwisho, nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## TAARIFA YA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 inayosema “Wakati wa kikao, Spika anaweza kutoa taarifa nyinginezo kadiri atakavyoona inafaa.”

Waheshimiwa Wabunge, Jumatatu tarehe 16 Juni, 2008 Mheshimiwa Spika alitoa Taarifa Bungeni kuhusu tukio lililokuwa limevumishwa kuwa, Jumatatu tarehe 9 Juni, 2008 majira ya saa 2.30 hivi usiku, watu wawili, mmoja akielezwa kuwa ni Mbunge na mwingine Afisa wa Bunge, waliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge na mmoja wa watu hao kusemekana kutupa vitu fulani kwenye viti vya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Kutokana na taarifa hiyo, Mheshimiwa Spika aliviagiza vyombo vinavyohusika na ulinzi na usalama wa majengo ya Bunge, yaani Idara ya Usalama wa Taifa, Polisi pamoja na Kampuni ya Mkandarasi aliyefunga mitambo na kamera za usalama kwenye majengo ya Bunge (*SSTL Group*), kufanya uchunguzi wa kitaalamu ili kubaini kama vitu vilivyosemekana kutupwa kwenye Ukumbi wa Bunge vilikuwa vina madhara kwa afya na maisha ya Waheshimiwa Wabunge au la. Taarifa ya uchunguzi ilipokelewa na Kaimu Katibu wa Bunge na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Spika.

Jana Alhamisi tarehe 10 Juni, 2008, Mheshimiwa Spika alititisha kikao cha pamoja cha Tume ya Huduma za Bunge na Kamati ya Uongozi ya Bunge ili kujadili na kuzingatia yaliyomo kwenye taarifa hiyo ya uchunguzi.

Tume ya Huduma za Bunge na Kamati ya Uongozi ya Bunge waliipokea na kuipitia taarifa hiyo pamoja na vielelezo vya picha na kuamua kama ifuatavyo:-

Kwa kauli moja, Wajumbe walivipongeza vyombo vya Ulinzi na Usalama na Mkemia Mkuu kwa kufanya kazi kwa uharaka na umakini mkubwa baada ya kuombwa na Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

(a) Kikao kimeridhika na taarifa ya Mkemia Mkuu na taarifa ya vyombo vya Ulinzi na Usalama kuhusu matokeo ya uchunguzi na mapendekezo yaliyotolewa. (*Makofi*)

(b) Wajumbe wameagiza kuwa, mapendekezo yaliyotolewa yatekelezwe mara moja ili kuimarisha usalama wa Ukumbi wa Bunge na watumiaji wa Ukumbi huo. (*Makofi*)

(c) Aidha, Wajumbe wanampongeza Mheshimiwa Spika kwa hatua za haraka na muafaka alizozichukua katika kulishughulikia suala hili linalohusu usalama wa afya na maisha ya Waheshimiwa Wabunge na watumiaji wengine wote wa Ukumbi huo. (*Makofi*)

(d) Kwa kuzingatia wajibu alionao Mheshimiwa Spika, kikao kilimpongeza kwa tabia yake ya uwazi na uwajibikaji kulitaarifu Bunge na Watanzania kuhusu hali ya Usalama wa Ukumbi wa Bunge na kwamba Mheshimiwa Spika alifanya vizuri kwa

kuagiza vyombo vya Ulinzi na Usalama na Mkemia Mkuu kufanya uchunguzi wa kina kuhusu uwezekano wa uwepo wa vitu vya sumu ya kisasa, kama vile, kimeta au *anthrax*.

Huo ni utaratibu wa kawaida katika Mabunge. Mfano mzuri ni mwaka 2004 katika Bunge la Uingereza ambapo ulitupwa unga ndani ya Bunge hilo uliodhaniwa kuwa ni kimeta. Spika wa Bunge la Uingereza aliagiza Wabunge na wageni wote waliokuwa Ukumbini kutoka nje ya Ukumbi na kuwekwa chini ya uangalizi mkali kwa lengo la kuchunguzwa na kupimwa afya zao. Ipo mifano mingi ya aina hii ikiwemo ile ya usafiri wa ndege ambapo ikitokea taarifa ya tishio la kuwepo bomu ndani ya ndege, safari husimamishwa na uchunguzi hufanyika mara moja. (*Makofi*)

(e) Kikao kimesikitishwa sana na baadhi ya watu na magazeti kwa kupotosha suala hili. Narudia, Kikao kimesikitishwa sana na baadhi ya watu na magazeti kwa kupotosha suala hili. (*Makofi*)

(f) Kikao kilisisitiza kuwa, hakuna wakati wowote ndani ya Bunge letu Tukufu, suala hili limehusishwa na ushirikina au mambo yanayofanana na hayo. Maelezo yaliyopo kwenye ukurasa wa kwanza na wa pili wa Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) za tarehe 16 Juni, 2008 yanadhihirisha ukweli huo. wanaopenda wanaweza kwenda kusoma. (*Makofi*)

(g) Kutokana na matokeo ya uchunguzi uliofanywa, suala hili sasa limefungwa na kwamba, kikao kiliagiza kuwa jambo lolote litakaloonekana kudhalilisha Bunge letu Tukufu, Ofisi ya Spika au Spika mwenyewe, lichukuliwe hatua haraka kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bunge tulizonazo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hizi ndizo taarifa ya Spika.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadiirio ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 Wizara ya Maliasili na Utalii

(*Majadiliano yanaendelea*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati Bunge linasitishwa mchana, Wabunge wote ambao waliomba kuchangia ukiacha wale ambao wamechangia zaidi ya mara mbili walimalizika. Kwa hiyo, sasa hivi kutokana na harakati kutokana na Kamati ya Matumizi nitaomba Naibu Waziri aanze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambaye yeye atatumia dakika kumi na tano na Mheshimiwa Waziri dakika sitini au inategemea mtakavyogawana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nitoe shukrani za kipekee sana kwa Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoionyesha kwangu na kunitua kuwa kwenye nafasi hii na hivyo kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza kabisa nikitetea Bajeti ya Serikali.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoionyesha kwangu na kwa mara nyingine kama nilivyomhakikishia wakati wa kiapo changu, basi niseme tu kwamba nitafanya kila niliwezalo kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Watanzania wenzangu kuyafikia maisha bora ambayo tunayatumainia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitoe shukrani za kipekee sana kwa Mheshimiwa Waziri wangu niseme ninapata malezi mazuri sana, ananifundisha kazi kwa upendo na ninajiona mtu ambaye nina bahati sana katika maisha yangu ya kwanza Serikalini kwamba nimepata Waziri ambaye ni wa malezi wa msaada mkubwa kama hivi. Nakushukuru sana mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru sana ndugu zangu, wananchi wenzangu wa Jimbo la Msalala Wilayani Kahama ambao daima tumekuwa pamoja na ni vizuri nikakiri kabisa kwamba kuna wakati walini-*miss*. Maana wakati tunaendelea kuzungumzia michango mbalimbali wako kadhaa walikuwa wananitumia meseji wananiuliza kwamba Mheshimiwa mbona hatukusikii ukiuliza maswali?

Nashukuru kwamba tumeendelea kufahamishana kwamba sasa maswali yetu yanayohusu mambo ya Msalala tunayazungumza Serikalini na wamelielewa hilo na wameendelea kuniunga mkono, nawashukuru sana. Naomba waendeleo na moyo huo huo kwa kuniamini na kunisaidia na mimi nitawasaidia kwa kushirikiana nao kuyafikiri maendeleo ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shukrani zangu, naomba nisikusahau wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Niseme nimepata pia changamoto nyingi sana kutoka kwao, nawashukuru sana hasa kwa maswali yao mazito ambayo yamenifanya nisilale usingizi hasa ninapojua kesho au kesho kutwa nina swali. Kwa hiyo, ninawashukuru sana, lakini pia nawashukuru sana kwa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo nimekuwa nikiyapata.

Kwa kumalizia, naomba nitambue msaada mkubwa sana ninaoupata kutoka kwa mke wangu mpenzi Liberata, amekuwa ni mtu wa msaada sana. Kadhalika kijana wetu Godlucky amekuwa akinipa changamoto kila nimwonapo huwa ananikumbusha majukumu mazito niliyonayo ya kifamilia, nawashukuru sana wanafamilia wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ni la Mheshimiwa Waziri mwenyewe, lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba ninamshukuru sana ameona na ameniagiza kwamba baadhi ya maeneo niyazungumzie. Kwa hiyo, katika mchango wangu nitaomba nigusie baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge ambazo wamezielekeza kwenye Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilikuwa nyingi sana na zinalenga maeneo mengi. Lakini ukiangalia sura nzima ya mjadala niseme inatoa taswira moja tu ya kutusaidia kutoa wito. Ukisikia kwamba kuna matatizo ya wanyamapori wanavamia mashamba ya watu, kuna simba wanakula watu, kuna mamba wanaharibu maisha ya watu na mali. Hii ina maanisha dhahiri kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge watatuunga mkono ili

tuweze kupata vitendea kazi, tuweze kupata pesa za kununua risasi, za kukabiliana na hao simba. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wao watatuunga mkono kwenye hoja hii ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia hoja moja moja, nikiacha chache ambazo Mheshimiwa Waziri mwenyewe atazizungumzia, hoja ya kwanza ilizungumzwa na Mheshimiwa John Samwel Malecela ametoa hoja yake kwa maandishi. Hoja yake kubwa anazungumzia kufungua mawasiliano kutoka hapa Dodoma kwenda kwenye Mbuga ya Ruaha. Jukumu hili la kutengeneza barabara hii kwanza tunakiri kwamba barabara hii ni ya muhimu sana, inayoanzia Mpunguzi, Mwitikila, Mgulo, Huzi, Manda, Ilangali hadi Hifadhi ya Ruaha.

Jukumu la kutengeza barabara hii kwanza ilivyo katika hali yake ya sasa kwa kweli inahitaji fedha na vyombo ambavyo vimekuwa vikiisimamia ambayo ni Halmashauri vimekuwa vikijitahidi. Tuseme hili tumelipokea katika mkakati wetu wa kuboresha mawasiliano na kufungua maeneo mbalimbali ya utalii. Kwa hiyo, naomba nimshukuru Mheshimiwa Malecela kwa ombi lake na nimhakikishie kwamba tutashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kupitia Halmashauri barabara hiyo inapopita ili tuweze kushirikiana kuangalia ni namna gani tunaweza tukafanya katika kuiboresha na kuifungua mawasiliano kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyozungumziwa ni yakutambua maeneo mbalimbali ya vivutio vya utalii yaliyoko nchini kwetu. Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia wapo wengi ni Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Ole-Telele, Mheshimiwa Dunstan Mkapu, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Dr. Sigonda na Mheshimiwa Mlata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikifanya zoezi la uanishaji wa Vituo vya Utalii nchi nzima. Kuna maeneo mengi tumeyafikia, jitihada bado zinaendelea. Maeneo ambayo tumeshafikia tayari na tumeshakamilisha ni pamoja na Iringa, Mbeya, Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga, Ruvuma, Mara, Singida, Kagera na Mwanza. Kwa hiyo, kuna Mikoa ambayo bado mkakati wetu ni kuendelea katika kipindi kijacho. Hoja nyingine iliyozungumzia ni ya Mheshimiwa Eustacy Katagira, inazungumzia kutambua vivutio vya utalii vilivyoko jimboni kwake Kwera. Wizara inamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri wake na niseme kwamba eneo hili nalo tutaliangalia. Tutaliweka kwenye orodha yetu ya maeneo ambayo tutayapitia katika muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Pia ipo hoja ya kuongeza bajeti ya Sekta ya Utalii ambayo imesemwa na Mheshimiwa George Lubeleje. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hili ni kweli kwamba Bajeti ya Utalii ni ndogo. Lakini pia bajeti kwa ujumla ya Kiserikali siyo kubwa kutokana na mapato ya Serikali yetu. Tutaendelea kuongeza pesa kwenye eneo hili jinsi mapato yanavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imezungumziwa na Mheshimiwa Lubeleje anasema mwaka 2006/2007 na 2007/2008 sekta ya utalii iliingizia Taifa letu mapato ya kiasi gani. Mwaka 2006/2007 sekta ya utalii iliingiza dola 950,000 na mwaka wa fedha 2007/2008 iliingiza dola bilioni 1.3 ambao ni wastani wa asilimia 17.2 ya pato la Taifa. Mheshimiwa Job Ndugai amezungumzia hoja kwamba baadhi ya hoteli zilizopo nje ya Hifadhi hasa ya Wilaya ya Ngorongoro, Monduli, Longido, Simanjiro na Serengeti kwamba hazilipi chochote kwa Wizara. Wizara kwa kifupi imetunga Kanuni za Utalii wa picha ambazo zitaanza kutumika mwaka ujao wa fedha mwaka 2008/2009. Nikupitia kanuni hizi tutaweza kuwabana waliojenga mahoteli kwenye maeneo hayo ili Serikali nayo iweze kupata kiasi kikubwa cha fedha kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja pia ilitolewa na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto akisema Wizara iboreshe programu ya utalii, *cultural tourism* na akashauri ni vizuri Wizara ikawa na dawati maalum ya kusimamia shughuli hii. Niliarifu tu Bunge lako Tukufu kwamba kwenye Bodi ya Utalii kuna dawati maalum linalosimamia shughuli hii. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba pengine tuongeze tu *publicity* ya dawati hili la *TTB* ambalo lipo ndani ya Wizara yetu kuona kwamba wananchi wanaohitaji maelezo, basi waweze kuyapata. Kwa hiyo, tumewahimiza wenzetu wa *TTB* waendele kufafanua mambo ambayo wanayafanya kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo imezungumziwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, dada yangu Mheshimiwa Sakaya, anashangaa au ananung'unika kwamba ujenzi wa Chuo cha Utalii ulichelewa. Niseme ni kweli ulichelewa, tulikusudia kuanza mwaka jana lakini sio uchelewaji mkubwa na sababu kubwa ya uchelewaji huo ni mchakato mzima wa kizabuni ambalo sio tatizo kubwa sana kwa sababu pia mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano na wabia, sio pesa zetu peke yetu, wako wengine na wana utaratibu wao mrefu kidogo unaohitaji ku-*approve* pesa zao ziweze kutumika. Tunashukuru kwamba mradi huu angalau umeanza ingawaje umechelewa kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushauri umetolewa na Mheshimiwa Charles Mlingwa, Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga ambao unasema *TTB* itengewe fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake. Ni kweli Bajeti ya *TTB* imekuwa ni ndogo sana kwa miaka ya nyuma, lakini tumekuwa tukiongeza jinsi pesa zinavyopatikana. Mwaka wa fedha huu tunaomaliza tulikuwa tumetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.5 na mwaka ujao wa fedha tumeongeza kidogo kiasi cha shilingi bilioni 4.1 na tutandelea kuongeza kwa jinsi fedha zinavyokuwa kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata pia ushauri mzuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Mlingwa na Mheshimiwa Kaboyonga ambao unasema kwamba Shirika la Ndege la *ATC* na *Precision Air* yaimarishwe. Ni ushauri mzuri, jitihada nyingi zinafanyika kupitia Wizara ya Miundombinu, nafikiri Waheshimiwa Wabunge wanafahamu *ATC* sasa hivi imekodisha ndege kadhaa na imeanza kwenda kwenye maeneo ambayo zamani ilikuwa haiendi. Naamini juhudi hizi zitaendelea na baada ya muda sio mrefu, shirika letu ambalo ni *National Carrier* litakuwa kwenye nafasi yake kiuchumi katika nchi na tutaweza kufanya shughuli zetu za utalii kwa ufanisi zaidi.

Kuna hoja pia imetolewa na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga pamoja na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Wanasema unahitajika mkakati wa kuendeleza ujenzi wa hoteli za kitalii na kuharakisha au kusaidia wawekezaji wadogo. Tuseme kuna majadiliano yanaendelea sasa hivi kati ya Benki ya *CRDB* pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *AFD* kwa ajili ya kuona ni namna gani waweze kuwa na mfuko wa kukopesha wenye hoteli ndogo ndogo. Majadiliano yanaendelea na naamini jambo hili likikamilika kutakuwa ni ufumbuzi mkubwa sana kwa wale ambao wana nia ya kuwekeza kwenye hoteli. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wawe wavumilivu kidogo, mchakato unaendelea, naamini baada ya muda mfupi tutaweza kupata ufumbuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja pia imetolewa na Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro Mbunge wa Mkinga. Yeye anashauri hasa tuimarisha utalii wa maeneo yanayozunguka Wilaya yake ya Mkinga, amezungumzia fukwe za bahari na zimezungumziwa na Wabunge wengi. Tuseme ushauri huu ni mzuri na tutauweka kwenye mikakati yetu ya kutangaza utalii na kufungua *corridor* mbalimbali za utalii katika nchi yetu.

Hoja nyingine imetolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, dada yangu Mheshimiwa Sakaya, anasema Serikali iweke mwongozo utakaoweka wazi hoteli katika hadhi fulani fulani akimaanisha madaraja ili wageni waweze kulipa *rates* kwa kufuatana na daraja. Tumesema katika hotuba yetu kwamba zoezi la kupanga *grade* linaendelea, limekamilika katika Mikoa ya Arusha na Manyara na mwaka ujao wa fedha tutalifikisha kwenye Mikoa mingine, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo, tutaweza kulikamilisha zoezi hilo muda sio mrefu.

Mheshimiwa Fuya Kimbita na Mheshimiwa Lubeleje wao wameuliza kwamba Serikali ina mpango gani kuanzisha Mfuko wa Utalii? Niseme tu kwamba mwaka huu Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria mpya ya utalii. Katika Sheria hiyo, imeruhusu kuanzishwa kwa *Tourism Development Levy*. Tozo hii itakapoanzishwa ndiyo itakuwa msingi wa kupata fedha za kuweza kuendeleza utalii. Kwa hiyo, tuna matumaini makubwa kwa sababu Sheria imeshapitishwa, basi imebaki tu utekelezaji na mchakato wa kuingia kwenye hiyo hatua. Upo kwenye hatua nzuri kabisa.

Hoja nyingine imezungumziwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally - Mbunge wa Viti Maalum, yeye anazungumzia mambo ya kale anasema kuna utafiti wowote uliofanyika wa mambo ya kale katika Mikoa mbalimbali ya nchi yetu? Nasema, ni kweli kuna utafiti umefanyika lakini haujamaliza nchi nzima. Mikoa ambayo tumeshaifikia hadi sasa ni pamoja na Arusha, Lindi, Iringa na Pwani na maeneo mengine tutayafikia katika muda mfupi ujao katika Bajeti ambazo tutakuwa tunaziwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imezungumziwa na Mheshimiwa Binilith Mahenge. Kaka yangu huyu amezungumzia kuhusu kufungua barabara za Kusini hasa zinazolingia kwenye Kitulo *National Park* na Milima ya *Livingstone* pamoja na

*Matema Beach*. Ni kweli hoja hii ni nzito na tumekuwa na mazungumzo na wenzetu wa miundombinu kwa baadhi ya barabara ambazo zinaingia kwenye *National Park* kama tunavyojua kisheria zipo chini ya *TANROADS* na sisi tunasimamia barabara ambazo ziko ndani ya hifadhi yenyewe. Tumezungumza na wenzetu wa miundombinu na ninaamini kabisa kwamba jambo hili wamelichukua wataongeza bajeti yao kwenye eneo hili na tunaamini kwamba hata sisi wenyewe tutakuwa tunashirikiana nao pale ambapo tunaona kwamba wanahitaji msaada zaidi ya kile ambacho wanakusudia kukifanya.

Kuna hoja imetolewa na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda - Mbunge wa Songwe, yeye anaombwa kwamba Bonde la Songwe liwe *National Park* au liwe hifadhi maalum. Ni wazo zuri, tuseme wazo hili tumelipokea. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge awe tayari tutakapohitaji msaada wake katika mchakato mzima wa kulitimiza lengo lake tuweze kushirikiana.

Hoja nyingine imetolewa na Mheshimiwa Maulida Komu, yeye anasema mchango wa sekta ya misitu ni ndogo sana kwenye nchi yetu. Tunasema ni kweli mchango ni mdogo na jitihada zinaendelea za kuimarisha sekta hii. Sekta hii hasa kuziba mianya kwenye maeneo kadhaa wa kadhaa ambayo kuna mapungufu ya kiusimamizi. Llakini pia kuna faida nyingine nyingi ambazo ni nje za mti wenyewe zinazotokana na mti huu. Tunajitahidi kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu faida za misitu na tunaamini jitihada hizo zikifanyika, sote tutaweza ku-*appreciate* umuhimu wa misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imezungumzwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally. Yeye anasema Serikali iangalie namna ya kuimarisha njia ya utumwa kutoka Bagamoyo hadi Kigoma. Wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri sana, tunashukuru, lakini kama tulivyosema, kwenye Bajeti yetu jambo hili tunalo na tumelitaja kabisa kipekee kwamba tuna mpango wa kufufua njia hiyo na kuna vituo saba ambavyo vimeshatambuliwa na sasa hivi vinaendelezwa ili viweze kutumika katika shughuli za utalii. Kuna hoja kutoka kwa Mheshimiwa Herbert Mntangi yeye anasema Wizara itengeneze Kanuni za Utalii. Mchakato uendelea na ninaamini utakamilika katika muda sio mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona hoja zilizoelekezwa kwenye maeneo kadha wa kadha ambayo Mheshimiwa Waziri alinielekeza nizungumzie zinapungua. Kuna hoja imezungumzwa na Mheshimiwa Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati yeye anasema kuna tofauti kubwa sana ya mishahara kati ya Watumishi wa Idara ya Wanyamapori na *TANAPA*. Hili ni kweli tumelichukua ingawa watumishi hawa wapo kwenye sekta mbili tofauti. Wengine wapo kwenye Serikali ambao wanaongozwa na Kanuni za Utumishi wa Umma, wakati wengine wapo kwenye Shirika linalojitegemea, lakini ni hoja ambayo tumeichukua na tutaangalia namna ya *synchronize* kwenye maeneo ambayo yanawezekana ingawa *TANAPA* wana uhuru wa kujipangia mishahara kwa mujibu wa *approvals* wanazozipata kwenye Bodi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imezungumzwa na kaka yangu Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba - Mbunge wa Busanda, amesema kuna tatizo la mamba eneo la Bukondo na Kasamwa. Kwa kifupi, Wizara itapanga kampuni ya kwenda kufanya



uwindaji kule. Kwa sababu maeneo mengi ambayo yana mamba huwa tunapangia kampuni kwenda kufanya uwindaji wa kitalii kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, tutapanga kampuni moja yenye nia ya kufanya uwindaji huo iende kuwinda kwenye maeneo hayo.

Kuna hoja imetolewa na mama yangu Mheshimiwa Chilolo, yeye anazungumzia tatizo la mbung'o kwenye maeneo ya Muhesi na Kizigo. Ni kweli tatizo hili lipo, lakini kwa kifupi sana, kwa utafiti uliofanyika ni kwamba mbung'o hawaathiri wanyamapori ingawa wana madhara makubwa kwa binadamu na mara nyingi wanapokuwa wanatoka nje ya hifadhi, basi huwa wanadhibitiwa na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Wizara imekuwa ikifanya kazi hii vizuri sana na naamini tutaendelea kuifanya kazi hiyo.

Baada ya kusema hoja hizo, kama nilivyosema kwenye maneno yangu ya utangilizi naomba kusema naiunga mkono hoja hii asilimia mia moja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii. Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni wengi na hoja walizochangia ni nyingi. Hali hii inaonyesha wazi kuwa, Waheshimiwa Wabunge wapo makini sana na Wizara hii na wapo tayari kutoa ushauri wa kuboresha utendaji wake kwa manufaa ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Aidha, kwa namna ya pekee, naomba kumshukuru Naibu wangu, Mheshimiwa Ezekiel Maige, kwa kutoa majibu ya baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingi kuhusu Wizara yangu zilianza kutolewa tangu wakati wa kuchangia Muswada wa Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma wa mwaka 2008, ambapo jumla ya Wabunge sita walichangia masuala yanayohusu Wizara yangu. Aidha, hoja nyingine zilitolewa wakati wa kujibu hoja ya Hali ya Uchumi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo Waheshimiwa Wabunge 26 walichangia hoja kuhusu Wizara yangu.

Halikadhalika, wachangiaji wengine wawili walichangia kuhusu Wizara yangu wakati wa kujadili Hotuba za Wizara ya Miundombinu na Afrika Mashariki. Napenda nikiri kwamba, kwa kuzingatia kuwa nina miezi mitano tu tangu Mheshimiwa Rais aniteue kuwa Waziri wa Wizara hii, maswali yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, yamenisaidia sana kuielewa zaidi Wizara yangu, kwani nimelazimika kujua mazingira ya vijiji vya ndani ambavyo isingekuwa rahisi kuvifahamu katika muda huu mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa dakika 50 nilizonazo, nitajitahidi kujibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge na iwapo muda utanifanya nishindwe kumaliza hoja hizo, naomba kuliahidi Bunge lako tukufu kuwa, ushauri uliotolewa tumeupokea na tutaufanyia kazi. Aidha, kwa vile ninayo majibu ya hoja zilizowasilishwa hapa,

nitahakikisha ninayatuma kwa maandishi kwa kila Mbunge ambaye nitakuwa sijajibu hoja yake hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili hoja ya Wizara yangu, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 27 wamechangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge 91 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza niwatambue kwa majina Wabunge waliochangia kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' na Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge waliochangia kwa maandishi katika hoja hii ni Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa John S. Malecela, Mheshimiwa Reynald A. Mrope, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Sophia M. Simba, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Sigifrid S. Ng'itu, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro na Mheshimiwa Janeth M. Massaburi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Mercy M. Emmanuel, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa James D. Lembeli na Mheshimiwa Dr. David M. David.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Ludovick J. Mwanzila, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Zabein M. Mhita na Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kupitia Bajeti za Wizara zilizokwishatangulia. Waliochangia kwa kupitia Bajeti ya Ukaguzi wa Mahesabu ni Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe. Waliochangia kupitia Makadirio ya Uchumi ni wafuatao: Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha na Mheshimiwa Yono S. Kevela.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, wakati bajeti ilipowasilishwa ni Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Alhaj Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyechangia kupitia Hotuba ya Miundombinu ni Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan A. Ngwilizi na aliyechangia kupitia Wizara ya Afrika Mashariki ni Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda sasa niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo kama ifutavyo:-

Naanza na maelezo ya jumla. Hoja ya wanyama waharibifu na wakali; matatizo ya wanyama waharibifu na wakali hususan Tembo, Simba na Fisi, yamekuwa yakijitokeza katika maeneo mbalimbali nchini. Hali hii inathibitisha kuwa pamoja na mafanikio mazuri ya uhifadhi wa wanyamapori hawa, mafanikio hayo yamegeuka kuwa adha na tatizo kwa wananchi. Kwa kutambua changamoto inayotokana na ongezeko la migongano kati ya wanyamapori na binadamu, Wizara yangu imejipanga kukabiliana na hali hiyo kwa kutumia askari wa wanyamapori wa Serikali na kwa kushirikiana na askari wa wanyamapori wa Halmashauri za Wilaya, kuendesha doria za msako wa wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, kupitia Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori, Wizara yangu itanunua risasi na vitendea kazi vingine kwa ajili ya kupambana na wanyamapori hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hizo, Wizara yangu itaendeleza mkakati wa kutoa mafunzo kwa askari wa wanayamapori wa vijiji, ambao wanatarajia kusaidia katika maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (*WMAs*), pamoja na michango ya makampuni ya wawindaji wa kitalii. Pia kama nilivyoieleza kwenye hotuba yangu, Wizara yangu itaendeleza upanuzi wa mbinu zilizotokana na matokeo ya tafiti za kukabiliana na Tembo na Simba, ambazo katika miradi ya majaribio zimeonyesha mafanikio. Aidha, kutokana na matokeo ya tafiti hizo, Wizara yangu itatoa elimu kwa wananchi katika kuwasaidia kupunguza migongano na wanyamapori hususan kwenye yale maeneo yenye matatizo makubwa. Wizara itaendelea na utaratibu wa kutenga idadi ya wanyamapori watakaowindwa kila mwaka hususan mamba kwa kutoa kipaumbele kwa yale maeneo yenye matatizo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kueleza ya kwamba, taarifa tuliyoipata leo hii ni kwamba, kwa upande wa Mkoa wa Singida, tayari Simba mmoja jike ameuwawa kwa kushirikiana askari wa wanyamapori na wananchi. Halikadhalika, sasa hivi wanamtafuta Simba dume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji kitalii: Naomba kuliarifu Bunge lako kuwa, jumla ya makampuni 54 yaliruhusiwa kuendesha shughuli za uwindaji wa kitalii mwaka 2007. Kati ya hayo, makampuni 33 yanamilikiwa na Watanzania, 12 wageni na 9 ni ubia kati ya wageni na Watanzania. Mgawanyo wa vitalu kwa makampuni hayo ni kuwa vitalu 68 vimegawiwa kwa makampuni ya Watanzania, 33 kwa makampuni ya ubia na 57 kwa makampuni ya wageni. Ugawaji wa vitalu hivyo ulifanyika kufuatia ushauri wa Kamati ya Ushauri wa Kugawa Vitalu, iliyoundwa mwaka 1996 kwa kuzingatia kuwa, kulingana na utaratibu wa kanuni za uwindaji wa kitalii za mwaka 2002, umiliki wa vitalu wa sasa utamalizika baada ya msimu wa uwindaji wa mwaka 2009 kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, ikiwemo hoja binafsi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, Mbunge wa Kwera, aliyowasilisha kwenye Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge hili, Wizara yangu imeanza mchakato wa kutathmini hadhi na sifa za vitalu vya uwindaji wa kitalii vilivyoko nchini.

Kazi hii inafanywa na Taasisi yetu ya Utafiti wa Wanyamapori (*TAWIRI*), ikishirikiana na Wizara ya Ardhi, pamoja na *Institute of Resource Assessment* – Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Aidha, Wizara yangu imeunda Kamati Maalum, itakayofanya uchambuzi maalum wa mapendekezo ya taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kuhusu uboreshaji wa tasnia ya uwindaji wa kitalii ili uandaliwe utaratibu stahiki wa kugawa vitalu baada ya msimu wa 2009.

Kwa taarifa tu ni kwamba, Kamati hiyo Maalum itaanza kazi baada ya kumaliza Bunge hili. Pia tutahakikisha kwamba, mpaka kufika mwezi Desemba, 2008, Kamati itakuwa imemaliza uchambuzi huo kwa ajili ya kuanza shughuli za maandalizi ya ugawaji baada ya 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kuhusu mabadiliko ya ada za uwindaji wa kitalii za mwaka 2007; Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 48 katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Pamoja na vyanzo vingine, kiasi hiki kilitarajiwa kutokana na nyongeza ya viwango vya ada za vitalu vya uwindaji wa kitalii na ada za baadhi ya wanyama. Viwango vya ada hizo vilipandishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 159 la tarehe 29 Juni, 2007, kwa kiasi cha kati ya aslimia 380 hadi 500 chini ya kifungu cha 94 cha Sheria ya Wanyamapori. Kwa bahati mbaya, viwango hivi vipya vya ada vilishindwa kuhimili ushindani wa kibiashara wa soko la uwindaji wa kitalii kwa sababu zifutazo:-

- Kulingana na utaratibu wa biashara ya uwindaji wa kitalii, uuzaji wa safari za uwindaji kwa mwaka 2007 ulikuwa umefanyika zaidi ya muda wa kati ya miezi sita na miaka mitatu iliyotangulia na kwamba, mikataba ya kuuza safari hizo ilikuwa imeshafungwa kwa kutumia viwango vya ada za mwaka 2006. Ni vyema ikaeleweka pia kuwa viwango hivyo vya mwaka 2006 vilikuwa vimefanyiwa marekebisho ya kuongezwa mwaka 2005.

- Uwindaji kwa msimu wa mwaka 2007, ulikuwa umeshaanza na hivyo baadhi ya wawindaji walikuwa tayari maporini wanawinda kwa kutumia viwango vya ada ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, wageni waliokuwa tayari wamepanga kuja kuwinda Tanzania, walianza kufuta safari zao kwa madai kuwa, hawakujiandaa kwa bei mpya. Ili kuokoa mapato ya Serikali yasiathirike kwa kiwango kikubwa zaidi na kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na wadau wa biashara ya uwindaji wa kitalii, Wizara ililazimika kufanya marekebisho ya viwango hivyo kwa kuvipunguza bei.

Hatua hiyo ilichukuliwa kulingana na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura ya 283, kifungu cha 94, ambacho kinampa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia wanyapori, mamlaka ya kuunda kanuni za matumizi ya wanyamapori, ikiwa ni pamoja na kuweka viwango vya ada mbalimbali zikiwemo ada za uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ilifanywa kwa nia njema kabisa ili kuhakikisha kwamba hatupati hasara kubwa zaidi angalau tuweze kupata chochote. Hata hivyo, ilikuwa kwamba madhumuni ya Wizara katika bajeti ya mwaka huu, kwa vyovyote vile tungekuja kutoa hiyo taarifa ya mambo yaliyotukuta na jinsi tulivyojitahidi kuyaokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya usafirishaji wa magogo kwenda nchi mbalimbali za nje: Katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa maelezo yafuatayo ya ujumla:-

Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 ilipiga marufuku usafirishaji wa magogo ya miti ya aina zote nje ya nchi kupitia Kanuni za Misitu na Tangazo la Serikali Namba 153 lililochapishwa tarehe 21 Mei, 2004. Aidha, usafirishaji wa mbao nje ya nchi zenye unene wa nchi sita, ulipigwa marufuku kwa Tangazo la Serikali Namba 236 la tarehe 7 Desemba, 2007 na kuruhusu mbao zenye unene usiozidi nchi nne zisafirishwe na kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, jumla ya makontena 52 ya mpingo yalisafirishwa nje ya nchi kupitia Bandari ya Dar es Salaam mwaka 2007 ni kwamba, kwa takwimu zilizopo, makontena yaliyosafirishwa nje ya nchi ni 13 ya vibao vidogo vinavyotumika kutengeneza vifaa vya muziki (*Clarinets*) na vinyago na siyo magogo 24. Jumla ya makontena ya mazao ya mpingo yaliyosafirishwa ni 37 kwa mwaka 2007, ambapo utaratibu wa sheria ulizingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Sakaya, walitaka Bunge lipewe taarifa ya Kamati iliyoahidiwa kuundwa na aliyekuwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kufuatilia kuchunguza suala la magogo nchini China. Mnamo Agosti, 2007, Kamati ya watu wanane iliundwa ili iweze kushughulikia tofauti iliyojitokeza kuhusu mita za ujazo wa mbao nene zaidi ya nchi nne, zilizodaiwa kupelekwa China na mita za ujazo zilizosajiliwa Bandarini Dar es salaam. Kutokana na ufinyu wa bajeti, Kamati haikuweza kwenda China. Hata hivyo, kamati ilifanya tathmini ya viwanda vinavyochakata magogo humu humu nchini. Kilichobainika ni kwamba, viwanda vikuu hususan vya Dar es Salaam vilikuwa na tofauti kati ya ujazo uliopitishwa bandarini, ujazo wenye nyaraka halali na ujazo halisi uliokuwa viwandani. Hii inamaanisha kwamba, wamiliki wa viwanda hivyo walikuwa na mbao nene zaidi ya nchi nne ambazo zilipatikana kinyume cha sheria. Baada ya kubaini hilo, Wizara iliandaa taratibu za kuwafikisha wahusika kwenye vyombo vya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magogo yaliyozagaa mikoani na bandarini baada ya tangazo la kupiga marufuku usafirishaji nje ya nchi, magogo hayo yalikusanywa na kupigwa mnada. Wizara imeagiza wenye magogo halali, kuendelea kukusanya magogo ambayo hayakuonekana hapo awali na kuyaondoa kwa ajili ya uchakataji ifikapo

mwezi Agosti, 2008. Magogo yatakayokuwa hayajaondolewa kwa muda uliopangwa, yataitaifishwa na kupigwa mnada na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kuendeleza maeneo ya kiutamaduni kuwa vivutio vya utalii: Idara ya Mambo ya Kale imekuwa ikifanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979. Sheria hii haitoi nafasi kwa matumizi endelevu ya kiutalii wala kushirikisha Sekta Binafsi katika Uhifadhi na Uendelezaji wa Urithi wa Kiutamaduni hususan ule usioshikika. Sheria hii ilijikita kwenye vitu vinavyoshikika na vyenye umri wa zaidi ya miaka 100. Hata hivyo, Sera ya Mali Kale ambayo imepitishwa mwezi Mei, 2008, itatoa fursa ya kuhifadhi urithi huo.

Kwa Mtazamo huu, Wizara yangu itahakikisha kuwa, marekebisho ya sheria yatakayofanyika, yatawezesha kwa kiwango kikubwa kutekeleza mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kurekebisha masalio ya mijusi (*Dinosaur*) yaliyoko Berlin, Ujerumani. Suala la kurudisha vifaa vya urithi wa utamaduni ikiwa ni pamoja na mijusi wa kale vilivyoko nje ya nchi, unasimamiwa na Mkataba wa *UNESCO* wa mwaka 1970 na pia Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 1995. Mikataba hii inaelekeza kuwa ni lazima ifanyike mijadala ya makubaliano kati ya nchi husika na kuwepo uhakika wa mazingira mazuri ya kuhifadhi vifaa, masalia hayo kwa maana ya mahali na utaalum stahili kabla ya kuvirejesha. Kwa msingi huo, yanahitajika maandalizi makubwa ya ujenzi wa majengo ya kutosha ya kuhifadhi masalia hayo, maabara ya kisayansi na wataalam stahiki. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imekuwa na mawasiliano na Wataalam wa Chuo Kikuu cha Chicago cha Marekani katika kuandaa mazingira mazuri, ambayo masalia ya mijusi ya namna hiyo inaweza kuhifadhiwa na kutumiwa kiendelevu kama kivutio cha utalii hapa nchini na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na jitihada hizo, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara inakamilisha utaratibu wa kurudisha nchini masalio ya Akiolojia na Pantolojia yaliyoko katika Makumbusho ya Nairobi nchini Kenya. Masalia haya yatahifadhiwa katika Makumbusho ya Nyumba ya Utamaduni ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya jumla, naomba sasa kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja za Wabunge, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, pamoja na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda na Mheshimiwa Fuya Kimbita, wao walikuwa na hoja ya kwamba, fedha za Miradi ya Ujirani Mwema zipelekwe kwenye Halmashauri husika kwa kuwa Halmashauri ndizo zinajua matatizo ya wananchi. Napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo: Lengo la Miradi ya Ujirani Mwema ni kusaidia jamii zinazoishi jirani na Hifadhi za Taifa na ndio maana fedha hizi hutolewa na *TANAPA*, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vijiji jirani. Katika kusimamia Miradi hiyo, wanavijiji jirani hupewa kipaumbele katika shughuli zote za ujenzi. Vijiji hivi ndio huibua Miradi wanayoitaka na kisha kuwasilisha mchanganuo wao *TANAPA*, kwa ajili ya utekelezaji. Pamoja na maelezo hayo, Wizara yangu ipo tayari kushiriki kwenye

mazungumzo na Halmashauri, ikiwa ni pamoja na Uongozi wa Vijiji husika ili kuona njia nzuri ya kuboresha matumizi ya fedha za ujirani mwema. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba mpunguze sauti wote mlioko ndani ya ukumbi! Hata wengine nje huko wanazungumza, naomba mpunguze sauti.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Hoja nyingine iliyotolewa na Wabunge niliowataja ni kuhusu vigezo vinavyotumika kutoa fedha za ujirani mwema kwamba havieleweki. Utaratibu unaotumiwa na *TANAPA* katika Miradi ya Ujirani Mwema kwanza ni kuwaelimisha wananchi namna ya kuibua miradi itakayowasaidia mahali walipo na kisha kutayarisha mchanganuo wa gharama za ujenzi. Baada ya hapo, wanajamii pia huwa wanatakiwa kuchangia asilimia 30 na Shirika linachangia asilimia 70. Hata hivyo, pale inapoonekana jamii husika inahitaji mradi lakini haina uwezo huo wa kuchangia gharama, mara kadhaa Shirika la *TANAPA* limekuwa likichangia zaidi ya hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Miradi ya Ujirani Mwema, *TANAPA* mwaka hadi mwaka, imekuwa ikiongeza kiwango cha fedha kwa ajili ya Miradi hiyo katika bajeti yao kulingana na ukubwa wa kazi na majukumu ya shirika yaliyopo. Tukumbuke pia kwamba, kati ya Hifadhi 15 zote ni Hifadhi 5 tu ndizo zinazozalisha fedha na hifadhi zilizobakia zinategemea msaada kutoka *TANAPA* ili kuweza kuzikuza na kuziendeleza. Kwa hali hiyo basi, napenda niwasihi Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutajitahidi na *TANAPA* itajitahidi, pale panapowezekana itakuwa ikiongeza na pale ambapo tunajua Halmashauri haijiwezi, *TANAPA* pia itakuwa ikichangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Benson Mpesya, hoja yao ilikuwa ni kuhusu Wizara imetenga kiasi gani kwa ajili ya Wananchi wa Mbarali waliohamishwa katika zoezi la kuwaondoa wananchi katika eneo la Ihefu. Zoezi la kufidia Wananchi hao waliohamishwa katika eneo la Ihefu, limegharimu kiasi cha shilingi bilioni sita kwa ajili ya kufidia wananchi waliohamishwa katika maeneo hayo. Kwa kutambua umuhimu wa kutengeneza miundombinu bora, maeneo mapya yalitengwa kwa ajili yao. Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kupitia Shirika la Hifadhi la *TANAPA*, katika mwaka wa fedha 2008/2009, imetenga kiasi cha shilingi 100,099,535 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama vile shule, nyumba za walimu, vyoo, pamoja na samani ambazo zitakuwa zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya alitoa hoja kwamba, njia ya Machame katika Mlima Kilimanjaro itengenezwe mahema kwa ajili ya kulala wapagazi wanaopeleka wageni katika Mlima Kilimanjaro. Njia ya Machame ni eneo linalofahamika kitaalam kama ni *wilderness area*, ambalo ni maalum kwa safari za kupiga mahema. Aidha, mahema ya kudumu hayataweza kudumu kwa muda mrefu kulingana na hali ya hewa ya baridi kali na hivyo kulazimika kubadilishwa mara kwa mara, suala ambalo ni gharama kubwa. Hata hivyo, Wizara yangu kupitia *TANAPA*, itakaa na wadau wa utalii katika eneo hili, kuangalia namna bora ya kuboresha huduma katika eneo hili bila ya kuathiri mazingira asilia ya eneo hilo.



Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Owenya alikuwa na hoja nyingine kwamba, kuwepo na vyama vingi vya wapagazi. Kuwepo kwa vyama vingi vya wapagazi ni suala la kisheria, ambalo linahitaji kupitiwa upya kwa sheria iliyopo. Ni wazi kuwa, uwepo wa vyama vingi vya wapagazi utasababisha uhibitwa kuwa mgumu na pia kuharibu biashara ya utalii. Hata hivyo, hivi karibuni Wizara yangu iliagiza wananchi kujiunga katika vyama vidogo vidogo katika milango mbalimbali ya kupandisha Mlima Kilimanjaro na kisha wawe chini ya mwamvuli wa chama kimoja kikubwa, kitakachotambulika kisheria, pamoja na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yake nyingine ilikuwa ni nyumba za watu wanaohusika na upokeaji wa wageni zimejengwa na bati na baridi ni kali sana; hivyo, kuwafanya washindwe kufanya kazi sawa sawa. Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, imeshatambua tatizo hilo na hatua kadhaa zimechukuliwa ili kurekebisha hali hiyo ambapo tayari mabanda mawili yameshajengwa katika maeneo ya *Mweka Hut* na *Machame Hut*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni lini Barabara ya *Old Moshi* itafunguliwa ili kuvutia kuongeza idadi ya watalii. Tumeupokea ushauri huo. Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge na ushauri huo Wizara itaufanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa *Sopa Lodge* iwekewe kiwango maalum cha kulipa, kwani wanacholipa sasa ni kidogo, pamoja na gharama za tozo kwa ajili ya wageni wanaotembela Hifadhi ya Taifa ya Gombe ni kidogo sana kulinganisha na nchi nyingine. Shirika lipo katika mchakato wa kupitia upya viwango vyake vyote vya tozo na ada mbalimbali zilizopitwa na wakati na ili kufanikisha hilo, majadiliano na wadau yanaendelea na yanatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, alikuwa na hoja inayosema kwamba, Njombe Mjini kuna hoteli nyingi nzuri, lakini huduma ni za chini sana. Anaomba wataalam waweze kwenda kule kutoa mafunzo mafupi kuinua kiwango cha huduma. Katika mwaka 2008/2009, Wizara imepanga kufanya uhakiki wa hoteli (*Hotel Inventory*) na huduma nyingine za malazi Mkoani Iringa. Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Utalii, itatoa mafunzo ya utoaji huduma hata kabla ya zoezi la uhakiki wa hoteli. Wataalam wangu wapo tayari kujadiliana suala hili kwa kina na Mheshimiwa Anne Makinda. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndesamburo alitoa hoja kwamba, urefushaji wa magari ya kubebea wageni unahatarisha usalama wa abiria. Utoaji wa leseni kwa magari yanayobeba watalii, huzingatia taarifa ya ukaguzi wa magari husika unaofanywa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kitengo cha Usalama Barabarani, hivyo Wizara yangu itashauriana na Wizara husika ili kuangalia suala hili kwa makini. Hata hivyo, ningependa kutoa wito kwa wadau wetu wanaoshughulika na usafirishaji kwamba, wangeliangalia wazo hili kwa

sababu ni tatizo ambalo litatuharibia sifa yetu Tanzania, hali kadhalika kufukuza Watalii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa kuuimarisha Uwanja wa Ndege wa Moshi ili usaidie kusafirisha Watalii wanaotembelea Mlima Kilimanjaro. Uwanja huu ni kweli unaweza kutumika kwa ndege ndogo ndogo kuleta watalii. Wizara yangu imewasiliana na Wakala wa Viwanja vya Ndege na wametoa taarifa kuwa, wanaendelea na mchakato ambapo matengenezo ya kuwezesha ndege ndogo kutua yatafanyika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, hoja yake inasema kwamba, kwa nini Serikali imeruhusu ujenzi wa *Lodge* ya *Afrique* kwenye mapitio ya wanyama kati ya Hifadhi ya Tarangire na Manyara. Ujenzi wa *Lodge* hii ulifanyika baada ya Wawekezaji hao kuingia Mikataba na wanavijiji wa vilima vitatu. *Lodge* hii ipo katika eneo la Mdori, ambalo ni mapitio ya wanyama kati ya Hifadhi ya Tarangire na ile ya Manyara. Taarifa tulizonazo hivi sasa ni kuwa, kuna mgogoro kati ya wawekezaji na wenyeji wa Kabila la Wamang'ati wanaotumia eneo hilo kwa malisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mgogoro huu umepelekwa katika Baraza la Ardhi la Wilaya kwa ufumbuzi zaidi. Sisi kwa sababu ni wadau huko, naahidi kwamba, tutafuatilia kwa karibu mgogoro huu unavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa James Lembeli hoja yake ilikuwa kwamba, utangazaji kupitia *CNN America* ambao uligharimu fedha nyingi, umeleta manufaa gani hadi sasa. Tangazo liliwekwa kwenye *television* ya *CNN* baada ya ushauri wa kina uliofanyika kati ya Wizara, Taasisi husika na Balozi huko Marekani. Baada ya tangazo kutolewa, taarifa za awali zimeonyesha kuwa, uelewa wa Wamarekani kuhusu vivutio vyetu umeongezeka, pia idadi ya Wakala wanaoitangaza Tanzania wameongezeka, hali kadhalika maulizo ya kutaka kuja Tanzania yameongezeka na pia watu zaidi ya milioni 152 wa Marekani wameona tangazo hili, hivyo tuna imani kuwa idadi ya watalii kutoka Marekani itaongezeka siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Fuya Kimbita, wameuliza fedha zilizopelekwa kwenye Balozi zetu za Nje kutangaza utalii zimefanya kazi gani hadi sasa. Balozi zetu zilizoko nchi za nje, ndiyo kiungo kikubwa cha kukuza masoko yetu ya utalii, mara nyingi huwa tunatumia balozi zetu kusaidia juhudi za kuhamasisha na kutangaza utalii wetu. Kwa ujumla, fedha zilizopelekwa katika Balozi hizi zimetumika kuboresha mazingira ya mapokezi kwa wageni wanaotembelea Balozi hizi na kununua vifaa na nyenzo mbalimbali za kutangaza na kuhamasisha wageni kuitembelea Tanzania. Fedha hizi zilipelekwa kwa maelekezo maalumu kwani Wizara ndiyo ilitoa maelekezo fedha zitumikeje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Alyoce Kimaro, hoja yake inasema kwamba, je, Kamati ya Brand Tanzania bado ipo; na kama ipo, ipo chini ya Wizara gani? Hapo awali Kamati ya Brand Tanzania ilikuwa chini ya Ofisi ya Rais na kwa sasa Kamati imeundwa upya na ipo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hivi sasa Kamati

imeshaanza kazi ndogondogo za maandalizi na tulikuwa tukisubiri baada ya bajeti hii, tuweze kupata fedha na Kamati ianze kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya, hoja yake ilikuwa vyama vingi vya wapagazi, yaani *porters* viruhusiwe kutoa huduma Mlima Kilimanjaro. Wizara imechukua pendekezo hili na itafuatilia kwa ushirikiano na vyombo vingine kama vile *KINAPA*, *TATO* na *TCT* ili liweze kutekelezwa. Pia shughuli za *tour operators* zifanywe na Watanzania tu. Sheria ya Utalii ya 2008, imeainisha shughuli zifuatazo zifanywe na Watanzania tu, shughuli hizo ni kama *tour guiding*, *travel agency*, *mountain climbing* na *car hire*. Ili kuwezesha wananchi wengi kushiriki katika biashara ya utalii, nitahakikisha kwamba, Wizara yangu inasimamia kuhakikisha kwamba, kazi hizi zote zinashikwa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mtangi, alisema Serikali itenge fedha ili kuwezesha ukaguzi wa Wakala Utalii Moshi, Tanga, Mwanza, Musoma, Manyara na Kusini mwa Tanzania. Katika mpango kazi 2008/2009, zoezi la ukaguzi wa Wakala wa Utalii limejumuishwa kwa Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Mwanza. Katika mpango wa kazi wa mwaka utakaofuatia, tutajumuisha mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine Wizara iboreshe na kuongeza hadhi ya karatasi ya leseni za wakala wa utalii. Wizara inamshukuru Mheshimiwa Herbert Mtangi, kwa ushauri huu na tutaufanyia kazi. Hoja nyingine, Wizara iboreshe mafunzo katika Chuo cha Utalii kwa kuanzisha mafunzo ya lugha mbalimbali za kimataifa. Sasa hivi chuo kinatoa mafunzo ya lugha za kiingereza na kifaransa, hata hivyo, chuo kipya kinatakiwa kuwa na maabara ya lugha ambapo lugha nyingi zaidi zitafundishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mtangi, pamoja na Mheshimiwa George Lubeleje pia wana hoja inayosema kwamba, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kwamba, kunakuwa na ulinzi na usalama wa kutosha kwa watalii wanapoingia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kuimarisha usalama kwa Watalii. Hivi sasa Wizara hizi zinaendelea na mchakato wa kuanzisha Kitengo cha Polisi kwa ajili ya watalii (*Tourism Policy Unit*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, alisema kwamba, kwa muda mrefu Mapango ya Amboni yamekuwa kivutio kikubwa na kitega uchumi kwa Mkoa wa Tanga, lakini miaka ya hivi karibuni Mapango haya yamekuwa yakipoteza sifa na kutosikika. Wizara inakubaliana na ushauri huo na itaanza kukiboresha kituo hicho katika mwaka wa fedha huu wa 2008/2009.

Hoja ya pili, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa, imeangalia ni vipi eneo lenye maji moto yenye *sulphate*, ambalo limeachwa bila uangalizi kuona ni jinsi gani ya kufanya na kuweza kupatumiwa kama sehemu ya kitalii na utafiti kwa faida ya nchi nzima. Wizara ina taarifa na eneo hili lenye maji yenye uvuguvugu lakini kwa mujibu wa Sheria

ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979, eneo hili halipo chini ya Wizara yangu. Hata hivyo, Sera ya Mali Kale iliyopitishwa, itawezesha marekebisho ya Sheria hii ya Mambo ya Kale ili kuongeza wigo wa rasilimali za kale.

Mheshimiwa John Malecela, pamoja na Mheshimiwa Godfrey Zambi walikuwa na hoja zifuatazo; Wizara itambue umuhimu wa michoro ya miamba ya Kolo Kondo, ambayo ni kivutio kikubwa sana kwa Watalii nchini na kwamba, iboreshe mazingira ya sehemu hii muhimu duniani na pia ifanye juhudi kutangaza duniani michoro hii ili kuvutia zaidi watalii. Halikadhalika, Wizara iishirikishe *UNESCO* katika jambo hili na pia miundombinu kwenda kwenye michoro hii iboreshwe. Mwisho Wizara itangaze Kimondo cha Mbozi Mkoani Mbeya kwa makini maana ni kitu adimu.

Wizara inatambua umuhimu wa michoro hii ya miambani na hasa kuhusiana na faida yake katika utalii wa utamaduni. Kwa sababu hiyo, Wizara imefanikiwa kuliingiza eneo la michozo hiyo katika orodha ya maeneo ya urithi wa dunia tangu mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara inakubaliana na ushauri na itaufanyia kazi kuhakikisha kwamba, ushauri wote uliotolewa tutautumia. Hoja ya pili, ilikuwa inahusu kuboresha mazingira na miundo ya kufika mahali kilipo hicho Kimondo, ikiwa ni pamoja na kukitangaza kwa jamii yetu ili wajue kuwepo kwake na pia iweke Mtaalam wa masuala ya Sayansi, anayeweza kutoa maelezo fasaha kuhusu Kimondo hicho kwa wageni hasa wa nje. Wizara kwa kutambua umuhimu wa Kimondo hicho, ilikitangaza kuwa Kumbukumbu ya Taifa kwa *GN* Namba 90, tarehe 3 Machi, 1967. Wizara inakubaliana na ushauri huu na itaendelea kuufanyia kazi ili kupata mtaalam fasaha, atakayeweza kuwaeleza wananchi kuhusu Kimondo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Severina Mwijage, alikuwa ana hoja mbili; ya kwanza, kunyanyaswa kwa wafanyakazi wa hoteli iliyobinafsishwa Seronera na kutokulipwa fidia, hoja yake ya pili ni mwekezaji kuchukua wanyama na kuwapeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza, kulingana na maelezo ya Uongozi wa Hoteli, suala la kufanya kazi kwa mkataba wa muda mrefu bila kuajiriwa; limepatiwa suluhisho kwa watumishi 22 kuthibitishwa kazini kuanzia tarehe 1 Juni, 2008. Aidha, lalamiko la kupunjwa malipo na *PSRC*, hili bado lipo na Wafanyakazi wamelipeleka mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhusu kuchukua wanyama; Wizara yangu imelifuatilia kwa karibu na haijapata ushahidi wowote wa wanyama kusafirishwa kinyume cha sheria, iwapo kuna Mheshimiwa Mbunge mwenye ushahidi, Wizara ipo tayari kushirikiana naye ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, alikuwa na hoja mbili; hoja ya kwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti haipati mapato yoyote kutokana na hoteli zilizojengwa kwenye hifadhi hiyo na hoja ya pili, Serikali irudishe ushuru wa kitanda cha Halmashauri Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara haina kipingamizi kwa Halmashauri za Wilaya kukusanya mapato kutoka kwenye hoteli zilizo ndani ya Hifadhi ya Taifa iwapo zitawasiliana na Wizara ya Fedha ili kupata idhini stahili. Ushuru huu wa kitanda ulifutwa na Serikali, kama hatua ya kuondoa kodi na tozo zilizoonekana kuwa kero.

Mheshimiwa Lucy Owenya, anasema makampuni ya kigeni hayakuifurahia Sheria ya Utalii ya mwaka 2008; yanatoa taarifa za kupotosha kupitia vyombo vya habari vya nje kuwa watu 20 hufa kila mwaka wakati wakipanda Mlima Kilimanjaro, Serikali itoe tamko kuhusu upotoshwaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la Utalii wa Mlima Kilimanjaro, Wizara kupitia Shirika la Hifadhi ya Taifa, lina jukumu la kusimamia shughuli zote za utalii ikiwa ni pamoja na kutunza kumbukumbu za idadi ya watalii wanaopanda mlima na matukio ya vifo. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge ni kweli kuwa, katika Gazeti la *The East African Newspaper* la tarehe 2 - 8 Juni, 2008, iliandikwa mada iliyodai kuwa, waongoza wageni na wabeba mizigo wapatao 20 wanakufa kila mwaka katika Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, makala hiyo ilinukuliwa katika *The London Based Times*, takwimu hizi hazikuwa sahihi, kwani kulingana na kumbukumbu za Wizara kati ya mwaka 2000 hadi Juni, 2008, jumla ya waongoza wageni na wabeba mizigo tisa tu walifariki. Wizara ya Maliasili na Utalii, imetoa tamko kukanusha taarifa hiyo kupitia Magazeti ya Mwananchi, *The Citizen*, *Majira*, *The African*, *Uhuru* na *Mtanzania*. Aidha, Gazeti la *The East African* la tarehe 23 Juni, 2008 lilichapisha makala ya kuomba radhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Estherina Kilasi ana hoja mbili; hoja ya kwanza, inahusu tathmini iliyofanyika kwa ajili ya kufidia wananchi waliohamishwa ili kupisha upanuzi wa Hifadhi ya Ruaha, inalalamikiwa sana na wananchi. Hoja ya pili ni ahadi nyingi zilizotolewa na Serikali wakati wa maandalizi ya kuwahamisha wananchi hao hazitekelezeki na wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini kwa ajili ya kuwafidia wananchi waliohama ili kupisha upanuzi wa Hifadhi ya Ruaha, ilifanywa na Wataalam kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na kukaguliwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Kufuatia tathmini hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TANAPA*, iliwezesha malipo wananchi 1571 ambao ni sawa sawa na asilimia 98 kati ya 1600 katika awamu ya kwanza. Katika awamu ya pili, vijiji vilivyosalia ambapo ni jumla ya wananchi 3137, vimefanyiwa ukaguzi wa mali zao ikiwa ni mazao, majengo, mashamba na Taasisi za Serikali. Malipo kwa ajili ya wananchi hao, tayari yametumwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na yameanza kulipwa kuanzia mwezi Mei, 2008.

Baada ya malipo hayo, yamejitokeza malalamiko; tumepokea jumla ya barua 1149 zikidai kupunjwa stahili zao. Malalamiko hayo yamefanyiwa kazi na kupatiwa majibu, ikiwa ni pamoja na malipo ya ziada kwa wale waliostahili. Kwa wale wananchi waliolipwa fidia, tayari wameshamia katika vijiji walivyotakiwa kuhamia na baadhi ya miundombinu imeanza kutengenezwa. Wananchi wachache waliosalia, wanaendelea

kufidiwa kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji (*DED*) wa Wilaya ya Mbarali. Iwapo kuna madai ya ziada, Wizara yangu ipo tayari kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri ya Mbarali ili kutafuta suluhu stahiki katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja nyingine inahusu mazingira ya waliohamishwa na kuvamiwa na wafugaji kwenye bonde hilo. Eneo la Hifadhi ya Taifa ni lazima taarifa za kitaalam kuhusu umuhimu wa eneo hilo ki-ikolojia, kiuchumi na kijamii ziandaliwe. Kwa suala la hifadhi mpya, mchakato wake unapaswa kuanzia kwa wananchi, pamoja na Halmashauri husika. Tunakuomba Mheshimiwa Mbunge, uwahamasishe Wananchi wa Halmashauri husika ili mchakato wa kubadili hadhi ya eneo hilo, uweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa James Lembeli, hoja yake inayosema kwamba, *concession fees* inayolipwa kwa Hifadhi za Taifa kwa ajili ya huduma ya hoteli ni ndogo mno. Wizara ya Maliasili na Utalii, inafahamu kuwa viwango vinavyototwa ni vidogo na vimepitwa na wakati. Kwa kutambua hilo na suala zima la dhana ya ushirikishwaji, Wizara kupitia Shirika la *TANAPA*, ipo kwenye mazungumzo na wadau kwa lengo la kupandisha viwango hivyo.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, hoja yake kuhusu kuchunguza suala la magogo nchini China; nilianza mwanzoni kwa kuijibu. Hoja nyingine ilikuwa inahusu Halmashauri za Wilaya ziwe mawakala wa kukusanya mapato na pia *TRA* wawe waratibu wa mapato haya. Mapato ya Maliasili yataongezeka kwa asilimia 90, ambapo makusanyo yatakuwa shingi bilioni moja ikiwa tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, Wizara imeshawasiliana na *TRA* na kubaini kuwa, kuna uwezekano wa *TRA* kufanya uratibu. Hata hivyo, *TRA* inaweza kusaidia ukusanyaji katika eneo hilo kama Serikali itaiagiza. *TRA* kwa kufanya hivyo na marekebisho kufanyika katika sheria na kuidhinishwa na Bunge, kwa hali hiyo tutatekeleza hayo ili kuleta kwa Waheshimiwa Wabunge, muweze kuidhinisha hilo liweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Janet Kahama, alisema vianzishwe viwanda vya kuchakata mbao nchini na Serikali iache kuingiza samani toka nchi za nje. Pendekezo hili linaendana na Sera ya Taifa ya Misitu, inayohimiza kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao hayo. Wawekezaji wanakaribishwa kuanzisha viwanda vya kuchakata mbao za hapa nchini na kutengeneza thamani ziletazo ushindani katika soko la ndani na nje. Tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutumbusha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, yeye aliomba Waziri atoe maelezo wakati akiwasilisha hotoba yake ya bajeti kuhusu kuzuia Wananchi wa Vijiji vya Jimbo la Mlalo, kupitisha barabara kwenye msitu. Wizara haijazuia Wananchi wa Vijiji vya Jimbo la Mlalo, kupitisha barabara kwenye msitu. Katika mchakato huo, Idara ilitoa maelezo kwamba, urefu wa barabara ni kilomita 45 na

upana ni mita 8; hivyo, kuathiri hekta 30 za msitu ambapo ulihifadhiwa kwa lengo la kutunza vyanzo vya maji, udongo na bioanuai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002 na Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004, eneo kama hilo la msitu wa Shagau ni lazima lifanyiwe tathmini ya athari za mazingira wakati wa kujenga barabara. Hivyo, tunaishauri Halmashauri ya Lushoto, ifanye tathmini ya athari za mazingira na ikiwa itakubalika, sisi hatuna pingamizi; barabara hiyo ipite pale panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary anasema kwamba, kuna mbao zinazosafirishwa kutoka Tanzania kwenda Kenya na kugongwa nyundo ili zionekane kuwa za Kenya. Kiutaratibu, mbao zinazotoka Tanzania, huwa zinagongwa nyundo zenye alama ya Idara ya Misitu na Nyuki Tanzania. Sanjari na alama hizo za nyundo, mbao hizo huambatana na Hati Maalum ya Usafirishaji mbao kwenda nchi yoyote. Kwa hali hiyo, zikishafika Kenya zinakuwa ni mali ya Kenya na pia kama Kenya watauza kwingine, sasa ile mali inakuwa imetoka Kenya ni mali yao wameuza kwingine, kwa sababu sisi mkataba wetu unaishia pale tukishawauzia Wakenya.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anasema kwamba, Serikali imeshindwa kufikisha lengo la kuwa na watalii milioni moja kwa mwaka. Lengo la milioni moja kwa mwaka, tulikuwa tumelipanga lifikie ifikapo mwaka 2010. Mategemeo ya kufikia lengo hilo, ilikuwa ni kuwa na sekta nyingine zinazohusiana na utalii, hususan kuliimarisha Shirika la Ndege la Taifa, Viwanja vya Ndege, Barabara na Miundombinu mingine. Hata hivyo, Wizara inaendelea na jitihada za kuhamasisha wawekezaji kupitia ziara na mikutano maalum ili tuhakikishe kwamba, mwaka 2010 tumefikisha lengo la milioni moja na 2012 tuna dhamira ya kufikisha lengo la milioni 1.2.

Mheshimiwa Prof. Mtulia alisema kwamba, Serikali inapoteza mapato kwa kuwa watalii wengi wanalipa huduma nje kwa *tour operators*; hivyo, Serikali inapoteza shilingi bilioni 67. Utafiti umeonyesha kuwa, watalii wengi hutumia zaidi ya asilimia 60 ya fedha za safari kwa usafiri tu. Hii ina maana kuwa, Shirika letu la Ndege, likiimarishwa na kufanya safari kwenye masoko ya utalii, fedha zinazobaki nje kupitia tiketi za usafiri, zitakuja nchini kwetu. Kwa hali hiyo, tutashirikiana na ATC kuhamasisha wenzetu watusaidie haraka ili ndege yetu iweze kwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Fatma Mikidadi, swali lake la mjusti tumeshalijibu na swali kuhusu vivutio vya utalii ni kwamba, Wizara inatangaza na itaendelea kutangaza vivutio vya utalii. Mwaka 2006, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake, iliadhimisha Miaka 100 vya Vita vya Majimaji kwa lengo la kutangaza utalii na kuuelimisha umma. Kwa hali hiyo, sasa hivi pia kwa upande wa Pwani tuna Mradi maalum unaoitwa *MACEMP*, ambao ni uhamasishaji wa utalii katika Wilaya ya Kilwa na Mafia. Kwa hali hiyo, tutaendelea na juhudi hizo ili kuhakikisha kwamba, sehemu mbalimbali zikiwemo za Rufiji, Mafia na Kilwa, zote zinapatiwa ufumbuzi wa kuweza kutangaza vivutio vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mikidadi pia aliongelea kuhusu viboko wanaoongea na binadamu. Usimamizi wa viboko hawa upo kwa familia moja ambayo ndiyo yenye uwezo wa kuwaamrisha. Aidha, mkakati wa kuliendeleza eneo hilo kuwa kivutio cha utalii, utahitaji ridhaa ya familia hiyo husika. Kwa hiyo, hatua ya kwanza kulitumia eneo hili kibiashara au kiutalii ni lazima kushirikisha jamii hii, ikiwa ni pamoja na Serikali ya Kijiji husika na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Tutatuma Wataalam wetu watakwenda kuangalia hali hii na kuweza kuwashirikisha hawa ili tuone jinsi ya kuweza kutumia hawa viboko katika utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Col. Feteah Saad Mgeni, amesema Serikali iwe na mikakati ya kutangaza vivutio vya Mambo ya Kale vilivyopo Zanzibar, Bagamoyo, Kilwa na Kigoma. Wizara imechukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa, vivutio vya utalii nchini vinatangazwa ndani na nje ya nchi kupitia Bodi ya Utalii. Kati ya vivutio vilivyotangazwa hadi sasa ni pamoja na Mji Mkongwe wa Zanzibar na Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, aliongelea kuhusu ukwepaji wa ulipaji wa kodi kwa baadhi ya *camp operators Selous*. Mpango wa usimamizi wa uendeshaji wa Pori la Akiba la *Selous* umebaini maeneo 20 kwa ajili ya ujenzi wa Kambi za Utalii wa Picha. Kati ya maeneo hayo, maeneo saba yana makambi ambayo yanafanya kazi, 11 yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi na mawili hayafanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Mbuyu, ambayo ilikuwa inaendeshwa na Kampuni ya *Southern Tanganyika Game Safaris*, kwa makusudi hawakulipa ada ya uhifadhi, au kuwasilisha USD 12,000 kwa mwaka na ada ya kiingilio ya USD30 kwa siku. Kampuni hiyo haifanyi kazi tena, ilisimamishwa mwaka 2002. Hatua hii iliifanya Kampuni ya *Mbuyu Camp* kufungua kesi dhidi ya Wizara, kesi hiyo ilimalizika mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba radhi kwa yale ambayo sikuyagusia, nitatoa majibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja hii imeungwa mkono lakini nitapenda kwa wakati muafaka, Mheshimiwa Waziri uweze kuelezea kuhusu ujenzi wa kiwanda kule *Lake Natron*. Naitaka hii kwa sababu jana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, alitoa kuhusu utaratibu kwa wale waliochangia suala hilo na akawa ameeleza jinsi alivyoingia pale, hapakuwa mahali penyewe alipoingia na nikasema kwamba, Waziri wa Maliasili na Utalii atajibu. Kwa hiyo, ningependa tafadhali ujibu kabla hatujaendelea na vifungu vingine.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hiyo, kwa suala hilo ambalo nilikuwa sijamalizia kulijibu.



Ninapenda kujibu kwamba, kwa hivi sasa Mradi huu bado upo katika maandalizi na pia sehemu mbalimbali ambazo zilikuwa zimechaguliwa, zimeonekana kwamba kutokana na *Environmental Impact Assessment* hazikukubalika.

Kwa hiyo, bado maandalizi yanaendelea na uchunguzi zaidi unafanywa. Kwa hali hiyo, napenda kusema kwamba, Mheshimiwa Marmo alichooonga jana ni kweli kwamba, imefikia kwenye kilomita 30 na uchunguzi bado unafanywa na baada ya hapo pasipofaa tutazidi kuendelea kutafuta mahali ambapo ni muafaka, ambapo hapataweza kuleta athari za aina yoyote.

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1001 - *Administaration and General* .... Shs. 2,474,376,800

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza; Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Kilasi, Mheshimiwa Aziza Ally, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Zambi, Mheshimiwa Dr. Mahenge, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Kimaro, Mheshimiwa Blandes, Mheshimiwa Kawawa, Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Mfaki, Mheshimiwa Batenga na Mheshimiwa Kabuzi. Kwa hiyo, hawa ndio wa upande wa kulia.

Upande wa kushoto ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Mpanda, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Paul J. Lwanji, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. Tumewaandika wote. Wabunge 35 mara 5 ni dakika ngapi na tuna saa saa moja kamili?

Kwa hiyo, tukubaliane utaratibu; kila mtu atauliza swali lake vizuri asirudie vinginevyo, tunakwenda tu. Ile Kanuni yetu inasema ukimaliza unaanza kuuliza tena, lakini kwa maana hii ili ninyi nyote muweze kusema msirudie. Kila mmoja aulize swali lake moja vizuri na haturudii. Tunaanza na Mheshimiwa Peter Serukamba. Naomba msirudie kile kifungu, mshahara wa Waziri na wala si mtu mwingine.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu ambao kwa bahati mbaya Waziri hakuweza kujibu hata mmoja, niliongelea suala la kutumia fedha ya Tanzania katika ku-*bill* kwenye *tourism* ya nchi yetu. Nilitaka kujua sasa Waziri anasemaje, haoni sasa umefika wakati tuache kutumia fedha za wenzetu tutumie fedha za nchi ili tuweze na sisi kufaidika kama nchi? La kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, lilikuwa ni suala la tozo ya kuangalia *Chimpanzee* kule Gombe na Mahale. Ruanda kuangalia wale *Gorilla* ni dola 500 kwa saa moja. Sisi pale Gombe na Mahale ambapo wale *Chimpanzee* wetu ukienda na mafua tu umewaachia. Kwa hiyo, ni hatari kwa maana hata ile *specie* yenyewe kupotea tusipokuwa waangalifu. Kuwaangalia pale ni dola 50 mpaka utakapochoka wewe. Nataka Waziri atuambie; huu mchakato wa kupandisha bei unahitaji kitu gani cha maana na kwa nini hawajapandisha bei mpaka leo?

**NAIBU SPIKA:** Haya tukubaliane ajibu la pili au la kwanza; maana atajibu moja tu? Tumekubaliana hapa ni moja.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zinasema ni maswali mawili, nadhani ni vizuri tuheshimu taratibu.

**NAIBU SPIKA:** Tunapenda sana kuheshimu taratibu na kwa mujibu wa Kanuni mimi nina madaraka ya kuliongoza Bunge hili vizuri, watajibu maswali yako mawili wenzako wote wataachwa na tutaishia kwenye *guillotine*. Mimi sipenda kabisa *guillotine*. Kwa hiyo, amua moja; *Chimpanzee* au lingine hilo? Jibu la pili, kwa sababu la *Chimpanzee* ni *unique*.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupokea ushauri wa Mheshimiwa Serukamba na kwamba tutaufanyia kazi. Tutatuma wataalam wetu wakaangalie bei za wenzetu zikoje ili tuhakikishe kwamba, uamuzi tutakaotoa utakuwa ni wa halali na wa haki. Tutawashirikisha wadau mbalimbali tuone hali ilivyo. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Majibu niliyopata kwa Mheshimiwa Waziri, mimi nilichokisema hapa cha msingi ni kwamba, fidia wananchi wamepewa na waliopunjwa wanaendelea kulalamika kama alivyosema ni sahihi. Hapa kilio changu kikubwa kilikuwa ni kwa upande wa miundombinu na ahadi ya Serikali ambayo ilitolewa; kwamba, wananchi hawa wakishapewa *compensation* yale maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kuhamia, miundombinu itajengwa ili wananchi waende pale. Cha kushangaza, mpaka sasa ninapozungumza, shilingi milioni 196 hizi ni za ujirani mwema tu; ni hela kidogo sana ukilinganisha na shilingi bilioni mbili ambapo tuna madarasa 78 ambayo yamevunjwa na wananchi ni nguvu zao hizo. Nyumba za walimu 25, nyumba 15 kwa vijiji vyote hivyo 9, vyoo matundu 138 ambayo kwa gharama hii vilitakiwa vijengwe na Serikali ili wananchi waende pale.

Miundombinu kwa mfano maji, mtu atahamiaje pale hakuna maji, barabara hazijapasuliwa, hiki kinachozungumzwa kwamba, kimeanza kujengwa ni madarasa matano ambayo *TANAPA* walijitolea kujenga kwenye moja tu hilo. Sidhani mpaka sasa tulivyokaa nao, kama wana mpango wa kwenda; hawana fedha hizi bilioni 2.9 ambazo wametuahidi. Kwa hiyo, 196 ni vyumba 28 tu vya madarasa, ukilinganisha na vyumba 78. Ninachoomba, Waziri aniambie mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, haya yote ambayo Serikali iliyaahidi ni lini wataanza kufanya hii kazi, kwa sababu 196 milioni ni kitu kidogo ni madarasa 28 tu, ndiyo nilitaka ufafanuzi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kusema kwamba, *TANAPA* inajitahidi kuchangia; kwa uwezo tulionao kama nilivyosema awali kwamba, *TANAPA* ina mzigo mkubwa wa kulea hifadhi zote 15, kwa upande huo *TANAPA* inatoa milioni 196 na pia ni kazi shirikishi. Tutashirikiana na Wizara nyingine husika na shughuli za maendeleo ili tuweze kwa pamoja, kujua tutashirikiana namna gani kuweza kufanya kazi hii. Hata sisi tuna uchungu na wananchi hao na tunajua wapo katika hali mbaya. Sisi pia kwa upande wa *TANAPA*, tutazidi kuangalia kiasi gani zaidi tunaweza tukajikung'uta katika kuongezea hiyo. (*Makofi*)

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wakati Mheshimiwa Waziri akijibu, nimemsikia akisema ya kwamba, kuna kifungu cha sheria ambacho Waziri ana mamlaka nacho ambacho kinazidi mamlaka ya Bunge. Kilichonisukuma kuyasema hayo ni kifungu ambacho katika Bunge mwaka jana wakati wa bajeti, tulipitisha bei za wanyamapori na Waziri kwa mamlaka ya kifungu hicho hicho alichokitaja, akasema ya kwamba, kifungu kinamruhusu Waziri kubadili bei hizo. Je, kuna kifungu ambacho kinazidi mamlaka ya Bunge na kama ameona Waziri kulikuwa na tatizo; je, wale waliobadilisha wamechukuliwa hatua gani na anaonaje bajeti hii leo waende wakaipeleke kwenye kile kile kifungu Wizarani wakaipitishie? (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kazi ipo. Mnatusumbua bure tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, kifungu nilichokinukuu ni kifungu ambacho kinampa madaraka Waziri aweze kufanya kazi hiyo. Naomba kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, Waziri alifanya kazi hiyo katika kuhakikisha kwamba, angalau tuweze kuokoa hata baadhi ya fedha.

Tungeacha hali ilivyo, tunganubiri labda mpaka turudi tena huku, ingeweza kuchukua muda mrefu na mwaka ukaisha tukajikuta tunashindwa kuja kuwaambieni tumepata chochote. Hata hivyo ni kwamba, baada ya kuchukua hiyo, naomba kusema kwamba, ilikuwa ni nia yetu lazima turudi huku kueleza kwa nini tumefanya hivyo.

Pia baada ya hapo, mimi naomba tu niseme tena kwamba ni jambo ambalo tulilifanya kwa nia nzuri ya kujaribu kutenda kazi vizuri ili Waheshimiwa Wabunge wetu waone kwamba, tunaokoa fedha. Hatukuwa na nia mbaya yoyote na mimi naomba tena niseme kwamba, kosa kama hilo ambapo tunaona kwamba ni jambo ambalo lazima turudi Bungeni, aidha tutafanya hivyo au tutapitisha taarifa kwa Mheshimiwa Spika, ili aweze kuifahamu na yeye atatusaidia kama kitu cha dharura sana. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia kwa maandishi, nilitaka kupata ufafanuzi wa juu ya migogoro iliyopo kwa wananchi na shughuli za uhifadhi kule Jimboni Kisesa katika Vijiji vya Semu, Mbugayabanya, Malwilo, Butuli, Matale na Mwasengela. Serikali imekuwa ikinihidi na

imeniahidi muda mrefu sasa kwamba, itatenga eneo kwa ajili ya kitoweo kwa wananchi ambao wanaishi mpakani mwa hifadhi na kwamba eneo hilo pia litatumika kama *buffer zone* kwa ajili ya kutenganisha shughuli za binadamu na shughuli za uhifadhi na Serikali ilishakubali. Basi labda iniambie sasa ni lini hawa wananchi wataanza kufaidi kitoweo? Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengi ambayo yanahusu vijiji ambayo tumewapa mamlaka Halmashauri zetu za Wilaya, huwa yapo chini yao. Mara nyingi hata mgao/*quarter* za vitoweo kwa ajili ya wananchi ni Halmashauri ambazo huwa zinahusika moja kwa moja. Sasa mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge kama kuna tatizo lolote kwamba Halmashauri inafanya kinyume na yale maagizo yalivyo na mimi namuahidi kwamba, nitatuma maafisa wangu waende ili kuelimishana na Halmashauri hiyo, tuone kama haki inatendeka na wananchi wanapata kitoweo kufuatana na taratibu walizojiwekea Halmashauri jinsi ya kutoa *quarter*.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi. La pili, nampongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri waliyoifanya isipokuwa wakati anajibu juu ya magogo alisema kwamba, Serikali haikupata fedha kwenda kufuatilia Uchina. Tumesikitishwa kidogo na jibu hilo, labda kwa sababu ya ugeni wa Waziri na upya wake, ningependa tu aahidi kwamba hili suala atalifuatilia kwa sababu bado biashara ya magogo kwenda China, pamoja na takwimu alizonazo yeye, haziridhishi na nafikiri kunahitaji kulifuatilia kwa undani zaidi na kufuatilia mpaka China kuangalia kwa kiasi gani magogo yanaendelea kwenda. Kwa taarifa tulizonazo, sisi bado biashara hiyo inafanyika kinyume cha utaratibu na Wachina wanapata fedha nyingi sana kutokana na magogo yetu yanayokwenda huko kinyume cha utaratibu. Sasa la kwamba, hakuna fedha za kwenda kufuatilia; mimi nafikiri si majibu mazuri kwa Watanzania. Ningeomba hilo lisahihishwe. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa jinsi alivyotaribu kuifafanua hiyo hoja yake. Ni kwamba, nimepokea ushauri wake na labda ningengelea kidogo kwamba, tulipojaribu kufanya ule ufafanuzi wa mwanzo na tulipoona kwamba kweli sheria zinakiukwa, ndipo tukaamua kupiga marufuku moja kwa moja magogo yasiende nchi za nje, ili kusiwe na kisingizio cha aina yoyote kwamba mtu kapeleka magogo au vipi.

Kwa sasa hivi ni msimamo wetu na ni msimamo wa Serikali na hatutabadilika kwamba, hakuna hata kipande cha gogo kwenda nchi za nje.

Hata hivyo, napenda kuupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutajaribu kuangalia uwezekano wa fedha ili tuweze kuhakiki na hilo. Zaidi tumepiga marufuku pia tujihakikishie kama bado kuna njia za panya zinazoweza kuvusha magogo yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa na mimi nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na

kuwa hii ni mara ya kwanza lakini wamejibu maswali vizuri sana. Kwa hiyo, hongera sana Waziri. (*Makofi*)

Jambo ambalo nilikuwa nataka kuliuliza la msingi ni kuhusu *GN*, lakini tumeshauriana jambo hili tuliulize wakati wa *Finance Bill*, kwa sababu matumizi ya *GN* yanazidi katika kugeza *Finance and Appropriation Bills* ambazo tunazipitisha kwenye Bunge.

Sasa nataka kuulizia fidia kwa wananchi wetu ambao mazao yao yanaliwa na wanyama. Kule kwangu Longalombogo, Mwasinasi, Ng'waswale, Mwamtani, kila siku ni kazi ngumu sana. Halafu hatujui hata utaratibu wa kupata fedha kidogo mnayotupa.

Ukienda kwenye Halmashauri wanakutupia mpira nenda Wanyamapori, ukienda wanyamapori, wanakwambia anzia Halmashauri! Kwa hiyo, tungependa Mheshimiwa Waziri atoe tamko, kwanza, hicho kidogo tutakipataje na kwa haraka, lakini pia je, kuna uwezekano wa kuongeza hizi *rates* maana yake ni kama mchezo tu wa kuigiza kwa fidia ambayo inatolewa kwa sasa hivi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali hilo ni kwamba, kwa sasa hivi tumeandaa Muswada mpya wa Wanyamapori, ambao tutaleta Bungeni humu mwezi Agosti, 2008 kabla hatujamaliza Bunge hili. Katika Muswada huu mpya, tumeweka vizuri kabisa kuhusu mambo ya hizi fidia za vifuta machozi na mambo mbalimbali. Katika *regulations* tutaeleza waziwazi kabisa kila kitu kinaendaje na nani atahusika na nani atakayewajibika katika shughuli hizo mbalimbali. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza na mimi nikiri na niipongeze Serikali kwa uamuzi wa kutopeleka tena magogo nje, ambapo ilikuwa inapelekwa *raw materials* na kurejeshewa vitu vya samani ambavyo tulikuwa tunavinunua kwa bei kubwa.

Nilitaka Waziri atufafanulie kwa maana hiyo, sasa nini hatima ya viwanda ambavyo vilikuwa chini ya *TWICO*, baada ya kubinafsishwa na utakwendaje sambamba na uamuzi huo wa kutopeleka magogo na kufaidika vipi na samani ambazo zinaweza kutengenezwa sasa hivi Tanzania wakati viwanda hivyo vimebinafsishwa? Hebu Mheshimiwa Waziri, tunaomba utufafanulie au utueleze. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa pongezi na msimamo ni huo kwamba, hatutapeleka tena magogo nchi za nje. Pia sasa hivi tuna jukumu kubwa la kuwahamasisha wananchi waweze wenyewe kutengeneza bidhaa zinazotokana na mbao hapa hapa nchini. Kwa kuanzia pia ni kwamba, kuna baadhi ya viwanda tumeshafanya nao mikutano na kuna baadhi tumeshawatembelea na pia tumejaribu kuangalia ubora ulivyo.

Ubora wa bidhaa zetu bado upo chini na sababu ni kwamba, tunahitaji kuboresha ujuzi huo. Kwa hali hiyo basi, napenda pia kusema kwamba, hata baadhi ya mashine tulizonazo bado hazina ubora wa kutosha na nyingi ni chakavu.

*(Hapa king'ora kinachoashiria moto kililia)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Niendeleee?

Tunaomba pia wale wote ambao wataingia katika biashara hiyo, waweze kukopa kwenye mabengi, waweze kununua mashine nzuri zaidi za kufanyia kazi. Sisi pia tuna mpango wa kuongea na mabengi waweze kuwakopesha wafanyakazi na wao wawekeze katika shughuli za mbao, waweze kushindana na nchi za nje katika kutengeneza samani ambazo zina ubora na zinazokubalika kimataifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante najua *alarm* imeleta *disturbance* lakini ni vitu vya namna hiyo kuwa-*alert* wakati wowote milango ipo mingi. *(Kicheko)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi katika mchango wangu wa maandishi, nilichangia kuwa kulikuwa na suala kuhusu kero za wavunaji mbao wadogo wadogo, ambao mchakato wao huanzia vijijini kwa Sheria Namba 14, baadaye huenda katika Wilaya huku Vijijini Kamati huamua na hutakiwa wavunaji kutoa *social support* na baadae huenda katika Halmashauri ya Wilaya ambako Mwenyekiti huwa ni Mkuu wa Wilaya.

Vilevile hupata usajili, usajili huu ni shilingi 205,000 lakini katika mchakato huu, inapofika wakati wa kutoa leseni, wavunaji hawa wadogo wadogo kuna tatizo kwamba hutoka amri Wizarani kwamba, wamesimamisha wakati wameshagharamia usajili ambao ni Sh. 205,000 na pengine leseni wameshatoa ambayo hapa ninayo makaratasi ni shilingi milioni tano. Vilevile wameshatoa *social support*.

Msimu wa uvunaji unakuwa umeishia kwamba, wanapokataza kipindi hiki hakuna kuvuna, ina maana hawawezi kuvuna tena mpaka kipindi kijacho. Mimi nilitaka ufafanuzi kwamba, je, hizi shilingi milioni tano ambazo kwa mfano huyu ambaye ameniletea shilingi milioni tano na shilingi 205,000, atarudishiwa au wakati wa msimu mwingine utakapokuja ataruhusiwa kuvuna kwa gharama hizi hizi licha ya kuzitaja zile za *social support*? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuongea kwa upande wa Wizarati tunavyohusika na shughuli ya uvunaji wa magogo. Uvunaji wa magogo ...

**MWENYEKITI:** Ilikuwa magogo au mbao? Nafikiri ni mbao.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Nilielewa kama ni magogo.

**MWENYEKITI:** Eleza tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kawaida miti inavunwa ndiyo hayo magogo yanachakatwa na ndiyo yanageuka mbao. Sasa sisi tunahusika kutoa vibali vya mtu kwenda kuvuna miti. Akienda kuvuna miti, ndiyo huko sasa kuna kuchakata zigeuke kuwa mbao. Huko tena kunakuwa siyo kwetu. Sisi tutajihusisha naye, ikiwa sasa atayasafirisha kwenda nchi za nje, pale ndiyo itabidi tumppe leseni ya kuweza yeye kufanya *export*. (*Makofi*)

Narudia kusema kwamba, hata uvunaji unakwenda kwa msimu, kwa sababu kuna msimu lazima tuachie miti ikue. Miti mingine ikishapunguzwa, inapewa muda wa kukua na kuna miti mingine inapandwa, kwa hiyo, haiwezi kuvunwa mwaka mzima.

Sasa hapa ninachoona, tunachoweza sisi kufanya ni kwamba, tutawasiliana na Halmashauri husika, tuwape ratiba zetu wajue msimu fulani tunatoa vibali vya watu kuvuna miti ili na wao waendane na hiyo. La sivyoyote, tunaweza kuwa na mawasiliano ya karibu watuletee kwamba, kuna hao watu ambao tayari wana leseni, lakini kwa sababu msimu umekwisha tunaomba msimu ujao wawe wa kwanza katika kufikiriwa; hayo yote yanawezekana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, kwa suala hili mwone Mheshimiwa Waziri pengine ataelewa vizuri zaidi kuliko alivyojibu, maana alikuwa anajibu hivyo kwa sababu ameelewa hivyo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye *vote* hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nawasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani tuliyooyatoa, nilipenda kujua taratibu zilizotumiwa na Serikali, kummilikisha Mwekezaji Raia wa Marekani, kilomita za mraba 149, eneo la *Gulumet Game Reserve*, ambaye amekuwa ni tatizo kubwa kwa wananchi wanaoishi katika eneo linalozunguka Hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kuhusiana na hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwekezaji wa Gulmet ni kwamba amewekeza katika sehemu mbalimbali. Kuna sehemu ambayo amejenga hoteli ipo kwenye Kijiji cha Sasakwa na kuna sehemu ambayo ipo kwenye vitalu vya uwindaji ambapo ndiyo kuna Ikorongo na Gulumet. Sasa basi huyo mwekezaji, upande alikojenga hoteli kile kiwanja hakupewa na Wizara yetu isipokuwa amekinunua kutoka kwa mwekezaji mwingine, ambaye anaitwa *VIP* na huyo *VIP* aliuziwa kiwanja kile na wanakijiji.

Sasa ni mlolongo huo kwamba, wanakijiji walimuuzia *VIP* na *VIP* kamuuzia huyo Gulumet ndiyo akajenga hiyo hoteli hapo. Kwa upande wa vile vitalu ambako ndiko

kuna Gulumet na Ikorongo, vitalu vile amegawiwa kama watu wengine walivyogawiwa na umri wake mwisho miaka mitano. Kwa hali hiyo, mwakani vitalu vile vitagawiwa upya kama tulivyokwishaeleza hapo awali.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Suala langu la kutaka kupata ufafanuzi lilikuwa lile la magogo, nashukuru amekwisha kulijibu, lakini nina swali dogo nataka nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *Sub-vote* zote za Wizara, katika Wizara hii kuna hiyo *Sub-vote* ndogo 080300 ambayo haipatikani katika Wizara nyingine zote. Nilikuwa naomba kujua hii *Sub-vote* katika Wizara hii ni ya nini? Hii ya Kwanza inaitwa *Non-Financial Public Enterprises Rent*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umeiona? Ndiyo Tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *Sub-vote* ni ya *Non Financial Enterprises Rent*, ambayo kwa sasa jumla imehama imekwenda katika *Sub-vote* 260702, ambapo sasa huko inaitwa *Rental Expenses*. Kwa mwaka huu ni shilingi milioni 30, ambapo kwa mwaka uliopita zilikuwa shilingi milioni 36. Kwa hiyo, imehama, ipo mbele zaidi katika *Sub-vote* hiyo niliyoitaja 260702.

**MWENYEKITI:** Tuendeleo, naona hii ni ya hesabu hebu rudia hapo. Umeielewa ama swali lako hakulielewa vizuri?

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani amelielewa Mheshimiwa Waziri, ila tatizo anasema imehamishiwa kwenye *Vote* nyingine, lakini pia inaonekana hapa. Sasa nashindwa kuelewa kama *sub-vote* mbili zinafanya kazi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo zaidi maana sijaelewa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *Sub-vote* hii, ambayo inaeleweka kwa sasa hivi kama nilivyosema kwamba, inaitwa *Rental Expenses*, imehamishiwa katika *Sub-vote* 260702 na inaitwa *Office*.

Kifungu hiki ni kwa ajili ya kulipia gharama ya pango kwa ajili ya Ofisi za Makao Makuu ya Wizara. Idara imekuwa ikitenga fedha hizi kwenye kifungu cha *Rent from Government Quarters and Offices*, sasa imebadilishwa ndiyo imewekwa huko kimakosa. Hata hivyo, baada ya kufuatilia zaidi fedha hizi, sasa zimerejeshwa katika kifungu hicho nilichokitaja.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hakuna mabadiliko katika kitabu hiki?



**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni makosa ya uchapishaji ambapo kufuatana na bajeti jinsi ilivyokwenda ndivyo nilivyoelekeza.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutakapofika kwenye hiyo *Sub-vote* niliyoitaja hapo, ndiyo wataikuta hiyo sasa.

**MWENYEKITI:** *Okay.* Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilieleza kwamba, Wilaya ya Mpanda eneo ambalo ni misitu ni zaidi ya asilimia 63 ya eneo zima la Wilaya ya Mpanda. Jukumu kubwa la Serikali ni kuangalia ustawi na maendeleo ya watu, pamoja na rasilimali kwa sababu ya kuongezeka kwa idadi ya watu.

Watu wameingia katika Hifadhi za Misitu ya Misaginya na Hifadhi ya Misitu ya Mwasisi na Ugala. Nilikuwa nimeomba nipate ufafanuzi ni utaratibu gani utumike, kwa sababu watu hawa wamekwisha kuweka mashamba yao na makazi na vijiji vyao vimesajiliwa; leo wanasumbuliwa wanaondolewa katika maeneo hayo wakati tunayo misitu mingi. Je, inawezekana Wizara ikaachia maeneo hayo kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya wananchi?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa sasa hivi kuna baadhi ya wananchi wameingia kwenye maeneo ambayo ni mapato na sababu mojawapo ikiwa ni kwamba katika kujitafutia riziki. Lakini pia watu wameongezeka zaidi, wanazidi kusogea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mimi napenda kusema kwamba kama mara nyingi mipaka ile ya zamani iliwekwa, lakini kwa sasa hivi tukiongeza mipaka ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sehemu muhimu ikiwemo vyanzo vya maji pamoja na njia za wanyama ndiyo hiyo ambayo tunajaribu kuzilinda. Lakini kama ni sehemu yenyewe haihusiani na chanzo muhimu, mimi napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba aongee na Halmashauri husika ili waweze kuomba kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili waweze kutengeneza *GN* ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi ile ili wananchi waweze kuruhusiwa pale ni mahala pao. (*Makofi*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kuulizia, nipate ufafanuzi kuhusu kiwanda. Lakini nataka kujua kwamba hiki kiwanda...

**MWENYEKITI:** Kiwanda gani?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Kiwanda cha *Soda Ash Lake Natron*. Kwa hiyo, nilitaka kujua kwamba iko katika Wizara ipi tupate ufafanuzi vizuri. Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko au katika Wizara ya Maliasili na Utalii? Kwa sababu huko kwetu imekuwa kero. Kwa hiyo, nilitaka nijue ni Wizara ipi itatupa ufafanuzi mzuri. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Michael Laizer, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi huu wa kiwanda cha magadi, soda, *soda ash* ambacho kinasimamiwa na Shirika letu la Maendeleo ya Taifa (*NDC*) chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na hapa tunavyozungumza suala la kibali au idhini ya kiwanda kujengwa pale bado hakijatolewa. Lakini kilichotolewa ni sisi kuwapa idhini wafanye *environmental impact assessment*. Ya kwanza ilifanyika na kukawa na mapungufu ambayo tuliwaeleza na kutokana na mapungufu hayo kiwanda kikaamua kuhamisha ujenzi wake takriban kilometa 32 kutoka eneo la Ziwa. Kwa hivyo sasa hivi wameniandikia kuniomba idhini tena ya kuweza kufanya *environmental impact assessment*. Tumekubali kuwapa idhini ya kufanya *environmental impact assessment*. Hapo hapo Wizara ya Maliasili na Utalii inafanya *integrated management plan* eneo lile kama eneo la *rams site weak land*. Sasa baada ya pale pamoja na hiyo *environmental impact assessment*, tutaona ni namna gani ya kuweza kutoa kibali cha kiwanda kujengwa ama kutokutoa kibali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ndiyo majibu umepewa.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa Wizara tu.

**MWENYEKITI:** Ni Serikali tu. Ndiyo maana nimemwita hata huyu. Leo unaweza kuwa hapa kesho ukawa mahali pengine.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunapata taabu kwa sababu ya maelekezo kwamba tuulize moja tu. Sasa basi niseme tu kwamba kweli nilikuwa nimeeleza matatizo ya viboko kwenye Ziwa Babati ambalo kwa kweli wamesababisha sana vifo vya watu. Lakini kwa sababu ni moja. Hilo tutawasiliana kiofisi na Mheshimiwa Waziri. Nilitoa ombi kwamba kuna migogoro mingi kati ya vijiji pamoja na Hifadhi za Taifa na hasa Hifadhi ya Tarangire. (*Makofi*)

Niliomba kwamba Wizara itume timu ili tuje tuongee, tuone kwamba tunaweza tukatatua namna gani. Sasa nilitaka ufafanuzi kutoka kwa Waziri kama alikubali hilo ombi au yeye mwenyewe anaweza kuja kwanza akajielimisha kuhusu matatizo hayo au atume timu. Nilitaka tu ufafanuzi huo. Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya mambo mawili, la kwanza nitatuma timu ije ijionee kwamba hali ikoje, walete ripoti na baada ya hapo nitakuja mimi ili na Mheshimiwa Mbunge tukae na wananchi, tuongee nao. (*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati nachangia Bajeti nilizungumzia matatizo yanayowakumba

wananchi wa Tunduru hasa kwa kushambuliwa na askari wa wamiliki wa vitalu. Matatizo haya nimeyapata wakati natembelea vijiji kadhaa hasa Vijiji vya Kazamoyo, Kijiji cha Twendembele na vijiji vya Tarafa ya Nakapanya. Wananchi wamekuwa wakishambuliwa na wamiliki wa vitalu hivyo bila hata kufuata zile taratibu za nchi yetu. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya mashambulizi haya wanayofanyiwa wananchi? Nashukuru sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kusema kwamba kama askari anafanya kinyume na wajibu wake kwa kunyanyasa wananchi, hilo ni kosa na sisi tutalichukulia hatua. Lakini pia napenda kusema kwamba naomba wananchi wa vijiji hivyo vikiwemo Kazamoyo, Twendembele na Nakapanya nawapa pole na kwamba sisi tutahakikisha kwamba mambo kama hayo hayatokei tena na nitatuma wataalam wetu waje waone hali waweze kurekebisha jambo hilo mara moja. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Swali ambalo ilikuwa nipate ufafanuzi nashukuru Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba Muswada utakuja kwa ajili ya fidia ya watu wanaodhuliwa na wanyama wakali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimezungumzia suala la uwindaji haramu na nikasema kwamba inaonekana kwamba mbuga zetu za wanyama ziko *prone* sana kwa majangili na kumekuwa kunakamatwa nyara za Taifa nyingi sana. Kwa mfano, hivi karibuni kule Iringa nadhani ulikuwa mwezi wa nne, tumeambiwa kupitia vyombo vya habari kwamba yamekamatwa meno ya tembo tani nyingi hatuelewi kiasi gani na kwa maana hiyo fedha nyingi zimepotea. Sasa nilikuwa najiuliza tatizo ni nini? Tuna ulinzi hafifu au maofisa wetu wanajihusisha. Kwa hiyo, nikataka maelezo zaidi kwa Waziri, bahati mabaya hakujibu.

Sasa nataka awaeleze Watanzania, meno ya tembo yaliyokamatwa kule Iringa ni ya kiasi gani na pengine ni tani ngapi ili Watanzania wajue kwamba ni kwa kiasi mbuga zao zinahujumiwa lakini pia Waziri atueleze hatua ambazo Wizara inazichukua katika kukabiliana na hali hiyo ili kulinda wanyama wetu. Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Godfrey Zambi, kwamba ni kweli kuna ujangili wa kila aina unaoendelea, kwanza ukiwemo wa kuwinda wanyama. Lakini pia kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu, pia wanaiba nyara kwa njia mbalimbali, kwa njia ambazo wenyewe wanazitumia. Hata hivyo, Wizara yangu imejitahidi kwa kushirikiana na raia wema pamoja na polisi, tumejitahidi mara nyingi kukamata na nyara zote zinazokamatwa huwa tunaziweka kwenye Bohari yetu ziko huko. (*Makofi*)

Lakini napenda nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi sitakuwa na takwimu kamili ya kuweza kumwambia. Ila namwomba aidha, tutamjibu kwa maandishi au namwomba swali hili ili wananchi waweze kusikia sehemu mbalimbali aliulize kwa njia ya swali ili tulijibu katika vipindi vya Maswali na Majibu katika Bunge lako hili Tukufu. (*Makofi*)

**MHE. DR. BINLITH S. MAHENGE:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Wakati nachangia kwa maandishi niliomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ili kupisha uendelezwaji wa *Mpanga-Kipengere Game Reserve* wananchi wangu wapatao 328 walilazimika kuondoa katika vijiji vya Ikovo na baadhi ya vitongoji vya vijiji vya Usamwami na Kimwani na tathmini au mthamini wa Serikali alipofanya, ilionekana wananchi hao wanatakiwa kulipwa fidia ya shilingi milioni 221 na hii ilifanywa mwezi Januari, 2008 na tulipofuatilia malipo Wizara ikasema kwamba kwa Bajeti ya mwaka 2007/2008 haikupanga. Kwa hiyo, ikaahidi kwamba italipa mwaka 2008/2009. Nilitaka ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri awajulishe wananchi hawa kwamba je, watalipwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 na ni lini? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba shilingi hizo milioni 221 zitalipwa katika kipindi hiki. Lakini tarehe kamili ya kusema kwa hapa sitaweza kuiahidi. Lakini tutailipa haraka iwezekanavyo baada ya kupatiwa pesa katika Bajeti hii. (*Makofi*)

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi wakati nachangia, nimechangia kwa maandishi nilielezea kuhusiana na suala la mazao ya nyuki. Mazao ya nyuki hivi sasa ni moja ya mazao muhimu sana na mazao ambayo yanatoa kipato cha juu sana na hata katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameeleza na amezitaja baadhi ya Wilaya ambazo alichukua sampuli mbalimbali kuhusiana na mazao haya nyuki. Lakini akaelezea ubora huu ulikwenda na ukawa umeingia kwenye soko la Jumuiya ya Ulaya na hata Wilaya ya Manyoni ilipata medali ya dhahabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka ufafanuzi tu Wilayani Iramba haya mazao ya nyuki na kwa kweli nyuki ni wengi sana na mfano mzuri Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Iramba mwezi Mei, kidogo wamzuie hata kuzindua shule ya sekondari ya Kinyangiri kwa sababu ya hao nyuki. Nataka ufafanuzi anieleze, je, Iramba mnaifikiriaje kwamba mtawaletea wataalam ili sasa ishiriki na yenyewe kuweza kuzalisha hili zao la nyuki? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Alichokuwa anataka ni soko la asali hiyo. Sasa amezunguka weee, haya Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kupitia idara yangu ya Misitua na Nyuki tutawapa ushirikiano Wilaya ya Iramba ili na yenyewe waweze kunufaika kwani sisi wenyewe ni mashahidi kwamba Mkoa wa Singida mzima ni Mkoa ambao unatoa

asali nzuri sana ya nyuki ikiwemo na asali ile nyeupe sana ambayo ni nzuri sana.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mlima Kilimanjaro ni kivutio kikubwa sana cha utalii duniani na kwa siku za hivi karibuni mlima umetangazwa sana na njia za kupandia mlima Kilimanjaro kwa watalii sasa zinaelekea zimejaa sana. Katika mchang wangu wa maandishi niliomba Wizara iruhusu njia ya Maua ambayo inatumika sasa kwa utawala nayo itumike kwa kupandia watalii ambapo itaongeza ajira sana. Naomba ufafanuzi kwa hilo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sasa hivi njia zilizopo ni chache na pia kunahitajika kuongezwa njia ikiwepo ya Maua na pia kuna baadhi ya Wabunge walikuja kuomba ushauri na wenyewe wanataka njia ya Masama. Kwa hiyo, kwa upande wa sisi Wizara ni vitu ambavyo kwa kweli tunavihitaji sana kwa sababu jinsi tutakavyopanua njia zetu na ndivyo tutakavyoweza kuongeza watalii wengi na pia kipato vile vile kitaweza kuongezeka. Kwa hiyo, kwa jambo hilo mimi nitawakabidhi wataalam wetu wahusika ili waweze kwenda kufanya utafiti na kuona uwezekano wa njia hiyo na pia kuangalia na *environmental impact assessment* inasemaje kwa jambo hilo ili njia hiyo iweze kutumika.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia katika mchango wangu wa maandishi nilitoa mchango mzito sana kwa masikitiko kuhusiana na wanyama wakali tembo, ndovu.

**MWENYEKITI:** Na tembo pia ni jina tunalolifahamu kwa kweli. Wala isikusumbue kabisa.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa masikitiko yangu kuhusiana na hawa wanyama kwamba katika Kata ya Nyakakika katika jimbo la Karagwe, Kata ya Kihanga, Kata ya Nyakasimbi, Kata ya Ihembe, Kata ya Nyabiyonza, na sehemu zingine imekuwa ni jambo la kawaida kupishana na tembo wapatao 300 au zaidi wakiingia kwenye mashamba ya watu na vile vile wamesababisha vifo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karagwe haina ofisi ya wanyamapori, haina mtumishi hata mmoja wa wanyamapori. Mara nyingi haina hata risasi, hata bunduki. Sana sana tembo wanaposhambulia mashamba ya watu huwa tunapata msaada kutoka *Ibanda Game Reserve* ambayo iko mpakani mwa Uganda na Tanzania – Mrongo ni zaidi ya kilometa 150, kwa hiyo, wakija kufika pale wanakuta madhara tayari yameshatokea. Sasa nilitaka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, yeye ni mama na nadhani ana huruma, kwa nini asitenge fedha za kujenga Ofisi ya Wanyamapori Wilayani Karagwe katika mji wa Kayanga ambao uko kwenye *centre* ya kuweza kusaidia uharibifu huo mara moja. Nashukuru.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba Mheshimiwa Blandes hata kabla ya hapa alishatuletea barua ya kuhusu tembo hao. Mimi katika safari za mkoa huo ni kweli njiani tulikuwa tunakutana na mavi ya tembo mengi kuonyesha kwamba kweli kule tembo wanatembea kila mahala na sasa mimi napenda kumwambia kwamba ushauri huo na ombi tumelipokea. Tatalifanyia kazi na kuona kwamba kipi kitachowezekana. Aidha, kuongeza askari, au kuweka kituo kidogo. Kile kitakachowezekana kufuatana na mfuko tulionao tutakifanya ili kuhakikisha kwamba tunanusuru maisha ya watu na kuhakikisha kwamba tembo wazuiliwe kwenda sehemu ambazo watu wapo. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia kuhusu suala la gawio la mapato ya uwindaji katika Halmashauri zetu. Sisi Halmashauri zetu ni maskini. Kwa hiyo, tunategemea sana mapato kutoka katika Utalii ambao ni wa uwindaji. Sasa ili tuweze kuwa na uhakika wa mapato hayo yatokanayo na uwindaji tulikuwa tunaomba baada ya msimu kwisha, tungepatiwa *list* ya wanyama waliogawiwa katika vitalu vile na wanyama waliowindwa katika vitalu vile kwa msimu ule ili na thamani yake pia ili tuweze kuingiza katika vitabu vyetu kama *income* ya Halmashauri kwa mwaka ule kuliko ilivyokuwa zamani tulikuwa tunapewa fedha hizi kama hisani vile.

Tunakuomba mama, Mheshimiwa Waziri ufanye kama ulivyokuwa Wizara ya Maji, ulikuwa unatupa mapema fedha za miradi ya maji inayokwenda katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, tunaomba na hili mfumo ule utuletee katika Wizara yako, uwe unatupa ni kiasi gani na thamani gani ya wanyama waliowindwa baada ya msimu tuweze kujua nini tunapata kisheria. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea ushauri huo na tutajitahidi kushirikiana na Halmashauri ili kuweza kuwapatia mawindo yanayofahamika ili waweze kujua kiasi chao ni kiasi gani. *(Makofi)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumsikiliza kwa makini Mheshimiwa Waziri akifafanua juu ya hoja yangu niliyoitoa jana na hoja ambayo ameitoa sasa hivi Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, japo nimeridhika kwa shingo upande. Napenda kutengua usemi nilioutoa jana kwamba sitaunga mkono hoja hii. Sasa naunga mkono hoja hii kwa asilimia 99. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Wakati nachangia hapa jana kwa kuzungumza na kwa maandishi nilitoa kilio changu kuhusu simba wanaomaliza watu huko Singida.

Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hapa, amejibu kwa ujumla sana, nilitegemea kwa jinsi tatizo lilivyokuwa na uzito wake Singida, Wilaya ya Singida tu Vijijini watu wameshaliwa 14, Manyoni watu 7, jumla 21. Haya ni maafa makubwa, nilitegemea tungepata jibu rasmi kwa ajili ya Singida kupata askari wanyamapori. Kwa sababu sasa hivi wanaolinda ni wananchi na wanachangishwa pesa kwa ajili ya kuwapelekea watu wanaolala porini. Serikali inasema vipi katika hili janga zito namna hii. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba uzito wa jambo hilo tunaufahamu. Ndiyo sababu tulisema kwamba tutatumia na askari wetu wa Serikali Kuu pamoja wakishirikiana na wa Halmashauri na pia tutaendelea sasa kufunza hata wanavijiji ambao wana uwezo ili kuongeza nguvu hiyo. Lakini kwa mambo yaliyotokea katika Mkoa wa Singida na zaidi katika Wilaya ya Manyoni na Singida Vijijini ni kwamba huko nakumbuka pia hata Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili aliligusia na aliongelea na ni kwamba tutapeleka kikosi maalum kwenda kufanya hiyo kazi. (*Makofi*)

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini naomba nimpongeze mdogo wangu Mheshimiwa Waziri kwa mazuri anayofanya ya kujibu maswali vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimechangia katika maandishi yangu kwamba nilitaka kujua michoro ya Kijiji cha Kolo, Kondoa ambayo tayari imeingizwa katika urithi wa dunia. Je, kuna faida yoyote au msaada wowote uliopatikana kwa kuingizwa huko katika urithi wa dunia? Ama kama hakuna je, Serikali inafanya nini ili kuweza angalau wananchi wa Kondoa pale wafaidike na huo mpango wa urithi wa michoro yao katika urithi wa dunia? Ahsante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ahsante, faida ya hicho kitu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jinsi ilivyo katika sehemu mbalimbali zenye vivutio vya kitamaduni na vivutio vyetu vya mambo ya kale ambavyo tumevirithi ni kwamba wananchi wa sehemu hizo kwa njia moja au nyingine huwa wananufaika kwa shughuli mbalimbali zinazozidi kujengeka na kujitokeza pale. Kwa mfano watalii wanapokwenda pale watanunua vitu vya aina mbalimbali. Vijana watapata ajira, na hali kadhalika pia kuna pesa ambazo zitakuwa zinatolewa pale kijiji husika kwa ajili ya mambo ya ujirani mwema na wenyewe watakuwa wananufaika.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliuliza mengi lakini hoja kubwa ilikuwa ni suala la eneo la Matabe ambalo liko katika eneo lililo chini ya Maliasili. Eneo la Matabe lilikuwa zamani chini ya *Barrick* ikifanya uchunguzi, baadaye ikawaachia wachimbaji wadogo na walipochukua wachimbaji wadogo ikaonekana kwamba inabidi waombe kibali ndipo waweze kukubaliwa kuendelea na shughuli pale.

Sasa Wizara ya Nishati na Madini, Waziri akaandika barua Wizara ya Maliasili na Utalii hapakutokea majibu mpaka leo. Lakini wananchi wapo kama 500 wanasubiri. Eneo hili sasa hivi lina wachoma mkaa na wakulima. Tunaomba majibu wapewe eneo hili. Kwa sasa hivi hakuna chochote ambacho kinaweza kikaleta uzalishaji isipokuwa kuwaachia hawa wachimbaji wadogo, sijui Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa nini inaona ugumu kuwapa eneo hilo wakati *Barrick* ilipewa? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala hilo tumelipokea. Lakini bado tunalifanyia kazi ili kuweza kuona athari za aina mbalimbali kabla hatujajua uamuzi wa mwisho uwe nini. Bado tunalifanyia kazi. Ahsante.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa kuweka *pending* maswali mazito ambayo nilitaka kuuliza ya Mheshimiwa Cheyo na Mheshimiwa Mwanawetu. Naomba kuuliza swali moja ambalo limebakia kwamba je, yale mapango yaliyoko katika Tarafa ya Kipatimu mna mpango nayo gani maana yalisaidia sana katika Vita Kuu vya Maji Maji. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na nashukuru Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapango hayo yaliyoko katika Tarafa ya Kipatimu ni mapango ambayo tuna habari nayo. Lakini hata hivyo tutawatuma wataalam wetu wa Mambo ya Kale ili waje kule waangalie na waweze kufanya tathmini tujue sasa tuanze kuyarudishaje katika hali ya kuwa chenyewe kivutio bora zaidi. (*Makofi*)

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa kuzungumza nilieleza masikitiko yangu kwa kukiukwa makubaliano kati ya RCC na Wizara hii na jinsi wananchi wa Msangaji, Kiwale, Idunda, Sololwambo, Upagama, Ukoga, Ukwaheri na Tagavano walivyokuwa kwa uzalendo kuhama maeneo tengefu ya Ihefu ili kupisha eneo hili liweze kunawiri. Shule zao, barabra zao, zahanati, nyumba za walimu, vyoo, visima vya maji, vyote vimeangushwa. Gharama zake ni takriban shilingi bilioni 2.9 bila kuhusisha maji. Ninaomba ufafanuzi kwa Serikali ni hatua gani zitachukuliwa kabla ya masika, Watanzania hawa walio na upendo, hali hii watanusurika kabla ya mvua hazijaja, ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benson Mpesya, nasikitika kusema kwamba swali hilo limejibiwa na kwa sababu ni kifungu hicho hicho haturudii. Mpaka sasa nawasifu wote hakuna mtu aliyerudia, isipokuwa hapo. Kwa hiyo, naendelea na Mheshimiwa Kevela.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi. Katika mchango wangu wa kuzungumza, nilikuwa nimeeleza kuhusu kero na kilio cha mipaka, kuhusu hii hifadhi ya *Mpanga-Kipengere Game Reserve*. Wananchi wa vijiji vifuatavyo vya Mpanga Mpya, ambayo inaitwa Igalatilo, Malangali, Mambegu, Luduga, Imalilo na Wangama, wanaishi kwa wasiwasi sana. Hivyo inapelekea kwamba washindwe kulima na shughuli za uchumi.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze, anipe ufafanuzi je, hawa watu waambiwe nini? Kauli ya Serikali inasemaje kuhusu hii mipaka, ifuatwe ile mipaka ya zamani ambapo tayari walihama na wakapisha iwe *Mpanga Game Reserve* au bado wataendelea kuwasumbua wale wananchi kwa sababu mpaka sasa hivi wanaishi kwa wasiwasi sana na kwa taabu?



**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda labda Mheshimiwa Mbunge, afafanue. Wanaishi kwa wasiwasi kwani kwa sasa hivi wako wapi? Bado wamo kwenye hiyo *game reserve* au wameshatoka wako nje? Labda ningefahamu hilo ndio ningeweza kufafanua zaidi.

**MWENYEKITI:** Enhee ufafanuzi, wako ndani ya *game reserve* ama wameshatoka au nini kimetokea?

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi wamefuata ile mipaka ya zamani wako nje ya mipaka ya *game reserve* lakini bado wanaambiwa wahame tena kuna mipaka mipya. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Hiyo mipaka mipya itaonekana lini?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili jambo niweze kuwasiliana na wataalam ili tuweze kuona hiyo mipaka mipya ikoje na pia kama je, iko tayari katika kutangazwa na pia tutaanza kuona mambo mbalimbali kama kuna athari za aina yoyote. Lakini mimi ninachosema ni kwamba, ningeomba kwamba ili kusije kukatokea usumbufu mwingine naomba kwamba hawa wananchi wasirudi kwenye huo mpaka mpya unaosema waendeleo kukaa huko waliko sasa hivi ili mipaka mipya isije ikawaathiri, lakini hata hivyo baada ya hapo tutajua kama kuna mambo yoyote ambayo yatawahusu hawa wananchi kusaidiwa. (*Makofi*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia kwa maandishi nilieleza juu ya vivutio mbalimbali vinavyopatikana katika Jimbo la Kalambo, ambayo ni maporomoko ya mto Kalambo ambayo yanafikia urefu wa mita 222 pamoja na ngome ya zamani ya Wajerumani pale Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sasa ni miaka saba niko ndani ya Bunge hili toka wakati wa mama Zakia Meghji, akiwa Waziri wa Maliasili, nazungumzia juu ya Wizara hii inafanya nini ili kuweza kutangaza vivutio hivi viwili? Wenzetu wa Zambia, wametumia vizuri hili eneo lakini sisi hatufanyi chochote pamoja na ile Ngome. Badala ya wananchi kwenda kutembelea na watalii kutoka nje kuja pale wanakatishwa tamaa kwa sababu Jeshi linakaa ndani ya hiyo Ngome ya zamani. Je, Wizara imefanya nini mpaka sasa ili kuweza kusaidia utalii katika Jimbo la Kalambo kwa manufaa ya nchi hii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, tumepanga kubaini maeneo mapya ya utalii na ni kweli kwamba kwa sasa hivi msukumo wa Wizara, pia ni kujaribu kuangalia vivutio vipya vya utalii ili tuweze kuhakikisha kwamba watalii wanapokuja nchini baada ya kutoka kuona wanyama na kupanda Mlima Kilimanjaro, wakae siku zingine zaidi kwa kuangalia vivutio mbalimbali tuweze kuingiza pesa nyingi zaidi. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutakuja pia kuanza kuangalia hiyo na tujue kitu gani cha kuanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapo hapo naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, kwa kazi ambayo yeye ameifanya katika *Mount Livingstone*. Alipoona kwamba kukle kunavutia, amechukua juhudi zake mwenyewe ametengeneza CD na ametuletea CD ya kutuambia jamani haya mambo ndio yako kule na ni CD nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yenyewe jinsi ilivyo peke yake sisi tunaweza tukaitumia kwa kuanza kuuza mambo ya *Mount Livingstone* na sehemu mbalimbali za *Matema Beach*. Kwa hali hiyo pia nawaomba na Waheshimiwa Wabunge, kwa yeyote kule sehemu anakotoka kama kuna vivutio vizuri, akitusaidia hata kuleta picha pia zitasaidia zaidi na kutusukuma sisi tujue kwamba sehemu gani za kwenda haraka haraka, asante sana. (*Makofi*).

**MWENYEKITI:** Ahsante, zawadi ya Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Maana yake umesifiwa afadhali useme kabisa. (*Makofi/Kicheko*).

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitazungumzia hilo, naomba nizungumzie kuhusu mradi wa magadi ya Ziwa Natron, lakini hoja yangu ni tofauti na ile waliyozungumza watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, na hata tuseme Mawaziri wote wawili waliozungumzia kuhusu suala hili wamezungumzia kana kwamba *issue* ya mradi ule ni *site* au *location* ya kiwanda. *Location* ya kiwanda ni kitu kidogo sana, *it's not a major issue*, tatizo la mradi ule kwenye eneo lile ni *hydro geology, hydro biology, ecology* na vitu kama hivi ambavyo tungependa kujua hali na *trends* za sasahivi zipoje? Ili tutakapoweka kiwanda tuweze ku-*predict* kwamba mabadiliko yatakuwa ni haya. Kwa sasa hivi hilo hatujui na inahitaji utafiti na utafiti huu unatakiwa ufanywe na Serikali na sio na mwekezaji, je, anaweza kunipa ufafanuzi kwamba hivi ndivyo inavyotakiwa kufanywa? Asante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Naomba kumjibu Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati yetu, inayoshughulika na masuala ya haya ya Mazingira, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hoja anazosema Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ni hoja za msingi na ndio maana *environmental impact assessment* ya kwanza tulirejesha tukitaka waeleze waangalie kwa kina *ecology* ya sehemu ile kwa maana ya sehemu ile kwa maana ya maji, lakini kuangalia *chemistry* ya maji pale, lakini pia kuangalia ujazo wa maji hasa baada ya mradi ule kuanza kufanyika.

Pia eneo lile kwa maana ya *site* ya kiwanda ilikuwa pia ni jambo la msingi, kwa hivyo baada ya kuhamisha *site* kwa kilometa 32 kama tulivyosema, nadhani ni umbali mpaka ufike eneo lile la Chamwino, kabla hujafika Chamwino, ni umbali mrefu. Lakini pia tukawaambia, pamoja na kuhamisha eneo lile, tunaomba katika *environmental impact*

*assessment* mtakayofanya muangalie masuala haya yote mliyotueleza ikiwa ni pamoja na miundombinu ambayo mmeleza mtakayoitumia kwa maana ya reli na barabara. Kwa hivyo, haya yote yameelekezwa na ndio maana tumewapa fursa wafanye hiyo *environmental impact assessment* na tuweze kujiridhisha katika hayo maeneo yote ambayo Profesa Mwalyosi umeyasema. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104, napenda kusema kuwa tutaongeza dakika 30 baada ya muda wake kwisha. Mheshimiwa Makwetta.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia kwa maandishi nilizungumzia msitu mdogo ulioko Njombe, unaitwa Nyumba Nitu. Msitu huu unaaminika kwamba ni chimbuko la makabila yote ya Nyanda za Juu pamoja na nchi kama Angola, Namibia, Malawi na nchi nyingine kama *South Africa* na kwamba ni chimbuko la watawala wa jadi wa makabila hayo ya Wanyakyusa, Wapangwa, Wabena na makabila mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba katika mchango kama Wizara, nilitaka kujua kama inatambua umuhimu wa eneo hili kwa sababu mpaka sasa watu kutoka makabila hayo wanakuja kufanya matambiko ya jadi au kuhiji Nyumba Nitu. Nilidhani ni muhimu katika suala la mali kale na kumbukumbu ambazo zinajenga umoja wa makabila mahali kama hapa pangetukuzwa na pakalindwa kwa sababu panazungukwa na mali ya kampuni ya *TANWAT* ambayo mara kwa mara huchoma na msitu unapungua ukubwa wake kwa sababu ya athari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mzee John Malecela, akiwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, nadhani aliingia katika msitu huu. Upande wa Magharibi kama kilometa moja na nusu kuna pango la Nyumba Nitu, tunachojua hapa ni msitu, lakini pango la Nyumba Nitu wakati wa vita za kale walikuwa watu wanajificha katika pango hilo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Makwetta, usianze *debate* tena, unataka kusemaje kwetu?

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemaliza. Kwa hiyo, nilikuwa nataka Wizara itambue kuwepo kwa Nyumba Nitu msitu na pango na kuweka mikakati ya kufanya mahali hapo patukuzwe kwa sababu ya umuhimu huo. (*Kicheko*).

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unakujua huko? (*Kicheko*).

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipajui lakini kwa sifa alizozitaja itabidi twende tukapaone. Lakini napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba tuna kikosi kizuri tu cha wataalamu wa mambo ya kale katika Wizara na pia watakuja huko kupaona na kwa sifa ulizotuambia ni kwamba tumeshapatambua kwamba ni mahali muhimu. (*Makofi*).

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Mheshimiwa Mzee John Malecela, anasema kuna vitabu kibao vilivyofanywa na *UNESCO* kuhusu eneo hilo, sasa ni kupitia tu na vipo, anavyo. Mheshimiwa Paul Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, na mimi pia baada ya kupata maelezo kwamba Serikali inakuja na Muswada mwezi Agosti, kuhusu suala la fidia ya wahanga wa wanyamapori na mazao yao na mifugo, basi na mimi naunga mkono hoja hii. Ila napenda kujua ni lini watakuja na Muswada wa kuunda Bodi ya Asali na Nta? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Bodi hiyo tayari mojawapo ya majukumu yetu na imeainishwa kisheria na sasa hivi tuko katika hatua mbalimbali za kuanza kuiunda hiyo Bodi.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa kusema na nililalamika sana kwamba Serikali haikututendea haki, kwa sababu pamoja na kwamba imesema iliteremsha bei ya misitu lakini iliteremsha kidogo sana ukilinganisha na bei ya vitalu vya wawindaji. Kwa mfano, ilikisia kwamba katika vitalu vya uwindaji itaingiza shilingi bilioni 49, lakini imepata shilingi bilioni 18 tu, lakini katika misitu ilikisia shilingi bilioni 15 lakini Serikali, imepata shilingi bilioni 20 na kwa kuwa katika hizi shilingi bilioni 20 sehemu kubwa imetoka Mufindi, mimi ningependa kabisa kumtaka Waziri, akaongee na wadau ambao ndio wateja wa misitu kule Mufindi kama anavyosema wateja ni wafalme, kwa hivyo ningemuomba sana afanye hilo. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea mwaliko huo na mingine mingi ambayo Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walialika kwamba niende, niko tayari yote nitakwenda. (*Makofi*).

**MWENYEKITI:** Enhe, atakuwa kazini. Mheshimiwa Dr. Sigonda.

**MHE. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi wakati nikichangia kuhusu suala la mamba wala watu, ambalo nimekuwa nikitolea ripoti tangu mwaka 2006 na jinsi Serikali, ambavyo imeshindwa kushughulikia suala hilo linaloendelea hivi sasa mamba hao kuendelea kuwala watu na hata wakamla dada yangu.

Nilikuwa nazungumza kwa uchungu sana nikitegemea Mheshimiwa Waziri, angalau baada ya kuona uchungu wa namna hiyo au kusikia uchungu wa namna hiyo, angalau atatamka kwamba hiyo kazi tunaianza kesho kushughulikia hao mamba, lakini hata ile pole, Mheshimiwa Waziri, hakuitoa. Sasa mimi naomba ufafanuzi, ni lini Serikali itaamua kushughulikia hilo suala ili kusudi hawa mamba wasiendeleo kuwala watu? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kwa sababu ya muda haukutosha, lakini jibu lake nilikuwa nalo na kwa ruhusa yako naomba nimsomee jibu ambalo nilikuwa nimemuandalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu lake nilisema kwamba Wizara inatambua tatizo hilo na kwa mwaka huu 2008, imeruhusu kampuni ya *Muze Crocodile Ranch* ya mjini Sumbawanga kuja kuvuna mamba 60 katika eneo alilolisema, katika maeneo ya Ziwa Rukwa yote. Pia na Wizara yangu, itaendelea kufuatilia kwa karibu utendaji wa kampuni hiyo ili kuhakikisha kweli mamba wanavunwa na aidha, baada ya Wizara yangu kupokea orodha ya waathirika na kuifanyia tathmini pia inaandaa malipo ya kifuta machozi kwa hawa waathirika wote na pia kwa familia ya Marehemu na malipo haya yatafanyika mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha 2008/2009. Na kwa hali hiyo pia naomba nikupe pole wewe pamoja na ndugu wote waliohusika na na hali hiyo. (*Makofi*).

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1002 – *Finance and Accounts* .....Shs. 773,279,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote* 260800, *training expenses*. Wote tunajua umuhimu wa wahasibu na hasa kuendana na dunia ya sasa hivi ya mahesabu, tulitegemea kwamba wahasibu katika Wizara hii, wangetengewa fungu kwa ajili ya kusoma ili waendane na mabadiliko ya sasa hivi na hivyo kuboresha kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utakubaliana nami kwamba kifungu hiki hakina pesa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba maelezo ni jinsi gani wanawaendeleza wahasibu wao ili waweze kufanya mahesabu vizuri?

**MWENYEKITI:** Umekiona Mheshimiwa Waziri? Kipo ukurasa 282, *Finance and Accounts*, iko cha tatu kutoka chini, imeonekana mwaka jana *zero* mwaka huu *zero*. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 260800, ambacho kinahusu *training expenses*, katika kifungu 260802, ambayo inasema *training*. Imeainishwa katika sehemu mbalimbali ambayo kuna *training materials* na pia tumeonesha katika *training materials* ambayo kuna kifungu hiki kimepunguzwa. (*Makofi*)

Lakini pia katika kifungu cha kuweza kuwaendeleza kwa mwaka huu hakikuwekwa kwa sababu tumeona kwamba maandalizi yaliyokuwa tayari yako pale yanatosha na wanafunzi na wafanyakazi mbalimbali watakaelimishwa pale bado uwezo upo, isipokuwa ni kwamba *training materials* tu peke yake ndio tumeweza kuongeza lakini pia na baadhi ya mafunzo mengine yatafanywa na Hazina kwa kupitia Idara zetu ambapo mafunzo hayo pia yapo. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 1003 – *Policy and Planning* .....Shs. 674,994,600/=  
 Kifungu cha 1004 – *Information, Communication and Education*.....Shs. 25,611,900/=  
 Kifungu cha 1005 – *Internal Audit*.....Shs. 61,570,300/=  
 Kifungu cha 1006 – *Procurement Management Unit*.....Shs. 131,203,100/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 1007 – *Legal Unit*.....Shs. 29,536,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benson Mpesya, hukuwa na haraka, tuko kwenye *Legal Unit*.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho cha 1007, kifungu kidogo cha 30010700, juu ya *feasibility studies, project preparations na design*. Kifungu hiki hakikupewa pesa na ninachojua katika kipindi hiki ndio hasa cha kuweza kufanya hizo *feasibility studies*. Nataka kujua wataendesha vipi bila kufanya haya mambo? Watatumia kifungu gani? Kwa sababu hapa pamewekwa sifuri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hiyo ilifanywa mwaka jana na ikakamilika kwa hiyo, ndio sababu hatukuwekea pesa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 2001 – *Wildlife* .....Shs. 10,981,268,780/=  
 Kifungu cha 3001–*Forestry and Beekeeping*...Shs. 11,630,204,500/=  
 Kifungu cha 3002 – *Fisheries*.....Shs. 0/=  
 Kifungu cha 4001 – *Tourism*.....Shs. 6,865,378,020/=  
 Kifungu cha 4002 – *Antiquities Unit*.....Shs. 4,528,244,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu cha 1001 – *Administration and General*Shs. 500,000,000/=  
 Kifungu cha 1002 – *Finance and Accounts*.....Shs. 495,081,500/=  
 Kifungu cha 1003 – *Policy and Planning*.....Shs. 5,993,450,000/=  
 Kifungu cha 2001 – *Wildlife*.....Shs. 7,311,096,710/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 3001 – *Forestry and Beekeeping*..Shs. 11,082,067,540/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi kuhusu mgao wa Bajeti kwa ajili ya Chuo cha Nyuki Tabora.

**MWENYEKITI:** Tupo kwenye fungu au ki-*subvote* 301 ina *sub-votes* ngapi? Nne, sasa *which one*?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni hii *participatory forestry management* kama masuala ya nyuki. Lakini nilichotaka kujua ni kwamba najua mafunzo hayafanyiki Tabora, yanafanyika Olmotonyi lakini kuna shughuli nyingi...

**MWENYEKITI:** Mmh, mmh, ngoja kwanza Mheshimiwa Mwalyosi. *Sub-vote* gani unayoizungumzia hapo? *Sub-vote* 301? Na *item* gani katika hizi? Ziko *item* nne tu.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si 3001?

**MWENYEKITI:** Hiyo ni *sub-vote*, *item* gani?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hapa. Nilidhani lakini labda *under participatory management* inaweza ikawa hapo kwa sababu sioni suala la *bee-keeping* likijitokeza *specifically*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ni 4628? *Participatory forestry management*.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kujua fedha kwa ajili ya ku-*rehabilitate* chuo kile, kuandaa mitaala ya chuo kile na kutayarisha walimu na kila kitu ili chuo kiweze kuanza mwaka kesho *full swing*, inahitaji fedha. Je, fedha hizo zipo na wametengewa Chuo cha Nyuki cha Tabora?

**MWENYEKITI:** Hapa sio penyewe, katika hizi zote hazifanani kabisa. Hii *participatory forestry management* has *nothing* kabisa *like* shule ya nyuki. Kwa faida tu ya watu kwa suala lako, lakini halipo hapa, Mheshimiwa unaweza kulijibu? Lakini haliko hapa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Chuo cha Nyuki Tabora, tunakifufua na kwa hivi sasa tayari tumeshachagua na Mkuu wa Chuo amekwishapatikana na ukarabati sasa hivi unaendelea na pia wanafunzi kwa kuanzia kwa sababu tunataka waanze muhula huu kwa hiyo, wataanza kwa kusomea kwenye Chuo cha Olmotonyi kwa muda mfupi,

baada ya hapo ukarabati ukiisha wanarudishwa chuoni. Kwa hiyo, fungu lipo na kazi inaendelea. (*Makofi*).

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 3002 – *Fisheries* .....Shs. 0/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 4001 – *Tourism*..... Shs. 4,546,618,100/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu kidogo 6367, *Utalii house, phase two project*. Nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri, ni kwa nini mwaka huu haijatangewa kiasi chochote? Je, imeshakamilika au ni vipi, ipo katika hali gani?

**MWENYEKITI:** Umekiona? Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi katika Chuo chetu cha Utalii ambacho kinajengwa kile chuo hatukifadhili sisi, kinafadhiliwa na Serikali ya Ufaransa na kimeshaanza kujengwa na kimeshatoka katika hatua ya *foundation* na kinaendelea vizuri na kitaisha mwishoni mwa mwaka huu na tuna uhakika kwamba mwakani mwezi wa pili wanafunzi wataingia kuanza kusoma. Lakini pesa hizo hazimo kwenye Bajeti yetu ni moja kwa moja za msaada.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Mimi sikuuliza Chuo cha Utalii, nimeuliza *sub-vote* 6367 ambayo ni *Utalii House*, siyo *National College of Tourism*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Eeh, hiyo ni 6367, *Utalii House, Phase Two Project*. Ina zero huko *location*.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Utalii House* ni nyumba ambayo ndio itakuwa ofisi zetu mpya na ambapo imemalizika kujengwa. Kwa hiyo, sasa hivi kilichobakia ni sisi tu kuanza kuhamia kwenye hilo jengo. (*Makofi*).

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 4002 – *Antiquities Unit*.....Shs. 3,871,537,150/=



*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi, bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri mtoa hoja, taarifa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lililokaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake ya kujadili hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi, ikubaliwe na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi kwamba wamekaa sijui miezi mingapi tu na kazi imeonekana ni njema sana. Sisi tunapenda kumtakia Waziri, Naibu Waziri na Wizara yote mafanikio mema, kazi wafanye kwa bidii na kwa uadilifu kama ilivyo tutakwenda mbele. Kwa hiyo, nakupongezeni sana. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili. Kwanza kabisa tangazo hili linatoka kwa Mwalimu Msaidizi wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, kwamba anapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho jioni kutakuwa na mechi ya mpira wa miguu kati ya Bunge na Viongozi wa Dini. Maana yake Masheikh na Maaskofu, kwenye uwanja wa Jamhuri, saa 10.00 jioni, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria bila kukosa. Hilo ni tangazo la kwanza, kwa hiyo msikose kuna mpira wa aina yake huo maana yake Masheikh na Maaskofu watakuwepo. *(Makofi)*.

Halafu tangazo la pili, hili linatoka Utawala wa Bunge, kwamba mnakumbuka tuna wale wageni Wabunge la Nigeria, ni Makamishna wapo hapa. Kwa hiyo, jioni hii Makamishna wote na Wenyeviti wote wa Kamati, wanakaribishwa kushiriki kwenye chakula cha usiku kule *Saint Gasper*, minibus ipo pale mbele muende. Tafadhali muende ili muweze kuwaaga wageni wetu. Baada ya kusema hayo...

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Muongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ndio, Muongozo wa Spika, Kanuni gani?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, 68(7).

**NAIBU SPIKA:** Inasema kanuni ya 68(7), utasimama na kuomba Muongozo wa Spika. Sasa Kanuni inayofanya wewe usimame ipi?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) inasema hali kadhalika Mbunge, anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge, mwingine anayesimama.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, hiyo naifahamu, sasa hiyo imekuruhusu usimame kusudi Muongozo wa Spika. Sasa uko katika kifungu gani huo Muongozo wako sasa?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haiko kichwani, naomba niendele. (*Makofi/Kicheko*)

Humu ndani kwa kumbukumbu nilizonazo kwamba hatujawahi kufanyiwa *fire drill* au zoezi la kutoka kama moto unaweza ukatokea au kama janga lolote linaweza likatokea. Sasa wakati Mheshimiwa Waziri, anazungumza kulitokea *alarm*, hatukujua *alarm* ile ni ya nini na hatujapata taarifa yoyote ya hiyo *alarm*. (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuyatabiri majanga. Linaweza likatokea janga lolote, linaweza likatokea tetemeko au nini. Tungeomba muongozo wako kama inawezekana wakaja wataalamu wakatufundisha jinsi ya kutoka likitokea janga la aina yoyote. Naomba muongozo wako. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Hivyo umeshtushwa na ile *alarm* iliyotokea, ni kweli? Ni kweli kuna umuhimu wa kuweza kupata *training* ya namna hiyo, na mahali pengine wanafanya *mock* tu *mock* halafu mnakuta wote mnapaswa kufanya hivi. Nadhani inaunganika na ile taarifa yangu ya nyuma kwamba kwa kweli hii kitu ni muhimu sana, kwa sababu nakumbuka mwaka 1982 *House of Commonwealth* iliungua moto. Kwa hiyo, bahati nzuri wenzetu wana utaratibu, sasa hivi kuna *detector* nzuri sana. Kwa hiyo, anachokisema ni kweli na ndio hiyo ninachomaanisha, usalama wa jengo. Hatujawahi kufanya kitu cha namna hiyo nadhani kuna haja wakati fulani kufanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Muongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ndio, Muongozo wa Spika.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7), lakini nataka kuzungumzia Kanuni ya 101. Katika Kanuni ya 101 kuna vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) mpaka cha (4) na (5), vifungu ambavyo vinaturuhusu tunapoinjia

kwenye Kamati ya Matumizi, Mbunge azungumzie hoja mahususi zisizozidi mbili lakini pia anaweza kupata ufafanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulipokuwa tunaanza suala la leo uliwataka Wabunge, wazungumze mara moja. Sasa mimi nakubaliana hiyo ni *rulling* ya Mwenyekiti. Lakini je, Mwenyekiti, huoni kwamba pengine tunabanwa na muda sana hasa tunapoingia kwenye jambo muhimu kwenye fungu la matumizi? Pengine Kanuni ziangaliwe ili tuwe na muda wa kutosha tunapojadili Bajeti kwenye fungu la matumizi ili Wabunge, wasibaki na dukuduku baada ya hoja zao kuachwa kutozungumzwa kwa sababu ya kubanwa tu na muda. Naomba Muongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge, na nina hakika ninyi wote mna ratiba ya jinsi tutakavyoendesha Wizara hizi na kwamba Wizara za siku mbili zinajulikana, Wizara ya siku moja inajulikana. Sasa kwa mujibu wa Kanuni hii, kanuni zote hizi, Mbunge, wakati tukifika kwenye Kamati ya Matumizi, anapaswa kuuliza *issues* mbili na kila atakapouliza lazima ni dakika tano na anaweza kumuuliza Waziri, mara ya pili. Sasa fikirieni nyie hapa mlikuwa 40, kwa hiyo, maana yake ukisema *strictly* hapa, tungeishia Wabunge 10 tu, halafu tunafika saa tuna *gillotin*, kwa hiyo, inabidi itumike busara kwamba tunayo mengi sana, na sio uwongo wala sio, Waziri ana majibu yote ya maneno yenu, yote anayo lakini ana saa moja, nyie mmezungumza siku mbili yeye ana saa moja tu ya kujibu.

Ni matatizo ya *time*, ni matatizo pia, labda ni Bunge letu kwa sababu juzi tulipokuwa na *Commissioners* wale wa Kenya, Mabunge mengi katika dunia yanakaa mwaka mzima isipokuwa wakati wa likizo tu, wakati wa *Christmas* na mwaka mpya na kitu kama hicho. Kwa hiyo, katika misingi hiyo mnaweza kuendelea tu kuzungumza zungumza lakini kwetu sisi ni siku mbili na hii ni lazima iishe leo, sasa unafanyaje? Kwa hiyo, ndio kifungu kinampa mamlaka Spika, ku-*over rule* vitu fulani kusudi kuweza kuwa na utaratibu *smooth* wa kuendesha Bunge. (*Makofi*)

Mimi ukiniuliza leo, niko *very happy*, sikutumia *gillotin*, sipendi kabisa *gillotin*, kwa sababu pale unasoma *heading* tu basi *full stop* umemaliza. Kwa hiyo, kwenye maendeleo hamfiki, hata katika *recurrent expenditure* hampiti ni zile mliyosema sema haya. *It's not a* namna nzuri ya kuendesha Bunge. Sasa hatuna namna kwa sababu ya muda uliopo, Waziri ana majibu yote haya lakini ana saa moja tu ya kuyajibu, kwa hiyo, na nyie mnakuja mnalipizia sasa wakati wa kipindi cha Kamati ya Bunge ya Matumizi, ambayo na yenyewe ina ma-*limitations*. Watu 40 *divide*, zidisha mara 10 kila mtu anatakiwa kusema dakika 10, za Waziri, huhesabu, kwa hiyo, haiwezekani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ila nina mmoja tu ambaye amesema Mheshimiwa Benson Mpesya, hapa yeye anasema; “Sijajua kwa nini umefanya hivyo, inawezekana ni taratibu za Kanuni zetu ila naomba nikujulishe kuwa nimekwazwa sana na ninakushukuru.” (*Makofi*)

Sasa nilisema hapa kwamba mimi nawapongezeni Wabunge wote. Nilifikiri ningekumbana na *issue* kama hii ya Mheshimiwa Benson Mpesya nyingi, kwa sababu

kulikuwa na wale tembo, walikuwa tembo mahali wapi sijui na kwingine, wakawa simba *several places* nilitegemea Wabunge, wataanza na huyu simba huku na huyu simba huku, ningewakatalia hivyo hivyo. Kwa sababu Kanuni zetu zinasema, ukiuliza katika kifungu kimoja suala moja huwezi tena suala lile likaendelea kuulizwa katika kifungu kile kile.

Sasa Mheshimiwa Benson Mpesya, anasema kwamba mimi sikutaka kuuliza, nilitaka mpango. Lakini Mheshimiwa Estherina Kilasi, aliuliza pesa zitatolewa lini kusudi ku-*accommodate* watu hawa katika mambo ya shule, maji, barabara na miundombinu? Akasema watatoa hela kiasi fulani na wengine watachangia, *honestly* halina tofauti na lile ulilouliza. Kama *my judgement* ndio uzuri wangu basi, lakini hakukuwa na tofauti. Kwa sababu huyu aliandika *specifically* pesa, huyu kasema mpango, ndio huo amesema wametoa shilingi 192,000,000/= na zingine zitachangiwa na wengine. Kitu ambacho ni muhimu tunachofikiri ni kwamba hawa watu waliahidiwa ni vizuri mkafanya mapema kuwa *rehabilitate* waliondoka kwa hiyari. Hiyo nafikiri Wizara mfanye haraka na hao mnaosema ni wabia wenu, hilo nafikiri nasema hivi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumeelewana, baada ya kutangaza yale matangazo niliyotangaza sikuwa na mengine. Napenda kuahirisha Bunge, mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 14 Julai, 2008 saa 03.00 asubuhi, tutakaposhughulikia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (*Makofi*)

*(Saa 02.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,  
Tarehe 14 Julai, 2008 saa 03.00 asubuhi)*